**30 JANUARI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 30 Januari, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA**

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa hapa ambayo inatolewa chini ya Kanuni ya 39(1) ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wetu wa Kumi na Tatu wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada mitatu ya Sheria ifuatayo: -

Kwanza, ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws Miscellaneous Amendments Bill 2023)*.

Pili, ni Muswada wa Sheria ya Maarekebisho ya Sheria mbalimbali Namba Nne wa Mwaka *2023 (The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 4 Bill of 2023)* na Tatu ni Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2023.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa tayari Miswada hiyo mitatu imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa Sheria za nchi. Sasa Sheria hizi zinaitwa majina haya: -

Sheria ya kwanza inaitwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria Na.11 ya Mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws Miscellaneous Amendments Act No. 11 of 2023)*.

Pili, inaitwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4, Sheria Na.12 ya Mwaka *2023 (The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 4, Act No. 12 of 2023)* na ya Tatu inaitwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote Namba 13 ya Mwaka 2023. Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo Taarifa tuliyo nayo.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:**

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu:

(i) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

(ii) Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Haya anakuja mwakilishi mwingine Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa kwa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Khadija Shaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 1

**Utendaji kazi Baraza la Ushauri la Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza: -

Je, kwa nini Baraza la kushauri masuala ya Watu Wenye Ulemavu linashindwa kufanya kazi kama ilivyokusudiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Patrobas Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Baraza la Ushauri la Taifa la Watu wenye Ulemavu limeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu

Na. 9 ya mwaka 2010 sehemu ya tatu Kifungu cha 8 hadi 12. Aidha, Sheria hiyo imefafanua majukumu ya Baraza hili ikiwa ni pamoja na kumshauri Waziri anayehusika na Watu Wenye Ulemavu juu ya utekelezaji wa Sheria za Watu wenye Ulemavu na Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 hususani katika utoaji wa haki, usawa baina ya Wanawake na Wanaume wenye Ulemavu, masuala ya afya, marekebisho, elimu, ajira, miundombinu, mafunzo ya ufundi stadi na haki nyingine kama zilivyo katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Baraza limekuwa likiendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kama nilivyoeleza katika aya ya kwanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini kwa kuwa kumekuwepo na minong'ono ya kutokukaa kwa Baraza hili, sasa naomba Serikali iuambie umma wa Tanzania ni lini mara ya mwisho hili Baraza limekaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Baraza hili mbali na minong'ono ambayo inasikika lakini uhalisia wa Serikali ni kwamba, Baraza hili tayari lilikwishaundwa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa kifungu cha 11 ambaye ndiye anakuwa na wajibu wa kumteua Mwenyekiti na Mwenyekiti wake ni Dkt. Kija Luhende na Katibu wake anakuwa ni Mkurugenzi wa masuala ya watu wenye ulemavu. Mara ya mwisho wamekaa katika kikao chao mwezi wa Disemba mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo majukumu yanaendelea kutekelezwa na wajumbe wanakuwa 15 ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Waziri na tayari wajumbe hao wapo na kazi

zinaendelea kufanyika. Hivyo, kazi mojawapo ambayo waliifanya ni pamoja na kushauri kuhusiana na marekebisho ya sera ya watu wenye ulemeavu ambayo kwa sasa imedumu kwa kipindi cha muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pia jukumu la pili, ni pamoja na kwenda kufanya maandalizi ya kuboresha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Mpango wa kuugawa Mkoa wa Morogoro**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, mpango wa kuugawa Mkoa wa Morogoro umefikia wapi hasa baada ya kuonekana kuwa na sifa ya kugawanywa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuimarisha utoaji wa huduma za kiutawala, kiuchumi, kijamii kupitia ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa vifaa katika

maeneo ya utawala yaliyopo ya Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Tarafa, Kata na Vijiji, endapo kuna ulazima wa kuanzisha maeneo mapya, Serikali itatoa maelekezo muda muafaka utakapofika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kwa kuwa, shughuli nyingi za maendeleo zinazofanyika vijijini zinafanywa na wananchi wenyewe na vijiji vingi ni vikubwa kiasi kwamba kumekuwa na mivutano. Serikali haioni kwamba ni wakati sahihi sasa angalau wa kufanya mgawanyo wa vijiji ili shughuli za maendeleo vijijini ziendelee kufanyika vizuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava, mchakato wa kuanzisha maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji ni mchakato unaofanywa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Wao wanatakiwa waanzishe wenyewe mchakato ule kupitia vikao vyao na kama ni katika ngazi ya Wilaya wanalipitisha kwenye *DCC* kisha inakwenda Mkoani kwenye *RCC* na ndipo mapendekezo yanaletwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuyaendeleza yale maeneo ambayo ni mapya ya kiutawala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali ya nyongeza.

**MHE. MWITA. M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwaka jana Serikali ilitoa maelekezo kwenye Majimbo yetu na Mikoa yetu na wakapeleka masharti wapendekeze maeneo ambayo

wanataka kuongeza vitongoji, vijiji na Kata. Kwa hiyo, Kata mbalimbali zilikaa na kutumaini kwamba watapewa maeneo hayo waliyoomba.

Kwa sasa, nini kauli ya Serikali juu ya maelekezo ambayo waliyatoa katika maeneo yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara. Ni kama kwenye majibu yangu ya msingi kwamba kwa sasa, Serikali imeweka kipaumbele katika kuhakikisha yale maeneo mapya ya kiutawala yaliyopo yanapata miundombinu ambayo ni stahiki kwa maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeona Halmashauri nyingi zimekwenda katika maeneo yao ya kiutawala na Serikali imepeleka fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ikiwemo ofisi za Halmashauri, ofisi za Wakuu wa Wilaya kwenye Wilaya mpya na kadhalika. Kwa hiyo, mpaka pale ambapo Serikali itakapokuwa imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya msingi katika maeneo yaliyopo sasa ndipo itaendelea na mchakato wa kuongeza maeneo mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, nimekuona umesimama. Utaratibu ni kwamba, mwenye swali ukiwa na swali la nyongeza unasimama, ukikaa maana yake umeridhika na majibu. Wewe ulikuwa umekaa mpaka nilipogeuka bado umekaa nikawaita waliosimama. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ndiyo utaratibu. Mheshimiwa Asenga swali la nyongeza na sasa utauliza swali moja siyo maswali mawili.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ahsante kwa maelekezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwamba, kuhusu kugawanywa kwa Mkoa wa Morogoro hapa katika Bunge lako Tukufu, majibu yamekwishakuja kama mara mbili, mara tatu na yanatofautiana. Sisi tumeyasikia maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba, tunajenga uchumi wetu na itakapofika wakati atagawa nchi yetu katika ugatuzi wa madaraka. Ombi letu kwa Wizara ya TAMISEMI, itakapotokea hivyo waukumbuke Mkoa wa Morogoro kwa sababu Wilaya yake moja tu inazidi Mikoa mingine mingi sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hilo nadhani ni ombi ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa umelipokea. Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo tulifuata taratibu zote, vikao vya Kata vilifanyika, Halmashauri (*DCC* na *RCC)* kuomba kugawanyika kwa vijiji na Kata: Je, Serikali wakati ukifika mtatupatia kipaumbele?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Namtumbo ni mojawapo ya maeneo ambayo yameshakamilisha mchakato mzima wa kuomba maeneo mapya ya kiutawala kama ilivyo katika Halmashauri na Wilaya nyingine na Mikoa mingine hapa nchini; na pale Serikali itakapoanza mgawanyo, basi kipaumbele pia kitawekwa kwa wenzetu wa kule Namtumbo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jimbo la Chemba lina Kata tano…

**SPIKA:** Simamisha kisemeo vizuri.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Chemba lina Kata tano ambazo zina vijiji zaidi ya vinane, hivyo imekuwa ni kazi kubwa sana kwa Watendaji wa Kata kufanya kazi. Nini sasa msimamo wa Serikali kugawa Kata hizo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, nirejee katika majibu yangu ya msingi, pale ambapo miundombinu itajengwa katika maeneo ya kiutawala yaliyopo sasa ya kukidhi mahitaji yote ya wananchi katika maeneo hayo, ndipo Serikali itaenda katika mchakato wa kugawa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu unapogawa kata, maana yake inabidi shule, zahanati na vituo vya afya na huduma nyinginezo ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa sote ni mashuhuda, Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka fedha nyingi katika kuhakikisha vituo vya afya vinajengwa, shule mpya zinajengwa katika kata ambazo zilikuwa hazina shule za sekondari. Kwa hiyo, mpaka pale mchakato huu utakapokamilika ndipo Serikali itaanzisha maeneo mapya ya kiutawala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 3

**Zabuni kutolewa kwa kuzingatia makundi maalum**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, zabuni ngapi zilitolewa na Halmashauri za Majiji, Manispaa na Wilaya kwa makundi maalum hasa wanawake kama sheria inavyotaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond**,** Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Marekebisho yake ya mwaka 2016 katika Kifungu cha 64 (2) (c) na Tangazo la Serikali Na. 333 la Mwaka 2016, taasisi zinapaswa kutenga asilimia 30 ya manunuzi kwa ajili ya makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeweka utaratibu wa kusajili Makundi Maalum ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Aidha, vikundi maalum vipatavyo 345 vimesajiliwa katika Halmashauri ambavyo vimekidhi vigezo vya kupewa zabuni. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya vikundi 228 vya makundi maalum vilipewa zabuni mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni sawa na asilimia 66. Aidha, kati ya hivyo, vikundi vya wanawake vipatavyo 70 vilipata zabuni.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa watendaji ngazi ya Halmashauri ili kuweza kusimamia na kuwahamasisha wananchi wenye sifa kujiunga na vikundi kwa ajili ya kupata fursa za zabuni kadri ya sheria zilizopo, ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini inaonekana dhahiri kwamba waliopata ni wachache sana na hapo inaonesha kwamba uelewa ni mdogo: Je, Serikali ina mpango gani sasa kupeleka elimu hii katika ngazi za chini za Kata?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa fedha hizo zipo lakini haziendi kama inavyotakiwa na wahusika hawazipati, ni lini sasa Serikali itaweka nguvu kubwa ili wote waweze kupata kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uelewa katika jamii yetu na hasa makundi ya wanawake vijana na watu wenye ulemavu kutumia fursa ya asilimia 30 ya zabuni bado iko chini. Mpango wa Serikali, kwanza tumeendelea kutoa elimu katika jamii kupitia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii na pia tumeelekeza Wakurugenzi na Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji kuwa ajenda hiyo ni ya kudumu katika vikao vyote vya vijiji ili wananchi wapate uelewa waweze kutumia fursa hii ya asilimia 30 ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kwamba kweli fedha zipo, lakini haya makundi hayapati, sababu ni ile ile kwamba wengi hawajajiunga

kwenye vikundi vile, lakini baadhi ya vikundi havina sifa na Serikali itaendelea kuhamasisha ili wajiunge na kutumia fursa hiyo ipasavyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na changamoto alizozisema Naibu Waziri za makundi hayo, bado vile vikundi vichache vilivyofanikiwa kupata zabuni havikuweza kulipa kwa wakati licha ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kueleza changamoto ya kutolipa hayo madeni kwa wakati. Nini mkakati mahususi wa kusaidia kulipa hizo fedha na hasa haya makundi mahususi ili kupunguza adha ya umasikini na kuendelea kufanya biashara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imeweka mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba tunawapa kipaumbele Makundi haya Maalum yanapopata zabuni ya asilimia 30 kulipwa mapema zaidi; kwa sababu tunajua kwamba ni makundi ambayo hayana mtaji wa kutosha.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuhakikisha inatoa kipaumbele na pale wanapomaliza zabuni zao wanapata malipo ili waweze kuendelea kufanya shughuli za ukandarasi au shughuli nyingine kwa ufanisi zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Utaratibu wa kuajiri Watendaji kwenye Halmashauri nchini**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, ni utaratibu gani unatumika kuajiri Watendaji kwenye Halmashauri nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kuajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata, ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga fedha za mishahara kwenye Bajeti na kuomba Kibali cha Ajira Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Baada ya kupata kibali Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekasimiwa jukumu la kutangaza, kuwafanyia usaili waombaji, kuwaajiri na kuwapangia vituo vya kazi Maafisa Watendaji waliokidhi vigezo vya ajira. Utaratibu huu unashirikisha Halmashauri na Mamlaka za Ajira za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka ya fedha ya 2020/2021 hadi 2022/2023 Serikali imeajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa 1,659 na Maafisa Watendaji wa Kata 394 na kuwapanga kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti na kutoa vibali vya ajira kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata kulingana na mahitaji kote nchini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo ya Serikali, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye maeneo ya Mitaa, Vijiji na Vitongoji kuhusiana na Watendaji hawa kuonekana kufanya shughuli ambazo ni kinyume na utaratibu. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa semina ama mafunzo maalum kwa Watendaji hawa ili waweze kufanya kazi kulingana na malengo ambayo wamepelekwa kwenye maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Watendaji wengi wamekuwa wakijishirikisha na masuala ya kisiasa, hivyo kusababisha wananchi kupata mkanganyiko wa kujua Watendaji hawa ni wa Serikali ama ni wanasiasa? Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na Watendaji hawa ili wananchi waweze kujua Watendaji wako pale kwa ajili ya majukumu yapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwaifunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Maafisa Watendaji wa Vijiji, Maafisa Watendaji wa Kata ni Watumishi wa Serikali na wanaelekezwa kutumia utaratibu wa utendaji wao kwa kufuata taratibu za Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, wale ambao wanakiuka kutekeleza majikumu yao, hatua za kiutumishi zitaendelea kuchukuliwa dhidi yao. Pia tutaendelea kuhakikisha tunawajengea uwezo kwa kuhakikisha kwamba tunawafanyia semina za mara kwa mara, tuna *job training* kwa Watendaji wetu.

Mheshimiwa Spika, pia jambo kubwa tumeshaelekeza kwamba Wakurugenzi Watendaji wanapoajiri Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata wawafanyie *orientation* ya majukumu yao lakini pamoja na kuwapa *job description* ili wajue majukumu yao na pia mipaka yao.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusiana na kujihusisha na siasa, kauli ya Serikali ni kwamba Watumishi wa Serikali, Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata wanatakiwa kufuata taratibu za Utumishi na kufuata miiko ya kazi zao, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Asilimia 50 ya Watendaji katika Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha wamekuwa wakifanya kazi kwa kujitolea, yaani wamekuwa wakikaimu kwa muda mrefu sana: Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Watendaji hao wanapata ajira rasmi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Halmashauri ya Longido na hata katika Halmashauri nyingine kote nchini wapo Watendaji wa Vijiji, wa Mitaa, wa Kata ambao wanajitolea na Serikali imeweka utaratibu, kila pale kibali cha ajira kinapotolewa, wale ambao wanajitolea katika maeneo hayo wanapewa kipaumbele; na kwa sababu ajira hizi zinatolewa katika ngazi za Halmashauri, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwasisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba wanawapa kipaumbele wale Watendaji

wanaofanya vizuri ambao wanajitolea katika maeneo yao kila mara ambapo kibali cha ajira kinatokea, ahsante.

**SPIKA:** Hivi Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, ule Mwongozo wa Ajira ambao mlisema, kwa wale watu wanaojitolea umeshakamilika ama bado? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, tunaendelea, lakini tumeshamaliza na ninadhani tutakuja kutoa tamko hapa Bungeni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunausuburi kweli huo mwongozo, kwa sababu vijana wanaojitolea huko kwenye sekta nyingi wako wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Watendaji hao wa Kata, Vijiji na hata wa Mitaa wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana kwa kukosa vitendea kazi na hivyo kutokutoa huduma kwa ufanisi kwa wananchi. Napenda kujua ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanapeleka vitendea kazi na hasa pikipiki kwa wale watendaji ambao wako kwenye maeneo ya vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Watendaji wa Kata na Vijiji wana changamoto ya vifaa na vyombo vya usafiri lakini Serikali na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaelekeza,

tumeanza kununua pikipiki kwa ajili ya Watendaji wa Kata na tunahakikisha kwamba tunatengea bajeti tayari wanalipwa shilingi 100,000 kila mwezi kwa ajili ya uendeshaji. Kwa hiyo, hatua hiyo tayari tumeanza kuichukua kama Serikali. Tunajua bado tuna kazi kubwa ya kufanya. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata na hususan katika eneo hili la usafiri, ahsante.

**SPIKA:** Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utumishi, alipokuja Iringa alikutana na tatizo la Watendaji ambao walikuwa wamejitolea muda mrefu na hawakupata ajira na aliwaambia kwamba wawaajiri na mpaka leo hawajaajiriwa: Je, ni kwa nini baadhi ya Wakurugenzi hawatimizi matamko yale ambayo Mawaziri wanatoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati alikuja Naibu Waziri wa Wizara gani?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, alikuja Naibu Waziri wa Utumishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa nani?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete yupo? Aaah, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, jibu swali lake Mheshimiwa. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nilipokuwa kwenye ziara Mkoa wa Iringa kwenye Manispaa ya Iringa nilikutana na

changamoto ya vijana ambao walikuwa wamejitolea ambao walikuwa wamefanya kazi kwa takribani miaka miwili, lakini pamoja na kwamba walikuwa wamefanya hivyo ilipofika kwenye jambo la ajira, walipokwenda kufanyiwa usaili walionekana kwamba hawafai, lakini Serikali kupitia taratibu zake ilijiridhisha kwamba kulikuwa na sintofahamu katika mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, tulielekeza kwamba mchakato ule urudiwe tena lakini pia wale vijana waliokuwa wanajitolea ambao walionekana kuonewa warudishwe kazini mara moja. Sasa juzi nilikuwa naongea na Mheshimiwa Mbunge akanihakikishia kwamba wale vijana bado hawajaajiriwa. Sisi kama Serikali tumeshatoa maelekezo kupitia Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi kulishughulikia jambo hilo mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hebu kidogo hapo kwenye hawafai, hebu fafanua kidogo kwenye "hawafai."

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa tulizopewa pale, vijana wale walionekana kwamba wamefeli katika mtihani, lakini kiukweli ni kwamba kulionekana kuna figisu zimefanyika katika kuhakikisha kwamba wamefikia hayo matokeo na ndipo Serikali ilipoelekeza mchakato huo uangaliwe tena upya. Ndiyo maana mpaka sasa hivi tunapozungumza hapa hakuna majibu ya wale ambao wameshaajiriwa kwa sababu ziko taratibu zinazofanyika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi wa Utumishi na Utawala Bora, nafikiri utagundua kwa nini ule Mwongozo ni wa muhimu kuja ili wale wanaojitolea wawe na hizo sifa. Kwa sababu kama hawana sifa, halafu wanajitolea maana yake kazi hiyo hawaifanyi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Maana yake kama ni Madaktari, kama ni Manesi maana yake hao hawapaswi kutibu watu maana hawana huo uwezo, na kama ni Walimu maana yake hawapaswi kuwa shuleni kuwafundisha watoto maana wao wenyewe walifeli. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuharakisha ule Mwongozo uwe tayari ili hata wale wanapoomba kujitolea wajitolee wenye sifa ili wakati wa ajira iwe ni rahisi zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Watumishi wanaotumia vibaya fedha za miradi ya Serikali**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Watumishi wanaohusika kutumia vibaya fedha za miradi ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia masuala ya nidhamu katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298

ambacho kimewapa Mamlaka Wakuu wa Taasisi kusimamia masuala ya nidhamu kwa watumishi walio chini yao pale wanapokiuka kiapo cha ahadi ya uadilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uvunjifu wa maadili katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Serikali imeendelea kuwachukulia hatua mbalimbali za kinidhamu Watumishi wa Umma wanaotumia vibaya fedha za miradi ya maendeleo ikiwemo kuwasimamisha kazi na kuwaanzishia mashauri ya kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, mathalan, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Desemba, 2023, TAKUKURU ilifuatilia matumizi ya rasilimali za umma kwenye utekelezaji wa miradi 2,541 yenye thamani ya shilingi trillioni 8.26, ambapo miradi 467 ilibainika kuwa na upungufu mbalimbali ikiwemo uvujaji na kutokuwa na thamani ya fedha. Kutokana na matokeo hayo, hatua kadhaa zilichukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329, ikiwa ni pamoja na kuanzisha uchunguzi kwa miradi 274 ambapo watumishi 51 walichukuliwa hatua za kinidhamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimesikia majibu ya Naibu Waziri, niseme kwamba sijaridhishwa. Nataka kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba watumishi elfu mbili na kitu wame…..

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga subiri kidogo. Hujaridhishwa kwa maana ya kwamba jibu la Mheshimiwa Waziri halijajibu swali lako…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ndio maana nataka niulize maswali mawili…

**SPIKA:** Maana kazi yangu ni kusimamia kanuni hapa mbele ili kama unaona swali lako halijajibiwa kikamilifu, huwezi kuuliza maswali ya msingi, maana yake jibu halipo.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, hapana, nipe nafasi niulize maswali mawili, labda nitapata majibu. (*Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa inabidi uwe umeridhika na hayo majibu ndiyo uulize, kwamba haya majibu yaliyoko hapa, lakini bado una maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, endelea Mheshimiwa, nimeelewa kwamba umeridhika na majibu sasa unataka kuuliza maswali yako ya msingi. *(Makofi)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba pamoja na watumishi elfu mbili na kitu hao waliobainika, nataka kujua, wangapi ambao wamefungwa kwa ajili ya makosa ya kutuhujumu wananchi pamoja na Mheshimiwa Rais anatafuta pesa anapeleka kwenye miradi ya maendeleo? Nawe ni shahidi, umesema kwamba watu elfu mbili na kitu walibainika; wangapi walioko magerezani mpaka sasa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Serikali ya Awamu ya Tano ilitangaza kwamba itatengeneza Magereza ya Mafisadi ambao wanabainika ili wasiende moja kwa moja Mahakamani, wakae kwenye *lockup* za Mahakama ya mafisadi? Je, hamuoni sasa ni wakati muafaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge la kutaka kujua wangapi wapo magerezani; naomba nisiwe muongo mbele ya Bunge lako naomba nijiridhishe juu ya idadi kamili ili niweze kuja kumwambia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, swali la pili juu ya utekelezaji wa magereza maalum kwa ajili ya hawa wanaohujumu uchumi wetu, nadhani jambo hili linategemea zaidi upatikanaji wa fedha ili kuweza kutekeleza azma hiyo ya viongozi wetu kama ambavyo iliahidiwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa atatekeleza yale yote ya walitangulia kabla yake na ya kwake yeye ni kuandaa Tanzania anayoitaka, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge jibu alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali la nyongeza la kwanza linalohitaji takwimu yuko sawa kabisa kikanuni inaruhusiwa Mheshimiwa Waziri kutoa majibu baadaye yale yanaohitaji takwimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge atakaupa takwimu Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tunafahamu kwamba Baraza la Madiwani ni mamlaka ya nidhamu kwa watumishi ngazi ya halmashauri. Je, Mkurugenzi ana mamlaka ya kutengua maamuzi ya Baraza la Madiwani pale wanapobaini kwamba watumishi wamefanya makosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, maamuzi ya Baraza la Madiwani hayapingwi na mtu yeyote na maamuzi hayo ni maamuzi yaliyokamilika ikiwa yamefuata taratibu na kama kuna mtu yeyote ambaye hatoridhika na maamuzi hayo, basi taratibu za kisheria zimewekwa wazi ili kuweza kutengua maamuzi hayo na siyo Mkurugenzi kujipa mamlaka juu ya maamuzi yanayofanya na Baraza la Madiwani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni mpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini niongezee kwenye jibu alilolitoa kwa Mheshimiwa Genzabuke. Kamati ya Halmashauri inapojigeuza kuwa Kamati ya Nidhamu, Katibu wake ni Mkurugenzi na Wajumbe ni wale Madiwani. Sasa haiwezekani Katibu na ile Kamati wamefanya maamuzi halafu Katibu akaenda akageuza. Kama kulikuwa kuna mabadiliko hayo basi angepaswa kurudi tena kwenye Kamati ile ile ili aweze kugeuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutajaribu kulichukua kwa kushirikiana na TAMISEMI, tulifuatilie tuone kilichotokea hasa ni kitu gani, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Daud Hassan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 6

**Uwepo wa rushwa katika vyuo nchini**

**MHE. AMINA DAUD HASSAN** aliuliza:-

Je, Serikali inatambua uwepo wa rushwa kwa wanafunzi katika vyuo vyetu hapa Nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Daud Hassan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa rushwa katika sekta ya elimu kwa kuzingatia matokeo ya utafiti wa Hali ya Utawala na Rushwa wa Mwaka 2020. Rushwa ya Ngono ni kosa la jinai kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329. Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuzuia rushwa katika vyuo vyote nchini kupitia tafiti na mikakati ya kuzuia rushwa ikiwemo programu mbalimbali za kuelimishaji umma na vilabu vya wapinga rushwa shuleni na vyuoni.

Mheshimiwa Spika, mathalani mwaka 2019, Serikali ilishirikiana na wadau kuendesha kampeni ya Vunja Ukimya kwa ajili ya kupiga vita rushwa hususani rushwa ya ngono kwa kuhamasisha jamii isikae kimya dhidi ya vitendo hivyo. Katika kipindi cha mwaka 2020 - 2023, taarifa 11 za malalamiko ya vitendo vya rushwa ya ngono katika vyuo vyetu zilipokelewa na majalada tisa ya uchunguzi yalianzishwa; ambapo majalada mawili yamefungwa baada ya kukosekana ushahidi. Jalada moja limepata kibali cha kumfikisha mtuhumiwa mahakamani na majalada mawili yamependekeza watuhumiwa wake wachukuliwe hatua za kinidhamu na jalada moja, kesi imeshindwa mahakamani. Majalada manne yanaendelea na uchunguzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Daud, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ni vigezo gani ambavyo vinatumika kwa wanafunzi wengine wachache ambao wamefanya vizuri kuachwa na kuchukuliwa wanafunzi wengine ambao wamefanya vibaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, samahani, sijaelewa swali lake.

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Elimu yupo? Waziri wa Elimu umelisikia swali lake?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Maana nahisi lile linahamia kwenu kwa sababu linahusu wanafunzi vyuoni, kwa nini wanaachwa waliofaulu wanachukuliwa waliofeli? Kama siyo rushwa.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nimeelewa swali lake, nili-*frame* vizuri ili niweze kulijibu. Kama anasema kwamba kuna wanafunzi wameomba kujiunga na chuo halafu kuna ambao wamefaulu zaidi wameachwa lakini ambao wamefaulu kidogo wakachaguliwa, maelezo yake yanaweza yakawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, unaweza ukawa umefaulu vizuri sana lakini *course* uliyoiomba wewe ina ushindani mkubwa zaidi kiasi kwamba waliofaulu kuliko wewe wamechukuliwa lakini *course* nyingine ambayo ungeomba ungeuipata hukuiomba wewe, halafu mtu ambaye hakufaulu kama wewe akaomba akaipata.

Mheshimiwa Spika, lakini ili kuhakikisha kwamba kuna haki wakati unapoomba kujiunga na chuo tunatangaza majina ya waliyoomba, tunatangaza *marks* zao, tunaonyesha *cut off* kwa kila *program*. Ili endapo unaona ulikuwa umefikia *cut off* kwenye *course* uliyoiomba na hujachukuliwa unaruhusiwa kulalamika na sisi tutafuatilia uingie chuoni na waliofanya hivyo wachukuliwe hatua mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala muhimu ni kuhakikisha kwamba unapoomba kujiunga na chuo ujue ile *program* unayoiomba angalia kwa mfano mwaka jana *cut off* ilikua kiasi gani. Unaweza ukawa umepata *first class* umeomba kusoma sheria *University of Dar es Salaam* lakini *University of Dar es Salaam* inachukua *first class* yenye *point* chache zaidi kuliko ulizoomba wewe. Halafu ungeomba kwenda kusoma *course* nyingine pale pale *University of Dar es Salaam* ungechaguliwa lakini hukuomba halafu mwenye *marks* kidogo kuliko wewe, *point* kidogo kuliko wewe

kaiomba ile kachukuliwa. Hiyo inaweza ikaonyesha kana kwamba pengine aliyefaulu vizuri hakuchukuliwa lakini kwa sababu ya *choice* uliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunashauri kila anayeomba kwenda kusoma aangalie matokeo. Kila kitu kipo kwenye *website*, anaweza akajua kama nikiomba *course* hii ni vipi naweza nikapata kuingia, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mamlaka ya Usimamizi wa Mitihani Vyuo Vikuu kuwa chini ya Wahadhiri imekuwa ni miongoni mwa sababu ya rushwa ya ngono vyuo vikuu. Sasa ni kwa nini sasa Wizara isione umuhimu wa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuondoa Mamlaka ya Usimamizi wa Mitihani kwa Wahadhiri ili kuzuia mianya ya rushwa ya ngono ambayo inaweza kujitokeza vyuo vikuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa unajua mimi nilikua mwalimu, sasa najaribu kuwaza huo uhuru unataka uelekee wapi? Yaani nani akaanze kusahisha mitihani ya kwangu mimi. Ndio maana huwa kuna *external examiners* wanakuja kwa ajili ya kuangalia kama umetenda haki au hujatenda. Hili nalo ni la Wizara ya Elimu, kwa hiyo Mheshimiwa ngoja amalizie Mheshimiwa Waziri wa Elimu. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, la kwanza, nashukuru sana kwa fursa hii. Vyuo vikuu vyenyewe vinaendeshwa kwenye mambo ya taaluma na *senate* zao na kama ulivyosema taratibu za kusahisha mitihani zipo, kuna Bodi za kupitia ile mitihani lakini vilevile kuna wanaokagua mitihani hiyo mara nyingi wanatoka chuo cha nje hata nje ya Nchi lakini naomba nitoe kauli ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, malalamishi yoyote ya rushwa ya aina yoyote hasa rushwa ngono tunahimiza yaripotiwe mara moja.

Tunachukulia *very serious* suala la kumuonea mwanafunzi kwa kutaka rushwa na hasa rushwa ya ngono na tuhuma tukizisikia hata kwa hisia sisi tunaanza kuzifanyia uchunguzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningetoa wito kwa Watanzania wote, wazazi na wanafunzi wakati ambapo kuna dalili yoyote kama hiyo tafadhali toa taarifa lakini muhimu kutoa taarifa ya ukweli. Kwa sababu ukitoa taarifa ambayo inajikanganya wakati mwingine kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri hapa wakati mwingine inakua vigumu sana ku-*establish* lakini Serikali inachukulia *serious* sana kuwa na haki katika usahihishaji wa mitihani ili tuhakikishe wanaofaulu kweli wamefaulu wamefauli kwa haki, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, sasa aulize swali lake.

Na. 7

**Hisa za Serikali kwenye makampuni**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza:-

Je, Serikali inamiliki hisa kiasi gani, kwenye makampuni mangapi na hisa hizo zina thamani kiasi gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa niaba ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji, majibu. Ama umehamia huko maana sina uhakika, ni sahihi? Umejipa Naibu.

Haya Mheshimiwa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imewekeza katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Kampuni zipatazo 304 na uwekezaji wa Serikali una thamani ya shilingi trilioni 76. Kati ya uwekezaji huo, Serikali ina hisa zipatazo milioni 420 katika kampuni 54 ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji fedha kwa ajili ya miradi yake. Sasa ni kiasi gani cha fedha ambacho kinatokana na uwekezaji huo wa Serikali kwenye mashirika hayo ambacho kimeenda katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa sababu hiyo ni *book value* na *what we need is actual cash*.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, kwa kuwa bajeti yetu ni trilioni 40 na ushee na uwekezaji wetu una thamani zaidi ya trilioni 76, nini mkakati wa Serikali kutumia hisa hizo ama kuongeza mtaji ili tukopee kwa ajili ya ku-*finance* miradi yetu ya kimkakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Londo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika takwimu au hesabu za kiuhasibu kwa mwaka 2022/2023 Serikali iliweza kukusanya mapato ambayo siyo ya kikodi kutokana na gawio na michango ya mashirika haya ambayo imeenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali zaidi ya trilioni 1.008 lakini lengo lilikuwa ni kupata bilioni 931. Kwa hiyo, tumeweza kufanya

vizuri kwa zaidi ya asilimia 108. Hizo fedha zote zaidi ya trilioni moja zimeingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa maana ya kuchangia katika bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili la Mheshimiwa Londo, moja ya mikakati ya Serikali ambayo inaendelea sasa? Mosi, ni kufanya mageuzi katika mashirika ya umma na taasisi za Serikali ambazo Serikali imewekeza fedha huko ili ziweze kuwa na tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, moja ya maelekezo ni kuona ni tunakuwa na sheria ambayo itampa mamlaka makubwa zaidi Msajili wa Hazina ili aweze kusimamia vizuri taasisi hizi ili ziweze kutoa gawio au kufanya vizuri ili fedha hizo sasa ndizo ambazo zuitaingizwa au zitaongezwa kwenye Bajeti Kuu ya Serikali kama ambavyo ulivyosema ambayo ni zaidi ya trilioni 40. Kwa hiyo, moja ya mikakati ni hiyo kwamba tuhakikishe tunasimamia vizuri ili michango na gawio zinazotokana na uwekezaji wa Serikali katika makampuni na taasisi hizi za Serikali yaweze kuwa na tija au yaongezeke zaidi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, sasa aulize swali lake.

Na. 8

**Ujenzi wa ukuta wa Ikulu Ndogo ya Muungano Pemba**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga ukuta wa Ikulu Ndogo ya Muungano Pemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Jimbo la Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaandaa mipango mahususi ya kutekeleza suala hilo ambapo tathmini ya kitaalamu ya kina imefanyika ili kupata gharama za ukarabati wa Jengo la Ikulu ndogo ya Muungano Pemba ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, inategemewa kuwa, utekelezaji utaanza katika mwaka wa fedha 2024/2025, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Ali Omar, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli iliyofanyika ya Serikali, je, Serikali ina mpango gani wa kufanya upembuzi yakinifu katika eneo lile kabla ya kujenga huo ukuta, kwa sababu hali ya pale iko mbaya kabisa, maji ya bahari yanakula katika lile eneo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri, je yuko tayari kwenda pamoja katika eneo lile kuona hasa hali halisi ilivyo katika eneo lile ambalo Serikali inataka kujenga hiyo Ikulu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunapotaka kufanya ujenzi ama ukarabati hasa kwa jengo kubwa la muda mrefu kama lile lazima tufanye upembuzi yakinifu lakini lazima tufanye tathmini kwa ajili ya kujua gharama na mambo mengine, zaidi ukizingatia kwamba jengo lile lipo karibu ama ufukweni mwa bahari. Kwa hiyo hilo jambo la kufanya upembuzi yakinifu ni jambo la msingi na lazima tutafanya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kwenda, nipo tayari kwa ajili ya kwenda kukagua kuona namna ambavyo tunaweza tukaanza harakati za ujenzi katika jimbo hilo lakini pia kuona namna ambavyo limeathirika jengo hilo kwa sababu ni la muda mrefu. Baada ya Bunge hili nimuahidi Mheshimiwa Mbunge tutakuwa Wete kwa ajili ya kukagua jengo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 9

**Utekelezaji wa Sheria ya kuhudhuria mafunzo ya JKT**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani Sheria ya Vijana kuhudhuria mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria inatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stagomena Tax, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 1964 imeweka ulazima wa vijana wa Tanzania wanaomaliza kidato cha sita kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka mmoja kwa mujibu wa sheria. Mafunzo hayo huwajengea vijana uzalendo, ukakamavu na uhodari.

Mheshimiwa Spika, mafunzo hayo yalisitishwa mwaka 1964 kutokana na hali ngumu ya uchumi iliyoikumba Dunia. Kutokana na umuhimu wa mafunzo haya, Serikali iliyarejesha tena hapo mwaka 2013 na sasa hufanyika kwa miezi mitatu. Kwa mwaka jana au kwa mwaka huu mwaka 2023 vijana idadi 260,061 ambayo ni sawa na asilimia 59 wameweza kujiunga na mafunzo haya. Serikali inaendelea kuongeza miundombinu lengo ikiwa ni kuwachukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita kufikia mwaka 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza ambalo linaendena na pongezi kwa Serikali kurejesha mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, swali langu; je, kwa kuwa vijana wengi wamekuwa na mwitikio mkubwa sana wa kupenda kujiunga na mafunzo ya JKT lakini nafasi hazitoshi kwa wale wa kidato cha sita wanaomaliza na wale wa kidato cha nne ambao wana mafunzo ya ziada kama ya ufundi na kadhalika.

Je, ndani ya mifumo ya Serikali iko tayari kuongezea nguvu Jeshi la Kujenga Taifa ili kila kijana mwenye sifa aweze kupata nafasi hiyo kwa nia ile ile ya kumjengea ukakamavu na uhodari katika utendaji kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato David Chumi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli mwitikio umekuwa mkubwa na Jeshi la Kujenga Taifa tumekwishaandaa mpango wa utekelezaji utakaowezesha kuwachukua vijana wengi zaidi. Utekelezaji wa mpango huu utatuwezesha kuwachukua vijana wengi lakini pia utategemea upatikanaji wa rasilimali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa *condition* hii ya kupita JKT na Serikali imekiri kwamba uwezo wa kuwachukua watu wote haupo lakini *recently* tumekuwa tunaona ajira nyingi zinazotangazwa zimeweka kigezo cha kwamba kijana awe amepita JKT. Kwa hiyo vijana wengi wanatamani waingie kwenye hizi ajira lakini kigezo cha kupitia JKT kinawanyima fursa na hawatendewi haki;

Je, hatuoni sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuondoa kigezo cha kupita JKT mpaka pale itakapokuwa tayari kuwahudumia watu wote ili ushindani uweze kuwa sawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba lalamiko hili limeshasikika, na kama tulifufatilia Taarifa ya Tume ya Jinai ni moja ya

mapendekezo yaliyotolewa na ni pendekezo linalofanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nilikuwa na swali kama hilo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate Mbunge wa Kyerwa sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Hitaji la Majisafi Wilaya ya Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, lini mradi wa maji wa vijiji 57 ambao utaanzia Kyerwa, Nyakatuntu mpaka Kimuli Wilayani Kyerwa utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante; kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate (Mb) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji katika vijiji 57 Wilayani Kyerwa. Hadi sasa, utekelezaji wa mradi huo unaendelea katika vijiji 27 ambavyo ni Nkwenda, Rwabwere, Karongo, Nyamiaga, Nyakatera, Kagu, Masheshe, Nyamweza, Kaikoti, Iteera, Muleba, Chanya, Kimuli, Rwanyango, Chakalisa,

Kikukuru, Karambi, Rwele, Mukunyu, Rukuraijo, Makazi, Kibimba na Mabira.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa katika miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa matenki matano (5) yenye jumla ya ujazo wa lita 1,450,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 110, ujenzi wa vituo 102 na vioski 18. Utekelezaji wa miradi hiyo umefikia wastani wa asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2024. Mradi utakapokamilikautawanufaisha wananchi wapatao 83,000. Miradi hiyo katika vijiji 30 vilivyobaki itatekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuulizwa maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa magari ya kuchimba visima kwenye kila mkoa, lakini magari haya yamekuwa yakienda kila wilaya yanachimba aidha visima viwili, vitatu na kuondoka. Kwa mfano kama Kyerwa tulipewa visima 16 lakini gari lilipokuja lilichimba visima vine;

Je, ni kwa nini magari haya yanapoenda kwenye wilaya yasikamilishe kazi ya kuchimba visima vyote ambavyo vimeainishwa ili kuondoa adha ya usumbufu unaojitokeza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mradi wa Lutunguru, Kaisho mpaka Isingiro unajengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza mkandarasi anajenga lakini mpaka sasa hivi anadai zaidi ya milioni 600 ili kukamilisha mradi huu;

Je, ni lini mkandarasi huyu atalipwa ili awamu ya pili iweze kuanza na kuondoa adha inayojitokeza kwa wananchi wangu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante; naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, gari likifika eneo la tukio likamilishe kazi. Katika kikao cha wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri Aweso tayari ameshawaagiza watendaji wote mikoani kulitekeleza hili; na hii ni baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pia kujionea hali iliyokuwepo pale Lindi. Kwa hiyo tayari kama Wizara tumeendelea kujipanga kuhakikisha kwamba ikifika wakati basi hata tuweze kufanya kazi kikanda. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge Bilakwate nikupongeze kwa maono yako haya ambayo tayari Wizara inafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya mradi ipo asilimia 80 na tunaelekea kukamilisha. Madai ya wakandarasi pamoja na mkandarasi huyu anayefanya kazi mradi huu tumeanza kupata fedha na tunaendelea kuanza kulipa kwa mafungu. Kwa hiyo nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge, nikupongeze kwa kufuatilia na madai haya tutakwenda kulipa ili kazi ziweze kuendelea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Kwa kuwa gari la kuchimba visima lililoletwa katika Mkoa wa Lindi halijawahi kufika katika Wilaya ya Kilwa;

Je, ni lini gari hili litaletwa Kilwa ili liweze kuchimba visima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu gari kufika Kilwa Mheshimiwa Waziri ameshaagiza lile gari likafanye kazi. Tutaendelea kumuelekeza *RM* Lindi ili Kilwa nanyi muweze kunufaika na gari lile.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe maswali mafupi upande wa Mawaziri au Naibu Mawaziri mnaokuja kujibu majibu mafupi. Lakini pia kwa sababu nakuwa nimeshamwita Mbunge wewe usimwite tena Mbunge ili tupunguze kutumia muda mrefu katika majibu yetu.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina Mbunge wa Kisesa sasa aulize swali lake. Haya Mheshimiwa Catherine Magige kwa niaba yake.

Na. 11

**Madeni ya Wazabuni na Wakandarasi wa Ndani**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE K.n.y. MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza: -

Je, Serikali imelipa au kukataa madeni mangapi ya wazabuni na wakandarasi wa ndani tangu ianze uhakiki wa madeni hayo ambayo ni ya muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya uchumi na Taifa imeendelea kutenga na kulipa madeni ya wazabuni na

wakandarasi yaliyohakikiwa na kukubaliwa. Aidha, Serikali imeongeza bajeti ya madeni kutoka wastani wa shilingi bilioni 400 hadi wastani wa shilingi bilioni 700 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi Desemba 2023 jumla ya madeni ya wazabuni na wakandarasi yaliyowasilishwa kwa uhakiki yalikuwa shilingi bilioni 3,110.33. Kati ya kiasi hicho madeni yaliyolipwa ni shilingi bilioni 2,128.54, ambapo shilingi bilioni 1,032.13 ni madeni ya wazabuni na shillingi bilioni 1,096.41 ni madeni ya wakandarasi. Madeni ya shilingi bilioni 981.79 yalikataliwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kukosekana kwa nyaraka, madeni kubainika kulipwa tayari pamoja na makosa ya ukokotoaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri bilioni elfu ndiyo trilioni?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ni trilioni tatu.

**SPIKA:** Ahaa, haya ahsante sana. Haya mwenye swali naona ameridhika, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ucheleweshaji wa madeni ya wakandarasi nchini hususani barabara ya Garbabi – Mbulu na barabara zingine nchini; na gharama hii kubwa inasababisha nchi kulipa madeni makubwa baadaye.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kulipa wakandarasi kwa wakati akiwemo yule wa Mbulu – Garbabi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mkakati ambao Serikali imefanya ni kuongeza fedha zinazokwenda kwa ajili

ya kulipa *certificate* ambazo zinaiva katika mwezi husika. Kwa sasa sisi, Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya *TARURA* ambazo zinasimamia masuala ya barabara tumeongeza kiwango tunachotenga katika kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwa upande wa barabara zinazosimamiwa na *TANROADS* tumeongeza kutoka takribani bilioni 52 kwa mwezi hadi bilioni 70 kwa mwezi ili kuweza kulipa kwa wakati wakandarasi ambao *certificate* zao zinaiva.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni ipi kauli ya Serikali kwa benki ambazo yamekuwa zinafilisi wazabuni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali ni kwamba benki wasiende haraka kwenye njia hiyo ya kuwafilisi wazabuni kwa sababu Mheshimiwa Rais tayari ameelekeza kila tunapotenga fedha asilimia kubwa ya fedha iende kwa wazabuni wa ndani, ambao wengi wao ndio wanaokopa kwenye benki hizi za ndani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Ubadilishaji wa fedha kati ya Tanzania, Zambia, Malawi na Msumbiji**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kurasimisha na kurahisisha ubadilishaji wa fedha za kigeni kati ya Tanzania, Zambia, Malawi na Msumbiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu imeendelea kurahisha taratibu za usajili wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni nchini ili wananchi wenye uwezo waweze kufungua na kuendesha maduka hayo katika sehemu mbalimbali, ikiwemo sehemu za mipakani. Hadi Desemba 2023, huduma za kubadilisha fedha katika mipaka ya Tunduma, Mtwara, Mtukula na Namanga zinapatikana katika matawi 25 ya benki na maduka mawili (2) ya kubadilisha fedha.

Mheshimiwa Spika, wananchi na wafanyabiashara katika mipaka ya Tanzania na nchi jirani ikiwemo Zambia, Malawi na Msumbiji wanashauriwa kutumia taasisi rasmi za fedha, yaani benki za biashara pamoja na maduka ya kubadilisha fedha ili kurahisisha miamala ya kibiashara za kigeni. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na jumuiya za kikanda, ikiwemo *EAC* pamoja na *SADC* zimetengeneza mifumo ya malipo ili kurahisha malipo baina ya nchi wanachama kwa lengo la kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika biashara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba ukienda kwenye maduka ya kubadilisha fedha za kigeni mara nyingi utakuta sarafu ambazo zimeandikwa ni za baadhi ya nchi kama *Ugandan*

*shilling, Kenyan shilling,* lakini sina uhakika kama ukienda kwenye zile mbao za kubadilisha fedha utakuta kwamba imeandikwa *exchange* kati ya pesa ya *Malawi Kwacha, Zambian Kwacha* na nchi kama *Mozambique*. Je, kutokana na hali ilivyo ya ukosefu wa dola na jinsi *pressure* ilivyo kwa sasa hivi, Serikali zetu hazioni kwamba ni wakati muafaka ma-*governor* wa nchi hizi hasa ambazo tunapakana wakakaa ili waje na utaratibu ambao tutaweza kutumia sarafu za kwetu kupunguza *pressure* ya hizo dola?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge makini kabisa wa Kalambo ni la msingi. Tutawaelekeza ma-*governor* wakae waendelee kuangalia hizi njia mbadala ambazo zinaweza zikafanyika, hasa katika nchi zinazofanya biashara mpakani ili kuweza kurahisisha biashara na kupunguza tatizo la uhitaji wa dola.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile Mbunge wa Kigamboni sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Kuendeleza eneo la viwanda Pembamnazi – Kigamboni**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza eneo la ekari 1,000 lililotengwa kwa matumizi ya viwanda Kata ya Pembamnazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Jerry William Silaa, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, eneo la Pembamnazi lipo Manispaa ya Kigamboni na lina ukubwa wa ekari 1,000. Eneo hilo limetengwa kama hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali inaendelea kutafuta wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwekeza katika eneo hilo. Hivyo, wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika maeneo hayo wawasilishe maombi yao Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam au kwenye mamlaka za uwekezaji wakiainisha kiasi cha ardhi wanachoomba na uwekezaji tarajiwa. Aidha, Wizara iko tayari kupokea ushauri Mheshimiwa Mbunge kuhusu uwekezaji katika eneo hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali lingine la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, eneo hili lilipimwa zaidi ya miaka mitano iliyopita na mahitaji ya ardhi kwa uwekezaji katika Wilaya ya Kigamboni ni kubwa sana.

Je, ni ipi mikakati ya Serikali ya kulitangaza eneo hili kwa ajili ya uwekezaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika jitihada zake anazofanya katika kukuza uwekezaji na tumeanza kupata maombi ya uwekezaji katika eneo hili. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge na yeye kwa kutumia *influence* yake na Bunge lako Tukufu kuendelea

kuwatangazia wawekezaji wote wenye nia ya kujenga viwanda kuweza kuwasilisha maombi yao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni ipi kauli ya Wizara ya Ardhi kuwasaidia wananchi ambao maeneo yote yaliyokuwa yametengwa ya kutumika ya umma yakaporwa na watu ambao wanajiita ni wawekezaji; kwa mfano, Kijiji cha Msungwe, ata ya Kapele yuko mwekezaji ambaye amepora ardhi ya kijiji yenye zaidi ya ekari 1000; ni upi msaada kutoka kwenye Wizara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, maeneo ya ardhi za vijiji kikiwemo Kijiji cha Msungwe kwenye Jimbo la Momba yanaongozwa na Sheria Na. 5 ya Ardhi ya mwaka 1999 ambayo inatoa mamlaka ya wananchi kusimamia ardhi yao na kutoa kiasi cha ardhi kinachogaiwa kwenye kila ngazi kutoka kijiji, wilaya na mpaka Kamati ya Uwekezaji ya Taifa. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge awasilishe malalamiko ya wananchi wao na tutaishughulikia na tutatoa majibu na haki ya wananchi itapatikana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge wa Kilosa swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dennis Londo.

Na. 14

**Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi – Kilosa**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi wa Jimbo la Kilosa kutokana na uwepo wa migogoro ya muda mrefu ya Wakulima na Wafugaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Wilaya ya Kilosa umeandaliwa mwaka 2008 na utamaliza muda wake mwaka 2028. Mpango huu ndio mwongozo wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vya wilaya.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Desemba, 2023 jumla ya vijiji 58 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya ya Kilosa kati ya vijiji 138 vilivyopo sawa na asilimia 42, ambapo kati ya vijiji hivyo, vijiji 23 vipo katika Jimbo la Kilosa na vijiji 35 vipo katika Jimbo la Mikumi. Wizara kupitia Tume itaendelea kuziwezesha mamlaka za upangaji katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji mbalimbali nchini vikiwemo vijiji 10 vya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Natoa rai kwa halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga fedha katika bajeti zake kila mwaka kwa ajili ya uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza Serikali kwamba, miji midogo ambayo inachipukia kwa kasi kama Dumila ambao una wakazi zaidi ya 47,000;

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kwenda kupima, kupanga na kumilikisha maeneo hayo?

(b) Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuungana nasi baada ya Bunge kuja Wilaya ya Kilosa, kwa maana ya Jimbo la Kilosa na

Mikumi, kwa ajili ya kuangalia migogoro ya ardhi ambayo inapelekea migogoro ya wakulima na wafugaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaelekeza maeneo yote siyo tu yanayokua kimiji kupangwa na kupimwa ili kuyatengenezea matumizi bora ya ardhi. Niungane mkono na Mheshimiwa Mbunge kwamba mji mdogo alioutaja unapaswa kufanyiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Nimuombe tushirikiane katika kuangalia kama halmashauri yake imetenga fedha na pale Wizarani kama tuna uwezo kupitia Mradi wa KKK tuweze kufanya jambo hilo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, swali la pili baada tu ya Bunge hili la mwezi Februari ninayo ziara ya Jimbo la Kilombero kwa Mheshimiwa Asenga, uko mgogoro kule wa Baba Askofu, nikifanya ziara hiyo namuomba Mheshimiwa Mbunge mara baada ya kikao hiki tukutane tupange ratiba; tutapita na Wilaya ya Kilosa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kuna mgogoro mkubwa sana kati ya wakulima na wafugaji Mkoa wa Lindi kwenye Wilaya ya Liwale, Kilwa, Nachingwea na Mchinga unaopelekea kuuana na mashamba ya watu kuliwa na mifugo.

Je, Serikali ina mpango gani kabambe kutokomeza suala hili ili wananchi waishi kwa amani?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna tatizo kubwa la migogoro baina ya

wakulima na wafugaji na katika Wilaya alizozitaja Mheshimiwa Mbunge za Liwale na Nachingwea Mkoani Lindi tatizo hili ni kubwa. Vilevile, lilijitokeza kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujipanga kupitia Wizara husika kwa maana Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo na Wizara ya TAMISEMI na itakuja na mpango kabambe wa kuhakikisha kadhia hii inaisha na wakulima na wafugaji wanaendelea kufanya shughuli zao katika matumizi bora ya ardhi bila ya kuingiliwa na kuleta machafuko na kuvunja amani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro kati ya Kata ya Makanya Ruvu na Makanya Bangalala ya muda mrefu. Je Serikali ina mpango gani wa kumaliza migogoro hii ya ardhi? Ahsante.

**SPIKA:** Hizo kata ziko wapi Mheshimiwa?

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Same, Jimbo la Same Magharibi.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wiki iliyopita nilipita Bangalala na Makanya na Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi Mheshimiwa David Mathayo. Tayari nimeunda timu ndogo itakwenda Bangalala na Makanya tarehe 07 ya mwezi huu na baada ya kuniletea taarifa nitafika tena kwenda kutoa majibu ya mgogoro huu ambao umekuwa ukiwasumbua wananchi kwenye mipaka yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika eneo la Himo, maeneo yale ya Lokolova na mjini ilipokuwa *estate* ya *sisal* kuna mgogoro mikubwa na ambayo pia inazuia maendeleo ya pale. Je, Waziri atakubali kuenda na mimi Jimboni baada ya Mkutano huu ili aweze kutatua migogoro hii?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mgogoro wa Lokolova pale Himo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Kimei ni mgogoro mkubwa baina ya Chama cha Ushirika na wakazi ambao wanadai kuwa ni wakazi wa asili wa eneo hilo. Mgogoro huu tayari taarifa yake imeshaandaliwa na tumeshakubaliana na Waziri wa Kilimo mara baada ya Bunge hili tutakwenda kwa pamoja kumaliza mgogoro huu uishe kabisa na usiendelee tena ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimwia Reuben Kwagilwa Nhamanilo.

Na. 15

**Kutoza kodi ya pango kwa fedha za kigeni**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO K.n.y MHE. JULIANA D. MASABURI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kusimamia sheria kikamilifu na kukomesha utaratibu wa wapangishaji nyumba kutoza pango kwa fedha za kigeni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna sheria mahsusi inayoelekeza aina ya fedha inayotakiwa kutumika katika kutoza pango kwa wapangishaji wa nyumba. Hata hivyo, Benki Kuu imekuwa ikitoa miongozo kuhusu matumizi ya fedha za kigeni nchini ambayo pamoja na mambo mengine inakataza matumizi ya fedha za kigeni kwa wakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kulipia bidhaa na huduma nchini. Mwongozo unaotumika sasa ulitolewa mwezi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utendaji wa soko la nyumba nchini, Wizara ipo katika mchakato wa kutunga Sheria ya Milki ambayo pamoja na masuala mengine itaweka utaratibu wa utozaji wa pango hususan kwa raia wa Tanzania. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa Reuben swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwenye swali hili la msingi.

Swali la kwanza, je, ukiacha hii Sheria ya Milki anayoizungumzia ni lini Serikali kwa ujumla wake kabisa italeta sheria kubwa na pana itakayo *govern* sekta ya makazi na upangishaji kwa maana ya *real estate?*

Swali la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kanzidata ya nyumba za kupangisha kwenye Majiji, Manispaa na Miji ndani ya nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi

tupo katika hatua za ndani za Serikali, kuandaa sheria itakayotoa mwongozo wa jinsi ya kuenenda kwenye soko la nyumba kwa maana ya *real estate*. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine itaunda chombo ambacho kitasimamia mawakala wote wa upangishaji na upangaji wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, swali pili Wizara inaendelea na mchakato na iko katika hatua za mwisho kabisa za kutengeneza mfumo mkubwa wa *management* ya ardhi nchini. Moja kati ya maeneo hayo unapotaja mfumo wa usimamizi wa ardhi, utataja nyumba zilizoko kwenye maeneo yetu vilevile itatoa matumizi ya nyumba ile ikiwa ni pamoja na matumizi ya ardhi ya kiwanja kile.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo huo tutazingatia ushauri wa Mbunge kwa kuweka uwezo wa kujua nyumba za upangaji ziko ngapi na kuweza kutoa miongozo na kuweza kuzisimamia ili wananchi wasiweze kupata taabu zilizopo sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na wananchi wanaoishi katika nyumba za Keko *Flats* ambao ni takriban miaka saba sasa waliambiwa kuna mwekezaji na wamekataliwa kulipa kodi hawapeleki *National Housing,* wako katika *dilemma.* Sasa sijui majibu ya Serikali yakoje, mwekezaji yupo au waendelee kukaa bila kulipa kodi, Je wakija kuwaambia waanze kulipa watadaiwa kuazia hiyo miaka saba iliyopita? Naomba majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Naona maswali yako yamekuwa mengi, uliza moja kati ya hayo.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ni upi mkakati wa Serikali kuhusiana na wananchi wanaoishi katika eneo lile la Keko *National Housing.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Kilave ni jirani yangu swali hili nitawasiliana na uongozi wa *National Housing* na nitampa majibu kwa haraka sana kwa sababu linahitaji *details* na nitampa majibu yake leo hii.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa mjibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi Mbunge wa Mahonda, sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Msimamo wa Tanzania katika Medani za Kimataifa**

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI** aliuliza:-

Je, nini maana ya *non-aligned* katika msimamo wa Tanzania Kimataifa wa kutofungamana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Mahonda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *non-aligned* ina maana ya kutofungamana ama kushikamana, kiitikadi na kimsimamo na nchi ama kundi la nchi

zenye nguvu na ushawishi mkubwa duniani. Dhana hii ilikuja mara tu baada ya kumalizika kwa Vita Kuu ya Pili ya dunia mwaka 1945, ambapo dunia ilishuhudia kuibuka kwa kambi mbili zilizokuwa zinahasimiana ambazo ni Marekani na washirika wake chini ya mwamvuli wa *NATO* na uliokuwa Umoja wa Jamhuri za Kisoshalisti za Kisovieti *(USSR)* na washirika wake chini ya mwamvuli wa *Warsaw Pact*.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, nchi ambazo ziliamini kutofungamana ama kuambatana na upande wowote zilianzisha Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote *(Non-Aligned Movement - NAM)*. Tanzania ilijiunga na umoja huu mwaka 1961 mara tu baada ya uhuru. Dhana ya kutofungamana na upande wowote ni miongoni mwa misingi ya sera yetu ya mambo ya nje.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama wa *NAM* kwa kutekeleza misingi ya kutofungamana na upande wowote katika maamuzi mbalimbali ambayo yanachukuliwa kwenye ajenda za kimataifa kwa kuzingatia uhuru na mipaka ya nchi *(sovereignty and territorial integrity),* kupinga matumizi ya nguvu za kijeshi, haki na usawa duniani na maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdullah Mwinyi swali la nyongeza.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri sina swali la nyongeza.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa John Marko Sallu Mbunge wa Handeni Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 17

**Ujenzi wa Barabara ya Segera - Manga hadi Chalinze**

**MHE. JOHN M. SALLU** aliuliza:**-**

Je, lini Serikali itaanza kupanua barabara ya kutoka Segera – Manga hadi Chalinze?

**SPIKA:** Mheshimia Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imetangaza zabuni kwa ajili ya kupata Mhandisi Mshauri wa kufanyakazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina wa barabara ya Segera - Manga - Chalinze yenye urefu wa kilomita 175 na zitafunguliwa tarehe 14 Febuari, 2024. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kukamilika Agosti, 2025. Baada ya kazi hiyo kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa barabara hiyo. Aidha, Serikali imekuwa ikipanua maeneo hatarishi kama kwenye milima na miinuko ili kupunguza ajali za barabarani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Marko Sallu swali la nyongeza.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu la Naibu Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Magole - Turiani - Mziha mpaka Handeni ni barabara ambayo inapita kweye Majimbo

manne lakini kuna kile kipande cha kutoka Mziha kwenda Handeni ni kibaya sana na magari yanakwama.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuweka kipaumbele kwenye barabara hiyo ili iweze kwenda kwenye kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo barabara ina changamoto lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Jimbo hilo na Watanzania kwamba kwenye swali lake la msingi kupanua ile barabara ni pamoja na Serikali sasa kuanza kujenga barabara mbadala ambayo moja wapo ni hiyo ya Handeni – Mziha – Turiani hadi Magole ambayo tunaamini itakuwa inapunguza msongamano kwenye hiyo barabara pamoja na barabara nyingine za Tanga – Pangani kwenda Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba katika bajeti tumepanga kuanza kujenga kilomita 30 kwa kiwango cha lami kuanzia Handeni, tayari tuko kwenye maandalizi ya kuitangaza hiyo Barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 18

## Ucheleweshaji wa malipo kwa Wakandarasi wazawa

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali inachelewesha malipo kwa wakandarasi wazawa ambao wamekamilisha miradi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha zimekuwa zikishirikiana kuhusu upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na kulipa madai na madeni ya wakandarasi. Malipo kwa wakandarasi wote nchini hufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, wakandarasi wazawa wamekuwa wakipewa kipaumbele katika malipo pindi fedha zinapotolewa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa, madeni haya yamekuwa makubwa sana ya wakandarasi na wengine wana mikopo benki ambayo inawasababisha wengine hata wafilisike. Serikali haioni umuhimu wa kutumia *either payment guarantee* au *letter of credit* kama inavyofanyika katika miradi ya *REA* kwa wakandanrasi wa maji pamoja na barabara? *(Makofi)*

Swali la pili, katika miradi mikubwa inayofadhiliwa na *World Bank* kama miradi ya *TACTIC* wakandarasi hawa ambao ni wazawa wameshindwa kupata hizo kazi ambazo zingewasaidia kupunguza machungu kwa sababu ya vigezo vikubwa. Serikali haioni sasa umuhimu wa ku-*guarantee* vile vigezo kwa wakandarasi wazawa ili wafanye kazi hizo za *World Bank?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme katika suala hili la madeni na madai ya wakandarasi limefafanuliwa na kutolewa maelezo vizuri sana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa akijibu swali la msingi Namba 11 lakini pia na maswali ya nyongeza ambayo nadhani yanaendana kabisa na swali la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri alioutoa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutauchukua kwa maana ya Wizara ya Ujenzi na wenzetu wa TAMISEMI ambao kwa sehemu kubwa ndiyo wanaotekeleza miradi hii ya *TACTIC* kama kutakuwa na uwezekano mzuri basi tutalifanyia kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha sehemu ya kwanza ya swali aliloliuliza Mheshimiwa Tarimo kwenye swali la nyongeza kuna mapendekezo ameyatoa, kwa sababu hapa kulikuwa na swali la nyongeza kuhusu wakandarasi wa ndani kufilisiwa na mabenki. Sasa kuna ushauri mzuri anautoa kwamba kwa nini Serikali isitumie huo ili hao wasifilisiwe pesa zao.

Nafikiri ni jambo ambalo ni muhimu kulifuatilia ama kama unaweza kutoa maelezo hapo ya ziada naweza kukupa nafasi ili wale wananchi au wale wakandarasi hasa wa ndani wasifilisiwe na mabenki, kwa sababu benki hazitaweza kuzuiwa kuendelea na zile dhamana ambazo wameziweka kwa sababu pengine ya kauli iliyotolewa, pengine utaratibu ukiwekwa vizuri kama anavyoshauri Mbunge mambo yataenda vizuri, Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametoa ushauri mzuri, naomba tulichukue ili tuweze kukaa pamoja na Mbunge pamoja na Wizara ya Kisekta na tumekaa na wenzetu wanaosimamia masuala ya manunuzi pamoja na Mwenyekiti wa Mabenki ili tuweze kuweka utaratibu kama ulivyoelekeza.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kuna Mkandarasi anajenga kilomita moja ya lami pale Mji wa Karumwa anaenda kwa kuasuasua takriban miezi 20 kwa kudai kwamba anaidai Serikali fedha.

Je, Waziri uko tayari kukamilisha malipo ya huyo Mkandarasi ili aweze kumalizia hiyo kilomita moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, moja ni kwamba ni kweli wakandarasi wengi ambao wanafanya kazi sasa hivi wamepunguza kasi kutokana na hali halisi kwamba hali ya mvua inayoendelea ni vigumu sana kufanya kazi hasa za barabara ikiwa ni pamoja na kuweka lami kwa sababu kitaalam inakuwa haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la malipo la huyo Mkandarasi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama tulivyosema tayari Serikali kwa maana Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha tumeanza kupokea fedha, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkandarasi huyo kama bado atakuwa hajalipwa na amesha-*raise certificate* basi atapewa kipaumbele ili aweze kukamilisha kazi mara mvua itakapokuwa imekata, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Makubaliano ya Mkataba wa SONGAS**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, makubaliano ya mkataba ujao kati ya SONGAS na Serikali yamefikia hatua gani ikiwa mkataba wa awali upo katika mwaka wa mwisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001, *TPDC* iliingia mkataba wa kuuziana gesi asilia iliyotengwa na Songas. Kiasi cha futi za ujazo bilioni 320 za gesi asilia iliyotengwa zilitengwa kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa miaka ishirini (20) kuanzia mwaka 2004 hadi mwaka 2024. Mwaka 2004, *TANESCO* iliingia mkataba wa kuuziana umeme ambapo kwa sasa kiwango kinachozalishwa ni *Megawatt* 189.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa *TPDC* na *TANESCO* wameanza majadiliano na *Songas* kuhusu mikataba hiyo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kunakuwa makubaliano ambayo yanazingatia maslahi ya pande zote mbili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Julai mwaka huu mkataba huu unatakiwa kusainiwa, nataka kujua majadiliano haya yatakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Mkataba wa Songas kwa takriban miaka 20 umekuwa una changamoto kubwa sana eneo la *shareholding structure*. Sasa, kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kwamba tuna *TEIT*, Je, serikali haioni kuna umuhimu wa ku-*list shares* zake kwenye *stock market* kwa sababu kule kuna *scrutiny* ya hali ya juu na hesabu zinawekwa wazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na lini majadiliano yatamalizika, majadiliano haya tunategemea yatamalizika ifikapo mwezi wa tatu mwishoni. Kuhusiana na suala la pili la Serikali kuweka *shares* zake kwenye *stock market,* tumezingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutafanyia kazi wakati tunaendela na majadiliano, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa vijiji 29 vilivyopo Jimbo la Ludewa vinahudumiwa na mzalishaji binafsi wa umeme na vinakabiliwa na changamoto ya bajeti kwa wazalishaji binafsi; na kwa kuwa Serikali imeshafanya kazi kubwa ya kutambua gharama za kufikisha umeme kwenye vitongoji na kuwasha umeme Mawengi na Milo: Je, nini ahadi ya Serikali kwa wananchi wale ikizingatiwa sasa tunaenda kwenye bajeti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uzalishaji wa umeme kwenye vijiji hivyo 29, nafahamu kuna changamoto ya umeme kwa sababu ya wazalishaji ni wawezeshaji binafsi, lakini Serikali kupitia *REA* tunao mpango wa kuwawezesha wazalishaji binafsi wa umeme na utaratibu upo. Vilevile, tutaendelea kushirikiana nao kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata umeme wa uhakika. Pia, tunao mkakati wa kuhakikisha wananchi hawa wanapata umeme kupitia miradi ya Serikali ambayo tunayo na tutahakikisha hilo linafanyika haraka iwezekanavyo ili wananchi waondokane na kadhia hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni sasa aulize swali lake. Mheshimiwa David Mathayo amesimama kwa niaba ya Mheshimiwa Ussi.

Na. 20

**Matokeo ya utafiti wa mafuta nchini**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, ni tafiti ngapi za mafuta zimefanyika nchini na yapi matokeo ya tafiti hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni za Kimataifa za Nishati imeendelea na tafiti za mafuta na gesi nchini kwa maeneo ya baharini na nchi kavu ambapo hadi kufikia mwezi Januari, 2024, jumla ya tafiti 84 zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, kupitia tafiti ambazo zimeshafanyika, tumeweza kugundua uwepo wa gesi asilia tu. Hata hivyo, *TPDC* inaendelea na utafutaji wa mafuta katika maeneo ambayo yana viashiria vya uwepo wa mafuta. Maeneo hayo yanajumuisha bonde la Eyasi Wembere, Ziwa Tanganyika na bonde la Kilosa-Kilombero, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID**: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza hapa. Kwanza, ningependa kujua katika maeneo haya ambayo yanafanya utafiti wa gesi na mafuta ni leseni ngapi zimetolewa kwa ajili ya uchimbaji wa gesi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, napenda kujua Serikali ina mkakati gani wa kuendelea kunadi vitalu hivi ili kupanua wigo wa uwekezaji na kuweza kuthibitisha zaidi kiasi cha rasilimali hizi ambazo tunazo nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika**,** ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kwa maeneo haya 84 ambayo tunafanya tafiti, tunazo jumla ya leseni 11 ambapo leseni nane ni za utafutaji na leseni tatu ni za uzalisahaji wa gesi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwa sasa hivi Wakala wa Udhibiti wa Mkondo wa Juu Wa Petroli *(PURA)* akishirikiana na Wizara

tunao mkakati wa kuendelea kufanya maandalizi ya kunadi zabuni za vitalu kwa ajili ya kuleta wawekezaji zaidi ili kufanya tafiti na kuthibitisha rasilimali hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali na sasa nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele. Ninalo tangazo la wageni, tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika. Ninao wageni kumi ambao nitawatangaza kama ifuatavyo:-

Kwanza ni wageni wanaotoka *Azania Bank*, kwanza ni Ndugu Esther Mang'enya ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji, ameongozana na Dkt. Rhimo Nyansaho ambaye ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara, na pia ameongozana na Ndugu Allan Msaliko ambaye ni Meneja Masoko, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Tunao viongozi wa timu ya Yanga; kwanza yupo Mhandisi Hersi Ally Said ambaye ni Rais wa Klabu ya Yanga na Jumuiya ya Vilabu Barani Afrika, ameongozana na Ndugu Ally Shaban Kamwe ambaye ni Afisa Habari wa Klabu ya Yanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao viongozi wa Klabu ya Simba. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, basi hayo makofi mmeshapiga tayari na inaonekana mmeshawajua tayari. Sawa sasa ili tuukomboe wakati nawataja wote halafu ndiyo tupige makofi. Maana sasa kwa makofi ya urefu huu tutachukua muda sana. *(Makofi)*

Yupo Imani Kajula ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu, ameongozana na Ahmed Ally ambaye ni Msemaji Mkuu, ameongozana pia na Salum Ally Kitumbika ambaye ni Katibu Tawi la Simba Dodoma; yupo pia Pendo Emmanuel Nyamwanji ambaye ni

Katibu Msaidizi Simba Dodoma. Hawa ndio viongozi wa Simba waliopo Bungeni leo. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ambaye ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hawa wageni wake ni Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu; tunaye Ndugu Anderson Mutatembwa, Naibu Katibu Mkuu; tunaye Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa; na tunaye Ndugu Mohamed Ally Ahmed, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Katiba na Sheria kutoka Taasisi ya Usuluhishi wa Migogoro Tanzania, karibuni sana.

Tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Abbas Tarimba ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Kijitonyama, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 46 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jiji la Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 24 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni Mchungaji na Kwaya ya Vine kutoka Kanisa la *New Vine Church* la Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunakumbushana tena, nikiwa nimesimama hapa tusizungumze na wale wanaozungumza na simu, hairuhusiwi kuzungumza na simu Bungeni. Kama unahitaji kuzungumza na simu, unatoka nje, na unasubiri nikiwa nimeketi, usinyanyuke nikiwa nimesimama na usizungumze nikiwa nimesimama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni rafiki yake kutoka nchini China, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Neema Lugangira kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 22 na walimu watatu wa shule ya *Bay Bridge* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika kundi hilo yupo mtoto wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Jerry Slaa, mtoto anaitwa Simba, yupo hapo, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Mtakatifu Yohana *(St. John University of Tanzania)* cha Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, nimesimama usizungumze.

Wapo wageni watatu kutoka *TAVYA (Tanzania Agricultural Visionary Youth Association)*, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi tisa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Kampasi ya Dodoma Mjini, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine sijajua yamechelewa kwa sababu gani? Kulikuwa na tangazo linalohusu michezo, lakini kwa sababu leo tuna shughuli nyingi sana hapa mbele yetu, nilitoe hilo tangazo kwa ujumla wake, lakini kwenye Taarifa Rasmi za Bunge tangazo hilo litakapokuja litaingia.

Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa tusome matokeo ya bonanza lililofanyika Jumamosi na timu zilizoshinda. Tangazo sina hapa mbele, lakini nitatangaza mshindi wa jumla halafu wale wengine nadhani wanafahamu walishinda vikombe gani. *(Makofi)*

Mshindi wa jumla katika michezo hiyo ambayo ilifanyika siku ya Jumamosi kwa udhamini mkubwa kabisa wa benki yetu ya Azania ambao tunawashukuru sana na ndiyo maana viongozi wao wako hapa leo, michezo hiyo ilifanyika vizuri na washindi wa jumla ni *Simba Sports Club*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana, nadhani tulishakubaliana ushangiliaji ni wa kupiga meza na siyo kunyanyua mikono juu. Kwa hiyo, tukumbuke yale ambayo tumekubaliana hapa ndani, siyo kupiga makofi wala kupunga mikono. *(Makofi/Kicheko)*

Haya tangazo lingine nililonalo hapa mbele ni tangazo kutoka kwa Katibu wa Wabunge Wanawake wa Chama cha Mapinduzi, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanawake wa Chama cha Mapinduzi kwamba kutakuwa na mkutano leo tarehe 30 Januari, 2024 baada ya kuahirisha kikao cha Bunge saa 7.00 mchana kwenye Ofisi za Umoja wa Wanawake Tanzania. Mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kutakuwa na kikao huko cha Wabunge wote wanawake wa Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya pili na kwa utaratibu wetu sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

Sasa ngoja nieleze utaratibu, naona Waziri anataka kujua hapo, utasoma mmoja huu ambao umesomwa na Katibu, halafu atakuja Mwenyekiti wa Kamati kusoma maoni ya Bunge kuhusu jambo hilo, halafu utakuja Muswada wa pili utanyanyuka tena kuja kusoma, atakuja Mwenyekiti wa Kamati na baadaye Muswada wa tatu utasoma halafu atakuja Mwenyekiti wa Kamati. Ndiyo utaratibu tutakaoutumia.

Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama aje awasilishe Muswada huo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima na taadhima kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, sasa niwasilishe maelezo ya Serikali Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Muswada huu uliosomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 10 Novemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kusoma Muswada huu, Mheshimwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan anaenda kuvunja rekodi nyingine kubwa katika kujenga masuala ya demokrasia ndani ya mfumo wa vyama vingi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwako kwa kunipa fursa ya kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Uchaguzi kwa ajili ya kuendeleza masuala yanayojitokeza katika Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza kipekee sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri na shupavu sana kwa nchi yetu katika nyanja zote. Hakika Mheshimiwa Rais ni kiongozi mzalendo, mchapakazi na anapenda nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi kubwa anazofanya za kuboresha demokrasia na mazingira ya kufanya siasa nchini chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa na hivyo kuwaletea Watanzania maendeleo makubwa ya kijamii na kiuchumi. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza demokrasia na kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na

kisiasa ilianza kuwekwa wazi mapema tarehe 22 Aprili, 2021 pale alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliahidi kudumisha Tunu za Taifa letu yaani Amani, Umoja na Mshikamano. Hata hivyo, alisisitiza zaidi nia yake ya kulinda misingi ya demokrasia na uhuru wa watu kwa kusema yafuatayo; ninaomba nimnukuu, "Uhuru na Demokrasia ni Msingi wa Amani katika Nchi na pia husaidia kuchochea maendeleo ya Kisiasa na Kiuchumi", mwisho wa kunukuu. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 01 Julai, 2022 Tanzania iliadhimisha miaka 30 tangu kurejea kwa mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa. Mheshimiwa Rais, alisisitiza tena dhamira yake ya kukuza Demokrasia nchini kupitia Makala aliyoiandaa ambapo alisema, naomba kunukuu "Nimedhamiria kwamba, Kwenye kuenzi miaka yetu ya Demokrasia ya Vyama Vingi, Serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya Kisiasa, Kiuchumi na Katika Sheria za Uchaguzi ".

Mheshimiwa Spika, leo tunashuhudia Mheshimiwa Rais, anatembea katika maneno yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wakati huo Mheshimiwa Rais alieleza falsafa yake ya kuongoza nchi inayojengwa katika misingi ya 'R' nne ambazo kwa lugha ya tafsiri maana yake ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi mpya wa Taifa. Falsafa hiyo, inatoa dira na mwongozo wa uongozi katika nchi yetu ili kudumisha amani, mshikamano na umoja wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini matokeo yake ni pamoja na kuundwa kwa Kikosi Kazi ambacho kilifanyia kazi masuala yanayohusu Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini kilichokuja na mapendekezo ya kuboresha

mfumo wa demokrasia ambapo matunda ya dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake imeanza kutekelezwa kwa vitendo. Hatuna budi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kifupi tumeshuhudia Serikali ya Awamu ya Sita ikifanya mageuzi makubwa katika kuimarisha Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini, kwa uchache sana ikiwa ni pamoja na; Mmemuona Mheshimiwa Rais, kwa dhamira ya dhati akiitisha mazungumzo na viongozi wa Kitaifa wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini mbalimbali, Viongozi wa Serikali wastaafu akiwa na lengo la kubadilishana nao mawazo kuhusu namna bora ya kuboresha na kudumisha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini, Pamoja na kudumisha mahusiano ya Kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, vilevile alianzisha mazungumzo baina ya Serikali, Chama Tawala (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa lengo la kufikia maridhiano ya pamoja na kuchukua hatua kadhaa za kuchajihisha maridhiano hayo na Chama cha Demokrasia na Maendeleo katika masuala muhimu na ya kimsingi yaliyowasilishwa Serikalini na chama hicho.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia Viongozi wa chama hicho ambao walikuwa katika kesi na wengine kufungwa kama wafungwa wa kisiasa wakiachiliwa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rais, ameweza kuruhusu kuanza kufanyika kwa mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa Nchini, lakini vilevile utungwaji wa Kanuni za kusimamia mikutano hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia kupitia Baraza la Vyama vya Siasa, amefanikisha kuliwezesha Baraza la Vyama vya Siasa Nchini kuwa na kifungu maalum cha bajeti ya kuendesha shughuli za Kidemokrasia katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa

na vilevile kufanikisha mikutano mikubwa mitatu (3) ya wadau wa Demokrasia ili kujadili mustakabali wa demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa katika Nchi yetu ya Tanzania. Kwa kweli Mheshimiwa Rais anahitaji apewe maua ya dhati kwa hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunashuhudia kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza mapendekezo ya Kikosi Kazi, mapendekezo ya Baraza la Vyama vya Siasa Nchini na Wadau wa Demokrasia kuhakikisha Sheria zinazosimamia Uchaguzi zinawasilishwa Bungeni, tena bila kupitia uwasilishaji wa Sheria kwa Hati ya Dharula ili kutoa fursa kwa Watanzania wote kutoa maoni katika Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi pamoja na nyingine zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuimarisha Utawala Bora na Mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini zinalenga kudumisha na kuboresha maslahi mapana ya Watanzania na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nawaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kuziona hatua hizi za Mheshimiwa Rais na Serikali yake ni hatua muhimu zinahitaji kupongezwa na siyo za kubezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taasisi mbalimbali duniani kwa kutambua mchango huu mkubwa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kukuza demokrasia nchini, zimemtunuku tuzo mbalimbali za heshima ikiwa ni pamoja na Tuzo ya Heshima kwa kutambua mchango wake katika kutetea, kulinda na kuimarisha haki za binadamu katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa iliyotolewa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu 2023.

Mheshimiwa Spika, tuzo hizi mbili zilizotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Watetezi wa Amani ambazo nazo ni Tuzo ya Amani Duniani ya 2022 na tuzo nyingine ni ya Rais wa Dhahabu. Nitarudia hapo, ni Tuzo ya Rais wa Dhahabu ya Malengo ya Maendeleo

endelevu ambayo ameweka rekodi ya kuwa Rais mwanamke wa kwanza kuipata tuzo hiyo Barani Afrika. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na kazi kubwa aliyoifanya, Tarehe 07 Disemba, 2021 alitambulika tena kimataifa na jarida maarufu na kubwa duniani la Forbes kuwa ni kati ya wanawake 100 wenye mvuto wa uongozi na ushawishi mkubwa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwa na mvuto na ushawishi huo kama hujakuza Demokrasia na kusimamia Utawala Bora. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, ninaomba sasa pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar kwa juhudi kubwa anazofanya katika kuleta maendeleo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninaomba kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yake katika kuhakikisha Serikali inafanikisha mchakato wa utunzi wa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, namshukuru Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na vilevile, kwa dhati kabisa ya moyo wangu, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu katika msaada wake wa kufanikisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi na shukrani za dhati ninaziwasilisha pia kwa Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la

Wawakilishi) pamoja na Ofisi yake kwa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha mchakato wa Muswada huu. Kwa dhati, napenda kuchukua nafasi hii adhimu, mbele ya Bunge lako Tukufu, kukupongeza wewe binafsi. Kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Mabunge Duniani, umeupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umechukua nafasi ya Rais wa kwanza mwanamke kutoka katika Bara la Afrika kushika wadhifa huo. Hii ni fahari na heshima kubwa kwa nchi yetu kwani inaonesha ukuaji wa Diplomasia na ni kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi Duniani wanayo juu ya nchi yetu na hasa wewe mwenyewe binafsi. Kwa dhati, ninakupongeza sana na ninakushukuru kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu tukufu. Umeonyesha umahiri na ubobezi wa hali ya juu. Wanawake na wasichana wengi, watajifunza kutokana na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Viongozi wote wa Bunge unaosaidiana nao katika kutumikia majukumu yako. Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake mbobezi Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia kaatika kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa, nzuri, ya kuchambua Muswada huu kwa makini, kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta majedwali ya marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Kamati hii kwa kazi kubwa ya kihistoria, tuipe maua yao. Kwa umuhimu huu mkubwa nimshukuru sana pacha wangu na mshauri wangu dhati, tena wa karibu sana, Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri

Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dada huyu ni mchapakazi, Hodari, mwenye mapenzi ya dhati na ana mchango mkubwa sana katika kuhakikisha Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza majukumu yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa ushirikiano mkubwa na uchapakazi walionao na hasa kutuwezesha kufikisha hatua hii ya Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Msajili wa Vyama vya Siasa, Naibu Msajili na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi na watumishi wao wote, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kushauri namna ya Miswada hii inavyoweza kiakisi Demokrasia ya Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa nchini. Ninanitoa shukrani za dhati kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake, vilevile Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar na Tume ya ya Uchaguzi Zanzibar kwa kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa kwa dhati, ninakishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani. Aidha, ninawashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuendelea kuniamini, kunipa ushirikiano na kukiamini Chama cha Mapinduzi na kuendelea kumuunga mkono Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika juhudi anazozifanya za mageuzi makubwa katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa Mwaka 2023 kwa lengo la kuweka masharti ya usimamizi wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa ujumla. Sheria inayopendekezwa kutungwa inakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa

ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Hatua hii inatokana na ukweli kwamba masharti ya Sheria hizo yanafanana na tofauti kubwa pekee ikiwa kwamba moja huweka masharti kuhusu uchaguzi wa Rais na Wabunge na nyingine huweka masharti kuhusu uchaguzi wa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kutungwa kwa Sheria inayopendekezwa ambayo itaunganisha masharti yote katika Sheria moja kutarahisisha usimamizi na utekelezaji wa masharti hayo ikizingatiwa kuwa Sheria hizo mbili zinatekelezwa na Mamlaka moja ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sura Kumi. Sura ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Sheria inayopendekezwa, mawanda ya matumizi, utaratibu wa kuanza kutumika, tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inaweka Mamlaka ya Tume kuandaa Kanuni, Maelekezo na Notisi, kubainisha maeneo ya uchaguzi, uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi, maafisa waandikishaji na waratibu wa uchaguzi. Aidha, Serikali inapendekeza Ibara ya 6 inayohusu uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi ifanyiwe marekebisho kwa kuruhusu Tume kuteua Mtumishi wa Umma Mwadamizi yeyote kuwa msimamizi wa uchaguzi kama inavyobainishwa katika Aya 'A' ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, sura ya pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu uandikishaji wa wapiga kura. Sura hii imegawanyika katika Sehemu Nne ambapo Sehemu ya Kwanza inaainisha sifa za mtu kuandikishwa au kukosa sifa za mtu kuandikishwa au kukosa sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, sehemu ya kupigia kura na masharti kuhusu Daftari la Awali na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Miongoni mwa sifa muhimu za kuandikishwa kuwa mpiga kura

zilizoainishwa katika Sehemu hii ni kuwa raia wa Tanzania na kutimiza umri wa miaka kumi na nane.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, inaweka masharti ya uandikishaji ambayo yanajumuisha muda wa uandikishaji, wakala wa uandikishaji, kadi ya mpiga kura, kubadili makazi, namna ya kupata kadi mpya endapo kadi ya awali imepotea ama imefutika au imeharibika na utaratibu wa uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura unaopendekezwa ufanyike mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na Uchaguzi Mkuu unaofuata.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inapendekeza Ibara ya 12, 20 na 21 zifanyiwe marekebisho kwa kuongeza hali ya ulemavu kuwa ni miongoni mwa taarifa zitakazokuwa kwenye Daftari la Kudumu la Mpiga Kura na kuondoa adha ya marekebisho ya taarifa na adha ya kupewa kadi mpya ya mpiga kura kama inavyobainishwa katika aya ‘B’, ‘C’ na ‘D’ ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inapendekeza Ibara ya 23 ifanyiwe marekebisho kwa kuweka muda kwa Afisa Mwandikishaji kutoa uamuzi wa maombi ya mapitio kuwa ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea maombi husika kama inavyobainishwa katika aya ‘E’ ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Sura hii inaainisha masharti kuhusu utaratibu wa kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa au dhidi ya jina la mtu kuendelea kubaki katika Daftari. Kwa mujibu wa Sehemu hii, pingamizi dhidi ya uandikishwaji litawasilishwa kwa Afisa Mwandikishaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inapendekeza Ibara ya 26, 27, 28 na 29 zifanyiwe marekebisho kumuondoa Mkurugenzi wa Uchaguzi au Afisa Mwandikishaji kuwa miongoni mwa waweka pingamizi pamoja na kufuta Mahakama ya Wilaya na kuweka Mahakama ya Mwanzo kama inavyobainishwa katika aya ‘F’, ‘G’, ‘H’ na ‘I’ ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne, inajumuisha masharti kuhusu rufaa dhidi ya pingamizi la kuongezwa au kufutwa katika daftari ambapo kwa mujibu wa Sehemu hii, rufaa dhidi ya uamuzi wa Afisa Mwandikishaji zitawasilishwa katika Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sura ya tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu uchaguzi wa Rais na imegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inajumuisha masharti ya uteuzi wa wagombea wa Kiti cha Rais, Makamu wa Rais, idadi ya wadhamini wanaopaswa kuwa nao na utaratibu wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za uteuzi. Sehemu hii pia inaweka utaratibu wa namna ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea wa Kiti cha Urais na Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Sura hii inaweka masharti mbalimbali yanayohusiana na taratibu za uchaguzi wa u-Rais ikijumuisha siku ya uchaguzi wa Rais, watu wanaostahili kupiga kura katika uchaguzi wa Rais, sifa za mgombea katika uchaguzi wa Rais, majumuisho ya kura katika uchaguzi wa Rais, mazingira yanayoweza kusababisha upigaji kura kurudiwa na masharti ya kutambulika kwa uchaguzi wa Rais kuwa uchaguzi wa Makamu wa Rais. Ili kuepuka kurudia masharti kuhusu taratibu za kupiga kura ambazo hufanana kwa uchaguzi wa mgombea wa kiti cha urais, ubunge na udiwani, Sehemu hii inaweka sharti la matumizi ya Sura ya Sita inayoainisha utaratibu huo. Aidha, Serikali inapendekeza Ibara ya 30 ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno Mahakama ya Wilaya na kuweka Mahakama ya Mwanzo kama ilivyoainishwa katika aya ya 'J' ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Nne ya Muswada inaweka masharti yanayosimamia uchaguzi wa Wabunge na imegawanyika katika Sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu sifa za mgombea katika uchaguzi wa ubunge. Sehemu ya Pili inahusu uteuzi wa wagombea ubunge ambapo inaainisha siku ya uteuzi wa wagombea, utaratibu wa namna ya kuweka dhamana kwa mgombea wa nafasi ya ubunge, masharti ya mgombea kuteuliwa katika jimbo moja tu,

pingamizi na uamuzi juu ya uhalali wa fomu ya uteuzi; na inaainisha pia utaratibu wa kufutwa endapo kuna mgombea mmoja tu halali wa nafasi ya ubunge na endapo hakuna mgombea mwingine. Kwa mujibu wa Sehemu hii, endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya ubunge ameteuliwa, Mbunge huyo atapaswa kupigiwa kura na atatangazwa kuwa amechaguliwa endapo atapata kura nyingi za ndiyo katika kura zote halali zilizopigwa.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Tano ya Muswada inahusu masharti ya uchaguzi wa Madiwani. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu, ambapo Sehemu ya Kwanza inabainisha masharti ya uendeshaji wa uchaguzi wa Madiwani, muda wa kuwa madarakani kwa Madiwani, namna na wakati wa kuitisha uchaguzi mdogo katika kata. Aidha, Serikali inapendekeza ibara ya 57 ifanyiwe marekebisho kwa kuipa Tume mamlaka kutangaza nafasi iliyo wazi ya udiwani baada ya kupata taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa katika aya ya ‘L’ ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu sifa za mgombea na mazingira ya mtu kukosa sifa ya kuteuliwa katika uchaguzi. Sehemu ya Tatu inajumuisha masharti kuhusu siku ya uteuzi, uteuzi wa mgombea, dhamana za mgombea, utaratibu wa kuweka pingamizi na utaratibu unaopaswa kufuatwa ikiwa kuna mgombea mmoja tu wa nafasi ya udiwani au ikiwa hakuna mgombea.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Sita ya Muswada inaweka masharti kuhusu uchaguzi, utaratibu wa kupiga kura na uteuzi wa Wabunge na Madiwani wanawake wa viti maalum. Sehemu hii imegawanyika katika sehemu sita, ambapo Sehemu ya Kwanza inaweka masharti mbalimbali kuhusu siku ya uchaguzi na tangazo la uchaguzi. Kwa mujibu wa masharti hayo, taarifa ambazo zitakuwa katika tangazo la uchaguzi ni pamoja na siku na muda wa kuanza na kufunga upigaji kura, na anwani ya vituo vya kupigia kura, wapiga kura waliopangwa kwa kila kituo cha kupigia kura na taarifa za

wagombea walioteuliwa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi. Sehemu hii pia ambayo ina Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu mgombea kujitoa na utaratibu unaopaswa kufuatwa endapo mgombea atafariki au hakuna mgombea.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu inaweka masharti kuhusu kampeni za uchaguzi na namna kampeni zinavyopaswa kuendeshwa, ikiwa ni pamoja na masharti kuhusu kuwasilisha ratiba ya mikutano kwa msimamizi wa uchaguzi kwa lengo la kuepuka migongano ya mikutano. Sehemu hii inaweka pia masharti kuhusu upatikanaji na wajibu wa vyombo vya habari vya umma na matakwa ya kutokuwa na upendeleo na kuepuka ubaguzi kwa mgombea yeyote katika utoaji wa matangazo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Sura hii inaainisha utaratibu wa uchaguzi unaojumuisha masharti kuhusu siku na muda wa kupiga kura, mawakala wa upigaji kura, masanduku ya kura, muundo wa karatasi za kupiga kura na tangazo la kura kuwekwa wazi. Aidha, Serikali inapendekeza Ibara ya 79 ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza sharti la karatasi ya kura kuwa katika muundo unaowezesha matumizi ya watu wenye mahitaji maalum kama ilivyobainishwa katika aya ya 'M' ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kupiga na kuhesabu kura. Masharti hayo yanajumuisha watu wanaostahili kupiga kura, mazingira yanayoweza kumfanya mtu kupoteza sifa za kupiga kura, utaratibu wa kupiga kura, watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura, mazingira yanayoweza kusababisha kuahirishwa kwa upigaji kura inapotokea vurugu, kufungwa kwa zoezi la kupiga kura na utaratibu wa kuhesabu kura. Kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii mawakala wa upigaji kura wanatambuliwa kuwa mawakala wa kuhesabu kura. Aidha, Serikali inapendekeza ibara ya 88 ifanyiwe marekebisho kwa kubainisha mazingira mengine yanayoweza kusababisha Tume kuahirisha kwa upigaji kura kama inavyobainishwa katika aya ya 'O' ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, vilevile Sehemu hii inaainisha wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura, utaratibu wa kujumuisha kura katika uchaguzi wa Wabunge na Madiwani na utaratibu wa kutangaza matokeo ya ubunge na udiwani. Sehemu ya Sita ya Sura hii inaweka masharti kuhusu uteuzi wa Wabunge na Madiwani wanawake wa viti maalum na utambuaji wa utaratibu ulioainishwa katika Katiba na Sheria za Serikali za Mitaa kuhusu Wabunge na Madiwani Wanawake Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Saba ya Muswada inaweka masharti kuhusu makosa mbalimbali yanayoweza kutendwa wakati wa uandikishaji, uteuzi wa wagombea na uchaguzi. Miongoni mwa makosa hayo ni pamoja na kutumia wadhifa kushawishi watu wengine kutoomba kuteuliwa, mwenendo usiofaa wa watendaji wa uchaguzi na maafisa waandikishaji, makosa yanayohusu fomu za uteuzi au karatasi za kura, vitendo vya ushawishi na rushwa, kutotunza siri katika uchaguzi kwa watu wanaoruhusiwa kuwa katika kituo cha kupiga kura au kuhesabu kura. Sambamba na kuainisha makosa mbalimbali, sehemu hii inaweka pia adhabu kwa mtu atakayetenda makosa hayo. Aidha, Serikali inapendekeza ibara ya 114, 115, 122, 123 na 132 zifanyiwe marekebisho kwa kuweka ukomo wa chini wa adhabu kama ilivyoainishwa katika aya ya Q, R, S, T, U na V za Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Nane ya Muswada inaweka masharti kuhusu kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya shauri la uchaguzi. Kwa mujibu wa Sura hii, mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya ubunge yatasikilizwa katika Mahakama Kuu na mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya udiwani yatasikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi. Miongoni mwa taratibu zilizoainishwa katika Sura hii ambazo mtu anayefungua shauri atapaswa kuzingatia ni utaratibu wa kuweka dhamana kama ulivyoainishwa katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, vilevile, sehemu hii inaweka pia masharti ya mamlaka ya Jaji Mkuu kutengeneza kanuni zitakazosimamia

usikilizwaji wa mashauri ya kupinga matokeo ya uchaguzi. Inapendekezwa kanuni hizo zitengenezwe kwa kushauriana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Tisa ya Muswada inahusu masharti ya jumla ambapo yanajumuisha mamlaka ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi kupata taarifa, malipo ya watendaji wa uchaguzi, mamlaka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria na matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Kumi ya Muswada inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na kufutwa kwa Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa inayoshughulika na Madiwani ya mwaka 1979 na kuweka utaratibu kwa masharti yatakayoendelea kutumika hata baada ya kufutwa kwa sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako tukufu lijadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kuwa sehemu ya sheria za nchi hii. *Bunge lako liendelee kuthamini mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais katika ukuzaji wa demokrasia na hasa katika mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MAELEZO YA MHESHIMIWA JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU) AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha

maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

**2. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tatu (13) wa Bunge la Kumi na Mbili (12), tarehe 10 Novemba, 2023.

**3. Mheshimiwa Spika,** naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa ya kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu.

**4. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa uongozi wake mahiri na shupavu kwa nchi yetu katika nyanja zote. Hakika Mheshimiwa Rais ni Kiongozi mzalendo, mchapakazi na anapenda nchi yetu. Ninamshukuru na kumpongeza sana kwa juhudi kubwa anazofanya za kuboresha demokrasia na mazingira ya kufanya siasa nchini chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa na hivyo kuwaletea Watanzania maendeleo makubwa ya kijamii na kiuchumi.

**5. Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza Demokrasia na kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ilianza kuwekwa wazi mapema tarehe 22 Aprili 2021 alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma. Mheshimiwa Rais aliahidi kudumisha Tunu za Taifa letu yaani Amani, Umoja na Mshikamano. Hata hivyo, alisisitiza nia yake ya kulinda misingi ya Demokrasia na Uhuru wa watu kwa kusema yafuatayo "**Uhuru na Demokrasia ni Msingi wa Amani katika Nchi na**

**pia husaidia kuchochea maendeleo ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii ".** Tarehe 01 Julai, 2022 Tanzania iliadhimisha miaka 30 tangu kurejea kwa mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa. Mheshimiwa Rais, alisisitiza tena dhamira yake ya kukuza Demokrasia nchini kupitia Makala aliyoiandaa ambapo alisema "**Nimedhamiria kwamba, Kwenye kuenzi miaka yetu ya demokrasia ya Vyama Vingi, Serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya Kisiasa, Kiuchumi na Katika Sheria za Uchaguzi** ".

**6. Mheshimiwa Spika,** ni wakati huo Mheshimiwa Rais alieleza falsafa yake ya kuongoza nchi inayojengwa kwa misingi ya Falsafa ya 'R' 4 ambazo maana yake ni **Reconciliation, Resilience, Reforms and Rebuild** ikiwa na maana ya Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi mpya wa Taifa. Falsafa hiyo, inatoa dira na mwongozo wa uongozi katika nchi yetu ili kudumisha amani, mshikamano na umoja wa Kitaifa. Kutokana na dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini matokeo yake ni pamoja na kuundwa kwa Kikosi Kazi ambacho kilifanyia kazi masuala yanayohusu Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini kilichokuja na mapendekezo ya kuboresha mfumo wa demokrasia ambapo matunda ya dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake imeanza kutekelezwa kwa vitendo.

**7. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi kifupi tumeshuhudia Serikali ya Awamu ya Sita ikifanya mageuzi makubwa katika kuimarisha Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini ikiwa ni pamoja na;

i. Kukutana na kufanya mazunumzo na Viongozi wa Kitaifa wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Serikali wastaafu akiwa na lengo la kubadilishana mawazo kuhusu namna bora ya kuboresha na kudumisha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa;

ii. Kuanzisha mazungumzo baina ya Serikali, Chama Tawala (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo

(CHADEMA) kwa lengo la kufikia maridhiano pamoja na kuchukua hatua kadhaa za kushajihisha maridhiano na Chama cha Demokrasia na Maendeleo katika masuala kadhaa muhimu na ya kimsingi yaliyowasilishwa Serikalini na CHADEMA;

iii. Kuruhusu kufanyika kwa mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa Nchini;

iv. Kupitia Baraza la Vyama vya Siasa, amefanikisha na kuliwezesha Baraza la Vyama vya Siasa Nchini kuwa na kifungu maalumu cha bajeti ya kuendesha shughuli za Demokrasia na Vyama vya Siasa na vilevile kufanikisha mikutano mikubwa mitatu (3) ya wadau wa Demokrasia ili kujadili mustakabali wa demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa katika nchi letu;

v. Na leo tunashuhudia kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza mapendekezo ya Kikosi Kazi, Baraza la Vyama vya Siasa Nchini, na Wadau wa Demokrasia kuhakikisha Sheria zinazosimamia Uchaguzi zinawasilishwa Bungeni, tena bila kupitia uwasilishaji wa Sheria kwa Hati ya Dharula ya Rais. Juhudu hizi pamoja na nyingine zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha Utawala Bora na Mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini zinalenga kudumisha na kuboresha maslahi mapana ya Watanzania na Taifa zima kwa ujumla.

**8. Mheshimiwa Spika,** niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuziona hatua hizi ni za kupongezwa na siyo za kubezwa.

**9. Mheshimiwa Spika,** Taasisi mbalimbali duniani kwa kutambua mchango wake mkubwa katika kukuza demokrasia nchini, zimemtunuku tuzo mbalimbali za heshima ikiwa ni pamoja na Tuzo

ya Heshima kwa kutambua mchango wake katika kutetea, kulinda na kuimarisha haki za binadamu katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa iliyotolewa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu 2023; tuzo mbili zilizotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Watetezi na Amani ambazo ni tuzo ya amani duniani ya 2022 na tuzo ya Rais wa Dhahabu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo ameweka rekodi ya kuwa Rais mwanamke wa kwanza kuipata Barani Afrika. Kutokana na kazi kubwa aliyoifanya, tarehe 7 Disemba, 2021 alitambulika kimataifa na Jarida maarufu na kubwa duniani la Forbes kuwa ni kati ya wanawake 100 wenye uwezo wa uongozi na ushawishi mkubwa duniani.

**10. Mheshimiwa Spika,** pia, nimshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar** kwa juhudi kubwa anazofanya katika kuleta maendeleo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

**11. Mheshimiwa Spika,** vilevile, nimshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa miongozo na maelekezo yake katika kuhakikisha Serikali inafanikisha mchakato mzima wa Muswada huu. Pia, nimshukuru **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar** na **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu** katika kufanikisha Muswada huu. Pongezi na shukrani za dhati ninaziwasilisha kwa **Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar** (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) na Ofisi yake kwa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha mchakato mzima wa Muswada huu.

**12. Mheshimiwa Spika,** kwa dhati, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Mabunge Duniani (Inter Parliamentary Union) na Rais wa kwanza mwanamke kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo. Hii ni fahari

na heshima kubwa kwa nchi yetu kwani inaonesha ukuaji wa diplomasia na ni kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi Duniani wanayo juu ya nchi yetu na wewe mwenyewe. Kwa dhati, nikupongeze sna na kukushukuru kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Umeonesha umahili na ubobezi wa hali ya juu.

**13. Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**14. Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu mkubwa nimshukuru sana sana pacha wangu na mshauri wangu wa karibu **Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),** kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kwani ni mchapa kazi hodari ambaye ana mchango mkubwa sana katika kuhakikisha Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza majukumu yake ipasavyo; **Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu** waliowezesha muswada huu kufikia hatua ya leo.

**15. Mheshimiwa Spika,** nitoe shukrani zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalam wake pamoja na wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

**16. Mheshimiwa Spika,** kipekee na kwa dhati kabisa ninakishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani. Aidha, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano, kukiamini Chama cha Mapinduzi na kumuunga mkono Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika juhudi anazofanya za kuleta maendeleo nchini.

**17. Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka, 2023 kwa lengo la kuweka masharti ya usimamizi wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Kwa ujumla, Sheria inayopendekezwa kutungwa inakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Hatua hii inatokana na ukweli kwamba masharti ya Sheria hizo hufanana, tofauti kubwa pekee ikiwa kwamba moja huweka masharti kuhusu uchaguzi wa Rais na Wabunge na nyingine huweka masharti kuhusu uchaguzi wa Madiwani. Hivyo, kutungwa kwa Sheria inayopendekezwa ambayo itaunganisha masharti yote katika Sheria moja kutarahisisha usimamizi na utekelezaji wa masharti hayo ikizingatiwa kuwa Sheria hizo mbili hutekelezwa na mamlaka moja ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

**18. Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sura Kumi. Sura ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Sheria inayopendekezwa, mawanda ya matumizi, utaratibu wa kuanza kutumika, tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa, mamlaka ya Tume kuandaa Kanuni, Maelekezo na Notisi, kubainisha maeneo ya uchaguzi, uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi, maafisa waandikishaji na waratibu wa uchaguzi. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 6** inayohusu uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi ifanyiwe marekebisho kwa kuruhusu Tume kuteua mtumishi wa umma mwadamizi yeyote kuwa msimamizi wa

uchaguzi kama inavyobainishwa katika **Aya 'A'** ya Jedwali la Marekebisho.

**19. Mheshimiwa Spika,** Sura ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu uandikishaji wa wapiga kura. Sura hii imegawanyika katika Sehemu Nne ambapo Sehemu ya Kwanza inaainisha sifa za mtu kuandikishwa au kukosa sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, sehemu ya kupigia kura na masharti kuhusu Daftari la Awali na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Miongoni mwa sifa muhimu za kuandikishwa kuwa mpiga kura zilizoainishwa katika Sehemu hii ni kuwa raia wa Tanzania na kutimiza umri wa miaka kumi na nane. Sehemu ya Pili inaweka masharti ya uandikishaji ambayo yanajumuisha muda wa uandikishaji, wakala wa uandikishaji, kadi ya mpiga kura, kubadili makazi, namna ya kupata kadi mpya endapo kadi ya awali imepotea, imefutika au imeharibika na utaratibu wa uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura ambao unapendekezwa ufanyike mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na uchaguzi mkuu unaofuata. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara za 12, 20 na 21** zifanyiwe marekebisho kwa kuongeza hali ya ulemavu kuwa miongoni mwa taarifa zitakazokuwa kwenye Daftari la Kudumu la Mpiga Kura na kuondoa ada ya marekebisho ya taarifa na ada ya kupewa kadi mpya ya mpiga kura kama inavyobainishwa katika **Aya 'B', 'C' na 'D'** ya Jedwali la Marekebisho. Aidha, Serikali inapendekeza ibara ya 23 ifanyiwe marekebisho kwa kuweka muda kwa Afisa Mwandikishaji kutoa uamuzi wa maombi ya mapitio kuwa ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea maombi husika kama inavyobainishwa katika **Aya 'E'** ya Jedwali la Marekebisho.

**20. Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Sura hii inaainisha masharti kuhusu utaratibu wa kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa au dhidi ya jina la mtu kuendelea kubaki katika Daftari. Kwa mujibu wa Sehemu hii, pingamizi dhidi ya uandikishwaji litawasilishwa kwa afisa mwandikishaji. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 26, 27, 28 na 29** zifanyiwe marekebisho kwa kumuondoa Mkurugenzi wa Uchaguzi na Afisa Mwandikishaji kuwa miongoni

mwa waweka pingamizi pamoja na kufuta Mahakama ya Wilaya na kuweka Mahakama ya Mwanzo kama inavyobainishwa katika **Aya 'F', 'G', 'H' na 'I'** ya Jedwali la Marekebisho. Sehemu ya Nne inajumuisha masharti kuhusu rufaa dhidi ya pingamizi la kuongezwa au kufutwa katika daftari ambapo kwa mujibu wa Sehemu hii, rufaa dhidi ya uamuzi wa afisa mwandikishaji zitawasilishwa katika Mahakama ya Wilaya.

**21. Mheshimiwa Spika,** Sura ya Tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu uchaguzi wa Rais na imegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inajumuisha masharti ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, idadi ya wadhamini wanaopaswa kuwa nao na utaratibu wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za uteuzi. Sehemu hii pia inaweka utaratibu wa namna ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea wa kiti cha Urais na Makamu wa Rais. Sehemu ya Pili ya Sura hii inaweka masharti mbalimbali yanayohusiana na taratibu za uchaguzi wa Urais ikijumuisha siku ya uchaguzi wa Rais, watu wanaostahili kupiga kura katika uchaguzi wa Rais, sifa za mgombea katika uchaguzi wa Rais, majumuisho ya kura katika uchaguzi wa Rais, mazingira yanayoweza kusababisha upigaji kura kurudiwa na masharti ya kutambulika kwa uchaguzi wa Rais kuwa uchaguzi wa Makamu wa Rais. Ili kuepuka kurudia masharti kuhusu taratibu za upigaji kura ambazo hufanana kwa uchaguzi wa mgombea wa kiti cha urais, ubunge na udiwani, Sehemu hii inaweka sharti la matumizi ya Sura ya Sita ambayo inaainisha utaratibu huo. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 30** iifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno Mahakama ya Wilaya na kuweka Mahakama ya Mwanzo kama inavyobainishwa katika **Aya ''J'** ya Jedwali la Marekebisho.

**22. Mheshimiwa Spika,** Sura ya Nne ya Muswada inaweka masharti yanayosimamia uchaguzi wa Wabunge na imegawanyika katika Sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu sifa za mgombea katika uchaguzi wa Ubunge. Sehemu ya Pili inahusu uteuzi wa wagombea Ubunge ambapo inaainisha siku ya uteuzi, uteuzi wa wagombea, utaratibu wa namna ya kuweka dhamana kwa

mgombea wa nafasi ya ubunge, masharti ya mgombea kuteuliwa kwa jimbo moja tu, pingamizi na uamuzi juu ya uhalali wa fomu ya uteuzi na inaainisha pia utaratibu wa kufuatwa endapo kuna mgombea mmoja tu halali wa nafasi ya ubunge au endapo hakuna mgombea. Kwa mujibu wa Sehemu hii endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya Ubunge ameteuliwa, mgombea huyo atapaswa kupigiwa kura na atatangazwa kuwa amechaguliwa endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa.

**23. Mheshimiwa Spika,** Sura ya Tano ya Muswada inahusu masharti ya uchaguzi wa Madiwani. Sura hii imegawanyika katika Sehemu Tatu, ambapo Sehemu ya Kwanza inabainisha masharti ya uendeshaji wa uchaguzi wa madiwani, muda wa kuwa madarakani kwa Madiwani, namna na wakati wa kuitisha uchaguzi mdogo katika Kata. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 57** ifanyiwe marekebisho kwa kuipa Tume mamlaka kutangaza nafasi iliyo wazi ya udiwani baada ya kupata taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kama inavyobainishwa katika **Aya 'L'** ya Jedwali la Marekebisho. Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu sifa za mgombea na mazingira ya mtu kukosa sifa ya kuteuliwa katika uchaguzi. Sehemu ya Tatu inajumuisha masharti kuhusu siku ya uteuzi, uteuzi wa mgombea, dhamana za wagombea, utaratibu wa kuweka pingamizi na utaratibu unaopaswa kufuatwa ikiwa kuna mgombea mmoja tu wa nafasi ya udiwani au ikiwa hakuna mgombea.

**24. Mheshimiwa Spika,** Sura ya Sita ya Muswada inaweka masharti kuhusu uchaguzi, utaratibu wa kupiga kura na uteuzi wa wabunge na madiwani wanawake viti maalum. Sehemu hii imegawanyika katika Sehemu Sita, ambapo Sehemu ya Kwanza inaweka masharti mbalimbali kuhusu siku ya uchaguzi na tangazo la uchaguzi. Kwa mujibu wa masharti hayo, taarifa ambazo zitakuwa katika tangazo la uchaguzi ni pamoja na siku na muda wa kuanza na kufunga upigaji kura, anwani ya vituo vya kupigia kura, wapiga kura waliopangwa kwa kila kituo cha kupigia kura na taarifa za

wagombea walioteuliwa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi. Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu mgombea kujitoa na utaratibu unaopaswa kufuatwa endapo mgombea atafariki au hakuna mgombea. Sehemu ya Tatu inaweka masharti kuhusu kampeni za uchaguzi na namna kampeni zinavyopaswa kuendeshwa, ikiwa ni pamoja na masharti kuhusu kuwasilisha ratiba ya mikutano kwa msimamizi wa uchaguzi kwa lengo la kuepuka migongano ya mikutano. Sehemu hii inaweka pia masharti kuhusu upatikanaji na wajibu wa vyombo vya habari vya umma na matakwa ya kutokuwa na upendeleo na kuepuka ubaguzi kwa mgombea yeyote katika utoaji wa matangazo.

**25. Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Sura hii inaainisha utaratibu wa uchaguzi unaojumuisha masharti kuhusu siku na muda wa kupiga kura, mawakala wa upigaji kura, masanduku ya kura, muundo wa karatasi za kura na katazo la kuweka wazi kura. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 79** ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza sharti la karatasi ya kura kuwa katika muundo utakaowezesha matumizi kwa watu wenye mahitaji maalum kama inavyobainishwa katika **Aya 'M'** ya Jedwali la Marekebisho. Sehemu ya Tano inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kupiga na kuhesabu kura. Masharti hayo yanajumuisha watu wanaostahili kupiga kura, mazingira yanayoweza kumfanya mtu kupoteza sifa za kupiga kura, utaratibu wa kupiga kura, watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura, mazingira yanayoweza kusababisha kuahirishwa kwa upigaji kura inapotokea vurugu, kufungwa kwa zoezi la upigaji kura na utaratibu wa kuhesabu kura.

Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, mawakala wa upigaji kura wanatambuliwa kuwa mawakala wa kuhesabu kura. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 88** ifanyiwe marekebisho kwa kubainisha mazingira mengine yanayoweza kusababisha Tume kuahirisha kwa upigaji kura kama inavyobainishwa katika **Aya 'O'** ya Jedwali la Marekebisho. Vilevile Sehemu hii inaainisha wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura, utaratibu wa kujumuisha kura katika uchaguzi wa wabunge na madiwani na utaratibu wa kutangaza

matokeo ya ubunge na udiwani. Sehemu ya Sita ya Sura hii inaweka masharti kuhusu uteuzi wa wabunge na madiwani wanawake viti maalum na unatambua utaratibu ulioainishwa katika Katiba na Sheria za Serikali za Mitaa kuhusu wabunge na madiwani wanawake viti maalum.

**26. Mheshimiwa Spika,** Sura ya Saba ya Muswada inaweka masharti kuhusu makosa mbalimbali yanayoweza kutendwa wakati wa uandikishaji, uteuzi wa wagombea na uchaguzi. Miongoni mwa makosa hayo ni pamoja na kutumia wadhifa kushawishi watu wengine kutoomba kuteuliwa, mwenendo usiofaa wa watendaji wa uchaguzi na maafisa waandikishaji, makosa yanayohusu fomu za uteuzi au karatasi za kura, vitendo vya ushawishi na rushwa, kutotunza siri katika uchaguzi kwa watu wanaoruhusiwa kuwa katika kituo cha kupigia kura au kuhesabia kura. Sambamba na kuainisha makosa mbalimbali, Sehemu hii inaweka pia adhabu kwa mtu atakayetenda makosa hayo. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara za 114, 115, 122, 123 na 132** zifanyiwe marekebisho kwa kuweka ukomo wa chini wa adhabu kama inavyobainishwa katika **Aya 'Q', 'R', 'S'**, **'T', 'U' na 'V'** za Jedwali la Marekebisho.

**27. Mheshimiwa Spika,** Sura ya Nane ya Muswada inaweka masharti kuhusu kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya shauri la uchaguzi. Kwa mujibu wa Sura hii, mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya ubunge yatasikilizwa katika Mahakama Kuu na mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya udiwani yatasikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi. Miongoni mwa taratibu zilizoainishwa katika Sura hii ambazo mtu aliyefungua shauri atapaswa kuzingatia ni utaratibu wa kuweka dhamana ya gharama za kuendesha shauri. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 144** ifanyiwe marekebisho kwa kupunguza muda wa kuamuliwa kwa mashauri ya uchaguzi kama inavyobainishwa katika **Aya 'Y'** ya Jedwali la Marekebisho. Vilevile, Sehemu hii inaweka pia masharti ya mamlaka ya Jaji Mkuu kutengeneza kanuni zitakazosimamia usikilizwaji wa mashauri ya kupinga matokeo ya uchaguzi. Inapendekezwa kanuni hizo zitengenezwe kwa kushauriana na

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa kanuni hizo.

Sura ya Tisa ya Muswada inahusu masharti ya jumla ambayo yanajumuisha mamlaka ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi kupata taarifa, malipo ya watendaji wa uchaguzi, mamlaka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria na matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Tume.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Sura ya Kumi ya Muswada inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1979 na kuweka utaratibu kwa masharti yatakayoendelea kutumika hata baada ya kufutwa kwa Sheria hizo.

**29.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

**30.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Jenista Joakim Mhagama (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(SERA BUNGE NA URATIBU)**
**30 Januari, 2024**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Kabla sijamwita Mwenyekiti hebu msaidizi nisaidie ile hotuba ya Mheshimiwa Waziri mara moja.

Waheshimiwa Wabunge dakika chache tuvumiliane. Haya ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kutusomea kwa mara ya pili Muswada wetu.

Sasa maelezo niliyonayo hapa mbele ambayo Mheshimiwa Waziri mengine ameyasoma, kwa hiyo wakati akisoma kuna maneno ya ziada ameyaongeza. Sisi kama Bunge tutachukua taarifa hii rasmi ambayo imeletwa kwetu kwamba ndio hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo hii ndiyo itakayoingia kwenye *Hansard* na yale aliyozungumza kwa ziada hayataingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Daktari Joseph Mhagama.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tatu, Kikao cha Kumi kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 10 Novemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu

kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa msingi wa Miswada hii ni falsafa ya 4R za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambazo ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga upya Taifa.

Mheshimiwa Spika, falsafa hizi ni mkakati mahususi wa uongozi wa Rais unaolenga kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi nchini, kwa kufungua milango ya mazungumzo na wadau mbalimbali wa kisiasa, kijamii na kiuchumi, ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia na sekta binafsi. Aidha, falsafa hii inalenga kupitia upya sera na sheria zinazohusu masuala muhimu kama vile siasa, afya, elimu, uwekezaji, biashara, usalama ikiwa ni pamoja na kujenga uhusiano mzuri na nchi jirani, wadau wa maendeleo na jumuiya za kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiwasilisha miswada hii kwa kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala Katiba na Sheria, ilieleza kuwa maudhui ya Miswada yanatokana na taarifa ya kikosi kazi kilicho undwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini. Aidha, maudhui mengine yanatokana na mijadala mbalimbali kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini iliyofanyika mara kwa mara kupitia Jukwaa la Vyama vya Siasa na Kituo Cha Demokrasia Tanzania *(Tanzania Centre for Democracy -TCD)*. Kwa muktadha huo, sheria hizi zimekusudia kutoa majawabu ya baadhi ya hoja zilizo jitokeza kwenye taarifa ya kikosi kazi na kwenye mijadala mbalimbali ya siasa na demokrasia nchini kupitia jukwaa la vyama vya siasa na *TCD*.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo, miswada hii mitatu inakusudia kuleta mapinduzi ya kisheria na kimfumo katika uchaguzi ili kupanua demokrasia nchini kwa kuongeza uhuru wa Tume ya Uchaguzi, kuboresha usimamizi wa uchaguzi na kuongeza ushiriki *(inclusion*) wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye uchaguzi. Miswada hii ya Sheria inakusudia kufanya mfumo wetu wa uchaguzi kuwa jumuishi zaidi na wa wazi zaidi, haki zaidi na wenye usawa zaidi.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 5 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kupokeaji wa maoni ya wadau. Kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) na 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya mikutano ya kusikiliza maoni ya wadau *(public hearings*) kwa siku nne kuanzia tarehe 6, 8 hadi 10 Januari, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Miswada minne iliyofanyiwa kazi na Kamati hii, ambayo ni: -

(a) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023;

(b) Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023;

(c) Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 na

(d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyoendesha vikao vya upokeaji wa maoni. Kamati ilipata heshima ya kupokea watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao walijitokeza na kutenga muda wao kwa ajili ya jambo hili la maana kubwa kwa taifa letu. Kamati ilihakikisha kuwa kila sauti ilipewa nafasi ya kusikilizwa kwa dhamira ya kuhakikisha Sheria tunazokusudia kuzitunga kwa niaba ya Watanzania zinawakilisha maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kusikiliza, kujifunza na kuyachukua maoni ya wadau wote kwa uzito unaostahili, kwa lengo la kufikia maamuzi ambayo yataleta mabadiliko chanya katika Miswada iliyopo mbele yetu. Kwa muktadha huo, Kamati ilitenga muda wa dakika thelathini kwa taasisi za Kidini kutoa maoni na nasaha kuhusu Miswada, dakika ishirini kwa vyama vya siasa, dakika kumi kwa taasisi na asasi za kiraia na dakika tano kwa wachangiaji binafsi. Hata hivyo, kwa wale ambao hawakuweza kumaliza michango yao kwa muda uliopangwa, Kamati iliwasihi kuwasilisha michango yao kwa maandishi ili iweze kufanyiwa kazi na Kamati yako.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuboresha Miswada iliyofanyiwa kazi na Kamati na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania *(TEC)* – Ujumbe ulioongozwa na Mhasham Baba Askofu Jude Thaddeus Rwaichi, Askofu Mkuu wa Jimbo la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao, katika kushughulikia Muswada huu naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo - Makamu Mwenyekiti
2. Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi – Mjumbe

3. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi - Mjumbe
4. Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yanaingia kwenye *Hansard* moja kwa moja bila kusomwa.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Dkt. Jim Yonazi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*. na kipekee Sekretarieti ya Kamati Ndg. Frank Nkya, Ndg. Ganjatuni Kilemile na Ndg. Ndoh'no William Abel kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Kamati pamoja na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

# MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

#### 1.1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na tatu, kikao cha kumi kwenye Bunge la 12, tarehe 10 Novemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

#### 1.1.2 Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa msingi wa Miswada hii ni Falsafa ya 4R za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambazo ni Maridhiano (*Reconciliation*), Ustahimilivu (*Resiliency*), Mabadiliko (*Reforms*) na Kujenga upya (*Rebulding*).

**Mheshimiwa Spika**, Falsafa hizi ni mkakati mahususi wa uongozi wa Rais unaolenga kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi nchini, kwa kufungua milango ya mazungumzo na wadau mbalimbali wa kisiasa, kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia na sekta binafsi. Aidha, Falsafa hii inalenga **kupitia upya sera na sheria** zinazohusu masuala muhimu kama vile siasa, afya, elimu, uwekezaji, biashara, usalama ikiwa ni pamoja na kujenga uhusiano mzuri na nchi jirani, wadau wa maendeleo na jumuiya za kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati serikali ikiwasilisha miswada hii kwa kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala Katiba na Sheria, ilieleza kuwa **maudhui** ya Miswada yanatokana na Taarifa ya Kikosi Kazi kilicho undwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini. Aidha, maudhui mengine yametokana na mijadala mbalimbali kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini iliyofanyika mara kwa mara kupitia Jukwaa la Vyama Siasa na Kituo Cha Demokrasia Tanzania (Tanzania Centre for Democracy -TCD). Kwa muktadha huo, sheria hizi zimekusudia kutoa majawabu ya baadhi ya hoja zilizo jitokeza kwenye Taarifa ya Kikosi Kazi na kwenye Mijadala mbalimbali ya Siasa na Demokrasia nchini, kupitia jukwaa la Vyama vya Siasa na TCD.

**Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huo, miswada hii mitatu inakusudia kuleta mapinduzi (reforms) za kisheria na kimfumo katika uchaguzi ili kupanua demokrasia nchini kwa kuongeza uhuru wa Tume ya Uchaguzi, Kuboresha usimamizi wa Uchaguzi na kuongeza ushiriki (inclusion) wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye uchaguzi. Miswada hii ya Sheria imekusudia kufanya Mfumo wetu wa Uchaguzi kuwa **jumuishi zaidi** na wa **wazi zaidi, haki zaidi, na wenye usawa zaidi**.

## 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 5 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

### 1.2.1 Upokeaji wa maoni ya Wadau

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) na 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano ya kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearings*) kwa siku nne kuanzia tarehe 6, 8 hadi 10 Januari, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Miswada minne iliyofanyiwa kazi na Kamati hii, Ambayo ni: -

a) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, wabunge na Madiwani wa mwaka 2023;

b) Muswada wa Sheria wa tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023;

c) Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa Mwaka 2023 [*The Political Parties Affairs Laws* (*Amendments) Bill, 2023*]; na

d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws* (*Miscellaneous Amendments*) *Bill, 2023*].

### 1.2.2 Namna Kamati ilivyoendesha vikao vya upokeaji wa maoni (*Public hearings*)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata heshima ya kupokea watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao walijitokeza na kutenga muda wao kwa ajili ya jambo hili la maana kubwa kwa taifa letu, Kamati ilihakikisha kuwa kila sauti ilipewa nafasi yakusikilizwa kwa dhamira ya kuhakikisha Sheria tunazokusudia kuzitunga kwa niaba ya Watanzania zinawakilisha maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kusikiliza, kujifunza na kuyachukua maoni ya wadau wote kwa uzito unaostahili, kwa lengo la kufikia maamuzi ambayo yataleta mabadiliko chanya katika Miswada iliopo mbele yetu. Kwa muktadha huo, Kamati ilitenga muda wa dakika thelathini kwa taasisi za Kidini kutoa maoni na nasaha kuhusu Miswada, dakika ishirini kwa vyama vya siasa, dakika kumi kwa taasisi na asasi za kiraia na dakika tano kwa wachangiaji binafsi. Hata hivyo, kwa wale ambao hawakuweza kumaliza michango yao kwa muda uliopangwa, Kamati iliwasihi kuwasilisha michango yao kwa maandishi ili iweze kufanyiwa kazi na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuboresha Miswada iliyofanyiwa kazi na Kamati na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) - Ujumbe ulioongozwa na Mhasham Baba Askofu Jude Thaddeus Rwaichi;

2. Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) – Ujumbe ulioongozwa na Askofu Dkt. Fredrick Shoo aliyekuwa Mkuu wa Kanisa la Kilutheri Tanzania na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania;

3. Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania - Ujumbe ulioongozwa Sheikh Mussa Yusuph Kundecha;

4. Taasisi na Asasi za Kiraia 31 zilizoshiriki kwenye majadiliano na zingine zaidi ya 400 zilizowakilishwa na zilizotuma kwa maandishi maoni na mapendekezo yao; pamoja na

5. Wadau binafsi Zaidi ya 1,700 waliopata fursa ya kushiriki katika mikutano ya kupokea maoni kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 25 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023 ukiwa umegawanyika katika sura tisa. katika hatua ya kwanza ya uchambuzi, kamati ilijielekeza kubaini kama **maudhui ya miswada hii yanakidhi matakwa ya falsafa ya R4, Taarifa ya Kikosi Kazi cha Rais, na hoja mbalimbali zilizo jitokeza wakati wa mijadala mbalimbali kupitia Jukwaa la Vyama Vya Siasa na TCD**.

Sheria hii inakusudia kuweka masharti ya kusimamia Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kufuta Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka

1979 pamoja na kuweka masharti mengine kadhaa kuhusu chaguzi hizo na matokeo ya kufutwa kwa Sheria zinazohusika. Lengo ni kuunganisha Sheria za Uchaguzi ili kukusanya pamoja masharti yanayofanana kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji na usimamizi wake.

## 2.2 Upembuzi wa Maudhui ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Katika Sheria inayopendekezwa yapo mambo makuu yanayojenga maudhui ya Sheria hii. Mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Daftari la Kudumu la Wapiga Kura *(Permanent Voter Register - PVR)*

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imempa raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka kumi na minane haki ya kupiga kura katika Uchaguzi unaofanywa Tanzania na Wananchi. Masharti ya kutumia haki hii yanaongozwa na Sheria iliyotungwa na Bunge inayoweka masharti kuhusu Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni Kitabu kinachotunzia Kumbukumbu kuhusu wapiga kura. Bunge lilitunga Sheria mbili zinazoanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Sheria hizo ni: Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292. Daftari lililoanzishwa na Sheria hizo liliandaliwa mwaka 2004 na kuanza kutumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Kwa mujibu wa Sheria hizo Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linapaswa kuboreshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na Mwingine.

**Mheshimia Spika**, Sheria inayopendekezwa inaendelea kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 5(3) (a) ya Katiba. Kwa Sheria hii, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, itaendelea kuamua kuhusu sehemu, Sura au mgawanyo mwingine

katika Muundo wa Daftari. Mkurungenzi wa Uchaguzi anaendelea kuwa na wajibu wa kuweka, kutunza na kuboresha Daftari hilo kwa mujibu wa Sheria.

### 2.2.2 Mawanda ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Mawanda ya matumizi ya Sheria yanasaidia kuzingatia muktadha wa maudhui na masharti ya Sheria inayohusika. Kwa sasa, masuala ya uchaguzi yapo chini ya Sheria mbili tofauti zilizotofautina mawanda ya matumizi. Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 inatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na Sheria ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa inatumika Tanzania Bara. Sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Zanzibar kwa uchaguzi wa Rais wa Jamhuri wa Muungano na Wabunge na itatumika Tanzania Bara kwa uchaguzi Rais, Wabunge na Madiwani. Kwa msingi huo masharti ya Sheria hiyo yanahitaji kuangaliwa kwa muktadha (context) tofauti. Muktadha wa masharti yanayohusu uchaguzi wa Rais na Wabunge ni Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, lakini muktadha wa masharti ya uchaguzi wa madiwani ni Tanzania Bara.

### 2.2.3 Uandikishaji wa wapiga kura

**Mheshimiwa Spika,** Uandikishaji wa wapiga kura ni unukuzi na utunzaji wa taarifa za Mpiga kura kwa kuorodhesha taarifa hizo kwenye Kitabu cha kudumu cha Wapiga kura. Kufanya hivyo, ni jambo linalofanikisha utaratibu wa raia kutumia haki yao ya kupiga kura pamoja na kuzingatia misingi ya uchaguzi wa kidemokrasia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa, vigezo, masharti na taratibu za pingamizi kwa wapiga kura wanaoandikishwa vimebainishwa katika sheria mbili: Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Sheria inayopendekezwa imejumuisha na kufafanua mambo hayo katika Sheria moja badala ya kuwa katika Sheria mbili tofauti. Lengo la kufanya hivyo ni kuendeleza msingi wa

uchaguzi huru na wa haki ikiwemo kujenga Imani ya wapiga Kura na Vyama vya Siasa kwa utaratibu wa Usajili wa Wapiga Kura.

### 2.2.4 Mambo Mengine Muhimu

**Mheshimiwa Spika,** Mambo mengine muhimu katika Sheria inayopendekezwa yanaendelea kuwa kama ilivyo kwa sasa. Mambo hayo ni: -

(i) Utaratibu wa uteuzi wa mawakala katika mchakato wa uchaguzi;

(ii) Utaratibu na masharti ya kupiga Kura kwa aliyeandikishwa kupiga Kura;

(iii) Utaratibu, sifa na vigezo vya uteuzi wa Wabunge wa Viti Maalumu;

(iv) Uteuzi wa Maafisa, waandikishaji, Wasimamizi wa Uchaguzi, wagombea na watendaji wengine;

(v) Masharti ya kupinga uchaguzi wa Wabunge na Madiwani

(vi) Mamlaka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuandaa Kanuni' maelekezo na notisi; na

(vii) Makosa yanayotokana na ukiukwaji wa masharti ya sheria inayopendekezwa.

## 2.3 Hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wadau

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Kamati ilipokutana na Wadau hoja 58 ziliibuliwa na Wadau kama ifuatavyo: -

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **1.** | CHADEMA, TEC, CCT, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL. | | **CHADEMA:** Jina la Muswada lisomeke: Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji.<br><br>**TEC:** Sheria haijajumuisha mapendekezo na maoni ya wadau ya kuitaka Tume iwe na Mamlaka ya Kusimamia chaguzi zote ikiwemo wa serikali za mitaa.<br><br>**CCT:** Sheria haijajumuisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Sheria ijumuishe uchaguzi huo ili Tume isimamie uchaguzi huo.<br><br>TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL: Jina la Sheria liwe Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na isiminye kuwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Lengo la marekebisho haya ni Tume iweze kusimamia chaguzi zote. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **2.** | TGNP, TAMWA, ZAFELA na WILDAF | Ibara ya 3 | **TGNP:** Tafsiri za Maneno au dhana za ya Kijinsia zilizotumika hazijawekwa katika kifungu cha 3 Cha Muswada. Kuongezea baadhi ya maneno na tafsiri zake kama Jinsi, Jinsia, Usawa wa kijinsia, Rushwa ya ngono, Ubaguzi, sera jumuishi.<br><br>**WILDAF**: Sheria iongeze tafsiri za maneno Jinsi, jinsia, ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi, ulemavu na usawa. Lengo la marekebisho haya Kuepusha matumizi kinzani ya maneno hayo. |
| **3.** | CCT, ACT WAZALENDO, CHADEMA | Ibara ya 5 | CCT: Sheria iweke idadi ya ukomo wa majimbo.<br><br>ACT WAZALENDO: sheria haijasema jinsi gani majimbo yanaundwa.<br><br>CHADEMA: Kifungu cha 5 hakijaweza kuondoa changamoto ya uundwaji wa Majimbo ya uchaguzi kwa kutumia kigezo cha uwiano wa idadi ya watu *(population quota)*. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Bado hakuna fursa ya kuhoji maamuzi ya Tume kwenye mgawanyo wa Majimbo Mahakamani hata kama kuna mapungufu au kutokuridhika na mgawanyo uliofanywa na Tume.<br><br>Kwa kifungu kilivyo bado tatizo la kuundwa kwa majimbo ya uchaguzi kwa upendeleo au sababu za kisiasa kupendelea Chama kilichopo madaralani halijapata suluhisho *(Gerrymandering)*.<br><br>Bado mamlaka ya mwisho ya kuidhinisha mipaka na mgawanyo wa majimbo ya Uchaguzi yameachwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa CCM ambaye anaweza kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais. |
| **4.** | ACT WAZALENDO, CHADEMA, WILDAF, ADC, UDSOL, CHACHA | Ibara ya 6 | **ACT WAZALENDO**: Vifungu hivi Virekebishwe badala yake Tume iteue wasimamizi wa uchaguzi na sifa ziwekwe ikiwemo kutoshiriki katika mchakato wowote wa kisiasa.<br>Lengo la marekebisho haya ni Wakurugenzi wa sasa ni wanasiasa walioshindwa uchaguzi |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | WANGWE, ABDUL NONDO, YOSEFA KOMBA TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CCT, TEC, NGOME YA VIJANA ACT WAZALENDO, JUMUIYA YA VIJANA CUF, VIJANA NCCR-MAGEUZI, ZAFELA, CCM | | wakateuliwa kuwa wakurugenzi. Hivyo wakisimamia uchaguzi wataleta mgongano wa kimaslahi.<br>Kukuza uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br><br>Wakurugenzi ni wateule wa Rais.<br><br>Kifungu hiki kiandikwe upya na kusomeka:<br>6 (1) Kwa madhumuni ya uchaguzi utakaofanyika chini ya sheria hii Tume ya Uchaguzi itateua Wasimamizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata na msimamizi huyo wa uchaguzi anaweza kuwa msimamizi wa uchaguzi kwa jimbo zaidi ya moja.<br><br>Kifungu 6 (2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kuteua kwa kuzingatia nafasi aliyonayo mtu katika ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa watumishi wa umma au Mtanzania yeyote wenye sifa sawa zitakazotajwa katika kifungu cha 6(4) cha Sheria hii idadi ya wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata.<br><br>(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1)<br>na (2), Tume inaweza, pale ambapo mazingira yatahitaji na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali,<br>kuteua mtu yeyote kutoka katika ofisi ya umma au Mtanzania mwengine yeyote mwenye sifa zitakazotajwa na Sheria hii kwa jina au kwa nafasi yake kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi katika jimbo au kata yoyote.<br><br>6 (4) Msimamizi wa uchaguzi atakuwa na sifa zifuatazo;<br>1. Awe raia wa Tanzania.<br>2. Mwaminifu na mwadilifu<br>3. Uzoefu katika uchaguzi.<br>4. Asiwe mwanachama wa au kufungamana na chama chochote cha siasa.<br>5. Asiwe amewahi kushiriki mchakato wowowte wa Kisiasa<br>6. Awe na kiwango cha elimu. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | kisichopungua astashahada<br>7. Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai ikiwemo unyanyasaji wa makosa ya kijinsia,kukwepa kodi, ugaidi<br>8. Awe amekula kiapo cha kuheshimu Sheria ya Utumishi wa Umma kuhusu makatazo ya watumishi wa umma kushiriki kwenye Vyama vya siasa.<br><br>Lengo la marekebisho haya ni Wakurugenzi wa sasa ni wanasiasa walioshindwa uchaguzi wakateuliwa kuwa wakurugenzi. Hivyo wakisimamia uchaguzi wataleta mgongano wa kimaslahi.<br><br>Kukuza uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br><br>Wakurugenzi ni wateule wa Rais.<br><br>Kukuza usawa wa kijinsi na kukuza ushirikishwaji wa vijana.<br><br>Kuchochea utendaji haki.<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 6(1) kinawarudisha |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Wakurugenzi ambao ni wateule wa Rais, waliopo chini ya Waziri wa TAMISEMI kuwa wasimamizi wa uchaguzi ambapo Wasimamizi hao wanaweza kupokea maelekezo ya Rais, Waziri wa TAMISEMI na Tume ya Uchaguzi. Hakuna maelezo kwamba ni maelekezo gani yatatamalaki ikiwa maelekezo hayo yanakinzana.<br><br>Kifungu cha 6(1) na 6(2) vifutwe ili kuruhusu kifungu cha 6(3) kuwa kifungu mama (main provision) kuhusu uteuzi wa Wasimamizi wa uchaguzi.<br><br>**WILDAF**: Kifungu cha 6 kiweke utaratibu wenye misingi ya kupata uwiano sawa wa ujumuishwaji wa jinsia na makundi maalumu katika kuwapata wasimamizi na watendaji wa uchaguzi watakaoajiriwa na Tume ya Uchaguzi na sio wenye nafasi za Ukurugenzi wa Jiji, Ukurugenzi wa Manispaa, Ukurugenzi wa Mji na Ukurugenzi wa Wilaya, au watumishi wengine wa umma.<br><br>**ADC**: Wakurugenzi wasiwe wasimamizi wa |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | uchaguzi.<br><br>**DEUS KIBAMBA:** Wasimamizi wa uchaguzi wachaguliwe kwa kuzingatia jinsi, vijana na makundi maalumu.<br><br>**CHACHA WANGWE:** Wakurugenzi wasiwe wasimamizi wa uchaguzi.<br><br>**TGNP:** Kifungu hiki hakijabainisha sifa za mtu kuteuliwa kuhudumu kama msimamizi wa uchaguzi au mtendaji wa tume, pia hakijabainisha utaratibu na namna ya uteuzi na pia hakijazingatia usawa wa Jinsia.<br><br>**MAMBO J. MAMBO:** Tume iajiri wasimamizi wa uchaguzi wa wilaya.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS na CSL:** kuendana na mapendekezo ya ripoti mbalimbali za uchaguzi, ikiwemo Taarifa ya Tume ya Uchaguzi kuhusu Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, 2020. Tunapendekeza kuwa Tume kuwa na watumishi wake wa kudumu au wa muda. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CCT**: Kifungu kiboreshwe au kiondolewe, tume iajiri watendaji wake wenyewe wafanyiwe usaili wa wazi.<br><br>**TEC:** Hawakubaliani na Wakurugenzi wa Halmashauri na watumishi wa umma kusimamia uchaguzi kwa kuwa hawawajibiki kwa tume ya uchaguzi bali wanawajibika kwa Rais na Chama Tawala hivyo wanakosa sifa ya kuwa mamlaka ya uchaguzi huru na haki. Vifungu hivyo vifutwe na Tume iajiri watumishi wake wenyewe.<br><br>**CCM**: ingawa Mahakama imeruhusu wakurugenzi kuwa wasimamizi wa uchaguzi, watendaji hao sio lazima sheria iwataje wazi wazi. |
| **5.** | CCT, CHADEMA, ZAFELA, WILDAF, TLS, LHRC, TWAWEZA, | Ibara ya 7 | **CCT:** Sifa ya Maafisa Waandikishaji kutokujihusisha na siasa iongezwe.<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 7(3) kiwe kifungu mama na kifungu cha 7(1) na 7(2) vifutwe ili kuwaondoa Wakurugenzi wa Halmashauri |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL | | kuwa Maafisa Waandikishaji wa Wapiga Kura.<br><br>Kiongezwe kifungu kidogo kitakacholazimu Mratibu wa uchaguzi wa Mkoa kuapa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi na kutoa tamko la kujitoa au kutokuwa Mwanachama wa Chama cha siasa.<br><br>Kiongezwe kifungu kidogo kingine kinachoipa Tume kiteua Mratibu wa uchaguzi wa Mkoa kuliko kulazimisha kutumia Makatibu Tawala wa Mikoa.<br><br>Kuwe na kifungu kidogo kitakachotoa masharti kwa Tume kuchapisha orodha ya majina na namba zao za simu ya Waratibu wa uchaguzi wa mikoa na vituo vyao vya kazi.<br><br>**ZAFELA**: Tume iajiri wafanyakazi wake kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na sio kutumia watu wenye nafasi za ukurugenzi wa jiji, manispaa, Mji, Wilaya au watumishi wengine wa kuwa maafisa waandikishaji. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL**: Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke; Afisa mwandikishaji Mkuu wa wapiga kura wa Jimbo kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi atafanya kazi yake na watumishi chini yake waliopatikana kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br><br>Kwa ajili ya upigaji kura kwa watanzania walioko nje ya nchi, ubalozi wa Tanzania katika nchi husika utakuwa kituo cha uandikishaji wapiga kura, na kwamba Tume itateua mtu mwenye sifa kuwa afisa mwandiksihaji wa wapiga kura katika kituo hicho. |
| **6.** | TAMWA, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL | Ibara ya 8 | Kifungu 8 (4) kinaweka uwezekano wa kuwa na mwakilishi mmoja tu mwanamke katika Kamati ya uchunguzi, ili hali uteuzi wa Kamati ya Uchunguzi unaweza kuzingatia usawa wa kijinsia.<br><br>Kifungu 8 (4) kiseme wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi watakaoteliwa na Rais |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | watateuliwa kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Kifungu 8 (4) kiseme 'Kamati iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (3) itajumuisha wajumbe wafuatao kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.<br><br>**TLS LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL**: Hakuna mfumo shindanishi wa upatikaji wa waratibu wa uchaguzi.<br><br>Tume itateua maafisa wake katika ngazi zote kuwa Waratibu wa uchaguzi katika ngazi hizo wakati wa uchaguzi kwa ajili ya kuratibu taarifa, upatikanaji wa vifaa, rasilimali na masuala mengine muhimu kwa ajili ya kuendesha uchaguzi kwa ufanisi katika majimbo ya uchaguzi na kata katika mkoa husika.<br><br>Kwa ajili ya upigaji kura kwa watanzania walioko nje ya nchi, ubalozi wa Tanzania katika nchi husika utakuwa kituo cha uandikishaji wapiga kura, na kwamba Tume itateua mtu mwenye sifa kuwa afisa mwandiksihaji wa wapiga kura katika kituo |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | hicho. Kwa madhumuni ya upigaji kura kwa wafungwa walioko gerezani, gereza husika litakuwa kituo cha uandikishaji na upigaji kura. |
| **7.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, KITUO CHA TAARIFA KWA WANANCHI, na USHIRIKI TANZANIA COALITION | Ibara 9 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL**: Kuondoka neno sheria nyingine yoyote na kifungu kisomeke;<br>Mtu yeyote ambaye ni raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane na ambaye hajapoteza sifa chini ya Sheria hii, atastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa mujibu ya masharti ya Sheria hii.<br><br>**KITUO CHA TAARIFA KWA WANANCHI:** Daftari la Wapiga Kura litumike kwa chaguzi zote.<br><br>**USHIRIKI TANZANIA COALITION**: kuondoa neno "sheria nyingine yoyote". Kifungu 9 (2) kisomeke:<br><br>"Bila kujali Masharti ya Kifungu kidogo cha kwanza na kwa kuzingatia uthibitisho wa umri, mtanzania yeyote ambaye hajapoteza sifa chini ya sheria au sheria nyingine ya uchaguzi ambaye wakati au kabla ya tarehe ya |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | uchaguzi atakuwa ametimiza umri wa miaka 18, atastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya sheria hii.<br><br>**TAMWA:** Kifungu kinatoa utashi wa Kamati ya Uteuzi kuteua wajumbe pendekezwa (tisa) na kuna uwezekano wa kuwa wote wanaume. Kamati haielekezwi kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia katika kuchuja na kupata majina tisa ya Wajumbe wa Tume wanaopendekezwa.<br><br>Kuna uwezekano wa Kamati ya Uteuzi kuteua wajumbe pendekezwa (tisa) kuwa wote wanaume. Kamati haielekezwi kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuchuja na kupata majina tisa ya Wajumbe wa Tume wanaopendekezwa. |
| **8.** | UDSM, CCT, TLS, LHRC, TWAWEZA & JAMII FORUM TEC, ABDUL NONDO, | Ibara ya 10 | **UDSM:** kila mwananchi ana haki ya kupiga kura hivyo wafungwa wasizuiliwe kupiga kura. Lengo la marekebisho haya ni<br><br>**CCT:** Wafungwa waruhusiwe kupiga kura<br><br>**TLS:** Haki ya mtu kupiga kura haiwezi kupotea |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | BONAVENTURE MWALONGO, LOVENESS MAMUYA, YOSEPHA KOMBA, SALIM DEWJI, IDDI MANDI, TAMWA. | | kwa kutiwa hatiani au kizuizini. Hivyo wanashauri wafungwa na watu waliowekwa kizuizini waruhusiwe kupiga kura.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA & JAMII FORUM:** kukosa sifa ya kuandikishwa na kupiga kura kwa kutiwa hatiani kwa kosa la jinai halimuondolei mtu haki ya kupiga kura.<br><br>Lengo la marekebisho haya ni kutoa haki ya mtu kupiga kura haiwezi kupotea kwa kuwa alifanya kosa la jinai. Haki ya kupiga kura hutegemea hadhi ya uraia na utimamu wa uwezo wa akili.<br><br>**TEC:** Kifungu 10(1)(c) hiki kipo kinyume na Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 1977. Kifungu hiki kifutwe kama Mahakama ilivyotoa Hukumu kwenye case ya Tito Magoti, Jaji Elinaza Luvanda alibatilisha wafungwa kuzuiwa kupiga kura.<br><br>**ABDUL NONDO:** Wafungwa waruhusiwe kupiga kura kwa kuwa Ibara ya 5(1) ya Katiba |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawaruhusu na vilevile nchi nyingi za Afrika Mashariki na nchi nyingi za Afrika zinaruhusu wafungwa kupiga kura hivyo kifungu hiki pia kiwaruhusu kupiga kura.<br><br>**BONAVENTURE MWALONGO:** kifungu hakijaonyesha namna gani ya kuandikishwa na kupiga kura kwa Raia wali nje ya nchi. Diaspora, wagonjwa waruhusiwe kupiga kura.<br><br>**LOVENESS MAMUYA:** Diaspora waruhusiwe kupiga kura electronically au kupitia balozi zao.<br><br>**YOSEPHA KOMBA:** Walioko vizuizini, wafungwa na Diaspora waruhusiwe kupiga kura. Iwekwe namna ya kuandikishwa na kupiga kura kwa wafungwa. Diaspora hawajakosa sifa kwenye Muswada lakini hawapigi kura. Iwekwe namna waruhusiwe kupiga kura.<br><br>**SALIM DEWJI:** Diaspora waruhusiwe kupiga kura. Vilevile wagonjwa wawekewe utaratibu waweze kupiga kura. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **IDDI MANDI:** MHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM SHULE KUU YA SHERIA (UDSM) - Haki ya kupiga kura kwa mtu kwa mtu aliye kizuizini au gerezani iwepo na waruhusiwe.<br><br>**TAMWA:** kusiwe na gharama za kupata kitambulisho kipya cha kupigia kura utakapopoteza. |
| **9.** | TAMWA, ZAFELA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL na WILDAF | Ibara 12 | **TAMWA:** ongeza hali ya ulemavu au umri kwenye kifungu cha 12 (4).<br><br>**ZAFELA**: kifungu hiki hakijaanisha taarifa za umri, hali ya ndoa na hali ya ulemavu ya mpiga kura. Kifungu cha 12 (4) kiongeze hali ya ulemavu, tarehe ya kuzaliwa, baada ya neno jinsi na kusomeka kama ifuatavyo: (4) "*Daftari litaonesha bayana kwa kila mpiga kura aliyeandikishwa, namba ya kadi ya mpiga kura iliyotolewa, jinsi, hali ya ulemavu, tarehe ya kuzaliwa na anwani ya makazi ya kawaida ya mpiga kura na taarifa nyingine kama Tume itakavyoelekeza.*" |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu kiwekewe matumizi ya teknolojia ili zoezi liwe endelevu. |
| **10.** | CHADEMA | Ibara ya 13 | Kifungu cha 13(2)(3) kinamtaka Mtu ambaye ameomba kurekebisha kadi na kukataliwa kukata rufaa Mahakamani. Kuwe na Kanuni au fomu maalum itakayotumika ili iwe rahisi kukata rufaa kwenda Mahakamani na kuepuka urasimu. |
| **11.** | CHADEMA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, HAMISI | Ibara ya 14 | **CHADEMA**: Wafungwa raia wa Tanzania wanaotumikia vifungo wawe na haki ya kupiga kura na kama kina Sheria inayowazuia ifanyiwe marekebisho kwa kuwa pamoja na kutumikia vifungo bado ni Watanzania na wanayo haki ya kuchagua viongozi.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Tunapendekeza sheria<br>iweke sharti la vitambulisho rasmi<br>vinavyotambuliwa kwa mujibu wa sheria.<br>Kwa mfano, leseni ya udereva, hati ya kusafiria, kitambulisho cha Taifa, kitambulisho cha ukaazi, n.k |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Lengo la marekebisho haya ni Kupunguza vikwazo vinvavyowazuia wananchi kushiriki katika uchaguzi na hivyo wigo wa ushiriki wa uchaguzi kwa kuanisha vitambulisho na vitakavyotambulika wakati wa zoezi la kupiga kura ili wananchi wengi zaidi waweze kushiriki kati uchaguzi.<br><br>**HAMISI**: Ianzishwe kanzidata ya wapiga kura wa taifa. Hii itasaidia katika mazingira ambayo mpiga kura amepoteza kadi ya kupiga kura hivyo ataweza kuangaliwa katika kanzidata hiyo na kuruhusiwa kupiga kura. |
| **12.** | CHADEMA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 15 | **CHADEMA**: Kifungu cha 15 kifanyiwe marekebisho ili kuwe na kiapo cha Mtu ambaye majina yake yamebadilika ili kuepuka kuongeza wapiga kura kwa sababu ya mtu kuwa majina tofauti.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Tunapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha pili, 15 (2) kisomeke;<br>"Mabadiliko ya jina yatathibitishwa kwa |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | kufuata nyaraka husika kwa mujibu wa sheria na kwamba, utambulisho wa sura na alama za vidole au alama zinginezo zinashabihiana. |
| **13.** | TAG, BEDANI KAPONGWA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 16 | Lengo la mapendekezo hii kuepusha matumizi mabaya ya madaraka. |
| **14.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CCT, WILDAF, CHADEMA, ZAFELA | Ibara ya 17 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu hiki hakitoi fursa kwa mtu binafsi au taasisi nyingine kuwa na mawakala.<br><br>Kuongeza Kifungu kipya 17 (8) kisomeke;<br>Kwa madhumuni ya kifungu cha 17 Mtu yeyote, kwa niaba yake au kwa kuwakilisha taasisi yoyote, anaweza, kushiriki kwenye mchakato wa uandikishaji.<br><br>**CCT**: Siku 7 ni chache kwa chama kuandaa mawakala. Tunapendekeza siku ziwe 14.<br><br>**WILDAF:** Kifungu 17 (3) kiweke taarifa za jinsi, umri, hali ya ulemavu ya wakala wa |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | uandikishaji. Pia ni muhimu uchaguzi wa wakala uzingatia usawa wa jinsia.<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 17(7) kifutwe, kusiwe na kiapo cha kutunza siri kwa Wakala wa uandikishaji. Wakala ameteuliwa na Chama na kwa maana hiyo awe na uhuru wa kutoa mrejesho wa kinachoendelea kwa mamlaka yake ya uteuzi.<br><br>**ZAFELA**: Tunapendekeza kuongeza kuongeza kifungu kipya 17(8) kisomeke: kwa madhumuni ya Kifungu cha 17 Mtu yeyote, kwa niaba yake au kwa kuwakilisha taasisi yoyote, anaweza, kuangalia zoezi la uandikishwaji.<br><br>Kifungu cha 17 (3) kiweke taarifa za jinsi, umri, hali ya ulemavu ya wakala wa uandikishaji. Pia ni muhimu uchaguzi waw akala uzingatia usawa wa jinsia.<br>Lengo la marekebisho haya ni<br>Kuongeza wigo wa wadau kuangalia mwenendo wa mchakato wa uandikishaji. Uchaguzi ni mchakato |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | wa umma siyo wa wanasiasa pekee.<br>Pia, kuhakiki uadilifu wa mchakato wa uchaguzi |
| **15.** | CHADEMA, | Ibara ya 18 | Kifungu cha 18 (3) kina makosa ya kimantiki hakijaeleza ni taarifa gani Tume inaweza kuzichukua kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na namna taarifa hizo zitatumika kwenye zoezi la kuandikisha wapiga kura. Kuhamisha taarifa au kuunganisha mifumo ya taarifa (Data migration and data integration) kwenye mifumo miwili tofauti inaweza kunyima watu wengi fursa ya kupiga kura kwakuwa bado watu wengi hawajaingizwa kwenye mfumo wa NIDA. |
| **16.** | ZAFELA, WILDAF, CCT, DEUS KIBAMBA, TAMWA, IDDI MANDI, ARIF NURAR FADHER, | Ibara ya 20 | **ZAFELA** - Kifungu hiki kinaweka sharti la kulipa gharama ili kupata kitambulisho kipya kwa kadi iliyopotea. Wanapendekeza gharama ziondolewe za kulipia fedha kwa kitambulisho kilichopotea.<br>**WILDAF** - Wanapendekeza gharama za kupata kitambulisho kipya ziondolewe. Sababu ni kutokuweka vikwazo vya kifedha |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | TGNP, SAMSON SAMUEL, SALIM DEWJI.PETRO USESA. | | na kuwezesha wanawake ambao wenzi wao wameficha vitambulisho vya kupigia kura waweze kupiga kura.<br><br>**CCT** - Ibara ya 20(2) na 21 uwepo wa ada utapunguza wigo wa wapiga kura hususan vijana na watu wenye ulemavu. Ada iondolewe.<br><br>**DEUS KIBAMBA** - Ibara ya 20(2) na 21(2) virekebishwe ili kuruhusu kutumia kitambulisho mbadala kama NIDA, LESENI na PASI YA KUSAFIRIA.<br><br>**TAMWA** - 20(2) na 21(2) kusiwe na gharama za kupata kitambulisho kipya cha mpiga kura.<br>**IDDI MANDI - MHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM SHULE KUU YA SHERIA (UDSM)** - kupotelewa na kitambulisho cha mpiga kura kusimzuie mtu kupiga kura. Kitambulisho cha NIDA kitumike.<br><br>**ARIF NURARI FADHER** - Upotevu wa kadi neno ada lifutwe kwa watu waliopetelewa vitu vyao kutokana na majanga ya asili kama vile |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | tetemeko la ardhi kama ilivyotokea Hanang.<br><br>**TGNP** - Ibara ya 20(2) na 21(2) gharama za kulipia kadi iliyopotea itawatoa wapiga wengi hususan vijana na wenye ulemavu. Gharama hizi ziondolewe na vitambulisho mbadala vitumike kama vile NIDA na PASI YA KUSAFIRIA.<br>**SAMSON SAMUEL** - Ibara ya 20(2) na 21(2) ada ya kitambulisho kilichopotea iondolewe.<br><br>**SALIM DEWJI** - Ada ya uandikishaji kuwe na kiwango kidogo sana.<br><br>**PETRO USESA** - Kupoteza kadi ya mpiga kura kama sio kwa uzembe, masharti haya yasitumike. |
| **17.** | WILDAF, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 21 | **WILDAF:** Kusiwe na uwezekano wa kuweka gharama za kupata kitambulisho kipya cha mpiga kura.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kusiwe na gharama za kupata kitambulisho kipya cha mpiga kura. Tunapendekeza kufuta kwa maneno “ada”. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Lengo la marekebisho haya ni Ili kuhakikisha haki ya kupiga kura. Pia. Ili kuhamasisha mwitikio wa wapiga kura kushiriki uchaguzi. |
| **18.** | ADC | Ibara ya 22 | Kiongezwe kifungu cha kutambua viambatanisho vingine mfano NIDA, RITA ili kubaini nani aliyefariki na aliyekuwa hai. Sheria itambue katiba ya Zanzibar kwa sababu wakati wa kesi itabidi itambulike au kutumika. |
| **19.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, | Ibara ya 23 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Sheria haijaeleza ukomo wa muda ambao afisa mwandikishaji, atafanyia kazi rufaa ya kukataliwa kwa maombi ya uandikishwaji. Tunapendekeza ukomo uwe ndani ya siku saba (7).<br><br>Lengo la marekebisho haya ni Kutoa uwezekano wa rufaa kufanyiwa kazi kwa muda usiyojulikana kisheria |
| **20.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII | Ibara ya 24 | Kuondoa takwa la muda wa kufanya ukaguzi wa Daftari la Awali la Wapiga kura.<br>Lengo la marekebisho haya ni Kurahisisha |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | FORUMS, CSL, | | wananchi kukagua daftari la wapiga kura. |
| **21.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA, | Ibara ya 27 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu kinaainisha gharama za dhamana ya pingamizi. Hii ni kinyume na uamuzi wa Mahakama Kuu katika kesi ya Ndyanabo dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.<br><br>**CHADEMA:** Vifungu vya 27(2) na 28(7) kuhusu kulipa dhamana ya fedha kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume kuhusu wale ambao hawataridhika na taarifa kwenye daftari la wapiga Kura kupinga taarifa hizo vifutwe. Itawafanya wananchi kutolalamikia makosa yaliyopo kwenye daftari kwa kuhofia kuingia gharama za kuweka dhamana hiyo. Mchakato wa wananchi kuhakiki daftari na kupinga taarifa ambazo sio sahihi usihusishe kuweka dhamana ya fedha. |
| **22.** | ABDUL NONDO | Ibara ya 28 | Ibara ya 28 (5) iondolewe. |
| **23.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, | Ibara ya 30 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu hiki kinazuia haki ya kukata rufaa |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA | | zaidi maamuzi ya Mahakama ya Wilaya. Tunapendekeza kurekebisha kifungu hiki kwa kuondoa ukomo wa Mahakama ya Wilaya kuwa mwisho wa rufaa.<br>Lengo la marekebisho haya ni<br><br>**CHADEMA**: Kifungu cha 30(1) kuhusu masharti ya kuweka dhamana ya fedha kabla ya kukata rufaa Mahakama ya Wilaya kuhusu kuongezwa au kufutwa kwenye daftari la Wapiga Kura masharti ya dhamana yafutwe.<br><br>Kifungu cha 30(2) kinaelekeza kwamba uamuzi wa Mahakama ya Wilaya kuhusu kufutwa au kuongezwa kwenye daftari la Wapiga ni wa mwisho. Kifungu kiboreshwe kwamba mtu asiporidhika na uamuzi wa Mahakama ya Wilaya anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu na asiporidhika anaweza kukata rufaa kwa masuala ya kisheria pekee kwenda Mahakama ya Rufani.<br><br>Kiongezwe kifungu kidogo cha 10 kwenye kifungu cha 30 kuonyesha kwamba kutakuwa na fomu maalum zitakazokuwa kwenye |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Kanuni zitakazotungwa na Jaji Mkuu ya namna ya kukata rufaa.<br><br>Kifungu cha 30 (4), (5), (6) kirekebishwe ili kuondoa masuala ya kutaifisha dhamana iliyowekwa kabla ya kukata rufaa ambayo tumependekeza ifutwe. |
| **24.** | TANLAP, USHIRIKI TANZANIA, WILDAF, ZAFELA , CHADEMA, UDSM (IDDI MANDI) | Ibara ya 32 | **TANLAP** - Haijaweka sharti mahsusi la kutaka vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia.<br><br>**USHIRIKI TANZANIA** - Ibara hii haijabainisha uzingatiaji wa usawa wa kijinsia. Hivyo kifungu hiki kiboreshwe.<br><br>**WILDAF, ZAFELA** - Ibara hii haijaweka sharti la kuzingatia ujumuishwaji wa kijinsia wakati wa uwasilishaji wa majina ya mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais. Ibara ifanyiwe marekebisho kiongezwe kifungu kidogo kipya kuleta usawa kijinsia kitakachovitaka vyama vya siasa vikitaka kuteua mgombea urais mwanaume basi Makamu wa Rais awe mwanamke na kinyume chake. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CHADEMA** - Kuwe na wagombea binafsi.<br><br>**UDSM (IDDI MANDI)** - suala hili limeachwa kwenye Muswada. Anapendekeza haki ya kugombea kama mgombea huru iwekwe kwenye Muswada. |
| **25.** | WILDAF, ZAFELA, SAHIRINGO | Ibara 33 | **WILDAF, ZAFELA** - Ibara hii inataka mgombea adhaminiwe na wadhamini angalau 200. Ibara hii imtake mgombea kutafuta wadhamini wanawake na wanaume kwa msingi wa 50/50 la sivyo athibitishe kuwa ameshindwa kuwapata wadhamini wa jinsi au kundi fulani.<br><br>**SAHIRINGO** - Ibara ya 33(1) wadhamini kila Mkoa wapungue kutoka 200 na kuwa 100 maana ni kazi kubwa ya kutafuta wadhamini. |
| **26.** | ZAFELA, WILDAF, TREE OF HOPE TANZANIA, CCT, TLS | Ibara 34 | **ZAFELA, WILDAF, TREE OF HOPE TANZANIA** - 34(3) Ibara hii ifanyiwe marekebisho na kuongeza maelezo muhimu yatayohitajika kwa mgombea ikijumuisha jinsi, hali ya ulemavu na tarehe ya kuzaliwa.<br>**CCT** - Kwenye fomu ya kugombea Urais |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | waweke fomu ya wenye mahitaji maalum ili waweze kushiriki.<br><br>**TLS** - Sheria ina ubaguzi hususan kwenye fomu za mgombea katika ngazi ya Urais haijazingatia watu wenye ulemavu. Vilevile fomu za mgombea katika uwasilishaji wake fomu ziwasilishwe kwa mtandao halafu nakala ngumu ndio ifuatie kuwasilishwa. |
| **27.** | CCT<br>UDSM - IDDI MANDI,<br>WILDAF,<br>ZAFELA,<br>CHECK MSUVA,<br>CHADEMA. | Ibara 35 | **CCT -** Dhamana iondolewe.<br>**UDSM - IDDI MANDI** - Dhamana ya gharama katika vifungu vyote iondoke.<br>**WILDAF**, **ZAFELA** - 35(2)(b) - Ibara hii inazuia uwanda wa ushiriki wa wananchi katika uchaguzi kwa kutokuwa au kuhofia kurudishiwa kwa dhamana zao. Wagombea wanawake, vijana na wenye ulemavu wasitoe dhamana ili kuwaondolea vikwazo vya kugombea.<br><br>**CHECK MSUVA** - Sharti la dhamana kwa makundi maalum ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu lisiwepo. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CHADEMA** - Ibara ya 35(2)(b) - Ibara hii ifutwe hakuna maana ya kuweka sharti hilo. |
| **28.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 36 | Kifungu hiki hakijaonesha taratibu za kukata rufaa dhidi ya kukatiliwa uteuzi, haki ya kusikiliza na haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi Tume. Kifungu kiweke kifungu kidogo cha pili kitakachoweka haki ya kukata rufaa.<br>Lengo la marekebisho haya ni Inakiuka ibara ya 13(6) (a) na Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya JAMHURI YA Muungano wa Tanzania 1977 |
| **29.** | ZAFELA, TUSONGE, CCT, WILDAF, CHADEMA, ACT WAZALENDO, TAMWA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 37 | **ZAFELA:** Kifungu hiki kiainishe makosa yanayotokana na ukatili wa wanawake katika siasa kama ni moja ya makosa ambayo mtu anaweza kupinga uteuzi wa mgombea.<br><br>**TUSONGE**: Kuwe na kosa la ukatili wa kijinsia kupinga uteuzi wa mgombea.<br><br>**CCT:** Kifungu kirekebishwe kwa kuondoa watendaji wa serikali.<br><br>**WILDAF:** Kifungu hiki kiainishe makosa |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | yanayotokana na ukatili wa wanawake katika siasa kama ni moja ya makosa ambayo mtu anaweza kupinga uteuzi wa mgombea.<br><br>Sheria ya Vyama vya siasa chini ya Kifungu cha 6B cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinakataza Ukatili wa Kijinsia.<br>Ongeza kifungu 37 (f) kinachosema<br>"Kama mgombea amethibitika amefanya makosa ya ukatili wa kijinsia."<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 37(6) kiandikwe upya kuruhu Mgombea Urais ambaye hajateuliwa na Tume kukata rufaa Mahakama Kuu na Rufaa husika kusikilizwa na kuamuliwa ndani ya 14 toka uamuzi wa kutoteuliwa au kuenguliwa kufanyika.<br><br>**ACT WAZALENDO:** Mgombea apewe haki kwa mujibu wa katiba JMT 1977 ibara ya 13(6)(a) kama hajaridhika na maamuzi ya Tume ya uchaguzi kukata rufaa na kupinga maamuzi hayo mahakama kuu.<br>Lengo la marekebisho hayo ni Mtu yoyote awe na uhuru na uwezo wa kuweka pingamizi |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | pale ambapo linahitajika<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu hakitoi fursa ya kurekebisha makosa madogo. Kifungu kitoe fursa kurekebisha makosa madogo yanayoweza kurekebishjika kuliko kutengua. Inakiuka ibara ya 13 (6) (a) na ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977<br><br>Tunapendekeza kuongeza maneno yafuatayo: Mtu hatokataliwa kuteuliwa kwa sababu za dosari za kiufundi, hivyo tunapendekeza Tume iweke muda wa kukagua fomu za wagombea kubaini fomu zenye kasoro na kutoa fursa ya kufanya masahihisho.<br><br>a) "…….na baada ya kupewa fursa ya kurekebisha au kuwasilisha kwa mujibu wa masharti ya sheria hii alishindwa kufanya hivyo.."<br>b)….na baada ya kupewa fursa ya kurekebisha au kuwasilisha kwa mujibu wa masharti ya sheria hii alishindwa kufanya |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | hivyo.<br>c)......Na baada ya kupewa fursa ya kurekebisha au kuwasilisha kwa mujibu wa masharti ya sheria hii alishindwa kufanya hivyo.<br><br>Kifungu cha 37 (3) kinawapa uzito mkubwa kupitiliza watendaji wa serikali kama Msajili wa Vyama na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweka pingamizi, jambo ambalo linaleta hisia za matumizi mabaya ya mapingamizi.<br><br>Tunapendekeza kuondoa mamlaka za serikali kuweka mapingamizi. Kifungu hiki kisomeke; Mtu yoyote anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mgombea wa Urais. |
| **30.** | CHADEMA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 38 | CHADEMA: Kifungu cha 38(2) kiandikwe upya ili Mgombea pekee wa Urais kupata 50% +1 ya kura zote halali ndipo atangazwe kuwa mshindi na kuondoa sharti la kura nyingi pekee.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu cha 38 (3) hiki kimeacha ombwe |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | la muda gani unahitajika hadi kufanya uteuzi mpya. Kifungu hiki kisome; Endapo mgombea pekee wa kiti cha Rais atashindwa kupata kura nyingi zaidi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), ndani ya siku thelathini (30) Tume itafanya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi wa Rais kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.<br>Lengo la marekebisho ni Kuweka muda maalumu ili kuepuka mgongano wa kisheria kipindi cha uchaguzi. |
| **31.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 39 | Kifungu hiki hakina mazingira na sababu zitakazo mfanya mgombea wa urais kujitoa kiholela. Kiujumla, tunapendekeza Tume kutoa nafasi kwa chama ambacho mgombea wake amejitoa, chama wateue mgombea mwingine. Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke kama ifuatavyo;<br>1) Endapo kutakuwa na mazingira yanayolazimu mtu kujitoa katika ugombea, mgombea wa kiti cha urais anaweza kujitoa ugombea kwakutoa taarifa ya maandishi aliyoisaini ikieleza sababau aliyeiwasilisha yeye |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | mwenyewe kwa Tume na nakala Katibu Mkuu wa chama kilichomdhamini. Tunapendekeza kuongeza kifungu kipya, kitakachosomeka;<br>Lengo la marekebisho haya pamoja na sababu nyingine ni<br>(a) Mapendekezo haya yanalenga kubainisha mazingira na sababu za mgombea kujitoa.<br><br>(b) Lengo ni kutoa nafasi kwa chama kuteua mgombea mwingine<br><br>(c) Kuziba mianya ya rushwa na ushawishi unaoweza kumrahishia mgombea mmoja kupita bila ushindani wenye maana ya kidemokrasia<br><br>Tunapendekeza chama kipewe nafasi ya kumteua mgombea mwingine. Pia, dhamana ya mgombea ifilisiwe.<br><br>Kuongeza kifungu kipya, kitakachosomeka; Mgombea yoyote aliyeshindwa kujitoa rasmi kwa mujibu wa kifungu cha kwanza na cha |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | pili 39 (1) na (2) hatoruhusiwa kugombea nafasi yoyote katika kipindi kinachofuata cha uchaguzi. |
| **32.** | CCT, James Masunga, Jukwaa la Katiba Tanzania na Salim Dewji, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL. | Ibara ya 41 | **CCT:** Sheria ianishe na kutaja siku ya uchaguzi. Lengo ni kuruhusu watu Kwenda kwenye ibada siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu hiki hakijainisha mazingira au sababu ambazo Tume inaweza kupanga siku tofauti au kutengua siku ya uchaguzi.<br>Lengo la marekebisho ni Ili kuweka sababu maalum za kupanga siku nyingine ya uchaguzi. |
| **33.** | CHADEMA, ACT-WAZALENDO | Ibara ya 43 | **CHADEMA:** Sifa za wagombea ziwe za kikatiba tu na siyo za ziada. |
| **34.** | MTANDAO WA TIBA ASILIA, TLS, LHRC, | Ibara 45 | **MTANDAO WA TIBA ASILIA:** Neno Mtu mwingine katika Ibara 45 (1) ni nani? Tunapendekeza waandishi wa Habari wajumuishwe. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA | | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Tunapendekeza kurekebisha kifungu cha 45 (1) (i) kisomeke;<br>Kwa makubaliano ya Tume na wadau wengine kwa mujibu wa kifungu hiki, Tume inaweza kumruhusu mtu mwingine yeyote kuingia katika kituo cha kupiga kura.<br><br>Kifungu kinaweka mwanya usiyo wa kisheria kwa kumtaka msimamizi wa uchaguzi kusubiri maelekezo ya Tume ili kubandika nakala ya taarifa ya matokeo. Kifungu kisomeke; Msimamizi wa uchaguzi, baada ya kuandaa taarifa ya matokeo chini ya kifungu kidogo cha (3), atabandika nakala ya taarifa hiyo katika sehemu ya wazi inayoonekana kwa mujibu wa masharti ya sheria hii.<br><br>Kifungu CHA 45 (10) hakiendani na matakwa ya wadau wa demokrasia kuhusu majumuisho ya kura za uchaguzi wa urais. Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke; "Mgombea yeyote wa kiti cha Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo amepata kura zinazofikia zaidi ya nusu ya kura zote |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | halali". Tunapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 45 (11) "Endapo hakuna mgombea atakayefikisha kura zinazohitajika katika kifungu 45 (10) hapo juu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza kuwa hakuna mgombea aliyechaguliwa kuwa Rais na ndani ya siku sitini (60) itateua siku ya uchaguzi wa marudio ambapo wagombea wawili waliyopata kura nyingi kuliko wengine watachuana katika duru ya pili.<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 45(10) kiandikwe upya ili mshindi wa kiti cha Urais atakiwe kupata 50%+1 ya kura zote halali ndipo atangazwe kuwa amechaguliwa.<br>23.<br>Kiongezwe kifungu cha 45(11) ili kama hakuna Mgombea wa kiti cha Urais aliyepata 50%+1 ya kura zote halal, uchaguzi urudiwe kwa Wagombea wawili waliopata kura nyingi zaidi. |
| **35.** | CHADEMA | Ibara 46 | Kifungu cha 46 cha marudio ya uchaguzi wa Rais kirekebishwa kiendane na masharti ya kifungu cha 45(10) baada ya marekebisho. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | |
| **36.** | TREE OF HOPE TANZANIA, ZAFELA | Ibara 50 | **TREE OF HOPE TANZANIA** - 50(3) ipo kimya kuhusu maelezo muhimu mfano jinsi, umri na hali ya ulemavu.<br><br>**ZAFELA** - Hakuna sharti la mgombea kuzingatia ujumuishwaji wa jinsia na makundi mbalimbali katika kutafuta wadhamini. Kifungu hiki kimtake mgombea kutafuta wadhamini kutoka kwa wanawake na wanaume kwa msingi wa 50/50 la sivyo athibitishe kuwa ameshindwa kuwapata wadhamini wa jinsi au kundi fulani.<br>50(2) - Ibara hii inazuia uwanda wa ushiriki wa wananchi katika uchaguzi kwa kutokuwa au kuhofia kutorudishwa kwa dhamana zao. Wagombea wanawake na wenye ulemavu wasitoe dhamana ili kuwaondolea vikwazo vya kugombea.<br><br>50(3) - Ibara hii ifanyiwe marekebisho na kuongeza maelezo muhimu yatakayohitajika kwa mgombea ikijumuisha jinsi, hali ya ulemavu na umri. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **37.** | CCT, UMOJA WA ASAS ZA VIJANA, CHADEMA. | Ibara 51 | **CCT -** Dhamana itolewe na vyama.<br>**UMOJA WA ASAS ZA VIJANA -** Dhamana iondolewe ili kuruhusu kundi maalum kushiriki.<br><br>**CHADEMA** - Ibara irekebishwe kuondoa sharti la kutaifisha dhamana mgombea wa ubunge asipata 1/10 ya kura zote halali. |
| **38.** | ACT WAZALENDO, CCT, ZAFELA, CHADEMA, | Ibara 53 | **ACT WAZALENDO -** Ibara iruhusu maamuzi ya Tume kupingwa mahakamani.<br>**CCT** - Ibara iruhusu mtu yeyote kuweka pingamizi.<br><br>**ZAFELA** - 53(6) Ibara hii irekebishwe ili kutoa haki kwa mtia nia ambaye hajaridhika kwenda mahakamani.<br><br>**CHADEMA** - 53(6) - Ifanyiwe marekebisho ili mgombea asiyeridhika na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu pingamizi akate rufaa moja kwa moja kwenda Tume ya Uchaguzi na sio kupitia kwa Msimamizi wa Uchaguzi. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **39.** | ABDUL NONDO, CAHDEMA | Ibara 54 | **ABDUL NONDO** - 54(2) kuwekwe sharti mgombea pekee anayepigiwa kura za ndio apate zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa ndipo aweze kutangazwa mshindi.<br><br>**CHADEMA** - 54(2) Iandikwe upya ili kuweka sharti kwa mgombea pekee wa ubunge kupata 50%+ 1 ya kura zote halali ndipo atangazwe kwamba amechaguliwa. |
| **40.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 57 | Kifungu kinampa mamlaka Waziri badala ya Tume ambayo ndiyo yenye dhamana. Mamlaka ya kutangaza kata iko wazai yabaki wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br>Lengo la marekebisho haya Ni kuepuka mkanganyiko miongoni mwa wagombea.<br><br>Kifungu hakijaainisha muda maalumu wa zoezi la kupokea fomu za uteuzi. Tunapendekeza muda uwe si zaidi ya saa kumi kamili alasiri kama ilivyo kwa nafasi za ugombea wa nafasi ya Urais na Ubugne teuzi wa wagombea wa uchaguzi katika kata ambayo nafasi wazi imetokea. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **41.** | UMOJA WA ASAS ZA VIJANA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 59 (2) | **UMOJA WA ASAS ZA VIJANA**: Miaka iwe 18 lengo la marekebisho ni Kuweka ushiriki mpana wa vijana. Kuweka ukomo ili kuruhusu vijana kushiriki katika nafasi za uongozi.<br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu kinaweka mianya ya tafsiri tofauti za sifa za mgombea wa udiwani, sifa hizo zinaweza kutafsiriwa tofauti mara baada ya mgombea huyo kushinda nafasi hiyo. Tunapendekeza kuongeza kifungu na kusomeka;<br>Sifa za mgombea wa udiwani zitaendelea kumuhusu mtu aliyechaguliwa kuwa diwani.<br><br>Kifungu kimeacha kundi la vijana wa miaka 18 ambao wanahaki ya kupiga kura. Pia, kifungu hakina ukomo wa umri wa mtu kugombea nafasi ya udiwani.<br>Lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa sifa za mgombea za udiwani zinaongezwa wigo hadi baada ya mtu kushinda nafasi ya udiwani. |
| **42.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, | Ibara 60 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu hakijaainisha sababu za |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA, WILDAF, TAMWA, | | kutengua siku iliyopangwa kwa ajili ya uteuzi. Pia, sheria imeweka muda mfupi wa kutoa taarifa ya siku ya uteuzi.<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 60(1)(e) kinamuondolea sifa Mtu aliyewekwa kizuizini kuteuliwa kugombea udiwani. Kifungu na Sheria ya kuweka watu kizuizini ifutwe.<br>.<br><br>**WILDAF:** tunapendekeza kuongeza kipengele Kama mtu atakutwa na hatia ya makosa yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa.<br>Lengo ni Kuepuka matumizi mabaya ya madaraka |
| **43.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, TGNP, WILDAF, | IBARA 62 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Tunapendekeza mgombea aape kwa kamishina wa viapo yeyote.<br>Lengo la marekebisho ni Kurahisisha zoezi la uapishaji kulingana na ufinyu wa muda uliopo<br><br>Tunapendekeza kuwa adhaminiwe na |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | wadhamini wasiopungua kumi(10) katika kila kijiji/mtaa wa kata husika.<br><br>**TGNP:** Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke:<br>(2) Uteuzi utafanyika kwa kutumia fomu itakayoainishwa ambayo itazingatia Jinsia na matumizi ya watu wenye mahitaji maalumu, itakayosainiwa na mgombea na watu wanaomdhamini mgombea huyo na itakuwa na taarifa zifuatazo:<br>(a) jina, Jinsi, tarehe ya kuzaliwa, anwani na kazi ya mgombea;<br>(b) majina, Jinsi, tarehe za kuzaliwa na anwani za wadhamini na namba za kadi zao za kupiga kura. |
| **44.** | TLS, WILDAF na CHADEMA | Ibara ya 63 | **TLS:** Takwa la dhamana katika fomu za uteuzi linakiuka haki ya kuchaguliwa ( Kifungu hiki kifutwe). Tunapendekeza kufutwa kwa takwa la dhamana katika uchukuaji wa fomu za utuezi.<br>Lengo la marekebisho haya ni kutoa furs kwa wananchi wengi Zaidi kushiriki katika mchakato wa uchaguzi |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **WILDAF:** Kiongezwe kifungu 61 (4) kinachosema wagombea udiwani wanawake watasamehewa kulipa gharama ya dhamana. |
| **45.** | **TLS, CHADEMA, CCT,** | Ibara 65 | **TLS**: Tunapendekeza kuondolewa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa sehemu wa waweka mapingamizi. Tunapendekeza wafuataو kuwa na sifa za kuweka mapingamizi<br>1. Mgombea<br>2. Chama cha siasa kilichomdhamini mgombea husika<br>3. Mpiga kura.<br>Lengo la marekebisho haya ni Kuondoa mwanya wa kuingilia haki za wagombea.<br><br>Tunapendekeza ndani ya siku saba (7) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi atamtaarifu mwekewe pingamizi juu ya uwepo wa pingamizi hilo.<br><br>**CHADEMA**: Kifungu cha 65(7) kirekebishwe ili Mgombea wa nafasi ya udiwani aweze |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | kukata rufaa moja kwa moja kwenda Tume. Baada ya kupokea rufaa Tume iamuru Msimamizi wa Uchaguzi kuwasilisha taarifa au utetezi wake ndani ya siku tatu toka siku ya uamuzi wake na Tume itaamua kuhusu rufaa ndani ya siku 10 toka siku rufaa husika ilipowasilishwa. Kuwe Na nafasi ya Mgombea udiwani kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Tume. |
| **46.** | **WILDAF** | Ibara ya 74 | Tunapendekeza kuongezwa kwa kifungu kitakachoweka adhabu kwa chombo ambacho kitakiuka matakwa ya sheria.<br><br>Tunapendekeza kujumuishwa kwa vyombo vya habari vya binafsi. |
| **47.** | **CHADEMA** | Ibara ya 77 | Kifungu cha 77(1) kirekebishwe ili kuondoa maneno "… baada ya kupata ridhaa ya Wagombea…" hii Ina maana kwamba Wakala wa upigaji Kura atateuliwa Na Chama baada ya Chama kupata ridhaa ya Mgombea jambo ambalo sio sahihi. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **48.** | ZAFELA, WILDAF, TUSONGE, TAMWA, AISHA SALEH MADOGA | Ibara ya 84 | **ZAFELA -** Tume ihakikishe kuna karatasi za kupigia kura ambazo zipo kwenye format ya nukta nundu ili kuwawezesha wapiga kura wenye ulemavu wa kuona kupiga kura kwa usiri.<br><br>**WILDAF** - 84(3) Tume ihakikishe kuna karatasi za kupigia kura ambazo ziko katika format ya nukta nundu ili kuwawezesha wapiga kura wenye ulemavu wa kuona kupiga kura kwa usiri.<br><br>**TUSONGE** - 84(3)(b) - Ibara ina pengo kubwa hivyo Tume ihakikishe kwamba karatasi za kupiga kura zilizo na format ya nukta nundu zinakuwepo.<br><br>**TAMWA** - 84(3)(b) - kuwe na karatasi za kupiga kura za aina tofauti kuwajumuisha na watu wenye ulemavu.<br><br>**AISHA SALEH MADOGA** - 84(3)(b) - kwa wapiga kura wasiojua kusoma na kuandika na wasioona kuwe na karatasi za nukta nundu. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **49.** | ACT WAZALENDO, TLS | Ibara ya 85 | **ACT WAZALENDO -** 85(5) - Ibara ifutwe kwani inahalalisha wapiga kura, wanausalama, watu wa huduma za kwanza na mawakala kutolewa nje ya vituo.<br>**TLS** - Neno mtu yeyote lina ukakasi. Neno "mtu yeyote" lifutwe. Inapendekezwa kujumuishwa kwa waandishi wa habari watakaoidhinishwa na Tume kama sehemu ya watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupiga kura.<br><br>85(2)(e) - neno "msaidizi" litafsiriwe kwa upana.<br>85(5) - Ibara inaainisha suala la utovu wa nidhamu. Kimsingi utovu wa nidhamu ni ngumu kuthibitisha kisheria. Inapendekezwa kifungu hiki kirekebishwe. |
| **50.** | TANLAP, TLS | Ibara ya 88 | **TANLAP** - 88(1) Ibara haijaeleza sababu nyingine zinazoweza kusababisha zoezi la kupiga kura kusitishwa. Vilevile hakijaeleza sababu zinazoweza kusababisha uchaguzi kuahirishwa kabla ya zoezi la upigaji kura kuanza. Inapendekezwa Ibara irekebishwe ili kuweka utaratibu wa kuahirisha uchaguzi kabla ya zoezi la upigaji kura kuanza |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | inapotokea sababu mbalibmali kama majanga ya asili.<br><br>**TLS** - Ibara hii imejibana kwenye vurugu pekee ingawa kuna mazingira mbalimbali yanayoweza kupelekea zoezi la kupiga kura kuahirishwa. |
| **51.** | TLS | Ibara ya 92 | **TLS** - 92(8) Ibara inanyima haki kwa mtu ambae hatotia saini fomu. Inapendekezwa kifutwe. |
| **52.** | TLS | Ibara ya 93 | **TLS** - 93((3) - Takwa la mlalamikaji au wakala kupewa nakala ya fomu ya malalamiko. |
| **53.** | TLS | Ibara ya 96 | **TLS** - 96(1)(a) - Ibara hii ifutwe ili kuendana na Ibara ya 84(3)(f) ili kuweka mtiririko wenye mantiki. |
| **54.** | **CHADEMA, TLS** | Ibara 102 | **CHADEMA**: Kifungu cha 102(c) maneno "… iwapo fomu za matokeo zipo za kutosha…." Yafutwe ili kulazimu Msimamizi wa uchaguzi kumpatia Wakala nakala ya matokeo ya uchaguzi. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS:** Kifungu 102 (1)(e) hiki kirekebishwe na kisomeke; "Atampa kila wakala wa kuhesabu kura nakala ya taarifa ya matokeo". |
| **55.** | **TLS** | Ibara 107 | Tunapendekeza kuondoa kifungu cha 107 (3) kinachopendekeza kuteketeza nyaraka za uchaguzi ndani ya miezi 6 kwa kuwa kifungu hiki kinakinzana na muda wa mashauri ya uchaguzi na Kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Taifa ya Utunzaji wa Kumbukumbu Nyaraka za Taifa Namba 3, 3002 (The Records and Archives Management Act No.2 of 2002) ambayo inaweka takwa la nyaraka za Taifa kutunzwa ndani ya miaka 30.<br>Lengo la marekebisho haya ni Ili kutoharibu vielelezo vya msingi vya mashauri ya uchaguzi na kuendana na Sheria ya Taifa ya Utunzaji wa Kumbukumbu wa Nyaraka. |
| **56.** | **TLS, KITUO CHA TAARIFA KWA WANANCHI, WILDAF** | Ibara 112 | Kifungu hakijaweka mchakato wa upatikanaji wa wabunge wa viti maalumu.<br><br>Kuwe na ukomo wa Viti Maalumu |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **57.** | **CHADEMA** | Ibara ya 125 | Kifungu cha 125 (1)(2)(3)(4)(5)(6) na (7) kuhusu kiapo cha kutunza siri na adhabu zake dhidi kwa Mawakala na Wagombea pamoja na kuwazuia Mawakala kutokuwa na mawasiliano na Chama au Mgombea kitatoa mwanya kwa Wasimamizi wa uchaguzi kufanya jambo lolote kwenye vituo vya kupigia kura na Wakala hatachukua hatua yoyote kwa sababu ya kiapo cha kutunza siri. Kifungu hiki kilitungwa wakati nchi ikiwa ya Chama kimoja na hakina nafasi kwa wakati huu wa demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa. |
| **58.** | **TLS, UMOJA WA ASAS ZA VIJANA** | Ibara 166 | Tunapendekeza kwamba badala ya kutumia neno inaweza, litumike neno Tume itatumia teknolojia.<br>Lengo ni kuondoa mwanya wa Tume kuwa na uhuru wa kutumia teknolojia kwenye ulimwengu wa sasa unaotegemea matumizi ya teknolojia kwa kiwango kikubwa. |

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa hoja hizo pamoja na maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika Muswada, baadhi ya changamoto zilizobainika utatuzi wake unahitaji mabadiliko ya Sheria zingine ambazo hazifanyiwi kazi na Kamati kwa sasa.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

(i) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 6(1) inaeleza kuwa kila Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya atakuwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika Jimbo au Kata.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikuwa ina maoni kwamba Sheria isiweke ulazima kwa Mkurugenzi Mtendaji kusimamia Uchaguzi na badala yake, kuwepo na masharti ya Mtumishi wa Umma mwandamizi ama mtu mwingine yoyote mwenye sifa kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi msaidizi wa Uchaguzi. Serikali iliona kuwa upo umuhimu wa Wakurugenzi Watendaji kutajwa kwenye sheria kwa kuwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania kwenye kesi ya madai na. 138/2019 na Mahakama ya Afrika ya Watu na Haki za Binadamu kwenye kesi ya madai na. 11/2020 ziliamua kuwa Wakurugenzi kusimamia Uchaguzi haukiuki masharti ya Katiba wala Mkataba wa Afrika wa Watu na Haki za Binadamu mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati bado ina maoni kuwa hakuna ulazima wa sheria kuweka sharti kwa Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya kuwa wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa kuwa uzoefu unaonyesha wapo Wakurugenzi kwa sababu mbalimbali wanapoteza sifa za kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati ya kuwatumia Watumishi wa Umma Waandamizi ama mtu yoyote mwenye sifa kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika Jimbo au Kata.

(ii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 8 inaweka masharti ya Uteuzi wa waratibu wa uchaguzi, Kamati ilikuwa na maoni kuwa Muswada utambue ofisi za Balozi Nje ya Nchi kuwa Waratibu wa Uchaguzi, ili kutoa fursa kwa Watanzania walio Nje ya Nchi kupiga kura, Kwa kuzingatia kuwa Ibara ya 5 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayompa haki raia wa Tanzania kupiga kura akiwa ametimiza umri wa miaka 18 na ikiwa hafungwi na masharti ya Ibara ya 5(2) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, katika hoja hii Serikali ilifafanua kuwa Uchaguzi una mifumo yake ambayo unatakiwa kuhakikisha kura zinazopigwa zinakubalika na kuaminiwa na wadau wa uchaguzi. Na kwamba bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha mifumo hiyo inawekwa ya kuwezesha watanzania walioko nje ya nchi kupiga kura na kura hizo kupatikana kwa wakati na kuaminiwa. Kwa Msingi huo, Kamati ina maoni kuwa suala hili linahitaji kufanyiwa utafiti wa namna ya utekelezaji wake.

(iii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 12 inaweka masharti ya Daftari la Kudumu la Wapiga kura, Kamati iliishauri Serikali kuongeza taarifa ya hali ya ulemavu wa mpiga kura, Kwa kuwa kuongeza hali ya ulemavu wa mpiga kura Kutaiwezesha Tume kuweka miundombinu stahiki kwenye vituo vya upigaji kura mapema iwezekanavyo.

Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(iv) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 13 inaweka masharti ya Uandikishaji wa wapiga kura Tanzania Zanzibar, Muswada unapendekeza kwa Uchaguzi wa Wabunge Tanzania Zanzibar kutumia daftari la mpiga kura linalotumika kuchagua Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar isipokuwa kwa kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, wapiga kura wataandikishwa na Tume ya Uchaguzi (NEC). Lengo ni kuwa na Daftari moja linalojitegemea ili kuratibu utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliifafanulia Kamati kuwa Msingi wa sharti hilo ni kuhakikisha kuwa Wabunge wa Zanzibar wanapigiwa kura na wakaazi wa eneo husika.

(v) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 15 inaweka masharti ya kubadili majina kwa mpiga kura aliyeandikishwa kutokana na sababu ya ndoa au sababu nyingine yoyote baada ya kuandikishwa, Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kidogo cha (2) kitakachoweka masharti kuwa mabadiliko ya jina yatathibitishwa kwa kufuata nyaraka husika kwa mujibu wa sheria. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(vi) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 20 inaweka masharti ya utaratibu wa kupotea, kufutika au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura, Kamati ilipendekeza Ibara ya 20(2) iondoe ada ya kulipia kitambulisho cha mpiga kura iwapo kimepotea, kuharibika ama kufutika. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(vii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 21 inaweka masharti ya urekebishaji wa taarifa kwenye Daftari la Awali la Wapiga kura, Kamati ilipendekeza kusiwe na ada ya marekebisho ya taarifa. Lengo ni kumuwezesha mpiga kura kutimiza haki yake ya Kikatiba

bila gharama yoyote. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(viii) **Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 23 inaweka masharti ya kukataliwa kwa maombi ya uandikishaji wa wapiga kura, Kamati iliishauri Serikali kuweka muda wa siku saba kwa mwombaji aliyekataliwa maombi kuwasilisha mapitio kwa Afisa Mwandikishaji na kwamba muda wa Afisa huyo kushughulika mapitio hayo haujawekwa bayana kama ambavyo muda wa Mahakama kushughulikia rufaa ulivyobainishwa katika ibara ndogo ya (3), lengo ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifafanua kuwa msingi wa kutoweka muda kwa Afisa Mwandikishaji kutoa uamuzi ni wingi wa mapingamizi yanayoweza kuwasilishwa ikilinganishwa na rasilimali watu iliyopo kwa wakati husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilishauri maboresho kwenye Ibara ya 23(2) kwa kuruhusu rufaa kuanzia Mahakama za Mwanzo. Lengo ni kuboresha huduma kwakuwa Kwa baadhi ya maeneo hususani vijijini Mahakama za Wilaya ziko mbali na Wananchi, hivyo ni vyema kutumia Mahakama za Mwanzo zilizokaribu zaidi na Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati kwa kuweka sharti kwa Afisa mwandikishaji kutoa uamuzi wa maombi ya mapitio ndani ya siku kumi na nne tangu kuwasilishwa kwa maombi hayo pamoja na kuweka sharti la rufaa kusikilizwa kuanzia Mahakama za Mwanzo, Maboresho hayo yamependekezwa na Kamati katika Ibara ya 28, 29 na 30 ya Muswada.

(ix) **Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 26 inaweka masharti ya pingamizi ya uwepo wa jina la mpiga kura katika Daftari la Awali la Wapiga kura, Kamati ilikuwa na maoni kuwa Ibara ya 26(2) inaruhusu Mkurugenzi wa uchaguzi au Afisa Mwandikishaji kuweka pingamizi kuhusu uwepo wa jina lolote katika daftari la awali la Wapiga Kura.

Utaratibu huu unasaidia kuweka kumbukumbu sahihi za Daftari lakini unakiuka misingi ya haki ya asili. Utaratibu uliopo katika Ibara ya 157 ya Muswada unahusu kuomba taarifa za ziada utaratibu huo unaweza kutumika badala ya Afisa mwandikishaji kuweka pingamizi. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(x) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 27 inaweka masharti ya utaratibu wa pingamizi, Muswada unapendekeza kuwa Afisa mwandikishaji hatokuwa na Wajibu wa kuwasilisha taarifa ya pingamizi popote, ikiwa pingamizi ni dhidi ya mtu aliyefariki. Kamati imeishauri Serikali kufanya maboresho kwa kuweka takwa la Afisa mwandikishaji kutoa tangazo kwa umma kupitia mbao za matangazo kuhusu pingamizi dhidi ya mtu aliyefariki. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xi) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 28 inaweka masharti ya Uchunguzi na uamuzi wa mapingamizi yanayofanywa na Afisa Mwandikishaji, ibara ndogo ya (8) inazuia Afisa mwandikishaji kuhojiwa kuhusu uhalali wa maamuzi ya pingamizi aliyoyaweka yeye mwenyewe, Kamati ilikuwa na mtizamo kuwa kwa kukiacha kifungu kama kilivyo kinaweza kutumika vibaya na maafisa waandikishaji. Serikali iliieleza Kamati kuwa watafanya maboresho ya ibara hiyo ili kuendana na masharti ya ibara ya 26(2).

(xii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 52 inaweka masharti yanayozuia mgombea wa Ubunge kuteuliwa kwenye nafasi zaidi ya moja, hata hivyo Ibara haijafafanua nafasi zaidi ya moja au nafasi nyingine yoyote ya kuchaguliwa ni ipi. Kamati iliitaka Serikali kufafanua zuio hilo lililenga nafasi ipi, Serikali iliifahamisha Kamati kuwa nafasi iliolengwa ni ya Udiwani na Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xiii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 57 inaweka takwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kutangaza kiti cha Udiwani

wa halmashauri kuwa wazi mara atakapo taarifiwa kwa maandishi na Mwenyekiti wa Halmashauri. Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho kwa kuipa Tume jukumu la kutangaza kiti cha Diwani kuwa wazi baada ya kupokea taarifa rasmi kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayompa wajibu Tume kutangaza kiti cha Diwani kuwa wazi baada ya kupata taarifa rasmi kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

(xiv) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 79 na 84 zinazohusu masharti ya muundo wa karatasi za kura na utaratibu wa kupiga kura mtawalia, Kamati iliishauri Serikali kuongeza aya mpya 79(d) itakayo weka utratibu utakaozingatia watu wasioona ama wenye uwoni hafifu (kwa kuweka karatasi za nukta nundu) kwenye karatasi za kura pamoja na kuweka mfumo ujulikanao kama *tactile ballot templates*. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xv) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 88 inaweka masharti ya kuahirishwa kwa upigaji kura wakati inapotokea vurugu, Kamati ilikuwa na maoni kuwa sababu za kuhairisha zoezi la upigaji kura linaweza kusababishwa na vitu vingine kama vile majanga ya asili tofauti na vurugu au ghasia, lengo ni kuweka wigo mpana wa sababu za kuhairishwa kwa zoezi la upigaji kura. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xvi) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 102 inaweka masharti na wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura, ibara ndogo ya (1)(e) inampa wajibu msimamizi wa kituo kutoa fomu za taarifa za matokeo kwa kila wakala iwapo fomu za taarifa za matokeo zipo za kutosha. Kamati imeshauri iwe ni sharti la lazima kwa msimamizi wa kituo kutoa fomu hizo kwa mawakala na kwamba ahakikishe fomu hizo zinapatikana za kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

(xvii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 112 na 113 inahusu masharti ya Uteuzi wa Wanawake wa viti maalumu kwa nafasi ya Ubunge na Udiwani mtawalia, Kamati ilikuwa na maoni kuwa ni muhimu kuwepo na mfumo mahsusi wa upatikanaji wa Wanawake wa viti maalum utakaotumiwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kuwachagua kwa mujibu wa Ibara ya 81 ya Katiba, kukosekana kwa mfumo mahsusi wa upatikanaji wa wazi kwa Vyama vya Siasa kuteua Wabunge na Madiwani wa Viti Maalum inachochea rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

(xviii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 33, 34, 50 na 62 kwa ujumla zinaweka masharti ya vigezo vya mgombea kuteuliwa, Kamati ilishauri maeneo haya yote yazinagatie usawa wa jinsi na hali ya ulemavu kwenye masharti mahususi ya Ibara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

(xix) **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikuwa na maoni kuwa ni muhimu kuanzisha kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia wakati wa uchaguzi, vitendo vya unyanyasaji wa Kijinsia hasa wakati wa uchaguzi unafifisha jitihada za kitaifa kufikia usawa wa malengo ya uwiano wa 50/50 katika uongozi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwako wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Akcson, Spika wa Bunge la Tanzania kwa kuiamini kamati na kuipa jukumu la kuchambua Muswada huu na Miswada mingine iliyoletwa mbele yako leo, na Mhe. Azzan Zungu Naibu Spika kwa ushirikianao wake wa karibu na kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Utawala katiba na Sheria kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe

20. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga (Mb) Naibu Waziri wa Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Jim Yonazi Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati Ndg. Frank Nkya, Ndg. Ganjatuni Kilemile na Ndg. Ndoh'no William Abel kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Kamati pamoja na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

30 Januari, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama aje awasilishe hoja hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge naomba uridhie maneno ya utangulizi katika Muswada huu kwa kuwa muktadha wake unafanana na maneno ya utangulizi ambayo yameambatana na Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Naomba sasa nijielekeze kwenye maudhui ya Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023, kwa ridhaa yako kama inakupendeza naomba kibali chako.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba maneno ya utangulizi yote, kama yalivyowekwa kwenye utangulizi wa sheria hii yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwasilishe maudhui ya Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2023 kwa lengo la kuainisha masharti mbalimbali kuhusu muundo, majukumu na uedeshaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na masharti yaliyoainishwa katika Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura namba 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura namba 292.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, baadhi ya maeneo ambayo Katiba imeelekeza kuwa, yafafanuliwe katika Sheria itakayotungwa na Bunge bado hayajatungiwa sheria. Maeneo hayo ni pamoja na masharti kuhusu Wajumbe wengine wa Tume, tofauti na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti (Ibara ya 74(1)(c)), nafasi mbalimbali ambazo mtu akishika zinamwondolea sifa ya kuteuliwa kama mjumbe wa Tume (Ibara ya 74(3)(a)), na utaratibu wa uteuzi na majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi (Ibara ya 74(7)). Hivyo, Sheria inayopendekezwa kutungwa itajumuisha masharti yanayotambua Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba na kuainisha masuala mengine muhimu kuhusiana na Tume.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada ni kuwasilisha mapendekezo ya kutunga Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka, 2023. Aidha, Serikali inapendekeza jina la Sheria lifanyiwe marekebisho kwa kuongeza maneno ‘Huru’ baada ya maneno Tume kama inavyobainishwa katika Aya ‘A’ ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tano. Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa, mawanda ya matumizi, utaratibu wa kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya sheria inayopendekezwa.

Aidha, Serikali inapendekeza jina la Sheria lifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno “Tume ya Taifa ya Uchaguzi” na

badala yake kuweka maneno "Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi" kama inavyobainishwa katika Aya B ya Jedwali la Marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na masharti mengine katika sehemu hii ni pamoja na muundo wa Tume, majukumu na sifa za wajumbe wa Tume, muda wa utumishi wa wajumbe, utaratibu wa vikao vya Tume, posho na stahili za wajumbe wa Tume na uhusiano kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vilevile sehemu hii inajumuisha pia masharti kuhusu uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Tume. Kwa mujibu wa Sehemu hii, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watateuliwa na Rais kwa kuzingatia masharti yaliyopo katika ibara ya 74 ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa wajumbe wengine watano utahusisha katika hatua za awali, Kamati ya Usaili ambayo itapokea na kufanya uchambuzi wa maombi ya watu wanaoomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume na kupendekeza majina ya watu wenye sifa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria inayopendekezwa inaweka utaratibu wa Rais kuweza kuunda Kamati ya Uchunguzi endapo ataona inafaa, ambayo itafanya uchunguzi na kumshauri ipasavyo kuhusu kuondolewa kwa wajumbe wa Tume. Aidha, Serikali inapendekeza ibara ya 5 kuhusu uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ifanyiwe marekebisho ili wapendekezwe na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano baada ya mashauriano na Jaji Mkuu wa Zanzibar kama inavyopendekezwa katika Aya F ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inapendekeza ibara ya 9 inayohusu Kamati ya Usaili ifanyiwe marekebisho ili kuipa Kamati

majukumu mawili ambayo ni kupendekeza kwa Mheshimiwa Rais majina matatu kwa ajili ya uteuzi wa Mwenyekiti na majina matatu kwa ajili ya uteuzi wa Makamu Mwenyekiti na Kufanya usaili wa wajumbe watano wa Tume kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ibara hiyo inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumwondoa Mkurugenzi wa Uchaguzi kuwa Katibu wa Kamati hiyo na badala yake kumwezesha Rais kuteua Afisa Mwandamizi katika Utumishi wa Umma kuwa Katibu wa Kamati ya Usaili kama inavyobainishwa katika aya ya kwanza ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali inapendekeza Ibara ya 6 inayohusu posho na stahili za wajumbe wa Tume ifanyiwe marekebisho kueleza bayana kuwa wajumbe wa Tume watalipwa mishahara kama inavyoainishwa katika Aya 'K' ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti kuhusu Sekretarieti ya Tume ya Uchaguzi ambayo inajumuisha Mkurugenzi wa Uchaguzi, watumishi na watendaji wengine wa Tume. Sehemu hii inaainisha sifa za mtu kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, majukumu yake, muundo wa utumishi wa sekretarieti ya Tume pamoja na kuweka takwa la kuzingatia Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa sifa zinazopendekezwa ili mtu aweze kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ni pamoja na kuwa raia wa Tanzania wa kuzaliwa, mtumishi wa umma mwandamizi, mwaminifu na mwadilifu. Sehemu hii inaweka pia masharti kwamba, mtu yeyote ambaye atakuwa anatekeleza majukumu ya Tume atachukuliwa kuwa mtumishi wa Tume kwa kipindi chote atakachokuwa anatekeleza majukumu hayo na atapaswa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu masharti ya fedha yanayojumuisha vyanzo vya fedha za uendeshaji wa Tume, gharama za uendeshaji wa Tume ya uchaguzi, ukaguzi wa hesabu na uwasilishaji wa taarifa za utendaji wa Tume Bungeni. Inapendekezwa kuwa chanzo cha fedha za uendeshaji wa Tume kitokane na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kupitia bajeti ya kila mwaka ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuhusu fedha zitakazotumika na Tume katika uendeshaji wa shughuli za uchaguzi, sehemu hii inapendekeza kuwa fedha hizo zitoke katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Aidha, ilivyo kwa taasisi nyingine za umma zinazoendeshwa kwa bajeti ya Serikali, hesabu za Tume zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu masharti mengine. Ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, inapendekezwa kuipa Tume mamlaka ya kutengeneza kanuni, kuandaa miongozo na kutoa maelekezo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake. Sehemu hii pia inaweka masharti ya mpito kuhusiana na wajumbe wa Tume ambao watakuwa madarakani wakati wa kuanza kutumika kwa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kuwa sheria ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**30 JANUARI, 2024**

**MAELEZO YA MHESHIMIWA JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU) AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZINAZOHUSU VYAMA VYA SIASA WA MWAKA 2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

**2. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tatu (13) wa Bunge la Kumi na Mbili (12), tarehe 10 Novemba, 2023.

**3. Mheshimiwa Spika,** naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa ya kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu.

**4. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa uongozi wake mahiri na shupavu kwa nchi yetu katika nyanja zote. Hakika Mheshimiwa Rais ni Kiongozi mzalendo, mchapakazi na anapenda nchi yetu. Ninamshukuru na kumpongeza sana kwa juhudi kubwa anazofanya za kuboresha demokrasia na mazingira ya kufanya siasa nchini chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa na hivyo kuwaletea Watanzania maendeleo makubwa ya kijamii na kiuchumi.

**5. Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza Demokrasia na kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ilianza kuwekwa wazi mapema tarehe 22 Aprili 2021 alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma. Mheshimiwa Rais aliahidi kudumisha Tunu za Taifa letu yaani Amani, Umoja na Mshikamano. Hata hivyo, alisisitiza nia yake ya kulinda misingi ya Demokrasia na Uhuru wa watu kwa kusema yafuatayo ***"Uhuru na Demokrasia ni Msingi wa Amani katika Nchi na pia husaidia kuchochea maendeleo ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii ".*** Tarehe 01 Julai, 2022 Tanzania iliadhimisha miaka 30 tangu kurejea kwa mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa. Mheshimiwa Rais, alisisitiza tena dhamira yake ya kukuza Demokrasia nchini kupitia Makala aliyoiandaa ambapo alisema ***"Nimedhamiria kwamba, Kwenye kuenzi miaka yetu ya demokrasia ya Vyama Vingi, Serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya Kisiasa, Kiuchumi na Katika Sheria za Uchaguzi ".***

***6. Mheshimiwa Spika**,* ni wakati huo Mheshimiwa Rais alieleza falsafa yake ya kuongoza nchi inayojengwa kwa misingi ya Falsafa ya 'R' 4 ambazo maana yake ni ***Reconciliation, Resilience, Reforms and Rebuild*** ikiwa na maana ya Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi mpya wa Taifa. Falsafa hiyo, inatoa dira na mwongozo wa uongozi katika nchi yetu ili kudumisha amani, mshikamano na umoja wa Kitaifa. Kutokana na dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini matokeo yake ni pamoja na kuundwa kwa Kikosi Kazi ambacho kilifanyia kazi masuala yanayohusu Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini kilichokuja na mapendekezo ya kuboresha mfumo wa demokrasia ambapo matunda ya dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake imeanza kutekelezwa kwa vitendo.

***7. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi kifupi tumeshuhudia Serikali ya Awamu ya Sita ikifanya mageuzi makubwa katika kuimarisha Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini ikiwa ni pamoja na;

i. Kukutana na kufanya mazunumzo na Viongozi wa Kitaifa wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Serikali wastaafu akiwa na lengo la kubadilishana mawazo kuhusu namna bora ya kuboresha na kudumisha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa;

ii. Kuanzisha mazungumzo baina ya Serikali, Chama Tawala (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa lengo la kufikia maridhiano pamoja na kuchukua hatua kadhaa za kushajihisha maridhiano na Chama cha Demokrasia na Maendeleo katika masuala kadhaa muhimu na ya kimsingi yaliyowasilishwa Serikalini na CHADEMA;

iii. Kuruhusu kufanyika kwa mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa Nchini;

iv. Kupitia Baraza la Vyama vya Siasa, amefanikisha na kuliwezesha Baraza la Vyama vya Siasa Nchini kuwa na kifungu maalumu cha bajeti ya kuendesha shughuli za Demokrasia na Vyama vya Siasa na vilevile kufanikisha mikutano mikubwa mitatu (3) ya wadau wa Demokrasia ili kujadili mustakabali wa demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa katika nchi letu;

v. Na leo tunashuhudia kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza mapendekezo ya Kikosi Kazi, Baraza la Vyama vya Siasa Nchini, na Wadau wa Demokrasia kuhakikisha Sheria zinazosimamia Uchaguzi zinawasilishwa Bungeni, tena bila kupitia uwasilishaji wa Sheria kwa Hati ya Dharula ya Rais. Juhudu hizi pamoja na nyingine zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha Utawala Bora na Mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini zinalenga kudumisha na kuboresha maslahi mapana ya Watanzania na Taifa zima kwa ujumla.

**8. Mheshimiwa Spika,** niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuziona hatua hizi ni za kupongezwa na siyo za kubezwa.

**9. Mheshimiwa Spika,** Taasisi mbalimbali duniani kwa kutambua mchango wake mkubwa katika kukuza demokrasia nchini, zimemtunuku tuzo mbalimbali za heshima ikiwa ni pamoja na Tuzo ya Heshima kwa kutambua mchango wake katika kutetea, kulinda na kuimarisha haki za binadamu katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa iliyotolewa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu 2023; tuzo mbili zilizotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Watetezi na Amani ambazo ni tuzo ya amani duniani ya 2022 na tuzo ya Rais wa Dhahabu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo ameweka rekodi ya kuwa Rais mwanamke wa kwanza kuipata Barani Afrika. Kutokana na kazi kubwa aliyoifanya, tarehe 7 Disemba, 2021 alitambulika kimataifa na Jarida maarufu na kubwa duniani la Forbes kuwa ni kati ya wanawake 100 wenye uwezo wa uongozi na ushawishi mkubwa duniani.

**10. Mheshimiwa Spika,** pia, nimshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar** kwa juhudi kubwa anazofanya katika kuleta maendeleo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

**11. Mheshimiwa Spika,** vilevile, nimshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa miongozo na maelekezo yake katika kuhakikisha Serikali inafanikisha mchakato mzima wa Muswada huu. Pia, nimshukuru **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar** na **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu** katika kufanikisha Muswada huu. Pongezi na shukrani za dhati ninaziwasilisha kwa **Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar**

(Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) na Ofisi yake kwa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha mchakato mzima wa Muswada huu.

**12. Mheshimiwa Spika,** kwa dhati, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Mabunge Duniani (Inter Parliamentary Union) na Rais wa kwanza mwanamke kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo. Hii ni fahari na heshima kubwa kwa nchi yetu kwani inaonesha ukuaji wa diplomasia na ni kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi Duniani wanayo juu ya nchi yetu na wewe mwenyewe. Kwa dhati, nikupongeze sna na kukushukuru kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Umeonesha umahili na ubobezi wa hali ya juu.

**13. Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**14. Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu mkubwa nimshukuru sana sana pacha wangu na mshauri wangu wa karibu **Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Wziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),** kwa ushirikianao mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kwani ni mchapa kazi hodari ambaye ana mchango mkubwa sana katika kuhakikisha Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza majukumu yake ipasavyo; **Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu** waliowezesha muswada huu kufikia hatua ya leo.

**15. Mheshimiwa Spika,** nitoe shukrani zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalam wake pamoja na wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

**16. Mheshimiwa Spika,** kipekee na kwa dhati kabisa ninakishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani. Aidha, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano, kukiamini Chama cha Mapinduzi na kumuunga mkono Rais wetumpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika juhudi anazofanya za kuleta maendeleo nchini.

**17. Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbili ambazo ni Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 na Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hizi yanalenga kuimarisha demokrasia, utawala bora na masuala ya kijinsia ndani ya Vyama vya Siasa.

**18. Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinapendekezwa kurekebishwa katika Sehemu zake.

**19. Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo Sheia zinapendekezwa kurekebishwa katika sehemu husika.

**20. Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. Kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuondoa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Wilaya na Afisa Mtendaji Kata na

badala yake ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

**21. Mheshimiwa Spika,** lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinawasilishwa kwa watu sahihi kwa kuwa si mara zote Mkurugenzi wa Halmashauri na Katibu Tawala wa Wilaya wanakuwa wasimamizi wa uchaguzi. Kifungu cha 9 kinarekebishwa kwa kuboresha utaratibu wa kuchukua na kuwasilisha fomu za tamko la gharama za uchaguzi ili fomu hizo zichukuliwe kwa msimamizi wa uchaguzi wakati mtia nia anachukua fomu za kuomba uteuzi na kuwasilishwa wakati wa kurejesha fomu za uteuzi. Lengo la marekebisho haya ni kutoa muda wa kutosha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia taarifa zinazowasilishwa na watia nia kuhusu gharama wanazokusudia kutumia katika uchaguzi kabla hawajaanza shughuli za kampeni.

**22. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka sharti kwa Vyama vya Siasa kuwa na mwongozo wa uchaguzi ndani ya vyama na mfumo wa kuwapata wagombea wake ikiwemo wagombea wa nafasi za Viti Maalumu vya Wabunge na Madiwani wanawake.

**24. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutenganisha muda wa mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kidini na asasi za kiraia kuwasilisha kwa Msajili taarifa za gharama zilizotumika katika shughuli za uchaguzi wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa kuwasilisha taarifa hizo kipindi cha uchaguzi mdogo kwa kuwa kipindi hicho shughuli zinakuwa chache ikilinganishwa na kipindi cha uchaguzi mkuu.

**25. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi wakati wa uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kutenganisha muda wa kuwasilisha taarifa hizo wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo kwa

kuwa chama cha siasa hakiwezi kusubiri miezi sita ndipo kiwasilishe taarifa ya gharama za uchaguzi panapokuwa na uchaguzi mdogo. Aidha, kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kuondoa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu.

**25. Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Tatu linapendezwa kurekebishwa ili kuzingatia masuala ya usawa wa jinsia na ujumuishwaji wa Makundi Maalum.

**26. Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu inapendekeza kurekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuboresha tafsiri ya msamiati "chama cha siasa" na kuongeza tafsiri ya misamiati mingine iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa misamiati iliyotumika katika Sheria inakuwa na maana iliyokusudiwa. Kifungu cha 6A kinapendekezwa kurekebishwa ili kuuwezesha Mkutano Mkuu wa chama cha siasa kukasimisha jukumu lake la kuteua mgombea wa urais wa Zanzibar. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu uteuzi wa mgombea wa urais wa Zanzibar kufanywa na Halmashauri Kuu ya chama.

**26. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6C kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka adhabu kwa chama cha siasa kitakachomruhusu mtu ambaye si raia wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya chama husika. Lengo la marekebisho ni kukomesha vitendo vya watu wasio raia kuingilia katika maamuzi ya vyama vya siasa kwa kuwa kwa sasa Sheria inaweka katazo lakini hakuna adhabu. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 11** ifanyiwe marekebisho ili kuweka ukomo wa chini wa adhabu inayopendekezwa kwa kosa husika kama inavyobainishwa katika **Aya 'A'** ya Jedwali la Marekebisho. Pia, Serikali inapendekeza kuongeza masharti mapya katika Muswada kwa lengo la kuondoa jinai kwenye makosa ya jumla kama inavyobainishwa katika **Aya 'B' na 'D'** ya Jedwali la Marekebisho.

**28. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka takwa kwa chama cha siasa kuwasilisha nakala ya kanuni zake wakati wa maombi ya usajili wa muda. Lengo la marekebisho haya ni kumpa Msajili fursa ya kujiridhisha endapo kanuni hizo zimezingatia masharti ya Sheria. Kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kuweka masharti ka Chama cha Siasa kutoruhusu wanachama wake kufanya kitendo chochote kinachohatarisha usalama wa nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa vyama vya siasa vinavyosajiliwa ni vile vinavyozingatia sheria, kanuni na taratibu mbalimbali kwa maslahi mapana ya nchi.

**29**. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu kipya cha 10C kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha nyaraka ambazo chama cha siasa kinapaswa kuwa nazo wakati wote. Miongoni mwa nyaraka hizo ni sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalumu, kanuni za fedha na usimamizi wa mali za Chama na kanuni za uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi wa Chama. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa Chama cha Siasa kinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, utawala bora, jinsia na kanuni kilizojiwekea.

**30. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha kuwa maandamano ya vyama vya siasa yatafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 322. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya kifungu cha 11 na masharti ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi ambayo imeainisha utaratibu wa kuzingatiwa kabla na wakati wa kufanya maandamano au mikutano ya hadhara. Kifungu cha 11A kinarekebishwa ili kuviruhusu vyama kushirikiana hata wakati wa uchaguzi mdogo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika Sheria.

**31. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 13A kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa pale anapogundua kuwa mtu mwingine ametenda kosa au anakusudia kutenda kosa lolote chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utendaji

wa makosa na kuhakikisha hatua zinachukuliwa dhidi ya mtu anayekiuka masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kumlinda mtoa taarifa.

**32. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sharti kuwa mgawanyo wa ruzuku utafanywa kwa kuzingatia pia matokeo ya uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu fedha za ruzuku kugawanywa kwa vyama vya siasa kwa kuzingatia idadi ya kura za ubunge na idadi ya wabunge na madiwani ambao chama cha siasa kinao kwa wakati husika badala ya kura za ubunge na idadi ya wabunge na madiwani ambao chama kilipata wakati wa uchaguzi mkuu pekee.

**33. Mheshimiwa Spika,** Vifungu vya 19, 20 na 21E vinapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha masharti kuhusu kusitishwa au kufutwa kwa usajili wa chama cha siasa na zuio kwa mwanachama kushiriki katika shughuli za siasa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa masharti ya vifungu hivyo yanaakisi maana iliyokusudiwa.

**34. Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Tatu linapendekezwa kuongezwa ili kuainisha masuala ambayo chama cha siasa kitapaswa kujumuisha katika sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ushiriki wa wanawake na makundi maalumu katika shughuli za siasa ndani ya vyama vya siasa. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya ibara ya 21 ya Muswada kwa lengo la kuvitaka Vyama vya Siasa kuweka katika Sera zao za jinsia na ujumishi wa makundi maalum tamko kuhusu uzingatiaji wa jinsia katika mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya Vyama kama inavyoainishwa kwenye Aya ‘E’ ya Jedwali la Marekebisho.

**35. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

**36. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Jenista Joakim Mhagama (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(SERA BUNGE NA URATIBU)**
**30 Januari, 2024**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, nawashukuru sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria. Kwa niaba yake, anakuja Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo. *(Makofi)*

**MHE. FLORENT L. KYOMBO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi *(The Proposed Electoral Commission Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 kifungu kidogo cha (5) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tatu, Kikao cha Kumi kwenye Bunge la 12, tarehe 10 Novemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi, kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha

Bunge lako tukufu kwamba Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, hadidu za rejea. Kwa kuwa hadidu za rejea hizi ni sawa na zile ambazo amewakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge katika Muswada aliousoma hapa mbele yako hivi punde, naomba kwa ruhusa yako hadidu za rejea za Muswada huu ziingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha wa Muswada huu. Umekusudia kuleta mapinduzi *(reforms)* za kisheria na kimfumo katika uchaguzi ili kupanua demokrasia nchini na kuongeza uhuru wa Tume ya Uchaguzi, kuboresha usimamizi wa uchaguzi na kuongeza ushiriki *(inclusion)* wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye uchaguzi. Muswada huu wa Sheria imekusudia kufanya mfumo wetu wa uchaguzi kuwa jumuishi zaidi na wa wazi zaidi, wa haki zaidi, na wenye usawa zaidi.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada huo. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 05 Januari 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliotumika kupokea maoni ya wadau ambayo katika kifungu 1.1.2 mpaka 1.2.2 katika ukurasa wa 4 na 6, naomba kwa ruhusa yako iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kwa kuwa ni sawa na ule aliowasilisha Mwenyekiti wa Kamati katika Taarifa aliyosoma hivi punde mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua ya kupokea maoni, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 25 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Mwenyekiti alizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati ilikamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati inakutana na wadau hoja 38 ziliibuliwa na wadau mbalimbali kama zinavyoonesha katika majedwali ambazo zinaanzia ukurasa wa 8 hadi wa 37 naomba. Kwa ruhusa yako, majedwali hayo yapokelewe katika Taarifa Rasmi za Bunge kwa ajili ya rejea.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa hoja hizo, pamoja na maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Kamati ilibaini changamoto na upungufu katika Muswada. Baadhi ya changamoto zilizobainika utatuzi wake unahitaji mabadiliko ya sheria nyingine ambazo hazikuwa zinafanyiwa kazi na Kamati katika muda huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 2023 *(The Proposed Electoral Commission Bill, 2023)* ukiwa umegawanyika katika sehemu kuu tano na zenye jumla ya ibara 28, ambao unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambao unalenga kuanzisha Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kubainisha muundo wa Tume na kuainisha majukumu ya Tume na taratibu nyingine za uendeshaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii Muswada unapendekeza kuwepo kwa utaratibu wa usaili wa nafasi za Wajumbe wengine watano wa Tume. Pia sehemu hii inampa mamlaka Rais, kuunda kamati ya uchunguzi ambayo itakuwa na jukumu la kufanya uchunguzi na kumshauri Rais iwapo litatokea suala la mjumbe kuondolewa katika nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inaanzisha Sekretarieti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuweka nafasi ya Mkurugenzi wa Uchaguuzi na Sifa za mtu anayestahili kuteuliwa katika nafasi hiyo na majukumu yake. Pia inaweka nafasi ya watumishi na watendaji wengine wa Tume na kuweka sharti kwao kuwa watachukuliwa kama watumishi wa Tume kwa kipindi chote watakapokuwa wakitekeleza majukumu ya Tume na kwamba watapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya sheria taratibu na kanuni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu Vyanzo vya Mapato ya Tume ambayo yatatokana na bajeti ya Serikali na masharti ya matumizi ya fedha za uendeshaji wa tume kutoka kwenye mfuko mkuu wa hazina ya Serikali. Vilevile sehemu hii inamtaka Mkurugenzi wa Uchaguzi kutunza vitabu vya hesabu vitakavyohusiana na tume na kuandaa taarifa ya hesabu za mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma ambazo zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Umma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada huu inahusisha Masharti mengine ambayo inapendekeza tume kupata mamlaka ya kutengeneza kanuni, miongozo na maelekezo mbalimbali yatakayoiwezesha tume kutekeleza majukumu yake kwa ubora na ufanisi. Aidha, sehemu hii inapendekeza kuwepo kwa masharti ya mpito ambayo yanamtaka mtu yeyote atakayeshika nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume kushika nafasi hiyo hadi ujumbe wake utakapokoma.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, kwa kiasi kikubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, kamati inayo maoni ya jumla na mapendekezo mahsusi ambayo yakizingatiwa yatarahisisha mchakato wa utekelezaji wa sheria hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Jina Refu. Hadhi ya tume katika Katiba, Ibara ya 77(7) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kwamba, Tume ni Idara Huru itakayotekeleza majukumu yake bila kuingiliwa na mtu yoyote au taasisi yoyote. Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho ya jina la tume, ili kuendana na masharti yaliyopo, Serikali ilikuwa na maoni kuwa kuongeza neno huru kwenye jina la sheria ni kubadili maudhui ya jina lililopo linalotokana na Ibara ya 74(1) ya Katiba inayotambua kwamba, tume itakuwa ni Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa matumizi ya neno HURU hayakinzani na matakwa ya Katiba kwa kuwa, Katiba haijaelekeza jina rasmi la kutumika na tume kama ambavyo Katiba imeelekeza majina ya kutumia kwenye uwanzishaji wa taasisi mbalimbali za Kikatiba mfano Ibara ya 112(1) wakati wa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Mahakama na Ibara ya 129(1) katika kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977. Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayopendekeza jina “Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi” litumike popote ilipotumika jina “Tume ya Taifa ya Uchaguzi”.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho Katika Ibara ya 5 na Ibara ya 10 ya Muswada. Masharti yaliyopo katika Ibara ya 5 ya Muswada yanazungumzia Muundo wa Tume ambao ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe watano ambao watateuliwa na Rais na Ibara ya 10 inahusu uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kuwa, masharti yaliyopo katika Ibara ya 5 na Ibara ya 10 yanafanana kimantiki na kuwa, yote yanahusu uteuzi wa Wajumbe wa Tume na kuapishwa kabla ya kushika Madaraka. Hivyo, Kamati ilishauri kuunganishwa kwa vifungu hivyo, ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali mapendekezo na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati kuhusiana na mpangilio wa ibara hizo.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Ibara ya 7 ya Muswada. Ibara ya 7 ya Muswada inahusu Sifa za Wajumbe wa Tume na Ibara ya 7(2)(d) Kamati ilishauri iainishe sifa ambazo zinakusudiwa kuongezwa. Aidha, Ibara ya 7(2)(a) inafanya rejea ya Sheria ya Uraia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kuwa jukumu la kuainisha sifa za Wajumbe wa Tume ibaki kwa Bunge pekee. Aidha, kamati iliishauri Serikali iandike Sura ya Sheria inayoyerejewa kwenye maelezo ya pembeni *(Marginal Note)* ya Ibara Ndogo ya 7(2)(a). Na tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Ibara ya 8 ya Muswada. Ibara ya 8(2)(e)(ii) ya Muswada imeweka sharti la maneno "tabia mbaya" kuwa ni miongoni mwa sababu zinazosababisha Mjumbe wa Tume kuondolewa katika nafasi yake. Kamati iliona matumizi ya maneno "tabia mbaya" yana tafsiri pana, hivyo Kamati iliona ni muhimu yakawekewa tafsiri.

Mheshimiwa Spika kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati linalofafanua matumizi ya maneno "tabia mbaya" kwa muktadha wa ibara hii.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Ibara ya 9 ya Muswada. Ibara 9(3) ya Muswada imemtaja Mkurugenzi wa Uchaguzi kuwa ndiye atakuwa Katibu wa Kamati ya Usaili wa Wajumbe wa Tume. Ibara ya 18(1) ya Muswada imeeleza kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa masharti ya upatikanaji wa Mkurugenzi wa Tume yanafuata baada ya kuwepo kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa msingi huo Kamati ilishauri Mkurugenzi wa Uchaguzi asiwe Katibu wa Kamati ya Usaili na badala yake atafutwe mtu mwingine miongoni mwa Watumishi wa Umma waandamizi kwa cheo chake ama sifa alizonazo.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Ibara ya 16(2) cha Muswada. Maudhui ya ibara hii yanaeleza kwamba, Wajumbe wa Tume watalipwa kiinua mgongo baada ya kumaliza kuhudumu nafasi za Ujumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, katika ibara hii Kamati ilitaka Serikali kuweka wazi kuwa, Wajumbe wa Tume watalipwa kwanza mishahara, ili wastahili kulipwa kiinua mgongo na kama ambavyo inavyopaswa kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho ya kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ibara ya 11 ya Muswada. Ibara ya 11 ya Muswada inaeleza majukumu ya tume kuwa yatahusiana na uratibu na usimamizi wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Sheria haijajumuisha mapendekezo na maoni ya wadau ya kuitaka

tume iwe ndicho chombo pekee cha usimamizi wa uchaguzi nchini, ikiwemo usimamizi wa chaguzi za Serikali za Vijiji, Vitongoji na Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ibara hii, serikali ilieleza kuwa uchaguzi wa Serikali za Vijiji, Mitaa na Vitongoji unfanyika mwaka huu (2024) na tayari maandalizi yamekwisha fanyika kwa hiyo, itakuwa vigumu kwa sasa kubadili majukumu ya usimamizi wa uchaguzi huu. Na kwamba, inaendelea kufanya utafiti juu ya namna bora ya kusimamia uchaguzi huo kwa siku za usoni. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato huo utakao wezesha kuwa na chombo kimoja pekee cha kusimamia chaguzi zote nchini, ikiwemo uchaguzi wa Serikali za Vijiji, Mitaa na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu, ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba orodha ya majina ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu. Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Dkt. Jim Yonazi Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa pekee, Sekretarieti ya Kamati Ndugu Frank

Nkya, Ndugu Ganjatuni Kilemile na Ndugu Ndoh'no William Abel kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja. Baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali, kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Kamati pamoja na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2023 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1** Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**1.1.1** Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na tatu, kikao cha kumi kwenye Bunge la 12, tarehe 10 Novemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala,

Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.1.2 Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa msingi wa Miswada hii ni Falsafa ya 4R za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambazo ni Maridhiano (*Reconciliation*), Ustahimilivu (*Resiliency*), Mabadiliko (*Reforms*) na Kujenga upya (*Rebulding*).

**Mheshimiwa Spika**, Falsafa hizi ni mkakati mahususi wa uongozi wa Rais unaolenga kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi nchini, kwa kufungua milango ya mazungumzo na wadau mbalimbali wa kisiasa, kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia na sekta binafsi. Aidha, Falsafa hii inalenga **kupitia upya sera na sheria** zinazohusu masuala muhimu kama vile siasa, afya, elimu, uwekezaji, biashara, usalama ikiwa ni pamoja na kujenga uhusiano mzuri na nchi jirani, wadau wa maendeleo na jumuiya za kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati serikali ikiwasilisha miswada hii kwa kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala Katiba na Sheria, ilieleza kuwa **maudhui** ya Miswada yanatokana na Taarifa ya Kikosi Kazi kilicho undwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini. Aidha, maudhui mengine yametokana na mijadala mbalimbali kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini iliyofanyika mara kwa mara kupitia Jukwaa la Vyama Siasa na Kituo Cha Demokrasia Tanzania (Tanzania Centre for Democracy -TCD). Kwa muktadha huo, sheria hizi zimekusudia kutoa majawabu ya baadhi ya hoja zilizo jitokeza kwenye Taarifa ya Kikosi Kazi na kwenye Mijadala mbalimbali ya Siasa na Demokrasia nchini, kupitia jukwaa la Vyama vya Siasa na TCD.

**Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huo, miswada hii mitatu inakusudia kuleta mapinduzi (reforms) za kisheria na kimfumo katika uchaguzi ili kupanua demokrasia nchini kwa kuongeza uhuru wa Tume ya Uchaguzi, Kuboresha usimamizi wa Uchaguzi na kuongeza ushiriki (inclusion) wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye uchaguzi. Miswada hii ya Sheria imekusudia kufanya Mfumo wetu wa Uchaguzi kuwa **jumuishi zaidi** na wa **wazi zaidi, haki zaidi, na wenye usawa zaidi**.

### 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 5 Januari, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

#### 1.2.1 Upokeaji wa maoni ya Wadau

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) na 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano ya kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearings*) kwa siku nne kuanzia tarehe 6, 8 hadi 10 Januari, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Miswada minne iliyofanyiwa kazi na Kamati hii, ambayo ni: -

a) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, wabunge na Madiwani wa mwaka 2023;

b) Muswada wa Sheria wa tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023;

c) Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa Mwaka 2023 [*The Political Parties Affairs Laws* (*Amendments) Bill, 2023*]; na

d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws* (*Miscellaneous Amendments*) *Bill, 2023*].

### 1.2.2 Namna Kamati ilivyoendesha vikao vya upokeaji wa maoni (*Public hearings*)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata heshima ya kupokea watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao walijitokeza na kutenga muda wao kwa ajili ya jambo hili la maana kubwa kwa taifa letu, Kamati ilihakikisha kuwa kila sauti ilipewa nafasi yakusikilizwa kwa dhamira ya kuhakikisha Sheria tunazokusudia kuzitunga kwa niaba ya Watanzania zinawakilisha maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kusikiliza, kujifunza na kuyachukua maoni ya wadau wote kwa uzito unaostahili, kwa lengo la kufikia maamuzi ambayo yataleta mabadiliko chanya katika Miswada iliopo mbele yetu. Kwa muktadha huo, Kamati ilitenga muda wa dakika thelathini kwa taasisi za Kidini kutoa maoni na nasaha kuhusu Miswada, dakika ishirini kwa vyama vya siasa, dakika kumi kwa taasisi na asasi za kiraia na dakika tano kwa wachangiaji binafsi. Hata hivyo, kwa wale ambao hawakuweza kumaliza michango yao kwa muda uliopangwa, Kamati iliwasihi kuwasilisha michango yao kwa maandishi ili iweze kufanyiwa kazi na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuboresha Miswada iliyofanyiwa kazi na Kamati na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) - Ujumbe ulioongozwa na Mhasham Baba Askofu Jude Thaddeus Rwaichi;

2. Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) – Ujumbe ulioongozwa na Askofu Dkt. Fredrick Shoo aliyekuwa Mkuu wa Kanisa la Kilutheri Tanzania na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania;

3. Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania - Ujumbe ulioongozwa Sheikh Mussa Yusuph Kundecha;

4. Taasisi na Asasi za Kiraia 31 zilizoshiriki kwenye majadiliano na zingine zaidi ya 400 zilizowakilishwa na zilizotuma kwa maandishi maoni na mapendekezo yao; pamoja na

5. Wadau binafsi zaidi ya 1,700 waliopata fursa ya kushiriki katika mikutano ya kupokea maoni kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 25 Januari, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023 ukiwa umegawanyika katika sura tisa. katika hatua ya kwanza ya uchambuzi, kamati ilijielekeza kubaini kama **maudhui ya miswada hii yanakidhi matakwa ya falsafa ya R4, Taarifa ya Kikosi Kazi cha Rais, na hoja mbalimbali zilizo jitokeza wakati wa mijadala mbalimbali kupitia Jukwaa la Vyama Vya Siasa na TCD**.

Sheria hii inakusudia kuweka masharti ya kusimamia Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kufuta Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 1979 pamoja na kuweka masharti mengine kadhaa kuhusu chaguzi hizo na matokeo ya kufutwa kwa Sheria zinazohusika. Lengo ni kuunganisha Sheria za Uchaguzi ili kukusanya pamoja masharti yanayofanana kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji na usimamizi wake.

## 2.2 Upembuzi wa Maudhui ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Katika Sheria inayopendekezwa yapo mambo makuu yanayojenga maudhui ya Sheria hii. Mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Daftari la Kudumu la Wapiga Kura *(Permanent Voter Register - PVR)*

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imempa raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka kumi na minane haki ya kupiga kura katika Uchaguzi unaofanywa Tanzania na Wananchi. Masharti ya kutumia haki hii yanaongozwa na Sheria iliyotungwa na Bunge inayoweka masharti kuhusu Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni Kitabu kinachotunzia Kumbukumbu kuhusu wapiga kura. Bunge lilitunga Sheria mbili zinazoanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Sheria hizo ni: Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292. Daftari lililoanzishwa na Sheria hizo liliandaliwa mwaka 2004 na kuanza kutumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Kwa mujibu wa Sheria hizo Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linapaswa kuboreshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na Mwingine.

**Mheshimia Spika**, Sheria inayopendekezwa inaendelea kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kama ilivyoelekezwa katika Ibara

ya 5(3) (a) ya Katiba. Kwa Sheria hii, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, itaendelea kuamua kuhusu sehemu, Sura au mgawanyo mwingine katika Muundo wa Daftari. Mkurungenzi wa Uchaguzi anaendelea kuwa na wajibu wa kuweka, kutunza na kuboresha Daftari hilo kwa mujibu wa Sheria.

**2.2.2 Mawanda ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** Mawanda ya matumizi ya Sheria yanasaidia kuzingatia muktadha wa maudhui na masharti ya Sheria inayohusika. Kwa sasa, masuala ya uchaguzi yapo chini ya Sheria mbili tofauti zilizotofautina mawanda ya matumizi. Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 inatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na Sheria ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa inatumika Tanzania Bara. Sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Zanzibar kwa uchaguzi wa Rais wa Jamhuri wa Muungano na Wabunge na itatumika Tanzania Bara kwa uchaguzi Rais, Wabunge na Madiwani. Kwa msingi huo masharti ya Sheria hiyo yanahitaji kuangaliwa kwa muktadha (context) tofauti. Muktadha wa masharti yanayohusu uchaguzi wa Rais na Wabunge ni Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, lakini muktadha wa masharti ya uchaguzi wa madiwani ni Tanzania Bara.

**2.2.3 Uandikishaji wa wapiga kura**

**Mheshimiwa Spika,** Uandikishaji wa wapiga kura ni unukuzi na utunzaji wa taarifa za Mpiga kura kwa kuorodhesha taarifa hizo kwenye Kitabu cha kudumu cha Wapiga kura. Kufanya hivyo, ni jambo linalofanikisha utaratibu wa raia kutumia haki yao ya kupiga kura pamoja na kuzingatia misingi ya uchaguzi wa kidemokrasia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa, vigezo, masharti na taratibu za pingamizi kwa wapiga kura wanaoandikishwa vimebainishwa katika sheria mbili: Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Sheria inayopendekezwa imejumuisha na kufafanua mambo hayo katika Sheria moja badala ya kuwa katika Sheria mbili tofauti. Lengo la kufanya hivyo ni kuendeleza msingi wa

uchaguzi huru na wa haki ikiwemo kujenga Imani ya wapiga Kura na Vyama vya Siasa kwa utaratibu wa Usajili wa Wapiga Kura.

### 2.2.4 Mambo Mengine Muhimu

**Mheshimiwa Spika,** Mambo mengine muhimu katika Sheria inayopendekezwa yanaendelea kuwa kama ilivyo kwa sasa. Mambo hayo ni: -

(i) Utaratibu wa uteuzi wa mawakala katika mchakato wa uchaguzi;

(ii) Utaratibu na masharti ya kupiga Kura kwa aliyeandikishwa kupiga Kura;

(iii) Utaratibu, sifa na vigezo vya uteuzi wa Wabunge wa Viti Maalumu;

(iv) Uteuzi wa Maafisa, waandikishaji, Wasimamizi wa Uchaguzi, wagombea na watendaji wengine;

(v) Masharti ya kupinga uchaguzi wa Wabunge na Madiwani

(vi) Mamlaka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuandaa Kanuni' maelekezo na notisi; na

(vii) Makosa yanayotokana na ukiukwaji wa masharti ya sheria inayopendekezwa.

## 2.3 Hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wadau

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Kamati ilipokutana na Wadau hoja 58 ziliibuliwa na Wadau kama ifuatavyo: -

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **1.** | CHADEMA, TEC, CCT, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL. | | **CHADEMA:** Jina la Muswada lisomeke: Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji.<br><br>**TEC:** Sheria haijajumuisha mapendekezo na maoni ya wadau ya kuitaka Tume iwe na Mamlaka ya Kusimamia chaguzi zote ikiwemo wa serikali za mitaa.<br><br>**CCT:** Sheria haijajumuisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Sheria ijumuishe uchaguzi huo ili Tume isimamie uchaguzi huo.<br><br>TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL: Jina la Sheria liwe Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na isiminye kuwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Lengo la marekebisho haya ni Tume iweze kusimamia chaguzi zote. |
| **2.** | TGNP, TAMWA, ZAFELA na | Ibara ya 3 | **TGNP:** Tafsiri za Maneno au dhana za ya Kijinsia zilizotumika hazijawekwa katika kifungu cha 3 Cha Muswada. Kuongezea baadhi ya maneno na tafsiri |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | WILDAF | | zake kama Jinsi, Jinsia, Usawa wa kijinsia, Rushwa ya ngono, Ubaguzi, sera jumuishi.<br><br>**WILDAF**: Sheria iongeze tafsiri za maneno Jinsi, jinsia, ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi, ulemavu na usawa. Lengo la marekebisho haya Kuepusha matumizi kinzani ya maneno hayo. |
| **3.** | CCT, ACT WAZALENDO, CHADEMA | Ibara ya 5 | CCT: Sheria iweke idadi ya ukomo wa majimbo.<br><br>ACT WAZALENDO: sheria haijasema jinsi gani majimbo yanaundwa.<br><br>CHADEMA: Kifungu cha 5 hakijaweza kuondoa changamoto ya uundwaji wa Majimbo ya uchaguzi kwa kutumia kigezo cha uwiano wa idadi ya watu *(population quota)*.<br><br>Bado hakuna fursa ya kuhoji maamuzi ya Tume kwenye mgawanyo wa Majimbo Mahakamani hata kama kuna mapungufu au kutokuridhika na mgawanyo uliofanywa na Tume. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Kwa kifungu kilivyo bado tatizo la kuundwa kwa majimbo ya uchaguzi kwa upendeleo au sababu za kisiasa kupendelea Chama kilichopo madaralani halijapata suluhisho *(Gerrymandering)*.<br><br>Bado mamlaka ya mwisho ya kuidhinisha mipaka na mgawanyo wa majimbo ya Uchaguzi yameachwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa CCM ambaye anaweza kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais. |
| **4.** | ACT WAZALENDO, CHADEMA, WILDAF, ADC, UDSOL, CHACHA WANGWE, ABDUL NONDO, YOSEFA KOMBA TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII | Ibara ya 6 | **ACT WAZALENDO**: Vifungu hivi Virekebishwe badala yake Tume iteue wasimamizi wa uchaguzi na sifa ziwekwe ikiwemo kutoshiriki katika mchakato wowote wa kisiasa.<br>Lengo la marekebisho haya ni Wakurugenzi wa sasa ni wanasiasa walioshindwa uchaguzi wakateuliwa kuwa wakurugenzi. Hivyo wakisimamia uchaguzi wataleta mgongano wa kimaslahi.<br>Kukuza uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br><br>Wakurugenzi ni wateule wa Rais.<br><br>Kifungu hiki kiandikwe upya na kusomeka:<br>6 (1) Kwa madhumuni ya uchaguzi utakaofanyika |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | FORUMS, CSL, CCT, TEC, NGOME YA VIJANA ACT WAZALENDO, JUMUIYA YA VIJANA CUF, VIJANA NCCR-MAGEUZI, ZAFELA, CCM | | chini ya sheria hii Tume ya Uchaguzi itateua Wasimamizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata na msimamizi huyo wa uchaguzi anaweza kuwa msimamizi wa uchaguzi kwa jimbo zaidi ya moja.<br><br>Kifungu 6 (2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kuteua kwa kuzingatia nafasi aliyonayo mtu katika ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa watumishi wa umma au Mtanzania yeyote wenye sifa sawa zitakazotajwa katika kifungu cha 6(4) cha Sheria hii idadi ya wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata.<br><br>(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1)<br>na (2), Tume inaweza, pale ambapo mazingira yatahitaji na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali,<br>kuteua mtu yeyote kutoka katika ofisi ya umma au Mtanzania mwengine yeyote mwenye sifa zitakazotajwa na Sheria hii kwa jina au kwa nafasi yake kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | msaidizi wa uchaguzi katika jimbo au kata yoyote.<br><br>6 (4) Msimamizi wa uchaguzi atakuwa na sifa zifuatazo;<br>1. Awe raia wa Tanzania.<br>2. Mwaminifu na mwadilifu<br>3. Uzoefu katika uchaguzi.<br>4. Asiwe mwanachama wa au kufungamana na chama chochote cha siasa.<br>5. Asiwe amewahi kushiriki mchakato wowowte wa Kisiasa<br>6. Awe na kiwango cha elimu. kisichopungua astashahada<br>7. Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai ikiwemo unyanyasaji wa makosa ya kijinsia,kukwepa kodi, ugaidi<br>8. Awe amekula kiapo cha kuheshimu Sheria ya Utumishi wa Umma kuhusu makatazo ya watumishi wa umma kushiriki kwenye Vyama vya siasa.<br><br>Lengo la marekebisho haya ni Wakurugenzi wa sasa ni wanasiasa walioshindwa uchaguzi wakateuliwa kuwa wakurugenzi. Hivyo wakisimamia uchaguzi wataleta mgongano wa kimaslahi. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Kukuza uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br><br>Wakurugenzi ni wateule wa Rais.<br><br>Kukuza usawa wa kijinsi na kukuza ushirikishwaji wa vijana.<br><br>Kuchochea utendaji haki.<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 6(1) kinawarudisha Wakurugenzi ambao ni wateule wa Rais, waliopo chini ya Waziri wa TAMISEMI kuwa wasimamizi wa uchaguzi ambapo Wasimamizi hao wanaweza kupokea maelekezo ya Rais, Waziri wa TAMISEMI na Tume ya Uchaguzi. Hakuna maelezo kwamba ni maelekezo gani yatatamalaki ikiwa maelekezo hayo yanakinzana.<br><br>Kifungu cha 6(1) na 6(2) vifutwe ili kuruhusu kifungu cha 6(3) kuwa kifungu mama (main provision) kuhusu uteuzi wa Wasimamizi wa uchaguzi.<br><br>**WILDAF**: Kifungu cha 6 kiweke utaratibu wenye misingi ya kupata uwiano sawa wa ujumuishwaji wa |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | jinsia na makundi maalumu katika kuwapata wasimamizi na watendaji wa uchaguzi watakaoajiriwa na Tume ya Uchaguzi na sio wenye nafasi za Ukurugenzi wa Jiji, Ukurugenzi wa Manispaa, Ukurugenzi wa Mji na Ukurugenzi wa Wilaya, au watumishi wengine wa umma.<br><br>**ADC**: Wakurugenzi wasiwe wasimamizi wa uchaguzi.<br><br>**DEUS KIBAMBA:** Wasimamizi wa uchaguzi wachaguliwe kwa kuzingatia jinsi, vijana na makundi maalumu.<br><br>**CHACHA WANGWE:** Wakurugenzi wasiwe wasimamizi wa uchaguzi.<br><br>**TGNP:** Kifungu hiki hakijabainisha sifa za mtu kuteuliwa kuhudumu kama msimamizi wa uchaguzi au mtendaji wa tume, pia hakijabainisha utaratibu na namna ya uteuzi na pia hakijazingatia usawa wa Jinsia.<br><br>**MAMBO J. MAMBO:** Tume iajiri wasimamizi wa uchaguzi wa wilaya. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS na CSL:** kuendana na mapendekezo ya ripoti mbalimbali za uchaguzi, ikiwemo Taarifa ya Tume ya Uchaguzi kuhusu Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, 2020. Tunapendekeza kuwa Tume kuwa na watumishi wake wa kudumu au wa muda.<br><br>**CCT**: Kifungu kiboreshwe au kiondolewe, tume iajiri watendaji wake wenyewe wafanyiwe usaili wa wazi.<br><br>**TEC:** Hawakubaliani na Wakurugenzi wa Halmashauri na watumishi wa umma kusimamia uchaguzi kwa kuwa hawawajibiki kwa tume ya uchaguzi bali wanawajibika kwa Rais na Chama Tawala hivyo wanakosa sifa ya kuwa mamlaka ya uchaguzi huru na haki. Vifungu hivyo vifutwe na Tume iajiri watumishi wake wenyewe.<br><br>**CCM**: ingawa Mahakama imeruhusu wakurugenzi kuwa wasimamizi wa uchaguzi, watendaji hao sio lazima sheria iwataje wazi wazi. |
| **5.** | CCT,<br>CHADEMA,<br>ZAFELA, | Ibara ya 7 | **CCT:** Sifa ya Maafisa Waandikishaji kutokujihusisha na siasa iongezwe. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | WILDAF, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL | | **CHADEMA:** Kifungu cha 7(3) kiwe kifungu mama na kifungu cha 7(1) na 7(2) vifutwe ili kuwaondoa Wakurugenzi wa Halmashauri kuwa Maafisa Waandikishaji wa Wapiga Kura.<br><br>Kiongezwe kifungu kidogo kitakacholazimu Mratibu wa uchaguzi wa Mkoa kuapa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi na kutoa tamko la kujitoa au kutokuwa Mwanachama wa Chama cha siasa.<br><br>Kiongezwe kifungu kidogo kingine kinachoipa Tume kiteua Mratibu wa uchaguzi wa Mkoa kuliko kulazimisha kutumia Makatibu Tawala wa Mikoa.<br><br>Kuwe na kifungu kidogo kitakachotoa masharti kwa Tume kuchapisha orodha ya majina na namba zao za simu ya Waratibu wa uchaguzi wa mikoa na vituo vyao vya kazi.<br><br>**ZAFELA**: Tume iajiri wafanyakazi wake kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na sio kutumia watu wenye nafasi za ukurugenzi wa jiji, manispaa, Mji, Wilaya au watumishi wengine wa kuwa maafisa waandikishaji. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL**: Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke;<br>Afisa mwandikishaji Mkuu wa wapiga kura wa Jimbo kwa kuzingatia maelekezo<br>ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi atafanya kazi<br>yake na watumishi chini yake waliopatikana kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br><br>Kwa ajili ya upigaji kura kwa watanzania walioko nje ya nchi, ubalozi wa Tanzania katika nchi husika utakuwa kituo cha uandikishaji wapiga kura, na kwamba Tume itateua mtu mwenye sifa kuwa afisa mwandiksihaji wa wapiga kura katika kituo hicho. |
| **6.** | TAMWA, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL | Ibara ya 8 | Kifungu 8 (4) kinaweka uwezekano wa kuwa na mwakilishi mmoja tu mwanamke katika Kamati ya uchunguzi, ili hali uteuzi wa Kamati ya Uchunguzi unaweza kuzingatia usawa wa kijinsia.<br><br>Kifungu 8 (4) kiseme wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi watakaoteliwa na Rais watateuliwa kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Kifungu 8 (4) kiseme 'Kamati iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (3) itajumuisha wajumbe wafuatao kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL**: Hakuna mfumo shindanishi wa upatikaji wa waratibu wa uchaguzi.<br><br>Tume itateua maafisa wake katika ngazi zote kuwa Waratibu wa uchaguzi katika ngazi hizo wakati wa uchaguzi kwa ajili ya kuratibu taarifa, upatikanaji wa vifaa, rasilimali na masuala mengine muhimu kwa ajili ya kuendesha uchaguzi kwa ufanisi katika majimbo ya uchaguzi na kata katika mkoa husika.<br><br>Kwa ajili ya upigaji kura kwa watanzania walioko nje ya nchi, ubalozi wa Tanzania katika nchi husika utakuwa kituo cha uandikishaji wapiga kura, na kwamba Tume itateua mtu mwenye sifa kuwa afisa mwandiksihaji wa wapiga kura katika kituo hicho. Kwa madhumuni ya upigaji kura kwa wafungwa walioko gerezani, gereza husika litakuwa kituo cha uandikishaji na upigaji<br>kura. |
| **7.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, | Ibara 9 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, na CSL**: Kuondoka neno sheria<br>nyingine yoyote na kifungu kisomeke;<br>Mtu yeyote ambaye ni raia wa Tanzania aliyetimiza |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | KITUO CHA TAARIFA KWA WANANCHI, na USHIRIKI TANZANIA COALITION | | umri wa miaka kumi na nane na ambaye hajapoteza sifa chini ya Sheria hii, atastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa mujibu ya masharti ya Sheria hii.<br><br>**KITUO CHA TAARIFA KWA WANANCHI:** Daftari la Wapiga Kura litumike kwa chaguzi zote.<br><br>**USHIRIKI TANZANIA COALITION**: kuondoa neno "sheria nyingine yoyote". Kifungu 9 (2) kisomeke:<br><br>"Bila kujali Masharti ya Kifungu kidogo cha kwanza na kwa kuzingatia uthibitisho wa umri, mtanzania yeyote ambaye hajapoteza sifa chini ya sheria au sheria nyingine ya uchaguzi ambaye wakati au kabla ya tarehe ya uchaguzi atakuwa ametimiza umri wa miaka 18, atastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya sheria hii.<br><br>**TAMWA:** Kifungu kinatoa utashi wa Kamati ya Uteuzi kuteua wajumbe pendekezwa (tisa) na kuna uwezekano wa kuwa wote wanaume. Kamati haielekezwi kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia katika kuchuja na kupata majina tisa ya Wajumbe wa Tume wanaopendekezwa. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Kuna uwezekano wa Kamati ya Uteuzi kuteua wajumbe pendekezwa (tisa) kuwa wote wanaume. Kamati haielekezwi kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuchuja na kupata majina tisa ya Wajumbe wa Tume wanaopendekezwa. |
| **8.** | UDSM, CCT, TLS, LHRC, TWAWEZA & JAMII FORUM TEC, ABDUL NONDO, BONAVENTURE MWALONGO, LOVENESS MAMUYA, YOSEPHA KOMBA, SALIM DEWJI, IDDI MANDI, TAMWA. | Ibara ya 10 | **UDSM:** kila mwananchi ana haki ya kupiga kura hivyo wafungwa wasizuiliwe kupiga kura. Lengo la marekebisho haya ni<br><br>**CCT:** Wafungwa waruhusiwe kupiga kura<br><br>**TLS:** Haki ya mtu kupiga kura haiwezi kupotea kwa kutiwa hatiani au kizuizini. Hivyo wanashauri wafungwa na watu waliowekwa kizuizini waruhusiwe kupiga kura.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA & JAMII FORUM:** kukosa sifa ya kuandikishwa na kupiga kura kwa kutiwa hatiani kwa kosa la jinai halimuondolei mtu haki ya kupiga kura.<br><br>Lengo la marekebisho haya ni kutoa haki ya mtu kupiga kura haiwezi kupotea kwa kuwa alifanya kosa la jinai. Haki ya kupiga kura hutegemea hadhi |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | ya uraia na utimamu wa uwezo wa akili.<br><br>**TEC:** Kifungu 10(1)(c) hiki kipo kinyume na Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 1977. Kifungu hiki kifutwe kama Mahakama ilivyotoa Hukumu kwenye case ya Tito Magoti, Jaji Elinaza Luvanda alibatilisha wafungwa kuzuiwa kupiga kura.<br><br>**ABDUL NONDO:** Wafungwa waruhusiwe kupiga kura kwa kuwa Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawaruhusu na vilevile nchi nyingi za Afrika Mashariki na nchi nyingi za Afrika zinaruhusu wafungwa kupiga kura hivyo kifungu hiki pia kiwaruhusu kupiga kura.<br><br>**BONAVENTURE MWALONGO:** kifungu hakijaonyesha namna gani ya kuandikishwa na kupiga kura kwa Raia wali nje ya nchi. Diaspora, wagonjwa waruhusiwe kupiga kura.<br><br>**LOVENESS MAMUYA:** Diaspora waruhusiwe kupiga kura electronically au kupitia balozi zao. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **YOSEPHA KOMBA:** Walioko vizuizini, wafungwa na Diaspora waruhusiwe kupiga kura. Iwekwe namna ya kuandikishwa na kupiga kura kwa wafungwa. Diaspora hawajakosa sifa kwenye Muswada lakini hawapigi kura. Iwekwe namna waruhusiwe kupiga kura.<br><br>**SALIM DEWJI:** Diaspora waruhusiwe kupiga kura. Vilevile wagonjwa wawekewe utaratibu waweze kupiga kura.<br><br>**IDDI MANDI:** MHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM SHULE KUU YA SHERIA (UDSM) - Haki ya kupiga kura kwa mtu kwa mtu aliye kizuizini au gerezani iwepo na waruhusiwe.<br><br>**TAMWA:** kusiwe na gharama za kupata kitambulisho kipya cha kupigia kura utakapopoteza. |
| **9.** | TAMWA, ZAFELA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 12 | **TAMWA:** ongeza hali ya ulemavu au umri kwenye kifungu cha 12 (4).<br><br>**ZAFELA**: kifungu hiki hakijaanisha taarifa za umri, hali ya ndoa na hali ya ulemavu ya mpiga kura. Kifungu cha 12 (4) kiongeze hali ya ulemavu, tarehe ya |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | na WILDAF | | kuzaliwa, baada ya neno jinsi na kusomeka kama ifuatavyo: (4) "*Daftari litaonesha bayana kwa kila mpiga kura aliyeandikishwa, namba ya kadi ya mpiga kura iliyotolewa, jinsi, hali ya ulemavu, tarehe ya kuzaliwa na anwani ya makazi ya kawaida ya mpiga kura na taarifa nyingine kama Tume itakavyoelekeza.*"<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu kiwekewe matumizi ya teknolojia ili zoezi liwe endelevu. |
| **10.** | CHADEMA | Ibara ya 13 | Kifungu cha 13(2)(3) kinamtaka Mtu ambaye ameomba kurekebisha kadi na kukataliwa kukata rufaa Mahakamani. Kuwe na Kanuni au fomu maalum itakayotumika ili iwe rahisi kukata rufaa kwenda Mahakamani na kuepuka urasimu. |
| **11.** | CHADEMA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, HAMISI | Ibara ya 14 | **CHADEMA**: Wafungwa raia wa Tanzania wanaotumikia vifungo wawe na haki ya kupiga kura na kama kina Sheria inayowazuia ifanyiwe marekebisho kwa kuwa pamoja na kutumikia vifungo bado ni Watanzania na wanayo haki ya kuchagua viongozi. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Tunapendekeza sheria<br>iweke sharti la vitambulisho rasmi<br>vinavyotambuliwa kwa mujibu wa sheria.<br>Kwa mfano, leseni ya udereva, hati ya kusafiria, kitambulisho cha Taifa, kitambulisho cha ukaazi, n.k<br>Lengo la marekebisho haya ni Kupunguza vikwazo vinvavyowazuia<br>wananchi kushiriki katika uchaguzi na hivyo wigo wa ushiriki wa uchaguzi kwa kuanisha vitambulisho na vitakavyotambulika wakati wa zoezi la<br>kupiga kura ili wananchi wengi zaidi waweze kushiriki kati uchaguzi.<br><br>**HAMISI**: Ianzishwe kanzidata ya wapiga kura wa taifa. Hii itasaidia katika mazingira ambayo mpiga kura amepoteza kadi ya kupiga kura hivyo ataweza kuangaliwa katika kanzidata hiyo na kuruhusiwa kupiga kura. |
| **12.** | CHADEMA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 15 | **CHADEMA**: Kifungu cha 15 kifanyiwe marekebisho ili kuwe na kiapo cha Mtu ambaye majina yake yamebadilika ili kuepuka kuongeza wapiga kura kwa sababu ya mtu kuwa majina tofauti. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Tunapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha pili, 15 (2) kisomeke;<br>"Mabadiliko ya jina yatathibitishwa kwa<br>kufuata nyaraka husika kwa mujibu wa sheria na kwamba, utambulisho wa sura na alama za vidole au alama zinginezo zinashabihiana. |
| **13.** | TAG, BEDANI KAPONGWA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 16 | Lengo la mapendekezo hii kuepusha matumizi mabaya ya madaraka. |
| **14.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CCT, WILDAF, CHADEMA, ZAFELA | Ibara ya 17 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu hiki hakitoi fursa kwa mtu binafsi au taasisi nyingine kuwa na mawakala.<br><br>Kuongeza Kifungu kipya 17 (8) kisomeke;<br>Kwa madhumuni ya kifungu cha 17 Mtu yeyote, kwa niaba yake au kwa kuwakilisha taasisi yoyote, anaweza, kushiriki kwenye<br>mchakato wa uandikishaji. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CCT**: Siku 7 ni chache kwa chama kuandaa mawakala. Tunapendekeza siku ziwe 14.<br><br>**WILDAF:** Kifungu 17 (3) kiweke taarifa za jinsi, umri, hali ya ulemavu ya wakala wa uandikishaji. Pia ni muhimu uchaguzi wa wakala uzingatia usawa wa jinsia.<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 17(7) kifutwe, kusiwe na kiapo cha kutunza siri kwa Wakala wa uandikishaji. Wakala ameteuliwa na Chama na kwa maana hiyo awe na uhuru wa kutoa mrejesho wa kinachoendelea kwa mamlaka yake ya uteuzi.<br><br>**ZAFELA**: Tunapendekeza kuongeza kuongeza kifungu kipya 17(8) kisomeke: kwa madhumuni ya Kifungu cha 17 Mtu yeyote, kwa niaba yake au kwa kuwakilisha taasisi yoyote, anaweza, kuangalia zoezi la uandikishwaji.<br><br>Kifungu cha 17 (3) kiweke taarifa za jinsi, umri, hali ya ulemavu ya wakala wa uandikishaji. Pia ni muhimu uchaguzi waw akala uzingatia usawa wa jinsia.<br>Lengo la marekebisho haya ni<br>Kuongeza wigo wa wadau kuangalia |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | mwenendo wa mchakato wa uandikishaji. Uchaguzi ni mchakato wa umma siyo wa wanasiasa pekee. Pia, kuhakiki uadilifu wa mchakato wa uchaguzi |
| **15.** | CHADEMA, | Ibara ya 18 | Kifungu cha 18 (3) kina makosa ya kimantiki hakijaeleza ni taarifa gani Tume inaweza kuzichukua kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na namna taarifa hizo zitatumika kwenye zoezi la kuandikisha wapiga kura. Kuhamisha taarifa au kuunganisha mifumo ya taarifa (Data migration and data integration) kwenye mifumo miwili tofauti inaweza kunyima watu wengi fursa ya kupiga kura kwakuwa bado watu wengi hawajaingizwa kwenye mfumo wa NIDA. |
| **16.** | ZAFELA, WILDAF, CCT, DEUS KIBAMBA, TAMWA, IDDI MANDI, ARIF NURAR FADHER, TGNP, | Ibara ya 20 | **ZAFELA** - Kifungu hiki kinaweka sharti la kulipa gharama ili kupata kitambulisho kipya kwa kadi iliyopotea. Wanapendekeza gharama ziondolewe za kulipia fedha kwa kitambulisho kilichopotea.<br>**WILDAF** - Wanapendekeza gharama za kupata kitambulisho kipya ziondolewe. Sababu ni kutokuweka vikwazo vya kifedha na kuwezesha wanawake ambao wenzi wao wameficha vitambulisho vya kupigia kura waweze kupiga kura. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | SAMSON SAMUEL, SALIM DEWJI.PETRO USESA. | | **CCT** - Ibara ya 20(2) na 21 uwepo wa ada utapunguza wigo wa wapiga kura hususan vijana na watu wenye ulemavu. Ada iondolewe.<br><br>**DEUS KIBAMBA** - Ibara ya 20(2) na 21(2) virekebishwe ili kuruhusu kutumia kitambulisho mbadala kama NIDA, LESENI na PASI YA KUSAFIRIA.<br><br>**TAMWA** - 20(2) na 21(2) kusiwe na gharama za kupata kitambulisho kipya cha mpiga kura.<br>**IDDI MANDI - MHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM SHULE KUU YA SHERIA (UDSM)** - kupotelewa na kitambulisho cha mpiga kura kusimzuie mtu kupiga kura. Kitambulisho cha NIDA kitumike.<br><br>**ARIF NURARI FADHER** - Upotevu wa kadi neno ada lifutwe kwa watu waliopetelewa vitu vyao kutokana na majanga ya asili kama vile tetemeko la ardhi kama ilivyotokea Hanang.<br><br>**TGNP** - Ibara ya 20(2) na 21(2) gharama za kulipia kadi iliyopotea itawatoa wapiga wengi hususan vijana na wenye ulemavu. Gharama hizi ziondolewe |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | na vitambulisho mbadala vitumike kama vile NIDA na PASI YA KUSAFIRIA.<br>**SAMSON SAMUEL** - Ibara ya 20(2) na 21(2) ada ya kitambulisho kilichopotea iondolewe.<br><br>**SALIM DEWJI** - Ada ya uandikishaji kuwe na kiwango kidogo sana.<br><br>**PETRO USESA** - Kupoteza kadi ya mpiga kura kama sio kwa uzembe, masharti haya yasitumike. |
| **17.** | WILDAF, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 21 | **WILDAF:** Kusiwe na uwezekano wa kuweka gharama za kupata kitambulisho kipya cha mpiga kura.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kusiwe na gharama za<br>kupata kitambulisho kipya cha mpiga kura.<br>Tunapendekeza kufuta kwa maneno "ada".<br>Lengo la marekebisho haya ni Ili kuhakikisha haki ya kupiga kura. Pia. Ili kuhamasisha mwitikio wa wapiga kura kushiriki uchaguzi. |
| **18.** | ADC | Ibara ya 22 | Kiongezwe kifungu cha kutambua viambatanisho vingine mfano NIDA, RITA ili kubaini nani aliyefariki na aliyekuwa hai. Sheria itambue katiba ya Zanzibar |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | kwa sababu wakati wa kesi itabidi itambulike au kutumika. |
| **19.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, | Ibara ya 23 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Sheria haijaeleza ukomo wa muda ambao afisa mwandikishaji, atafanyia kazi rufaa ya kukataliwa kwa maombi ya uandikishwaji. Tunapendekeza ukomo uwe ndani ya siku saba (7).<br><br>Lengo la marekebisho haya ni Kutoa uwezekano wa rufaa kufanyiwa kazi kwa muda usiyojulikana kisheria |
| **20.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, | Ibara ya 24 | Kuondoa takwa la muda wa kufanya ukaguzi wa Daftari la Awali la Wapiga kura.<br>Lengo la marekebisho haya ni Kurahisisha wananchi kukagua daftari la wapiga kura. |
| **21.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA, | Ibara ya 27 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu kinaainisha gharama za dhamana ya pingamizi. Hii ni kinyume na uamuzi wa Mahakama Kuu katika kesi ya Ndyanabo dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CHADEMA:** Vifungu vya 27(2) na 28(7) kuhusu kulipa dhamana ya fedha kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume kuhusu wale ambao hawataridhika na taarifa kwenye daftari la wapiga Kura kupinga taarifa hizo vifutwe. Itawafanya wananchi kutolalamikia makosa yaliyopo kwenye daftari kwa kuhofia kuingia gharama za kuweka dhamana hiyo. Mchakato wa wananchi kuhakiki daftari na kupinga taarifa ambazo sio sahihi usihusishe kuweka dhamana ya fedha. |
| **22.** | ABDUL NONDO | Ibara ya 28 | Ibara ya 28 (5) iondolewe. |
| **23.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA | Ibara ya 30 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu hiki kinazuia haki ya kukata rufaa zaidi maamuzi ya Mahakama ya Wilaya. Tunapendekeza kurekebisha kifungu hiki kwa kuondoa ukomo wa Mahakama ya Wilaya kuwa mwisho wa rufaa.<br>Lengo la marekebisho haya ni<br><br>**CHADEMA**: Kifungu cha 30(1) kuhusu masharti ya kuweka dhamana ya fedha kabla ya kukata rufaa Mahakama ya Wilaya kuhusu kuongezwa au kufutwa kwenye daftari la Wapiga Kura masharti ya dhamana yafutwe. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Kifungu cha 30(2) kinaelekeza kwamba uamuzi wa Mahakama ya Wilaya kuhusu kufutwa au kuongezwa kwenye daftari la Wapiga ni wa mwisho. Kifungu kiboreshwe kwamba mtu asiporidhika na uamuzi wa Mahakama ya Wilaya anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu na asiporidhika anaweza kukata rufaa kwa masuala ya kisheria pekee kwenda Mahakama ya Rufani.<br><br>Kiongezwe kifungu kidogo cha 10 kwenye kifungu cha 30 kuonyesha kwamba kutakuwa na fomu maalum zitakazokuwa kwenye Kanuni zitakazotungwa na Jaji Mkuu ya namna ya kukata rufaa.<br><br>Kifungu cha 30 (4), (5), (6) kirekebishwe ili kuondoa masuala ya kutaifisha dhamana iliyowekwa kabla ya kukata rufaa ambayo tumependekeza ifutwe. |
| **24.** | TANLAP,<br>USHIRIKI TANZANIA,<br>WILDAF,<br>ZAFELA ,<br>CHADEMA, | Ibara ya 32 | **TANLAP** - Haijaweka sharti mahsusi la kutaka vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia.<br><br>**USHIRIKI TANZANIA** - Ibara hii haijabainisha uzingatiaji wa usawa wa kijinsia. Hivyo kifungu hiki kiboreshwe. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | UDSM (IDDI MANDI) | | **WILDAF, ZAFELA** - Ibara hii haijaweka sharti la kuzingatia ujumuishwaji wa kijinsia wakati wa uwasilishaji wa majina ya mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais. Ibara ifanyiwe marekebisho kiongezwe kifungu kidogo kipya kuleta usawa kijinsia kitakachovitaka vyama vya siasa vikitaka kuteua mgombea urais mwanaume basi Makamu wa Rais awe mwanamke na kinyume chake.<br><br>**CHADEMA** - Kuwe na wagombea binafsi.<br><br>**UDSM (IDDI MANDI)** - suala hili limeachwa kwenye Muswada. Anapendekeza haki ya kugombea kama mgombea huru iwekwe kwenye Muswada. |
| **25.** | WILDAF, ZAFELA, SAHIRINGO | Ibara 33 | **WILDAF, ZAFELA** - Ibara hii inataka mgombea adhaminiwe na wadhamini angalau 200. Ibara hii imtake mgombea kutafuta wadhamini wanawake na wanaume kwa msingi wa 50/50 la sivyo athibitishe kuwa ameshindwa kuwapata wadhamini wa jinsi au kundi fulani.<br><br>**SAHIRINGO** - Ibara ya 33(1) wadhamini kila Mkoa wapungue kutoka 200 na kuwa 100 maana ni kazi kubwa ya kutafuta wadhamini. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **26.** | ZAFELA, WILDAF, TREE OF HOPE TANZANIA, CCT, TLS | Ibara 34 | **ZAFELA, WILDAF, TREE OF HOPE TANZANIA** - 34(3) Ibara hii ifanyiwe marekebisho na kuongeza maelezo muhimu yatayohitajika kwa mgombea ikijumuisha jinsi, hali ya ulemavu na tarehe ya kuzaliwa.<br>**CCT** - Kwenye fomu ya kugombea Urais waweke fomu ya wenye mahitaji maalum ili waweze kushiriki.<br><br>**TLS** - Sheria ina ubaguzi hususan kwenye fomu za mgombea katika ngazi ya Urais haijazingatia watu wenye ulemavu. Vilevile fomu za mgombea katika uwasilishaji wake fomu ziwasilishwe kwa mtandao halafu nakala ngumu ndio ifuatie kuwasilishwa. |
| **27.** | CCT<br>UDSM - IDDI MANDI, WILDAF, ZAFELA, CHECK MSUVA, CHADEMA. | Ibara 35 | **CCT -** Dhamana iondolewe.<br>**UDSM - IDDI MANDI** - Dhamana ya gharama katika vifungu vyote iondoke.<br>**WILDAF**, **ZAFELA** - 35(2)(b) - Ibara hii inazuia uwanda wa ushiriki wa wananchi katika uchaguzi kwa kutokuwa au kuhofia kurudishiwa kwa dhamana zao. Wagombea wanawake, vijana na wenye ulemavu wasitoe dhamana ili kuwaondolea vikwazo vya kugombea. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CHECK MSUVA** - Sharti la dhamana kwa makundi maalum ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu lisiwepo.<br><br>**CHADEMA** - Ibara ya 35(2)(b) - Ibara hii ifutwe hakuna maana ya kuweka sharti hilo. |
| **28.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 36 | Kifungu hiki hakijaonesha taratibu za kukata rufaa dhidi ya kukatiliwa uteuzi, haki ya kusikiliza na haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi Tume. Kifungu kiweke kifungu kidogo cha pili kitakachoweka haki ya kukata rufaa.<br>Lengo la marekebisho haya ni Inakiuka ibara ya 13(6) (a) na Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya JAMHURI YA Muungano wa Tanzania 1977 |
| **29.** | ZAFELA, TUSONGE, CCT, WILDAF, CHADEMA, ACT WAZALENDO, TAMWA, TLS, LHRC, TWAWEZA, | Ibara 37 | **ZAFELA:** Kifungu hiki kiainishe makosa yanayotokana na ukatili wa wanawake katika siasa kama ni moja ya makosa ambayo mtu anaweza kupinga uteuzi wa mgombea.<br><br>**TUSONGE**: Kuwe na kosa la ukatili wa kijinsia kupinga uteuzi wa mgombea. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | | **CCT:** Kifungu kirekebishwe kwa kuondoa watendaji wa serikali.<br><br>**WILDAF:** Kifungu hiki kiainishe makosa yanayotokana na ukatili wa wanawake katika siasa kama ni moja ya makosa ambayo mtu anaweza kupinga uteuzi wa mgombea.<br><br>Sheria ya Vyama vya siasa chini ya Kifungu cha 6B cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinakataza Ukatili wa Kijinsia.<br>Ongeza kifungu 37 (f) kinachosema<br>"Kama mgombea amethibitika amefanya makosa ya ukatili wa kijinsia."<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 37(6) kiandikwe upya kuruhu Mgombea Urais ambaye hajateuliwa na Tume kukata rufaa Mahakama Kuu na Rufaa husika kusikilizwa na kuamuliwa ndani ya 14 toka uamuzi wa kutoteuliwa au kuenguliwa kufanyika.<br><br>**ACT WAZALENDO:** Mgombea apewe haki kwa mujibu wa katiba JMT 1977 ibara ya 13(6)(a) kama hajaridhika na maamuzi ya Tume ya uchaguzi kukata rufaa na kupinga maamuzi hayo mahakama |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | kuu.<br>Lengo la marekebisho hayo ni Mtu yoyote awe na uhuru na uwezo wa kuweka pingamizi pale ambapo linahitajika<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL**: Kifungu hakitoi fursa ya kurekebisha makosa madogo. Kifungu kitoe fursa kurekebisha makosa madogo yanayoweza kurekebishjika kuliko kutengua. Inakiuka ibara ya 13 (6) (a) na ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977<br><br>Tunapendekeza kuongeza maneno yafuatayo: Mtu hatokataliwa kuteuliwa kwa sababu za dosari za kiufundi, hivyo tunapendekeza Tume iweke muda wa kukagua fomu za wagombea kubaini fomu zenye kasoro na kutoa fursa ya kufanya masahihisho.<br><br>a) "…….na baada ya kupewa fursa ya kurekebisha au kuwasilisha kwa mujibu wa masharti ya sheria hii alishindwa kufanya hivyo.."<br>b)….na baada ya kupewa fursa ya kurekebisha au kuwasilisha kwa mujibu wa masharti ya sheria hii |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | alishindwa kufanya hivyo.<br>c)......Na baada ya kupewa fursa ya kurekebisha au kuwasilisha kwa mujibu wa masharti ya sheria hii alishindwa kufanya hivyo.<br><br>Kifungu cha 37 (3) kinawapa uzito mkubwa kupitiliza watendaji wa serikali kama Msajili wa Vyama na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweka pingamizi, jambo ambalo linaleta hisia za matumizi mabaya ya mapingamizi.<br><br>Tunapendekeza kuondoa mamlaka za serikali kuweka mapingamizi. Kifungu hiki kisomeke; Mtu yoyote anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mgombea wa Urais. |
| **30.** | CHADEMA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara ya 38 | CHADEMA: Kifungu cha 38(2) kiandikwe upya ili Mgombea pekee wa Urais kupata 50% +1 ya kura zote halali ndipo atangazwe kuwa mshindi na kuondoa sharti la kura nyingi pekee.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu cha 38 (3) hiki kimeacha ombwe la muda gani unahitajika hadi kufanya uteuzi mpya. Kifungu hiki kisome; Endapo mgombea pekee wa kiti cha |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Rais atashindwa kupata kura nyingi zaidi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), ndani ya siku thelathini (30) Tume itafanya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi wa Rais kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.<br>Lengo la marekebisho ni Kuweka muda maalumu ili kuepuka mgongano wa kisheria kipindi cha uchaguzi. |
| **31.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 39 | Kifungu hiki hakina mazingira na sababu zitakazo mfanya mgombea wa urais kujitoa kiholela. Kiujumla, tunapendekeza Tume kutoa nafasi kwa chama ambacho mgombea wake amejitoa, chama wateue mgombea mwingine. Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke kama ifuatavyo;<br>2) Endapo kutakuwa na mazingira yanayolazimu mtu kujitoa katika ugombea, mgombea wa kiti cha urais anaweza kujitoa ugombea kwakutoa taarifa ya maandishi aliyoisaini ikieleza sababau aliyeiwasilisha yeye mwenyewe kwa Tume na nakala Katibu Mkuu wa chama kilichomdhamini. Tunapendekeza kuongeza kifungu kipya, kitakachosomeka; |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Lengo la marekebisho haya pamoja na sababu nyingine ni<br>(a) Mapendekezo haya yanalenga kubainisha mazingira na sababu za mgombea kujitoa.<br><br>(b) Lengo ni kutoa nafasi kwa chama kuteua mgombea mwingine<br><br>(c) Kuziba mianya ya rushwa na ushawishi unaoweza kumrahishia mgombea mmoja kupita bila ushindani wenye maana ya kidemokrasia<br><br>Tunapendekeza chama kipewe nafasi ya kumteua mgombea mwingine. Pia, dhamana ya mgombea ifilisiwe.<br><br>Kuongeza kifungu kipya, kitakachosomeka; Mgombea yoyote aliyeshindwa kujitoa rasmi kwa mujibu wa kifungu cha kwanza na cha pili 39 (1) na (2) hatoruhusiwa kugombea nafasi yoyote katika kipindi kinachofuata cha uchaguzi. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **32.** | CCT, James Masunga, Jukwaa la Katiba Tanzania na Salim Dewji, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL. | Ibara ya 41 | **CCT:** Sheria ianishe na kutaja siku ya uchaguzi.<br>Lengo ni kuruhusu watu Kwenda kwenye ibada siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.<br><br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu hiki hakijainisha mazingira au sababu ambazo Tume inaweza kupanga siku tofauti au kutengua siku ya uchaguzi.<br>Lengo la marekebisho ni Ili kuweka sababu maalum za kupanga siku nyingine ya uchaguzi. |
| **33.** | CHADEMA, ACT-WAZALENDO | Ibara ya 43 | **CHADEMA:** Sifa za wagombea ziwe za kikatiba tu na siyo za ziada. |
| **34.** | MTANDAO WA TIBA ASILIA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA | Ibara 45 | **MTANDAO WA TIBA ASILIA:** Neno Mtu mwingine katika Ibara 45 (1) ni nani? Tunapendekeza waandishi wa Habari wajumuishwe.<br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Tunapendekeza kurekebisha kifungu cha 45 (1) (i) kisomeke;<br>Kwa makubaliano ya Tume na wadau wengine kwa mujibu wa kifungu hiki, Tume inaweza kumruhusu mtu mwingine yeyote kuingia katika kituo cha kupiga kura. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Kifungu kinaweka mwanya usiyo wa kisheria kwa kumtaka msimamizi wa uchaguzi kusubiri maelekezo ya Tume ili kubandika nakala ya taarifa ya matokeo. Kifungu kisomeke; Msimamizi wa uchaguzi, baada ya kuandaa taarifa ya matokeo chini ya kifungu kidogo cha (3), atabandika nakala ya taarifa hiyo katika sehemu ya wazi inayoonekana kwa mujibu wa masharti ya sheria hii.<br><br>Kifungu CHA 45 (10) hakiendani na matakwa ya wadau wa demokrasia kuhusu majumuisho ya kura za uchaguzi wa urais. Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke; "Mgombea yeyote wa kiti cha Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo amepata kura zinazofikia zaidi ya nusu ya kura zote halali". Tunapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 45 (11) "Endapo hakuna mgombea atakayefikisha kura zinazohitajika katika kifungu 45 (10) hapo juu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza kuwa hakuna mgombea aliyechaguliwa kuwa Rais na ndani ya siku sitini (60) itateua siku ya uchaguzi wa marudio ambapo wagombea wawili waliyopata kura nyingi kuliko wengine watachuana katika duru ya pili. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CHADEMA:** Kifungu cha 45(10) kiandikwe upya ili mshindi wa kiti cha Urais atakiwe kupata 50%+1 ya kura zote halali ndipo atangazwe kuwa amechaguliwa.<br><br>Kiongezwe kifungu cha 45(11) ili kama hakuna Mgombea wa kiti cha Urais aliyepata 50%+1 ya kura zote halal, uchaguzi urudiwe kwa Wagombea wawili waliopata kura nyingi zaidi. |
| **35.** | CHADEMA | Ibara 46 | Kifungu cha 46 cha marudio ya uchaguzi wa Rais kirekebishwa kiendane na masharti ya kifungu cha 45(10) baada ya marekebisho. |
| **36.** | TREE OF HOPE TANZANIA, ZAFELA | Ibara 50 | **TREE OF HOPE TANZANIA** - 50(3) ipo kimya kuhusu maelezo muhimu mfano jinsi, umri na hali ya ulemavu.<br><br>**ZAFELA** - Hakuna sharti la mgombea kuzingatia ujumuishwaji wa jinsia na makundi mbalimbali katika kutafuta wadhamini. Kifungu hiki kimtake mgombea kutafuta wadhamini kutoka kwa wanawake na wanaume kwa msingi wa 50/50 la sivyo athibitishe kuwa ameshindwa kuwapata wadhamini wa jinsi au kundi fulani. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | 50(2) - Ibara hii inazuia uwanda wa ushiriki wa wananchi katika uchaguzi kwa kutokuwa au kuhofia kutorudishwa kwa dhamana zao. Wagombea wanawake na wenye ulemavu wasitoe dhamana ili kuwaondolea vikwazo vya kugombea.<br><br>50(3) - Ibara hii ifanyiwe marekebisho na kuongeza maelezo muhimu yatakayohitajika kwa mgombea ikijumuisha jinsi, hali ya ulemavu na umri. |
| **37.** | CCT, UMOJA WA ASAS ZA VIJANA, CHADEMA. | Ibara 51 | **CCT -** Dhamana itolewe na vyama.<br>**UMOJA WA ASAS ZA VIJANA -** Dhamana iondolewe ili kuruhusu kundi maalum kushiriki.<br><br>**CHADEMA** - Ibara irekebishwe kuondoa sharti la kutaifisha dhamana mgombea wa ubunge asipata 1/10 ya kura zote halali. |
| **38.** | ACT WAZALENDO, CCT, ZAFELA, CHADEMA, | Ibara 53 | **ACT WAZALENDO -** Ibara iruhusu maamuzi ya Tume kupingwa mahakamani.<br>**CCT** - Ibara iruhusu mtu yeyote kuweka pingamizi.<br><br>**ZAFELA** - 53(6) Ibara hii irekebishwe ili kutoa haki kwa mtia nia ambaye hajaridhika kwenda mahakamani. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **CHADEMA** - 53(6) - Ifanyiwe marekebisho ili mgombea asiyeridhika na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu pingamizi akate rufaa moja kwa moja kwenda Tume ya Uchaguzi na sio kupitia kwa Msimamizi wa Uchaguzi. |
| **39.** | ABDUL NONDO, CAHDEMA | Ibara 54 | **ABDUL NONDO** - 54(2) kuwekwe sharti mgombea pekee anayepigiwa kura za ndio apate zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa ndipo aweze kutangazwa mshindi.<br><br>**CHADEMA** - 54(2) Iandikwe upya ili kuweka sharti kwa mgombea pekee wa ubunge kupata 50%+ 1 ya kura zote halali ndipo atangazwe kwamba amechaguliwa. |
| **40.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 57 | Kifungu kinampa mamlaka Waziri badala ya Tume ambayo ndiyo yenye dhamana. Mamlaka ya kutangaza kata iko wazai yabaki wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.<br>Lengo la marekebisho haya Ni kuepuka mkanganyiko miongoni mwa wagombea.<br><br>Kifungu hakijaainisha muda maalumu wa zoezi la kupokea fomu za uteuzi. Tunapendekeza muda uwe |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | si zaidi ya saa kumi kamili alasiri kama ilivyo kwa nafasi za ugombea wa nafasi ya Urais na Ubunge teuzi wa wagombea wa uchaguzi katika kata ambayo nafasi wazi imetokea. |
| **41.** | UMOJA WA ASAS ZA VIJANA, TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL | Ibara 59 (2) | **UMOJA WA ASAS ZA VIJANA**: Miaka iwe 18 lengo la marekebisho ni Kuweka ushiriki mpana wa vijana. Kuweka ukomo ili kuruhusu vijana kushiriki katika nafasi za uongozi.<br>**TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu kinaweka mianya ya tafsiri tofauti za sifa za mgombea wa udiwani, sifa hizo zinaweza kutafsiriwa tofauti mara baada ya mgombea huyo kushinda nafasi hiyo. Tunapendekeza kuongeza kifungu na kusomeka;<br>Sifa za mgombea wa udiwani zitaendelea kumuhusu mtu aliyechaguliwa kuwa diwani.<br><br>Kifungu kimeacha kundi la vijana wa miaka 18 ambao wanahaki ya kupiga kura. Pia, kifungu hakina ukomo wa umri wa mtu kugombea nafasi ya udiwani.<br>Lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa sifa za mgombea za udiwani zinaongezwa wigo hadi baada ya mtu kushinda nafasi ya udiwani. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | |
| **42.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, CHADEMA, WILDAF, TAMWA, | Ibara 60 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Kifungu hakijaainisha sababu za kutengua siku iliyopangwa kwa ajili ya uteuzi. Pia, sheria imeweka muda mfupi wa kutoa taarifa ya siku ya uteuzi**.**<br><br>**CHADEMA:** Kifungu cha 60(1)(e) kinamuondolea sifa Mtu aliyewekwa kizuizini kuteuliwa kugombea udiwani. Kifungu na Sheria ya kuweka watu kizuizini ifutwe.<br>.<br><br>**WILDAF:** tunapendekeza kuongeza kipengele Kama mtu atakutwa na hatia ya makosa yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa.<br>Lengo ni Kuepuka matumizi mabaya ya madaraka |
| **43.** | TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL, TGNP, WILDAF, | IBARA 62 | **TLS, LHRC, TWAWEZA, JUKATA, JAMII FORUMS, CSL:** Tunapendekeza mgombea aape kwa kamishina wa viapo yeyote.<br>Lengo la marekebisho ni Kurahisisha zoezi la uapishaji kulingana na ufinyu wa muda uliopo |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | Tunapendekeza kuwa adhaminiwe na wadhamini wasiopungua kumi(10) katika kila kijiji/mtaa wa kata husika.<br><br>**TGNP:** Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke:<br>(2) Uteuzi utafanyika kwa kutumia fomu itakayoainishwa ambayo itazingatia Jinsia na matumizi ya watu wenye mahitaji maalumu, itakayosainiwa na mgombea na watu wanaomdhamini mgombea huyo na itakuwa na taarifa zifuatazo:<br>(a) jina, Jinsi, tarehe ya kuzaliwa, anwani na kazi ya mgombea;<br>(b) majina, Jinsi, tarehe za kuzaliwa na anwani za wadhamini na namba za kadi zao za kupiga kura. |
| **44.** | TLS, WILDAF na CHADEMA | Ibara ya 63 | **TLS:** Takwa la dhamana katika fomu za uteuzi linakiuka haki ya kuchaguliwa ( Kifungu hiki kifutwe).<br>Tunapendekeza kufutwa kwa takwa la dhamana katika uchukuaji wa fomu za utuezi.<br>Lengo la marekebisho haya ni kutoa furs kwa wananchi wengi Zaidi kushiriki katika mchakato wa uchaguzi |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **WILDAF:** Kiongezwe kifungu 61 (4) kinachosema wagombea udiwani wanawake watasamehewa kulipa gharama ya dhamana. |
| **45.** | **TLS**, **CHADEMA**, **CCT**, | Ibara 65 | **TLS**: Tunapendekeza kuondolewa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa sehemu wa waweka mapingamizi. Tunapendekeza wafuatao kuwa na sifa za kuweka mapingamizi<br>1. Mgombea<br>2. Chama cha siasa kilichomdhamini mgombea husika<br>3. Mpiga kura.<br>Lengo la marekebisho haya ni Kuondoa mwanya wa kuingilia haki za wagombea.<br><br>Tunapendekeza ndani ya siku saba (7) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi atamtaarifu mwekewe pingamizi juu ya uwepo wa pingamizi hilo.<br><br>**CHADEMA**: Kifungu cha 65(7) kirekebishwe ili Mgombea wa nafasi ya udiwani aweze kukata rufaa moja kwa moja kwenda Tume. Baada ya kupokea rufaa Tume iamuru Msimamizi wa Uchaguzi |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | kuwasilisha taarifa au utetezi wake ndani ya siku tatu toka siku ya uamuzi wake na Tume itaamua kuhusu rufaa ndani ya siku 10 toka siku rufaa husika ilipowasilishwa. Kuwe Na nafasi ya Mgombea udiwani kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Tume. |
| **46.** | **WILDAF** | Ibara ya 74 | Tunapendekeza kuongezwa kwa kifungu kitakachoweka adhabu kwa chombo ambacho kitakiuka matakwa ya sheria.<br><br>Tunapendekeza kujumuishwa kwa vyombo vya habari vya binafsi**.** |
| **47.** | **CHADEMA** | Ibara ya 77 | Kifungu cha 77(1) kirekebishwe ili kuondoa maneno "… baada ya kupata ridhaa ya Wagombea…" hii Ina maana kwamba Wakala wa upigaji Kura atateuliwa Na Chama baada ya Chama kupata ridhaa ya Mgombea jambo ambalo sio sahihi. |
| **48.** | ZAFELA, WILDAF, TUSONGE, TAMWA, AISHA SALEH MADOGA | Ibara ya 84 | **ZAFELA -** Tume ihakikishe kuna karatasi za kupigia kura ambazo zipo kwenye format ya nukta nundu ili kuwawezesha wapiga kura wenye ulemavu wa kuona kupiga kura kwa usiri. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | **WILDAF** - 84(3) Tume ihakikishe kuna karatasi za kupigia kura ambazo ziko katika format ya nukta nundu ili kuwawezesha wapiga kura wenye ulemavu wa kuona kupiga kura kwa usiri.<br><br>**TUSONGE** - 84(3)(b) - Ibara ina pengo kubwa hivyo Tume ihakikishe kwamba karatasi za kupiga kura zilizo na format ya nukta nundu zinakuwepo.<br><br>**TAMWA** - 84(3)(b) - kuwe na karatasi za kupiga kura za aina tofauti kuwajumuisha na watu wenye ulemavu.<br><br>**AISHA SALEH MADOGA** - 84(3)(b) - kwa wapiga kura wasiojua kusoma na kuandika na wasioona kuwe na karatasi za nukta nundu. |
| **49.** | ACT WAZALENDO, TLS | Ibara ya 85 | **ACT WAZALENDO -** 85(5) - Ibara ifutwe kwani inahalalisha wapiga kura, wanausalama, watu wa huduma za kwanza na mawakala kutolewa nje ya vituo.<br>**TLS** - Neno mtu yeyote lina ukakasi. Neno "mtu yeyote" lifutwe. Inapendekezwa kujumuishwa kwa waandishi wa habari watakaoidhinishwa na Tume kama sehemu ya watu wanaoruhusiwa kuingia |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | katika kituo cha kupiga kura.<br><br>85(2)(e) - neno "msaidizi" litafsiriwe kwa upana.<br>85(5) - Ibara inaainisha suala la utovu wa nidhamu. Kimsingi utovu wa nidhamu ni ngumu kuthibitisha kisheria. Inapendekezwa kifungu hiki kirekebishwe. |
| **50.** | TANLAP, TLS | Ibara ya 88 | **TANLAP** - 88(1) Ibara haijaeleza sababu nyingine zinazoweza kusababisha zoezi la kupiga kura kusitishwa. Vilevile hakijaeleza sababu zinazoweza kusababisha uchaguzi kuahirishwa kabla ya zoezi la upigaji kura kuanza. Inapendekezwa Ibara irekebishwe ili kuweka utaratibu wa kuahirisha uchaguzi kabla ya zoezi la upigaji kura kuanza inapotokea sababu mbalibmali kama majanga ya asili.<br><br>**TLS** - Ibara hii imejibana kwenye vurugu pekee ingawa kuna mazingira mbalimbali yanayoweza kupelekea zoezi la kupiga kura kuahirishwa. |
| **51.** | TLS | Ibara ya 92 | **TLS** - 92(8) Ibara inanyima haki kwa mtu ambae hatotia saini fomu. Inapendekezwa kifutwe. |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| **52.** | TLS | Ibara ya 93 | **TLS** - 93((3) - Takwa la mlalamikaji au wakala kupewa nakala ya fomu ya malalamiko. |
| **53.** | TLS | Ibara ya 96 | **TLS** - 96(1)(a) - Ibara hii ifutwe ili kuendana na Ibara ya 84(3)(f) ili kuweka mtiririko wenye mantiki. |
| **54.** | **CHADEMA, TLS** | Ibara 102 | **CHADEMA**: Kifungu cha 102(c) maneno "… iwapo fomu za matokeo zipo za kutosha…." Yafutwe ili kulazimu Msimamizi wa uchaguzi kumpatia Wakala nakala ya matokeo ya uchaguzi.<br><br>**TLS:** Kifungu 102 (1)(e) hiki kirekebishwe na kisomeke; "Atampa kila wakala wa kuhesabu kura nakala ya taarifa ya matokeo". |
| **55.** | **TLS** | Ibara 107 | Tunapendekeza kuondoa kifungu cha 107 (3) kinachopendekeza kuteketeza nyaraka za uchaguzi ndani ya miezi 6 kwa kuwa kifungu hiki kinakinzana na muda wa mashauri ya uchaguzi na Kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Taifa ya Utunzaji wa Kumbukumbu Nyaraka za Taifa Namba 3, 3002 (The Records and Archives Management Act No.2 of 2002) ambayo inaweka takwa la nyaraka za Taifa kutunzwa ndani ya miaka 30.<br>Lengo la marekebisho haya ni Ili kutoharibu vielelezo |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | vya msingi vya mashauri ya uchaguzi na kuendana na Sheria ya Taifa ya Utunzaji wa Kumbukumbu wa Nyaraka. |
| **56.** | **TLS, KITUO CHA TAARIFA KWA WANANCHI, WILDAF** | Ibara 112 | Kifungu hakijaweka mchakato wa upatikanaji wa wabunge wa viti maalumu.<br><br>Kuwe na ukomo wa Viti Maalumu |
| **57.** | **CHADEMA** | Ibara ya 125 | Kifungu cha 125 (1)(2)(3)(4)(5)(6) na (7) kuhusu kiapo cha kutunza siri na adhabu zake dhidi kwa Mawakala na Wagombea pamoja na kuwazuia Mawakala kutokuwa na mawasiliano na Chama au Mgombea kitatoa mwanya kwa Wasimamizi wa uchaguzi kufanya jambo lolote kwenye vituo vya kupigia kura na Wakala hatachukua hatua yoyote kwa sababu ya kiapo cha kutunza siri. Kifungu hiki kilitungwa wakati nchi ikiwa ya Chama kimoja na hakina nafasi kwa wakati huu wa demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa. |
| **58.** | **TLS, UMOJA WA ASAS ZA VIJANA** | Ibara 166 | Tunapendekeza kwamba badala ya kutumia neno inaweza, litumike neno Tume itatumia teknolojia.<br>Lengo ni kuondoa mwanya wa Tume kuwa na uhuru |

| NA. | MTOA HOJA | IBARA | MAONI SABABU NA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|
| | | | wa kutumia teknolojia kwenye ulimwengu wa sasa unaotegemea matumizi ya teknolojia kwa kiwango kikubwa. |

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa hoja hizo pamoja na maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika Muswada, baadhi ya changamoto zilizobainika utatuzi wake unahitaji mabadiliko ya Sheria zingine ambazo hazifanyiwi kazi na Kamati kwa sasa.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

(i) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 6(1) inaeleza kuwa kila Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya atakuwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika Jimbo au Kata.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikuwa ina maoni kwamba Sheria isiweke ulazima kwa Mkurugenzi Mtendaji kusimamia Uchaguzi na badala yake, kuwepo na masharti ya Mtumishi wa Umma mwandamizi ama mtu mwingine yoyote mwenye sifa kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi msaidizi wa Uchaguzi. Serikali iliona kuwa upo umuhimu wa Wakurugenzi Watendaji kutajwa kwenye sheria kwa kuwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania kwenye kesi ya madai na. 138/2019 na Mahakama ya Afrika ya Watu na Haki za Binadamu kwenye kesi ya madai na. 11/2020 ziliamua kuwa Wakurugenzi kusimamia Uchaguzi haukiuki masharti ya Katiba wala Mkataba wa Afrika wa Watu na Haki za Binadamu mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati bado ina maoni kuwa hakuna ulazima wa sheria kuweka sharti kwa Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Mji na

Wilaya kuwa wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa kuwa uzoefu unaonyesha wapo Wakurugenzi kwa sababu mbalimbali wanapoteza sifa za kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati ya kuwatumia Watumishi wa Umma Waandamizi ama mtu yoyote mwenye sifa kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika Jimbo au Kata.

(ii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 8 inaweka masharti ya Uteuzi wa waratibu wa uchaguzi, Kamati ilikuwa na maoni kuwa Muswada utambue ofisi za Balozi Nje ya Nchi kuwa Waratibu wa Uchaguzi, ili kutoa fursa kwa Watanzania walio Nje ya Nchi kupiga kura, Kwa kuzingatia kuwa Ibara ya 5 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayompa haki raia wa Tanzania kupiga kura akiwa ametimiza umri wa miaka 18 na ikiwa hafungwi na masharti ya Ibara ya 5(2) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, katika hoja hii Serikali ilifafanua kuwa Uchaguzi una mifumo yake ambayo unatakiwa kuhakikisha kura zinazopigwa zinakubalika na kuaminiwa na wadau wa uchaguzi. Na kwamba bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha mifumo hiyo inawekwa ya kuwezesha watanzania walioko nje ya nchi kupiga kura na kura hizo kupatikana kwa wakati na kuaminiwa. Kwa Msingi huo, Kamati ina maoni kuwa suala hili linahitaji kufanyiwa utafiti wa namna ya utekelezaji wake.

(iii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 12 inaweka masharti ya Daftari la Kudumu la Wapiga kura, Kamati iliishauri Serikali kuongeza taarifa ya hali ya ulemavu wa mpiga kura, Kwa kuwa kuongeza hali ya ulemavu wa mpiga kura Kutaiwezesha Tume kuweka miundombinu stahiki kwenye vituo vya upigaji kura mapema iwezekanavyo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(iv) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 13 inaweka masharti ya Uandikishaji wa wapiga kura Tanzania Zanzibar, Muswada unapendekeza kwa Uchaguzi wa Wabunge Tanzania Zanzibar

kutumia daftari la mpiga kura linalotumika kuchagua Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar isipokuwa kwa kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, wapiga kura wataandikishwa na Tume ya Uchaguzi (NEC). Lengo ni kuwa na Daftari moja linalojitegemea ili kuratibu utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliifafanulia Kamati kuwa Msingi wa sharti hilo ni kuhakikisha kuwa Wabunge wa Zanzibar wanapigiwa kura na wakaazi wa eneo husika.

(v) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 15 inaweka masharti ya kubadili majina kwa mpiga kura aliyeandikishwa kutokana na sababu ya ndoa au sababu nyingine yoyote baada ya kuandikishwa, Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kidogo cha (2) kitakachoweka masharti kuwa mabadiliko ya jina yatathibitishwa kwa kufuata nyaraka husika kwa mujibu wa sheria. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(vi) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 20 inaweka masharti ya utaratibu wa kupotea, kufutika au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura, Kamati ilipendekeza Ibara ya 20(2) iondoe ada ya kulipia kitambulisho cha mpiga kura iwapo kimepotea, kuharibika ama kufutika. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(vii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 21 inaweka masharti ya urekebishaji wa taarifa kwenye Daftari la Awali la Wapiga kura, Kamati ilipendekeza kusiwe na ada ya marekebisho ya taarifa. Lengo ni kumuwezesha mpiga kura kutimiza haki yake ya Kikatiba bila gharama yoyote. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(viii) **Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 23 inaweka masharti ya kukataliwa kwa maombi ya uandikishaji wa wapiga kura, Kamati iliishauri Serikali kuweka muda wa siku saba kwa mwombaji aliyekataliwa maombi kuwasilisha mapitio kwa Afisa Mwandikishaji na kwamba muda wa Afisa huyo kushughulika mapitio hayo

haujawekwa bayana kama ambavyo muda wa Mahakama kushughulikia rufaa ulivyobainishwa katika ibara ndogo ya (3), lengo ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifafanua kuwa msingi wa kutoweka muda kwa Afisa Mwandikishaji kutoa uamuzi ni wingi wa mapingamizi yanayoweza kuwasilishwa ikilinganishwa na rasilimali watu iliyopo kwa wakati husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilishauri maboresho kwenye Ibara ya 23(2) kwa kuruhusu rufaa kuanzia Mahakama za Mwanzo. Lengo ni kuboresha huduma kwakuwa Kwa baadhi ya maeneo hususani vijijini Mahakama za Wilaya ziko mbali na Wananchi, hivyo ni vyema kutumia Mahakama za Mwanzo zilizokaribu zaidi na Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati kwa kuweka sharti kwa Afisa mwandikishaji kutoa uamuzi wa maombi ya mapitio ndani ya siku kumi na nne tangu kuwasilishwa kwa maombi hayo pamoja na kuweka sharti la rufaa kusikilizwa kuanzia Mahakama za Mwanzo, Maboresho hayo yamependekezwa na Kamati katika Ibara ya 28, 29 na 30 ya Muswada.

(ix) **Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 26 inaweka masharti ya pingamizi ya uwepo wa jina la mpiga kura katika Daftari la Awali la Wapiga kura, Kamati ilikuwa na maoni kuwa Ibara ya 26(2) inaruhusu Mkurugenzi wa uchaguzi au Afisa Mwandikishaji kuweka pingamizi kuhusu uwepo wa jina lolote katika daftari la awali la Wapiga Kura. Utaratibu huu unasaidia kuweka kumbukumbu sahihi za Daftari lakini unakiuka misingi ya haki ya asili. Utaratibu uliopo katika Ibara ya 157 ya Muswada unahusu kuomba taarifa za ziada utaratibu huo unaweza kutumika badala ya Afisa mwandikishaji kuweka pingamizi. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(x) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 27 inaweka masharti ya utaratibu wa pingamizi, Muswada unapendekeza kuwa Afisa

mwandikishaji hatokuwa na Wajibu wa kuwasilisha taarifa ya pingamizi popote, ikiwa pingamizi ni dhidi ya mtu aliyefariki. Kamati imeishauri Serikali kufanya maboresho kwa kuweka takwa la Afisa mwandikishaji kutoa tangazo kwa umma kupitia mbao za matangazo kuhusu pingamizi dhidi ya mtu aliyefariki. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xi) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 28 inaweka masharti ya Uchunguzi na uamuzi wa mapingamizi yanayofanywa na Afisa Mwandikishaji, ibara ndogo ya (8) inazuia Afisa mwandikishaji kuhojiwa kuhusu uhalali wa maamuzi ya pingamizi aliyoyaweka yeye mwenyewe, Kamati ilikuwa na mtizamo kuwa kwa kukiacha kifungu kama kilivyo kinaweza kutumika vibaya na maafisa waandikishaji. Serikali iliieleza Kamati kuwa watafanya maboresho ya ibara hiyo ili kuendana na masharti ya ibara ya 26(2).

(xii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 52 inaweka masharti yanayozuia mgombea wa Ubunge kuteuliwa kwenye nafasi zaidi ya moja, hata hivyo Ibara haijafafanua nafasi zaidi ya moja au nafasi nyingine yoyote ya kuchaguliwa ni ipi. Kamati iliitaka Serikali kufafanua zuio hilo lililenga nafasi ipi, Serikali iliifahamisha Kamati kuwa nafasi iliolengwa ni ya Udiwani na Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xiii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 57 inaweka takwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kutangaza kiti cha Udiwani wa halmashauri kuwa wazi mara atakapo taarifiwa kwa maandishi na Mwenyekiti wa Halmashauri. Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho kwa kuipa Tume jukumu la kutangaza kiti cha Diwani kuwa wazi baada ya kupokea taarifa rasmi kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayompa wajibu Tume kutangaza kiti cha Diwani kuwa wazi baada ya kupata taarifa rasmi kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

(xiv) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 79 na 84 zinazohusu masharti ya muundo wa karatasi za kura na utaratibu wa kupiga kura mtawalia, Kamati iliishauri Serikali kuongeza aya mpya 79(d) itakayo weka utratibu utakaozingatia watu wasioona ama wenye uwoni hafifu (kwa kuweka karatasi za nukta nundu) kwenye karatasi za kura pamoja na kuweka mfumo ujulikanao kama *tactile ballot templates*. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xv) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 88 inaweka masharti ya kuahirishwa kwa upigaji kura wakati inapotokea vurugu, Kamati ilikuwa na maoni kuwa sababu za kuhairisha zoezi la upigaji kura linaweza kusababishwa na vitu vingine kama vile majanga ya asili tofauti na vurugu au ghasia, lengo ni kuweka wigo mpana wa sababu za kuhairishwa kwa zoezi la upigaji kura. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

(xvi) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 102 inaweka masharti na wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura, ibara ndogo ya (1)(e) inampa wajibu msimamizi wa kituo kutoa fomu za taarifa za matokeo kwa kila wakala iwapo fomu za taarifa za matokeo zipo za kutosha. Kamati imeshauri iwe ni sharti la lazima kwa msimamizi wa kituo kutoa fomu hizo kwa mawakala na kwamba ahakikishe fomu hizo zinapatikana za kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

(xvii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 112 na 113 inahusu masharti ya Uteuzi wa Wanawake wa viti maalumu kwa nafasi ya Ubunge na Udiwani mtawalia, Kamati ilikuwa na maoni kuwa ni muhimu kuwepo na mfumo mahsusi wa upatikanaji wa Wanawake wa viti maalum utakaotumiwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kuwachagua kwa mujibu wa Ibara ya 81 ya Katiba, kukosekana kwa mfumo mahsusi wa upatikanaji wa wazi kwa Vyama vya Siasa kuteua Wabunge na Madiwani wa Viti Maalum inachochea rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

(xviii) **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 33, 34, 50 na 62 kwa ujumla zinaweka masharti ya vigezo vya mgombea kuteuliwa, Kamati ilishauri maeneo haya yote yazinagatie usawa wa jinsi na hali ya ulemavu kwenye masharti mahususi ya Ibara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

(xix) **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikuwa na maoni kuwa ni muhimu kuanzisha kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia wakati wa uchaguzi, vitendo vya unyanyasaji wa Kijinsia hasa wakati wa uchaguzi unafifisha jitihada za kitaifa kufikia usawa wa malengo ya uwiano wa 50/50 katika uongozi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati inayozingatia masharti hayo.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwako wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Akcson, Spika wa Bunge la Tanzania kwa kuiamini kamati na kuipa jukumu la kuchambua Muswada huu na Miswada mingine iliyoletwa mbele yako leo, na Mhe. Azzan Zungu Naibu Spika kwa ushirikianao wake wa karibu na kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Utawala katiba na Sheria kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**

2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga (Mb) Naibu Waziri wa Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Jim Yonazi Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati Ndg. Frank Nkya, Ndg. Ganjatuni Kilemile na Ndg. Ndoh'no William Abel kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Kamati pamoja na mtoa hoja.

Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

30 Januari, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023*(The Political Parties Affairs Laws [Amendment] Bill, 2023]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge. Mheshimiwa Ummy Nderiananga aje awasilishe Taarifa ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU – MHE. UMMY H. NDERIANANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaomba uniruhusu niache maneno ya utangulizi kwa kuwa, yameshatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia, kipekee, kuwatakia heri ya mwaka mpya Watanzania wote, lakini na

wanawake walioniamini Mkoa wa Kilimanjaro na wanawake Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza, kipekee, mume wangu kwa kunivumilia na kunisaidia majukumu yangu kipindi chote hiki ambacho ninakuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielekee kwenye Muswada. Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbili ambazo ni Sheria ya Gharama ya Uchaguzi, Sura ya 278 na Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hizi yanalenge kuimarisha demokrasia, utawala bora na masuala ya kijinsia ndani ya vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tatu; ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha jina la muswada na namna ambavyo sheria zinapendekezwa kurekebishwa katika sehemu zake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinapendekezwa kurekebishwa katika sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria za Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. Kifungu cha 7 kinarekebishwa, ili kuondoa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Wilaya na Afisa Mtendaji Kata na badala yake ziwasilishwe kwa msimamizi wa uchaguzi na msimamizi msaidizi wa uchaguzi. Lengo la marejebisho haya ni kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinawasilishwa kwa watu sahihi kwa kuwa, si mara zote Mkurugenzi wa Halmashauri na Katibu Tawala wa Wilaya wanakuwa wasimizi wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 9 kinarekebishwa kwa kuboresha utaratibu wa kuchukua na kuwasilisha fomu za tamko la gharama za uchaguzi, ili fomu hizo zichukuliwe kwa msimamizi wa uchaguzi wakati mtia nia anachukua fomu za kuomba uteuzi na kuwasilishwa wakati wa kurejesha fomu za uteuzi. Lengo la marekebisho haya ni kutoa muda wa kutosha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia taarifa zinazowasilishwa na watia nia kuhusu gharama wanazokusudia kutumia katika uchaguzi, kabla hawajaanza shughuli za kampeni.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuweka sharti kwa vyama vya siasa kuwa na mwongozo wa uchaguzi ndani ya vyama na mfumo wa kuwapata wagombea wake, ikiwemo wagombea wa nafasi za Viti Maalum vya Wabunge na Madiwani wanawake.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa, ili kutenganisha muda wa mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kidini na asasi za kiraia kuwasilisha kwa msajili taarifa za gharama zinazotumika katika shughuli za uchaguzi, wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa kuwasilisha taarifa hizo kipindi cha uchaguzi mdogo kwa kuwa, kipindi hicho shughuli zinakuwa chache, ikilinganishwa na kipindi cha uchaguzi mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuainisha muda wa kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi wakati wa uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho hay ani kutenganisha muda wa kuwasilisha taarifa hizo wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo kwa kuwa, chama cha siasa hakiwezi kusubiri miezi sita ndipo kiwasilishe taarifa ya gharama za uchaguzi panapokuwa na uchaguzi mdogo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu hicho kinarekebishwa pia, ili kuondoa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, ili stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jedwali la 3 linapendekezwa kurekebishwa, ili kuzingatia masuala ya usawa wa jinsia na ujumuishwaji wa makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, hapa kipekee tuendelee kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tangu kuanzishwa kwa vyama vingi ni mara ya kwanza tutakuwa na sera hii mahususi kwa ajili ya ujumuishwaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu inapendekeza Kurekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258(3) kinarekebishwa kwa kuboresha tafsiri ya miasamiati "Chama cha Siasa" na kuongeza tafsiri ya misamiati mingine iliyotumika katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa miasamiati iliyotumika katika katika sheria inakuwa na maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(a) kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuuwezesha Mkutano Mkuu wa chama cha siasa kukasimisha jukumu lake la kuteuwa mgombea wa urais wa Zanzibar. Lengo la marekebisho hay ani kuruhusu uteuzi wa mgombea wa urais wa Zanzibar kufanywa na Halmashauri kuu ya chama.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(c) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka adhabu kwa chama cha siasa kitakachomruhusu mtu ambaye si raia wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya chama husika.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho ni kukomesha vitendo vya watu wasio raia kuingilia katika maamuzi ya vyama vya siasa kwa kuwa, kwa sasa sheria inaweka katazo, lakini hakuna adhabu. Aidha, Serikali inapendekeza Ibara ya 11 ifanyiwe marekebisho, ili kuweka ukomo wa chini wa adhabu inayopendekezwa kwa kosa husika, kama ilivyobainishwa katika aya (A) ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, pia, sheria inapendekeza kuongeza masharti mapya katika Muswada kwa lengo la kuondoa jinai

kwenye makosa ya jumla, kama ilivyobainishwa katika aja (b) na (d) ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuweka takwa kwa chama cha siasa kuwsilisha nakala ya kanuni zake wakati wa maombi ya usajili wa muda. Lengo la marekebisho haya ni kumpa msajili fursa ya kujiridhisha endapo kanuni hizo zimezingatia masharti ya sheria. Kifungu hicho kinarekebishwa pia, ili kuweka sharti kwa chama cha siasa kutoruhusu wanachama wake kufanya kitendo chochote kitakachohatarisha usalama wa chi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa, vyama vya siasa vinavyosajiliwa ni vile vinavyozingatia sheria, kanuni na taratibu mbalimbali kwa maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 10(c) kinapendekezwa kuongezwa, ili kubainisha nyaraka ambazo chama cha siasa kinapaswa kuwanazo wakati wote. Miongoni mwa nyaraka hizo ni Sera ya Jinsia na Ujumuisho, Kanuni za Fedha na Usimamizi wa Mali za Chama na Kanuni za Uteuzi wa Wagombea na Uchaguzi wa Viongozi wa Chama. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa chama cha siasa kinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, utawala bora, jinsia na kanuni ambazo kimejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa, ili kubainisha kuwa maandamano ya vyama vya siasa yatafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 322. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha masharti ya Kifungu cha 11 na Masharti ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi ambayo imeainisha utaratibu wa kuzingatiwa kabla na wakati wa kufanya maandamano au mikutano ya hadhara.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11(a) kinarekebishwa, ili kuviruhusu vyama kushirikiana hata wakati wa uchaguzi mdogo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13(a) kinapendekezwa kurekebishwa, ili kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa pale anapogundua kuwa mtu mwingine ametenda kosa au anakusudia kutenda kosa lolote chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utendaji wa makosa na kuhakikisha hatua zinachukuliwa dhidi ya mtu anayekiuka masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kumlinda mtoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sharti kuwa mgawanyo wa ruzuku utafanywa kwa kuzingatia pia, matokeo ya uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu fedha za ruzuku kugawanywa kwa vyama vya siasa kwa kuzingatia idadi ya kura za Ubunge na idadi ya Wabunge na Madiwani ambao chama cha siasa kinao kwa wakati husika badala ya kura za Wabunge na idadi ya Wabunge na Madiwani ambao chama kilipata wakati wa uchaguzi mkuu pekee.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 19, 20 na 21 (e), vinapendekezwa kurekebishwa ili kuyaainisha masharti kuhusu kusitishwa au kufutwa kwa usajili wa chama cha siasa na zuio kwa mwanachama kushiriki katika shughuli za siasa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa masharti ya vifungu hivyo yanaakisi maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Tatu linapendekezwa kuongezwa ili kuainisha masuala ambayo chama cha siasa kitapata kujumuisha katika Sera ya Jinsia na Ujumuishi wa Makundi Maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ushiriki wa wanawake na makundi maalumu katika shughuli za siasa ndani ya vyama vya siasa. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Ibara ya 21 ya Muswada kwa lengo la kuvitaka vyama vya siasa kuweka katika Sera zao za Jinsia na Ujumuishi wa Makundi Maalumu, tamko kuhusu uzingatiaji wa jinsia katika mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama, kama ilivyoainishwa kwenye aya hii ya Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba kutumia fursa hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Jenista, kwa malezi na kwa namna ambavyo anaendelea kunipa fursa ya kujifunza uongozi. Ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kuwa sehemu ya Sheria za Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU) AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZINAZOHUSU VYAMA VYA SIASA WA MWAKA 2023 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tatu (13) wa Bunge la Kumi na Mbili (12), tarehe 10 Novemba, 2023.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa ya kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa uongozi wake mahiri na shupavu kwa nchi yetu

katika nyanja zote. Hakika Mheshimiwa Rais ni Kiongozi mzalendo, mchapakazi na anapenda nchi yetu. Ninamshukuru na kumpongeza sana kwa juhudi kubwa anazofanya za kuboresha demokrasia na mazingira ya kufanya siasa nchini chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa na hivyo kuwaletea Watanzania maendeleo makubwa ya kijamii na kiuchumi.

5. **Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza Demokrasia na kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ilianza kuwekwa wazi mapema tarehe 22 Aprili 2021 alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma. Mheshimiwa Rais aliahidi kudumisha Tunu za Taifa letu yaani Amani, Umoja na Mshikamano. Hata hivyo, alisisitiza nia yake ya kulinda misingi ya Demokrasia na Uhuru wa watu kwa kusema yafuatayo "**Uhuru na Demokrasia ni Msingi wa Amani katika Nchi na pia husaidia kuchochea maendeleo ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii ".** Tarehe 01 Julai, 2022 Tanzania iliadhimisha miaka 30 tangu kurejea kwa mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa. Mheshimiwa Rais, alisisitiza tena dhamira yake ya kukuza Demokrasia nchini kupitia Makala aliyoiandaa ambapo alisema "**Nimedhamiria kwamba, Kwenye kuenzi miaka yetu ya demokrasia ya Vyama Vingi, Serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya Kisiasa, Kiuchumi na Katika Sheria za Uchaguzi** ".

6. **Mheshimiwa Spika,** ni wakati huo Mheshimiwa Rais alieleza falsafa yake ya kuongoza nchi inayojengwa kwa misingi ya Falsafa ya 'R' 4 ambazo maana yake ni **Reconciliation, Resilience, Reforms and Rebuild** ikiwa na maana ya Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi mpya wa Taifa. Falsafa hiyo, inatoa dira na mwongozo wa uongozi katika nchi yetu ili kudumisha amani, mshikamano na umoja wa Kitaifa. Kutokana na dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini matokeo yake ni pamoja na kuundwa kwa Kikosi Kazi ambacho kilifanyia kazi masuala yanayohusu Demokrasia ya

Vyama Vingi vya Siasa nchini kilichokuja na mapendekezo ya kuboresha mfumo wa demokrasia ambapo matunda ya dhamira hiyo ya dhati ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake imeanza kutekelezwa kwa vitendo.

7. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi kifupi tumeshuhudia Serikali ya Awamu ya Sita ikifanya mageuzi makubwa katika kuimarisha Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini ikiwa ni pamoja na;

i. Kukutana na kufanya mazunumzo na Viongozi wa Kitaifa wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Serikali wastaafu akiwa na lengo la kubadilishana mawazo kuhusu namna bora ya kuboresha na kudumisha mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa;

ii. Kuanzisha mazungumzo baina ya Serikali, Chama Tawala (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa lengo la kufikia maridhiano pamoja na kuchukua hatua kadhaa za kushajihisha maridhiano na Chama cha Demokrasia na Maendeleo katika masuala kadhaa muhimu na ya kimsingi yaliyowasilishwa Serikalini na CHADEMA;

iii. Kuruhusu kufanyika kwa mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa Nchini;

iv. Kupitia Baraza la Vyama vya Siasa, amefanikisha na kuliwezesha Baraza la Vyama vya Siasa Nchini kuwa na kifungu maalumu cha bajeti ya kuendesha shughuli za Demokrasia na Vyama vya Siasa na vilevile kufanikisha mikutano mikubwa mitatu (3) ya wadau wa Demokrasia ili kujadili mustakabali wa demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa katika nchi letu;

v. Na leo tunashuhudia kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza mapendekezo ya Kikosi Kazi, Baraza la Vyama vya Siasa Nchini, na Wadau wa Demokrasia kuhakikisha Sheria zinazosimamia Uchaguzi zinawasilishwa Bungeni,

tena bila kupitia uwasilishaji wa Sheria kwa Hati ya Dharula ya Rais. Juhudu hizi pamoja na nyingine zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha Utawala Bora na Mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa nchini zinalenga kudumisha na kuboresha maslahi mapana ya Watanzania na Taifa zima kwa ujumla.

**8.** **Mheshimiwa Spika,** niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuziona hatua hizi ni za kupongezwa na siyo za kubezwa. Taasisi mbalimbali duniani kwa kutambua mchango wake mkubwa katika kukuza demokrasia nchini, zimemtunuku tuzo mbalimbali za heshima ikiwa ni pamoja na Tuzo ya Heshima kwa kutambua mchango wake katika kutetea, kulinda na kuimarisha haki za binadamu katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa iliyotolewa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu 2023; tuzo mbili zilizotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Watetezi na Amani ambazo ni tuzo ya amani duniani ya 2022 na tuzo ya Rais wa Dhahabu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo ameweka rekodi ya kuwa Rais mwanamke wa kwanza kuipata Barani Afrika. Kutokana na kazi kubwa aliyoifanya, tarehe 7 Disemba, 2021 alitambulika kimataifa na Jarida maarufu na kubwa duniani la Forbes kuwa ni kati ya wanawake 100 wenye uwezo wa uongozi na ushawishi mkubwa duniani.

**9.** **Mheshimiwa Spika,** pia, nimshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar** kwa juhudi kubwa anazofanya katika kuleta maendeleo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

**10.** **Mheshimiwa Spika,** vilevile, nimshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa miongozo na maelekezo yake katika kuhakikisha Serikali inafanikisha mchakato mzima wa

Muswada huu. Pia, nimshukuru **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar** na **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu** katika kufanikisha Muswada huu. Pongezi na shukrani za dhati ninaziwasilisha kwa **Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar** (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) na Ofisi yake kwa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha mchakato mzima wa Muswada huu.

**11.** kwa dhati, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Mabunge Duniani (Inter Parliamentary Union) na Rais wa kwanza mwanamke kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo. Hii ni fahari na heshima kubwa kwa nchi yetu kwani inaonesha ukuaji wa diplomasia na ni kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi Duniani wanayo juu ya nchi yetu na wewe mwenyewe. Kwa dhati, nikupongeze sna na kukushukuru kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Umeonesha umahili na ubobezi wa hali ya juu.

**12. Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**13. Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu mkubwa nimshukuru sana sana pacha wangu na mshauri wangu wa karibu **Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Wziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),** kwa ushirikianao mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu

kwani ni mchapa kazi hodari ambaye ana mchango mkubwa sana katika kuhakikisha Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza majukumu yake ipasavyo; **Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu** waliowezesha muswada huu kufikia hatua ya leo.

**14. Mheshimiwa Spika,** nitoe shukrani zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalam wake pamoja na wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

**15.** Kipekee na kwa dhati kabisa ninakishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani. Aidha, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano, kukiamini Chama cha Mapinduzi na kumuunga mkono Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika juhudi anazofanya za kuleta maendeleo nchini.

**16. Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbili ambazo ni Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 na Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hizi yanalenga kuimarisha demokrasia, utawala bora na masuala ya kijinsia ndani ya Vyama vya Siasa.

**17. Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinapendekezwa kurekebishwa katika Sehemu zake.

**18. Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo Sheia zinapendekezwa kurekebishwa katika sehemu husika.

19. **Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. Kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuondoa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Wilaya na Afisa Mtendaji Kata na badala yake ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

20. **Mheshimiwa Spika,** lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinawasilishwa kwa watu sahihi kwa kuwa si mara zote Mkurugenzi wa Halmashauri na Katibu Tawala wa Wilaya wanakuwa wasimamizi wa uchaguzi. Kifungu cha 9 kinarekebishwa kwa kuboresha utaratibu wa kuchukua na kuwasilisha fomu za tamko la gharama za uchaguzi ili fomu hizo zichukuliwe kwa msimamizi wa uchaguzi wakati mtia nia anachukua fomu za kuomba uteuzi na kuwasilishwa wakati wa kurejesha fomu za uteuzi. Lengo la marekebisho haya ni kutoa muda wa kutosha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia taarifa zinazowasilishwa na watia nia kuhusu gharama wanazokusudia kutumia katika uchaguzi kabla hawajaanza shughuli za kampeni.

21. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka sharti kwa Vyama vya Siasa kuwa na mwongozo wa uchaguzi ndani ya vyama na mfumo wa kuwapata wagombea wake ikiwemo wagombea wa nafasi za Viti Maalumu vya Wabunge na Madiwani wanawake.

22. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutenganisha muda wa mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kidini na asasi za kiraia kuwasilisha kwa Msajili taarifa za gharama zilizotumika katika shughuli za uchaguzi wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa kuwasilisha taarifa hizo kipindi cha uchaguzi mdogo kwa kuwa kipindi hicho shughuli zinakuwa chache ikilinganishwa na kipindi cha uchaguzi mkuu.

23. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi wakati wa uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kutenganisha muda wa kuwasilisha taarifa hizo wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo kwa kuwa chama cha siasa hakiwezi kusubiri miezi sita ndipo kiwasilishe taarifa ya gharama za uchaguzi panapokuwa na uchaguzi mdogo. Aidha, kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kuondoa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu.

24. **Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Tatu linapendezwa kurekebishwa ili kuzingatia masuala ya usawa wa jinsia na ujumuishwaji wa Makundi Maalum.

25. **Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu inapendekeza kurekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuboresha tafsiri ya msamiati "chama cha siasa" na kuongeza tafsiri ya misamiati mingine iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa misamiati iliyotumika katika Sheria inakuwa na maana iliyokusudiwa. Kifungu cha 6A kinapendekezwa kurekebishwa ili kuuwezesha Mkutano Mkuu wa chama cha siasa kukasimisha jukumu lake la kuteua mgombea wa urais wa Zanzibar. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu uteuzi wa mgombea wa urais wa Zanzibar kufanywa na Halmashauri Kuu ya chama.

26. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6C kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka adhabu kwa chama cha siasa kitakachomruhusu mtu ambaye si raia wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya chama husika. Lengo la marekebisho ni kukomesha vitendo vya watu wasio raia kuingilia katika maamuzi ya vyama vya siasa kwa kuwa kwa sasa Sheria inaweka katazo lakini hakuna adhabu. Aidha, Serikali inapendekeza **ibara ya 11** ifanyiwe

marekebisho ili kuweka ukomo wa chini wa adhabu inayopendekezwa kwa kosa husika kama inavyobainishwa katika **Aya 'A'** ya Jedwali la Marekebisho. Pia, Serikali inapendekeza kuongeza masharti mapya katika Muswada kwa lengo la kuondoa jinai kwenye makosa ya jumla kama inavyobainishwa katika **Aya 'B' na 'D'** ya Jedwali la Marekebisho.

**27. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka takwa kwa chama cha siasa kuwasilisha nakala ya kanuni zake wakati wa maombi ya usajili wa muda. Lengo la marekebisho haya ni kumpa Msajili fursa ya kujiridhisha endapo kanuni hizo zimezingatia masharti ya Sheria. Kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kuweka masharti ka Chama cha Siasa kutoruhusu wanachama wake kufanya kitendo chochote kinachohatarisha usalama wa nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa vyama vya siasa vinavyosajiliwa ni vile vinavyozingatia sheria, kanuni na taratibu mbalimbali kwa maslahi mapana ya nchi.

**28. Mheshimiwa Spika,** Kifungu kipya cha 10C kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha nyaraka ambazo chama cha siasa kinapaswa kuwa nazo wakati wote. Miongoni mwa nyaraka hizo ni sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalumu, kanuni za fedha na usimamizi wa mali za Chama na kanuni za uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi wa Chama. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa Chama cha Siasa kinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, utawala bora, jinsia na kanuni kilizojiwekea.

**29. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha kuwa maandamano ya vyama vya siasa yatafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 322. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya kifungu cha 11 na masharti ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi ambayo imeainisha utaratibu wa kuzingatiwa kabla na wakati wa kufanya maandamano au mikutano ya hadhara. Kifungu cha 11A kinarekebishwa ili kuviruhusu vyama kushirikiana hata wakati

wa uchaguzi mdogo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika Sheria.

30. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 13A kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa pale anapogundua kuwa mtu mwingine ametenda kosa au anakusudia kutenda kosa lolote chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utendaji wa makosa na kuhakikisha hatua zinachukuliwa dhidi ya mtu anayekiuka masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kumlinda mtoa taarifa.

31. **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sharti kuwa mgawanyo wa ruzuku utafanywa kwa kuzingatia pia matokeo ya uchaguzi mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu fedha za ruzuku kugawanywa kwa vyama vya siasa kwa kuzingatia idadi ya kura za ubunge na idadi ya wabunge na madiwani ambao chama cha siasa kinao kwa wakati husika badala ya kura za ubunge na idadi ya wabunge na madiwani ambao chama kilipata wakati wa uchaguzi mkuu pekee.

32. **Mheshimiwa Spika,** Vifungu vya 19, 20 na 21E vinapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha masharti kuhusu kusitishwa au kufutwa kwa usajili wa chama cha siasa na zuio kwa mwanachama kushiriki katika shughuli za siasa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa masharti ya vifungu hivyo yanaakisi maana iliyokusudiwa.

33. **Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Tatu linapendekezwa kuongezwa ili kuainisha masuala ambayo chama cha siasa kitapaswa kujumuisha katika sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ushiriki wa wanawake na makundi maalumu katika shughuli za siasa ndani ya vyama vya siasa. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya ibara ya 21 ya Muswada kwa lengo la kuvitaka Vyama vya Siasa kuweka katika Sera zao za jinsia na ujumishi wa makundi maalum tamko kuhusu uzingatiaji wa jinsia katika mchakato wa uteuzi

wa wagombea ndani ya Vyama kama inavyoainishwa kwenye aya **'E'** ya Jedwali la Marekebisho.

**34. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

**35. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Jenista Joakim Mhagama (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(SERA BUNGE NA URATIBU)**
**30 Januari, 2024**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Abdullah Hassan Mwinyi, aje awasilishe mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws Armendment Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa 13 Kikao cha 10 kwenye Bunge la 12, tarehe 10 Novemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1), ikisomwa pamoja na na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7 (1) (b), cha Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulielekeza Muswada huu uje kwenye Kamati ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maoni ya wadau, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu pamoja na maoni hayo ya wadau.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 25 Januari, 2024, Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada. Baada ya hatua hiyo na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ninakujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bunge.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ilipokutana na wadau, hoja 11 ziliibuliwa na wadau na hoja zote zimeorodheshwa katika ukurasa wa 8 – 20. Kwa kuzingatia muda, naomba hoja hizo ziorodheshwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa hoja hizo pamoja na maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Kamati ilibaini changamoto

au mapungufu katika Muswada. Baadhi ya changamoto zilizobainika utatuzi wake unahitaji mabadiliko ya sheria zingine ambazo hazijafanyiwa kazi na Kamati kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada; Kamati ilichambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023, ukiwa umegawanyika katika sehemu tatu, na unapendekeza kufanya marekebisho katika sehemu mbili, kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni hizi zifuatazo: -

i) Marekebisho ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura 278 *(The Election Expenses Act)* na

ii) Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258 *(The Political Parties Act)*.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya Kwanza inayoelezea jina fupi la Muswada na Ibara ya Pili inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake. Sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura 278 *(The Election Expenses Act),* marekebisho ambayo yanafafanuliwa katika Ibara ya Tatu hadi Ibara ya Saba ya Muswada. Marekebishi katika sehemu hii kwa ujumla yanalenga kuondoa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Wilaya na Afisa Mtendaji katika siku mbili kabla ya kuanza kwa mchakato wa uteuzi au siku saba baada ya uteuzi na badala yake ziwasilishwe kwa Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi na Msimamizi Mkuu Msaidizi wa Uchaguzi ili kuhakikisha taarifa hizo zinawasilishwa kwa watu sahihi kwa kuwa si mara zote wakurugenzi wamekuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya pia yanakuja kuweka utaratibu wa vyama vya siasa, wagombea, asasi za kiraia na taasisi za kidini kutoa taarifa ya vyanzo vya mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi kabla na baada ya uchaguzi, ndani ya siku 90 kwa Uchaguzi Mkuu au siku 30 kwa Uchaguzi Mdogo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa kuwasilisha taarifa hizo kipindi cha uchaguzi mdogo kwa kuwa kipindi hicho shughuli zinakuwa chache ikilinganishwa na kipindi cha uchaguzi mkuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho haya yanakuja kuondoa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, badala yake stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Mkaguzi na kuondoa adhabu ya kulipa faini pamoja na kufungiwa kushiriki uchaguzi wa aina yoyote kwa vyama vya siasa vitakavyoshindwa kuwasilisha taarifa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, marekebisho yanalenga takwa la uwasilishaji wa taarifa za mapato na matumizi wakati wa uteuzi wa wagombea na baada uchaguzi, kuwasilishwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ndani ya siku 180 kwa uchaguzi mkuu na ndani ya siku 90 kwa uchaguzi mdogo, na ziambatanishwe na taarifa ya mapato na matumizi ya mgombea husika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258 *(The Political Parties Act, CAP. 258)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya Nane hadi Ibara ya 21 ambapo marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii, yanalenga kuongeza msamiati na kuboresha msamiati mbalimbali ili kutoa ufafanuzi wa maneno yaliyotumika kwenye sheria lakini hayajatafsiriwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa misamiati iliyotumika katika sheria hii inakuwa na maana iliyokusudiwa. Pia, marekebisho haya yanalenga kuongeza jedwali ambalo litaainisha masuala ambayo chama cha siasa kitapaswa kujumuisha katika Sera ya Jinsia na Ujumuishi wa

Makundi Maalumu; lengo likiwa ni kuongeza ushiriki wa wanawake na makundi maalumu katika shughuli za siasa ndani ya vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inayofanyiwa marekebisho katika Kifungu cha 10 kwa kuongeza Kifungu cha 10 (c) inapendekeza kuweka sharti kwa chama cha siasa chenye usajili wa kudumu kuwa na nyaraka muhimu za chama zikiwepo sheria, kanuni pamoja na Sera ya Jinsia na Ujumuishi wa Makundi Maalumu, kanuni za fedha na usimamizi wa mali na kanuni za uteuzi wa wagombea wa uchaguzi wa viongozi wa chama.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine katika sehemu hii yanalenga kukomesha vitendo vya watu ambao si raia wa Tanzania kushirikia katika mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya chama. Marekebisho haya yanafanyika ili kuweka adhabu kwa chama cha siasa kitakachomruhusu mtu ambaye si raia wa Tanzania kushiriki katika kufanya maamuzi ya chama. Pia, marekebisho haya yanalenga kuhakikisha vyama vya siasa nchini vinafuata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali kwa maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati, maelezo ya utangulizi. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati waliyatolea maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura 278. Katika Ibara ya Nne ya Muswada, Kamati iliomba ufafanuzi iwapo mapendekezo haya yatamnyima fursa mgombea, kubadili ama kuboresha taarifa za timu ya kampeni. Kamati ilishauri kuwa sheria iboreshe mashari ya Ibara hii ili yaweze kumruhusu mgombea kuwa na uwezo wa kubadili au kuboresha taarifa za timu yake ya kampeni pindi atakapoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, katika kutolea ufafanuzi hoja hii, Serikali ilieleza kuwa inatambua kuna uwezekano wa timu ya kampeni kubadilika, hivyo, maboresho yanayofanywa na Muswada hayamnyimi mgombea fursa ya kubadili timu yake. Kwa kutambua hilo, Kanuni ya 17 ya Kanuni ya Sheria za Gharama za Uchaguzi, Tangazo la Serikali Na. 246 la 2010, inaruhusu wagombea kubadili taarifa za timu zao za kampeni. Hivyo, Serikali ilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo ili masharti hayo yaendelee kuwa kwenye kanuni. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutolea ufafanuzi suala hilo na hivyo Kamati inakubaliana na Serikali kuwa Ibara ibaki kuwa kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 ambayo inarekebisha Kifungu cha 6(c) na kuongeza Kifungu Kidogo cha 7, kwa kuweka adhabu ya shilingi zisizozizidi milioni 20 kwa chama cha siasa kitachomruhusu mtu ambaye siyo raia kushiriki katika mchakato wa chama, katika kufanya maamuzi yake, Kamati ilikuwa na maoni kuwa adhabu ya faini inayopendekezwa, haijawekewa kiwango cha chini isipokuwa ina kiwango cha juu pekee. Hivyo, Kamati ilishauri kuwa Kifungu kiweke adhabu ya kiwango cha chini ili kuweka uandishi mzuri wa sheria. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuweka kiwango cha chini na kiwango cha juu cha adhabu kama ilivyoshauriwa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Ibara ya 11 inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuongeza Ibara Ndogo ya Nane na Tisa ili kuweka zuio kwa mtu aliyeshiriki katika kutoa maamuzi ya kinidhamu kwa mwanachama kutoshiriki katika rufaa iliyokatwa na wanachama husika. Kamati ilikuwa na mapendekezo kuwa Ibara hii ifutwe ili kuruhusu chama cha siasa, kiruhusu Wajumbe ambao wana mamlaka ya kuhudhuria katika ngazi zote za kinidhamu za chama kufanya hivyo. Msingi wa mapendekezo haya ni kuwa, vikao vya vyama vyenye ngazi ya awali havifanyi maamuzi ya mwisho bali vinatoa mapendekezo kwa ngazi za juu. Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Kamati, kwa kufuta Ibara Ndogo ya Nane na Tisa.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 16, Kamati ilitaka kupata ufafanuzi kama upo uwezekano wa ugawaji wa asilimia 10 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya ruzuku kwa vyama vyote vya siasa vyenye usajili kamili (usajili wa kudumu) kwa masharti kwamba chama husika kiwe kimeshiriki angalau Chaguzi Kuu mbili mfululizo. Katika kutolea ufafanuzi pendekezo hili Serikali ilishauri kuwa, kwa kuwa vyama vya siasa huwepa ruzuku ili kuhudumia maeneo ya utawala ambayo wameshinda, kuvipa vyama vyote ruzuku kunaweza kusababisha idadi kubwa ya vyama vya siasa kuanzishwa kwa lengo la kujipatia ruzuku, kuchochea migogoro ndani ya vyama, kunufaisha watu binafsi na kutengeneza makundi ndani ya vyama vya siasa, hali ambayo haitakuza demokrasia nakuongeza gharama kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuvipa ruzuku vyama vyote kunaweza kusababisha uwezekano wa kudai zaidi, kwa kuwa itakuwa ni haki ya vyama vya siasa kisheria. Endapo vitanyimwa usajli kwa kigezo kwamba Serikali haina fedha za kulipa ruzuku baada ya kuvisajili vinaweza kuishitaki Serikali kwamba inakiuka haki yao ya Kikatiba ya kushirikiana na wengine, kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufafanuzi huo, Kamati ilikubaliana na ufafanuzi wa Serikali na kukubali Ibara ibaki kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada. Kwa muktadha huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushuri wa Kamati na kufanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati, kwanza kwako wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiamini Kamati yetu kuipa jukumu la kuchambua Muswada huu na Miswada mingine iliyoletwa mbele ya Kamati yetu. Halikadhalika, shukrani zetu ziende kwa Kamati ya Uongozi kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa kuujadili na

kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yaliyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Naibu Waziri wa Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Eliezer Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Jim Yonazi, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Ndugu Onorius Njole pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kufanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati, Ndg. Frank Nkya, Ndg. Ganjatuni Kilemile na Ndg. Ndoh'no William Abel kwa uratibu wa shuguli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Kamati kuhusu hoja. Baada ya kusema hayo Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadii, kuukubali, kuupitisha Muswada huu pamoja la Jedwali la Marekebisho, kama ilivyowasilishwa na Kamati pamoja na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshasikiliza Serikali ikiwa imewasilisha maelezo yao kuhusu Miswada mitatu ambayo ilipelekwa mbele ya Kamati, katika maelezo yao baadhi ya mambo wamekubaliana na Kamati na Kamati pia imekuja kutueleza hapa mambo ambayo wamekubaliana na Serikali lakini yapo mambo mengine ambayo Kamati imesema italeta marekebisho.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu wetu kutakuwa na uchangiaji. Uchangiaji huu kwa sababu Miswada yote mitatu itachangiwa kwa kipindi hiki, kwa hivyo mtu akisimama mara moja maana yake unachangia yote hautapewa tena nafasi ya kuchangia. Hivyo kwa sababu utaratibu wetu kidogo muda huwa unatubana lakini kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge, kuweza kujadili Miswada hii kwa ukamilifu, kwa sababu ipo mingi. Mbunge atakayesimama, ukitumia muda kidogo tutakushukuru lakini muda utakaotolewa na Bunge kwa ajili ya majadiliano ya Waheshimiwa Wabunge, utakuwa ni dakika 15 kwa kila Mbunge. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge ambao watapewa nafasi ya kuchangia mchana kabla sijaleta matangazo yaliyokuja hapa ambao tutaanza nao kwa sababu mawasilisho yameshakamilika kwa upande wa Serikali na Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Mohamed Said Issa. Hao tutaanza nao tutakapokutana kipindi chetu cha pili kwa siku ya leo na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokuwa unakwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili hapa. Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge, anatutangazia waheshimiwa wabunge wote kuwa Taasisi ya Mifupa *(MOI)* wapo katika viwanja vya Bunge kuelezea huduma mpya ya matibabu kwa viongozi, yaani *fast track* iliyoanzishwa na taasisi hiyo. Aidha kutakuwa na madaktari bingwa wa magonjwa ya mifupa, magoti, nyonga, ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu ambao watatoa ushauri na upimaji.

Zoezi hili litaanza leo tarehe 30 Januari, 2024 na litaendelea hadi tarehe 4 Februari, 2024. Waheshimiwa Wabunge, huduma hii inatolewa nyuma ya Ukumbi wa Msekwa, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wote mnakaribishwa kutumia fursa hii.

Nafikiri Waheshimiwa Wabunge pia Mheshimiwa Waziri wa Afya, ama Naibu Waziri wa Afya atusaidie pia katika kipindi hiki maadamu hawa wametajwa *MOI* na wanatoka kule Muhimbili, pengine na Dokta Janabi aje atueleze vizuri. Daktari huyu, Dokta Janabi, lakini pia Profesa kwa machapisho na tafiti aje atueleze yale mambo ya chakula tunaona kama anatubana sana kwenye masharti, sasa kidogo anatutia wasiwasi, hasa akisema sisi ni wateja wake watarajiwa. Sasa hatutaki kwenda huko lakini katika kipindi hiki tutafurahi na yeye awepo hapo ili tuwe tunamuuliza maswali, sasa ugali tutakula lini, wali tutakula lini, maana anatukataza mambo mengi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho ni tangazo ambalo nilisema ile asubuhi na hatukupata nafasi ya kulisikia, tangazo limekamilika na lipo sasa mbele yangu nililete kwenu, hii ni taarifa inayotoka kwa viongozi wetu wa Bunge Bonanza.

Hii ni taarifa ya Azania Bunge Bonanza lililofanyika Jumamosi tarehe 27 Januari, 2024 Viwanja vya Jamhuri Dodoma. Azania Bunge Bonanza limetufungulia mabonanza ambayo yataendelea huko mwakani, kwa hiyo Bunge Bonanza la kwanza la mwaka huu lililofanyika Jumamosi tarehe 27 Januari, 2024 lilishirikisha Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wawakilishi Sita kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Watumishi wa Ofisi ya Bunge pamoja na Watumishi wa Benki ya Azania, ambapo Benki ya Azania ndiyo walikuwa wadhamini wakuu wa bonanza hilo lililobeba kauli mbiu ya "Utani wetu Umoja wetu". *(Makofi)*

Aidha, bonanza hili lilikuwa maalum kwa michuano kati ya Wabunge na watumishi ambao ni mashabiki wa timu za *Simba Sports Club* na *Young Africans Sports Club* kwa upande mwingine. Ambapo michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu, kufukuza kuku, kupenya kwenye pipa, bao, drafti, karata, kula chakula na soda kwa haraka ilishindaniwa.

Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya michezo ninayo hapa na naona nimeletewa nakala kadhaa kuashiria kwamba washindi

wanataka wajulikane. Nilikuwa nimekusudia kutokusoma tena lakini nimeletewa karatasi nyingi sana hapa mbele.

Haya, washindi wa medali. Washindi wa kwanza wa kila mchezo wa mtu mmoja mmoja waliyopewa medali ya dhahabu kwa upande wa Wabunge ni hawa wafuatao: -

Michezo ya burudani, yaani ya jadi. Kukimbia na yai kwenye kijiko, Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambaye anashabikia Yanga. Kukimbia na gunia, Mheshimiwa Flatei Massay anashabikia Simba. *(Makofi)*

Mchezo wa karata wanawake ni Mheshimiwa Esther N. Matiko wa Simba, mchezo wa drafti wanawake ni Mheshimiwa Grace Tendega wa Simba. Mchezo wa drafti wanaume mshindi ni Mheshimiwa George Mwenisongole wa Yanga. Mchezo wa bao wanawake mshindi ni Mheshimiwa Esther Matiko wa Simba. Mchezo wa bao wanaume mshindi ni Mheshimiwa Tabasam Mwagao wa Simba. *(Makofi)*

Michezo ya ndani, *(indoor games)*. Mchezo wa *pool table* wanawake mshindi ni Mheshimiwa Esther Matiko wa Simba. Mchezo wa *pool table* wanaume ni Mheshimiwa hapa ameandikwa Nkungu, wamekosea jina nadhani ni Mheshimiwa Hassan Z. Kungu wa Yanga. *(Makofi)*

Mchezo wa vishale wanaume mshindi ni Mheshimiwa Yahaya Massare wa Simba. Mchezo wa vishale wanawake ni Mheshimiwa Khadija Taya, wa Yanga. Hapa naambiwa wachezaji wa Simba *Sports Club* hawakutokea uwanjani kuashiria kwamba mchezo wa vishale wanawake Mheshimiwa Khadija Taya, alipata ushindi wa mezani. *(Kicheko/Makofi)*

Mpira wa meza wanaume mshindi ni Mheshimiwa Francis Isack Mtinga wa Simba. Kurusha tufe wanaume ni Mheshimiwa Constantine John Kanyasu wa Yanga. *(Makofi)*

Michezo ya nje *(outdoor games)*. Michezo ya mbio, mbio za vijiti wanawake timu ya Simba *Sports Club* ilishinda. Mbio za mita

1500 wanawake, mshindi ni Mheshimiwa Anatropia Theonest wa Simba. Kuvuta Kamba wanawake washindi ni Yanga walishinda seti mbili kwa sifuri kwani wachezaji wa Simba hawakutokea uwanjani. Kwa hiyo, kuvuta kamba upande wa wanawake Yanga walishinda ushindi wa mezani. *(Kicheko/Makofi)*

Kuvuta kamba wanaume, Yanga walishinda kwa seti mbili kwa sifuri. Michezo ya timu, mpira wa wavu wanaume, timu ya Yanga walishinda seti mbili kwa sifuri. Mpira wa wavu wanawake, Simba walishinda seti mbili kwa sifuri. Mpira wa pete timu ya wanawake Simba walishinda magori 24 kwa nne. *(Makofi)*

Mpira wa kikapu, wanaume Simba walishinda seti 20 kwa sifuri. Mpira wa kikapu wanawake, Simba walishinda seti 24 kwa 11. Mpira wa miguu Yanga walishinda kwa mikwaju ya penati magoli matano kwa nne. Haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, washindi wa jumla kwenye bonanza hilo walikuwa ni timu ya mashabiki wa Simba *Sports Club* ambao naona Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameghairi kupiga makofi kwa sababu anawasaidia yanga, dhidi ya wapinzani wao mashabiki wa Yanga *Sports Club*. Kwa hivyo, mashabiki wa Simba walishinda kwa alama 107 dhidi ya wapinzani wao mashabiki wa Yanga ambao walipata alama 106. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Kwa sababu pointi za mezani nazo zimehesabiwa! Kwa hiyo Yanga ndiyo hamuamini ama Simba ndiyo hamuamini? Aah! Simba hamuamini kama Yanga wamefikisha 106?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa, basi hakuna shida kwa sababu nia ilikuwa ni michezo watu wote wafurahi, basi wacha na Yanga nao wafurahi kwa kuwakaribia sana Simba kwenye nafasi zao. *(Kicheko/Makofi)*

**30 JANUARI, 2024**

**TAARIFA YA AZANIA BUNGE BONANZA LILILOFANYIKA JUMAMOSI, 27/01/2024 - VIWANJA VYA JAMHURI, DODOMA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

Bunge Bonanza la kwanza Mwaka huu lililofanyika Jumamosi tarehe 27/01/2024 likishirikisha Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wawakilishi Sita kutoka Baraza la Wakilishi Zanzibar, Watumishi wa Ofisi ya Bunge pamoja na Watumishi wa Benki ya Azania, ambapo Benki ya Azania ndio walikua Wadhamini Wakuu wa Bonanza hilo, lililobebwa na Kauli Mbiu " ***Utani wetu ni Umoja Wetu*** ".

Aidha, Bonanza hili lilikuwa maalumu kwa michuano kati ya Wabunge na Watumishi wanaoshabikia Timu za Simba Sports Club na Young Africans Sports Club kwa upande mwingine, ambapo michezo mbalimbali kama vile Mpira wa Mguu, Mpira wa Pete, Mpira wa Kikapu, Kufukuza kuku, Kupenya kwenye Pipa, Bao, Drafti, Karata, Kula chakula na Soda kwa haraka n.k. ilishindaniwa.

**Matokeo ya Michezo:**

1. **Washindi wa Medali;**

Washindi wa Kwanza wa kila Mchezo wa mtu mmoja mmoja waolipewa Medali ya dhahabu, kwa Upande wa Wabunge ni hawa Wafuatao:-

***(a) Michezo ya Burdani (Jadi):***

i. Kukimbia na Yai Kwenye Kijiko: Mhe. Jackson Kiswaga – Yanga SC;

ii. Kukimbia na Gunia: Mhe. Fratei Maasay - Simba SC

iii. Mchezo wa Karata: Wanawake: Mhe. Esther Matiko - Simba SC;

iv. Mchezo wa Drafti: Wanawake: Mhe. Grace Tendega - Simba SC;

v. Mchezo wa Drafti: Wanaume: Mhe. George Mwenisongole – Yanga SC;

vi. Mchezo wa Bao: Wanawake: Mhe. Esther Matiko - Simba SC;

vii. Mchezo wa Bao: Wanaume: Mhe. Tabasamu Mwagao - Simba SC;

***(b) <u>Michezo ya Ndani (Indoor Games):</u>***

viii. Mchezo wa *Pool Table*: Wanawake: Mhe. Esther Matiko - Simba SC;

ix. Mchezo wa *Pool Table* Wanaume: Mhe. Hassan Zidadu Kungu - Yanga SC

x. Mchezo wa Vishale: Wanaume: Mhe. Yahya Massare – Simba SC;

xi. Mchezo wa Vishale: Wanawake: Mhe Khadija Taya – Yanga SC. **Wachezaji wa Simba SC hawakutokea Uwanjani;**

xii. Mpira wa Meza: Wanaume: Mhe. Francis Issack Mtinga – Simba SC;

xiii. Kurusha Tufe: Wanaume: Mhe. Constantine John Kanyasu - Yanga SC;

***(c) <u>Michezo ya Nje (Outdoor Games):</u>***

(i) **<u>Michezo ya Mbio</u>:**

- Mbio za Vijiti: Wanawake Timu ya Simba SC ilishinda;

- Mbio za Mita 1,500: Wanawake: Mhe. Anatropia Theonest Simba SC

- Kutembea kwa Haraka: Mita 800: Mhe. Regina Ndege Qwaray - Yanga S.C.

**(ii) Kuvuta Kamba:**

- Wanawake: Yanga walishinda Seti 2 kwa 0, kwani **Wachezaji wa Simba SC hawakutokea Uwanjani**;
- Wanaume: Yanga walishinda Seti 2 kwa 0

**(iii) Michezo ya Timu:**

i. Mpira wa Wavu: Wanaume: Yanga walishinda seti 2 kwa 0;

ii. Mpira wa Wavu: Wanawake: Simba walishinda seti 2 kwa 0

iii. Mpira wa Pete: Wanawake Simba walishinda magoli 24 kwa 4;

iv. Mpira wa Kikapu: Wanaume: Simba walishinda seti 20 kwa 0; Kwani **Wachezaji wa Yanga SC hawakutokea Uwanjani**;

v. Mpira wa Kikapu: Wanawake: Simba walishinda seti 24 kwa 11;

vi. Mpira wa Miguu: Yanga SC walishinda kwa mikwaju ya penati, Magoli 5 kwa 4;

**Washindi wa Jumla** kwenye Bonanza hilo Walikuwa ni **Timu ya Washabiki wa Simba SC** ambao waliopata alama **107** dhidi wa Wapinzani wao Washabiki wa Yanga SC waliopata Alama **106**.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na uchangiaji mchana kwa hiyo niwahimize sote tuwahi. Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi na Moja Kamili jioni leo.

*(Saa 07.09 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023

### Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mwaka 2023

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mawasilisho yalishafanywa na upande wa Serikali na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kwa hiyo, tulishawataja Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao kuchangia mchana huu. Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Baada ya wasilisho la Serikali na Kamati, napenda sasa kutoa mchango wangu kuchangia hoja zilizopo Mezani ambazo ni Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023. Vile vile, Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema ambayo ametupa, tumeona na mwaka mpya mzuri na ametuamsha salama leo. Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuongoza nchi yetu vizuri, lakini zaidi kwa kuja na falsafa hii ya R4 ambayo ni

ustamilivu ama *Reconciliation*, *Resilience, Reforms and Rebuilding*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeamua nianze hivyo kwa sababu Miswada hii mitatu, ukiangalia dhana ambayo inaongoza Miswada hii yote ni hii dhana ya Mheshimiwa Rais ya R4. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa hilo. Vile vile, Mheshimiwa Rais, ameendelea kuonesha nia njema ya kuleta utulivu nchini kwa kufanya mijadala ili tuzungumze hatima ya nchi yetu. Amani na mshikamano wa Taifa letu ni bora kuliko kitu kingine chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri wa Sera na Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri na *Attorney General* kwa kuileta Miswada hii Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza na wewe kwa kutuongoza vizuri katika mijadala hii ambayo imevuta hisia kubwa ya Watanzania walio wengi. Vile vile naipongeza Kamati ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Kizito Mhagama na Wajumbe wake wote ambao ni mahiri kwa kweli, wamefanya kazi nzuri sana. Tulikuwa kwenye *spotlight* kama Kamati, Mwenyekiti wangu alikuwa kwenye *headline*s za magazeti kwa sababu ya mvuto wa Miswada hii ambayo ipo hapa Bungeni hapa. Kwa hiyo, tunafurahi kwamba hata sisi tume-*appear* kwenye magazeti kwa sababu tulikuwa tunafuatiliwa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, nawashukuru wadau waliokuja mbele ya Kamati; walikuwa ni wengi sana ambapo sijawahi kuona Miswada ambayo Watanzania walio wengi wamejitokeza kutoa maoni yao. Kwa kweli kama Kamati tumejfunza mengi sana kutoka kwa wadau hawa. Wadau karibu 1,700 siyo kidogo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuwapa Watanzania fursa ya kuzungumza kwa siku zote nne kuanzia asubuhi mpaka jioni. Sisi kama Kamati kwa kweli tumefarijika na mazungumzo na maoni yaliyotolewa na Watanzania walio wengi. Kwa kweli, kama Kamati ukiangalia Muswada na mabadiliko yake, naipongeza Serikali kwa kukubaliana na Kamati mambo mengi. Hata kwa yale

maeneo machache ambayo Kamati imeleta jedwali, bado Serikali imeonesha nia njema sana kwenye maeneo hayo. Sisi nia yetu ni moja, wote tunataka kujenga Tanzania iliyo njema kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi, hoja kubwa kubwa zilizojitokeza wakati wadau wanaleta hoja zao. Kubwa kuliko yote ilikuwa ni jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Wadau walio wengi walipendelea sana jina liwe ni Tume Huru ya ya Uchaguzi. Kwa mujibu wa Muswada wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ibara ile ya (1), Watanzania walio wengi walitamani jina hili libadilike na liitwe Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, baada ya majadiliano makubwa kati ya Kamati na Serikali tukaanza kufikiri, hivi tukibadilisha jina, itavunja Katiba ama la.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imeelezea Tume, utaona dhahiri kwamba Katiba inasema na ninanukuu: "*Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao.*" Kwa hiyo, mantiki ya Kisheria ya Kikatiba ni dhahiri kwamba Tume ama Katiba haikusema Tume hii iitwe nini? Haija-*name* jina la Tume. Kwa hiyo, hiyo imetupa sisi *comfort* zaidi na baada ya kushauriwa na Serikali na hata kwenye jedwali la Serikali, tunakubaliana kwamba hakuna neno lolote la kisheria iitwe Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, wale ambao walikuwa wanafikiri labda kuna shida ya Kikatiba, hakuna. *Article 74* ipo *very clear.*

Mheshimiwa Spika, Sheria hii hii ya Tume ya Uchaguzi hususan Kamati ile ya Usaili, kwa mara ya kwanza tuna Wajumbe ambao wanapitia kwenye Kamati ya Usaili. Ikaja hoja ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, wadau wengi walikuwa wanasema na wale wapitiwe kwenye Kamati ile ya Usaili. Zikaibuka hoja za kikatiba na kisheria ikatusumbua kidogo, kwa sababu ni kweli ni kama Katiba ilitenga Wajumbe wale, kwamba hawa wana sifa maalum fulani. Wale wengine; Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti na wale Wajumbe wengine, Katiba iliachia sheria inayotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano na tukiongozwa na *4R's* tukakubaliana na kwa kweli pendekezo la Serikali zaidi hapo, kwa sababu kama Kamati tulianza kuona huwezi kuwachanganya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, kwa sababu sifa ni tofauti, lakini kwa sababu ya *spirit* ya *4R* pendekezo la Serikali ni zuri zaidi, kwamba hata Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wapitie kwenye Kamati hii japo siyo kwa usaili. Kwa sababu ukisaili italeta mkanganyiko wa kisheria. Kwa hiyo, wanapendekezwa na Tume hii kwa Mheshimiwa Rais, halafu Mheshimiwa Rais, atateua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo yote bado inaonesha dhahiri kwamba Serikali ipo *open* kwa majadiliano, ambayo Mheshimiwa Rais ameweka *foundation* tayari. Kwa hiyo, lazima tutafute sababu za kuelewana, siyo sababu za kutokuelewana, kwa sababu msingi na dhana ya Mheshimiwa Rais, ipo *very clear.*

Mheshimiwa Spika, sifa za Wajumbe, wadau wengi walikuwa wanasema kuna sifa ya kufukuzwa ukiwa na tabia mbaya. Halafu sheria haijaelezea tabia mbaya ni nini? Baada ya mashauriano na Kamati na kuangalia walichosema wadau, tumeona sheria na Miswada hii lazima ieleze tabia mbaya maana yake nini? Ili tusije tukaacha *vacuum* ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, kwa mujibu wa Sheria hii ya Tume ya Uchaguzi, lingine kubwa lilikuwa ni Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi kuwa sehemu ya Kamati ya Usaili. Baada ya kuona *contradiction* iliyopo na *conflict of interest,* baada ya mashauriano na Serikali tukakubaliana, Afisa mwingine wa Umma achaguliwe kuwa kwenye Kamati ili kuondoa mgongano wa maslahi, kwa sababu Mkurugenzi wa Tume anapendekezwa na Wajumbe wa Tume hii. Serikali imekubali na tupo pamoja. Pia, wadau wengi walikuwa wanazungumza habari ya Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi kuwa kwenye Kamati hii ya Usaili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa lilikuwa ni usawa wa kijinsia. Watanzania walio wengi walikuja mbele ya Kamati na kuzungumza na kusema mambo mengi sana, kwamba suala la haki sawa kwa wote halina mjadala tena. Hilo halina mjadala

tena. Hakuna sheria ambayo itapita humu tena halafu ikawa na jicho la kutaka kukandamiza aina fulani ya Watanzania tena ambao walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuliongozwa na Falsafa ya Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Umoja wa Mataifa, hotuba yake ya kwanza na ninaomba niinukuu hapa. Mheshimiwa Rais, alisema hivi: "*As a first female President in the history of my country, the burden of expectation to deliver gender equality is heavier on my shoulder; aware that being passionate about gender equality is not sufficient, my government is reviewing policy and legal frameworks in order to come up with actionable and measurable plans to ensure economic empowerment of women but also other aspects pertaining to gender equality and gender parity.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kauli ni nzito sana, na kwa tafsiri ambayo siyo rasmi ya Kiswahili, Mheshimiwa Rais anasema hivi, "Kama Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya nchi yangu, mzigo wa matarajio ya kuleta usawa upo mabegani mwangu; na kwa kufahamu hilo na kuwa na shauku hiyo ya usawa wa kijisia haitoshi, Serikali yangu inapitia upya mifumo ya kisera na kisheria ilikuja na mipango inayotekelezeka ya kuwawezesha wanawake kiuchumi na kwa masuala mengine yanayohusu usawa wa kijinsia." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaandika sheria hapa, *reforms*, ndiyo maana katika mijadala wanachosema Watanzania wale waliokuwa kwenye Kamati, *Women Rights are Human Rights.* Haki za akina mama ni haki za binadamu na hawatafuti haki maalum, wanatafuta haki sawa. Haiwezekani tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko duniani siku hizi kuna mjadala ambao unaitwa sheria lazima ziwe na jicho la kijinsia. Kwa hiyo, ile habari ya kukaa na kusema '*he*' inamaanisha '*she*', haipo, ni ya zamani. Lazima sheria sasa tu-*vet* kutoka kwenye *angle* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa mijadala na Watanzania walio wengi walikuwa wananukuu Katiba Ibara ya 81, ya Katiba ya Nchi hii, ilikuwa inatarajia Tume ya Uchaguzi iwe na majukumu mawaili ya msingi. Naomba ninukuu Ibara ya 81 "*Bila kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumika na Vyama vya Siasa kwa ajili ya kuchagua na kupendekeza majina.*" Kwa muda mrefu ni kama Tume ilikuwa inataoa Mwongozo tu wa namna ya kupeleka majina lakini namna ya kuchagua haikuwepo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana baada ya kuchambua hoja za wadau, Kamati ikaja na jedwali la nyongeza kwa kuangalia Ibara ya 113 na kuweka kifungu kipya maalum ambacho kitawezesha Tume kufanya jukumu hilo ili tuweze kutimiza masharti ya Katiba. Kwa hiyo, utaona kwenye 113 na 114 inayoyohusu Wabunge wa Viti Maalum na Madiwani, kwamba sheria sasa iweke *field* sawa kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma Ripoti ya *World Bank,* kwamba ili twende kwenye *middle income,* huwezi kwenda huko uki-*ignore population* ya watu walio wengi ambao ni akina mama. Kwa hiyo, siyo mambo ya uongozi tu, hata *on economies*. Siku hizi duniani mijadala iliyopo na kwa mujibu *World Bank Report* wanasema, *globally* akina mama wana-*enjoy* 77.1% ya haki wanazopata wanaume. *Why not hundred?* Ni kwa sababu ya kuangalia sheria zilivyokaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, unakuta Sheria Serikali ya Kijiji, Wajumbe 25, akina mama wanasema wasipungue wanane; na hiyo ni sheria inasema hivyo. Sheria ikianza yenyewe kubagua haiwezekani. Hakuna sheria ya namna hiyo siku hizi. Ndiyo maana mijadala mingi wakati wadau wanakuja, wanasema tunataka kuona sasa Miswada na Sheria kutokana na hiyo *Gender Equality Angle*. Kwa hiyo, wazee hii haiwezekani tena, na hiyo ni *development* mpya ya dunia. *Women rights are not special rights,* ni haki tulizonazo sisi. Lazima mazingira yawekwe sawa na sheria. Kwa hiyo, ndiyo maana katika Muswada huu utaona mambo mengi yamebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *interesting!* Ukisoma Ibara ya 33 ya Muswada huu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kulikuwa na *condition* mbili pale.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Alah, muda umeisha eh! Dakika 15 zote zimeisha!

**SPIKA:** Zimeisha. Dakika moja malizia.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Haya, dakika moja namalizia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninamalizia tu kwamba kulikuwa na sheria inayoweka masharti mawili kwa mtu anayegombea hasa Urais, kwamba anayemdhamini ni watu 200 kwa Mikoa 10 ya Tanzania Bara na Mikoa miwili ya Zanzibar, lakini hakuna *requirement* ya kuleta sura ya jinsia. *Imagine!* Kwa hiyo, unaweza ukawa na mtu anayegombea halafu amedhaminiwa na watu ambao ni wanaume pekee yao au akina mama pekee yao. Kwa hiyo, ndiyo maana Muswada ukiona walicholeta Kamati ni kujaribu kuondoa hizo *injustices* ambazo zipo kwenye sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa heshima ya kuwa mchangiaji wa mwanzo mwanzo kwenye sheria hizi ambazo zimewasilisha leo hapa Bungeni. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri; Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy, kwa uwasilishaji mzuri. Hakika tumewaelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naipongeza Kamati chini ya uongozi wa Dkt. Mhagama kwa kuchakata vizuri majadiliano hadi kufikia uwasilishaji wa leo hapa Bungeni. Hongera sana Kamati na Wajumbe wote wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuelekeza mchakato huu ufanyike katika taifa letu. Mchakato huu umechukua muda mrefu tangu afanye uamuzi wa kutoa maelekezo. Kwanza yeye mwenyewe alikuwa na vikao vingi sana vya maridhiano. Tunaona anakutana na viongozi wa vyama vingine vya siasa. Vilevile, vikao vya wadau wa vyama vya siasa, lakini kitu kingine kikubwa ambacho alikifanya ni kuteua kikosi kazi ambacho kilikuwa huru zaidi katika kazi zake.

Mheshimiwa Spika, maana yake Mheshimiwa Rais angeweza tu kuteua kikosi kazi hiki kuindwe na Waheshimiwa Mawaziri na majaji basi, lakini kikosi kazi kile kilizingatia mchanganyiko wa Watanzania kutoka maeneo mbalimbali. Kutoka vyuo vikuu na maeneo mengine. Kwa hiyo, walijadili kwa kina mambo mengi na hatimaye walitoa mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ambazo zipo ni kwamba, mapendekezo ya kikosi kazi kile kwa asilimia zaidi ya 85 yamechukuliwa na kufanyiwa kazi kwenye mchakato huu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mchakato huu ambao hatimaye unatuwezesha leo tuweze kutunga sheria moja mpya ya Tume ya Taifa ya uchaguzi na kufanya marekebisho kwenye sheria mbili muhimu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo hasa ya mjadala huu ni hatimaye tutoke na Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo ni mara ya kwanza kabisa kutunga Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tumekuwa na maelekezo mbalimbali kutoka kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uendeshaji wake kupitia sheria mbalimbali lakini hatukua na sheria mahususi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hii ni mara ya kwanza Tanzania tunapata Sheria Mahususi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kuziunganisha sheria mbili, ile ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ili kuwa na sheria moja ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Hili jambo litawezesha kurahisisha mambo mbalimbali na michakato ya uchaguzi iende vizuri. kwa sababu sasa mikanganyiko ile ambayo ilikuwa inaletwa na Sheria mbili sasa itakuwa imeondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili kusisitiza uwazi katika uendeshaji wa vyama, kulinda haki za kijinsia ndani ya vyama na haki za makundi maalum. Hili ni jambo kubwa sana ambalo tunategemea tukipitisha hapa mambo mengi yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, hili jambo la mchakato huu wa kuja na hizi sheria tatu linamtafsiri Mheshimiwa Rais kwa sifa kuu nne. Sifa ya kwanza ni usikivu wake, kwamba aliyasikia maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo wanasiasa na akaamua kuyafanyia kazi. Sifa ya pili ni upendo wake, kwa maana ya uzalendo wa kuipenda nchi yake Tanzania ili kuhakikisha kwamba tunazidisha amani, umoja, ushirikiano na kadharika. Sifa ya tatu ni unyenyekevu kwa Mungu wake anayemuogopa. Ndiyo maana anataka kusimamia haki za Watanzania wote bila ubaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa ya nne ni utashi wa kisiasa wa kutaka kuiongoza nchi katika misingi shirikishi na jumuishi. Hii ni sifa pekee ya nne ambayo ni kubwa zaidi kuliko zote. Maana yake utashi wa kisiasa ndiyo unaoongoza kila kitu. Ndiyo maana mwaka mmoja baada ya kiapo chake Mheshimiwa Rais aliweka wazi mwelekeo wa uongozi wake. Kwamba, atazingatia msemo wa kale wa "wengi wape lakini wachache wasikilize" katika kuongoza nchi hii.

Mheshimiwa Spika, akaandika andiko lililofafanua mtazamo wake na ndiyo maana akaja na hizi *R* nne. Kwamba, tuwe na maridhiano ya kitaifa, tuwe na ustahimilivu, tusitahimiliane, lakini akaja na mabadiliko. Kwamba kutakuwa na mabadiliko kwenye mfumo na sheria ili kuweka sawa muundo mambo yetu yaende

vizuri zaidi. Mwisho kutumia hayo mambo matatu kuijenga upya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuonyesha mfano wa moja kwa moja wa mambo hayo, nitatoa mfano wa matukio mawili. Tukio la kwanza katika maridhiano ni kuwatoa nje baadhi ya viongozi ambao walikuwa kwenye magereza huko kwa tuhuma mbalimbali na kukaa nao mezani ili kujadiliana nao mambo ya maendeleo ya mustakabali wa nchi hii. Hiyo ni mfano mzuri katika kutekeleza hizi *R* nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili mkubwa kuliko yote, ni ule ambao umefanywa na yeye kiongozi pekee yake katika dunia hii. Kwenda kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya siku ya wanawake duniani. Maadhimisho ambayo yalikuwa wameandaliwa na chama cha upinzani, yeye akawa mgeni rasmi. Hakuna kiongozi yeyote duniani ambaye kafanya hivyo isipokuwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo. Niseme tu kwamba, upo umuhimu mkubwa wa Bunge lako Tukufu kupitisha hizi sheria zilizowasilishwa leo, kwa sababu zifuatazo: - *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza; Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ambayo ni mpya kabisa tunaitunga leo au tutakapopitisha. Nimesema hapo mwanzo kuhusu sifa za kuwa na sheria ambayo inaendesha chombo hiki. Hiki chombo humo ndani kinataja mambo mengi ambayo yanaonyesha umuhimu wa mahitaji ya chombo chenyewe katika nchi yetu. Ni miaka 46 tangu tupitishe Katiba mwaka 1977. Miaka 46 tumeendesha chaguzi mbalimbali na kadharika, hatukuwa na chombo hiki. Hatukuwa na sheria inayoendesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo Watanzania wote tunahitaji kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuja na wazo hili. Kwa kweli nawapongeza sana wale ambao wamekuwa wanatoa mifano ya nchi nyingine wamekuwa wanasahau kwamba, sisi Tanzania tunaongoza katika mambo

mengi. Siyo rahisi katika Afrika, ukute Rais anakubali kupunguza baadhi ya mamlaka yake kwa ajili ya nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika maelekezo yake, kuna mahali ambapo Mheshimiwa Rais anapunguza sehemu ya mamlaka yake katika uteuzi wa viongozi wa Tume. Amekubali kupunguza sehemu ya mamlaka yake. Sasa kutakuwa na kamati ya usahili, itasahili majina ya wajumbe wa Tume. Pia, kutakuwa na kamati maalum ya Majaji, ambayo itafanya *scrutiny* na kupendekeza majina kwa Mheshimiwa Rais. Mfano, labda mwenyekiti majina matatu na makamu mwenyekiti, majina matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ni sifa kubwa sana kwa nchi yetu lakini watu wengine hawaoni jambo hilo. Ni sifa kubwa sana, siyo rahisi. Mara nyingi katika nchi nyingi, Mheshimiwa Rais wameendelea na yeye anateua vile anavyoona inafaa lakini hapa atashauriwa. Hili ni jambo ambalo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kama kuna mjumbe ambaye amefanya kosa, haondolewi tu. Sheria hii imeweka utaratibu kwamba, kutakuwa na Tume, inaweza kuteuliwa Tume ya Uchunguzi, kuchunguza hilo kosa alilolifanya. Je, linamuondolea sifa ya kuendelea kuwa Mjumbe wa Tume? Kama linamuondolea sifa ya kuwa kiongozi wa Tume, ile Tume ya uchunguzi, itapendekeza kwa Mheshimiwa Rais kwamba, anaweza kuondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo ni zuri sana. Miongoni mwa sifa za Mkurugenzi wa Uchaguzi ni kwamba, awe raia wa Tanzania na awe mtumishi wa umma mwandamizi, mwaminifu na mwadilifu. Kwa hiyo, kwa ujumla sheria hii ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni nzuri sana. Niwashawishi Waheshimiwa Wabunge, tuweze kuipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiangalia Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na madiwani. Nimesema hapo mwanzo, sheria hii inaondoa mkanganyiko ambao ulikuwepo wa sheria mbili kuishi kwa pamoja. Kulikuwa na sheria ya uchaguzi wa Serikali za mitaa

na hii ilikuwa inaratibiwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Vilevile, kulikuwa na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985. Ambayo hii ndiyo Tume ya Uchaguzi ilikuwa inashughulika nayo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuziunganisha sheria hizi mbili, ndiyo tunapata sasa sheria mpya ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Chini ya sheria hii, sifa za wapiga kura zitaendelea kuwa zilezile. Awe Raia wa Tanzania, awe na umri wa miaka 18 na sifa zingine. Hakuna ubaguzi wa aina yoyote na hii ni sifa kubwa kwa Tanzania. Tangu nchi hii tulipopata uhuru, sisi tumekuwa tunajali sana kutokuwa na ubaguzi wa aina yoyote. Isipokuwa kumekuwa na mambo fulani fulani yanayoashiria unyanyasaji, hasa unyanyasaji wa kijinsia. Ndiyo ambayo tunataka tuyaondoe kupitia sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa nchi moja ambayo baadhi ya wenzetu wamekuwa wakijinadi sana kuitangaza kwamba, hiyo nchi ndiyo baba wa demokrasia. Nchi ya Marekani, iliwachukua muda mrefu sana hao wenzetu. Siyo kama sisi tunavyorekebisha mambo yetu ndani ya muda mfupi. Iliwachukua muda mrefu sana hao wenzetu kufanya marekebisho ya matatizo waliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, Nchi ya Marekani ilipata uhuru mwaka 1776. Wakakaa miaka 11 ndiyo wakapata Katiba ya Marekani. Mwaka 1787 ndiyo ikatungwa Katiba lakini chini ya Katiba hiyo walikuwa na ubaguzi mbaya sana. Moja, wanawake wote hawakuruhusiwa kupiga kura. Mbili; watu weusi wote hawakuruhusiwa kupiga kura. Tatu; vijana wote wenye umri wa chini ya miaka 21 hawakuruhusiwa kupiga kura. Iliwachukua miaka zaidi ya 195 kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namalizia kwa kusema kwamba, sheria hii ni nayo ni nzuri lakini ukiingia kwenye sheria ya vyama vya siasa nayo ni nzuri zaidi kwa sababu inalazimisha vyama vya siasa kuweka itikadi wazi, kuweka sera zinazozingatia jinsia, makundi ya jamii na uendeshaji wa vyama unaotambua watu wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sheria zote hizi ni nzuri. Naomba Bunge tuungane kwa pamoja kuweza kujipitisha.

**SPIKA:** Haya ahsante sana…

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia siku ya leo. Pili, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya. Tatu, namshukuru Mwenyezi Mungu ametukutanisha hapa mwaka huu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni baada ya zaidi ya miaka 30 sasa, Serikali imeleta Bungeni Miswada ya Sheria ya Uchaguzi na Siasa. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassani kwa ujasiri huu mkubwa, analeta sheria hizi wakati anaelekea kwenye uchaguzi. Ni ujasiri mkubwa ambao ni Marais wachache wana nguvu ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge mtanisamehe sana kwa mchango wangu wa leo. Mtanisamehe kwa sababu napambana ili uwanja wetu wa kampeni uende kuwa sawa. Kwa hiyo, itabidi mtanisamehe sana kama nitawagusa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tokea hii Miswada imekuja hapa Bungeni, ilikuwa ni tarehe 10 Novemba, 2023. Nimeiangalia vizuri na vya kutosha lakini kuna kitu sikukiona. Nitachangia muswada mmoja tu; Muswada wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023. Sikuona mahali ambapo vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia vimetambulika kama kosa la uchaguzi. Hakuna mahali popote, hilo nimeliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini hili nimeliangalia sana, ni mhanga, ni Mbunge wa jimbo mwanamke. Nimeanza kugombea jimbo tangu mwaka 2005 na nakutana na haya mambo ambayo wengi wanayachukua kwamba ni madogo. Lahasha manyanyaso ni makubwa sana wakati tunapogombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Kamati, nampongeza Mwenyekiti kwamba hapa yeye hili ameliona. Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana sisi kina mama, kwamba, umeona hapa kuna kitu kimeachwa, kwa hiyo, kipenyezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kikamilifu kwamba zipo sheria zinazosimamia masuala ya ukatili wa kijinsia lakini kwa umahususi wa unyanyasaji wa kijinsia na ukatili katika uchaguzi hii inabidi iwe maalum ndani ya uchaguzi. Hatuwezi kutumia ile ambayo inaendelea ile ya wote. Sasa mtanisamehe nizungumze kwa mifano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniwie radhi sana, kina baba mniwie radhi sana. Natoa mfano ili Serikali mnielewe. Kwa nini mama Anne Kilango anang'ang'ania kwamba, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwenye chaguzi uchukuliwe kama mnavyochukua rushwa. Kwa nini lichukuliwe kwamba, hili ni kosa la uchaguzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 wiki ya pili nagombea uchaguzi Jimbo la Same Mashariki, lakini ndugu zangu wote tuelewe kwamba, kuna vitu viwili ambavyo vyote ni vya kawaida huku duniani. Kupendwa ni kitu cha kawaida, kuachwa ni kitu cha kawaida. Hakuna kitu ambacho ni cha ajabu hapo. Sasa wiki ya pili ni mgeni, mwenzangu akasimama jukwaani akazungumza akaingia ndani ya ndoa yangu. Kwa hiyo, sasa ananifedhehesha, ananikatili na ananinyanyasa. Haikuwa haki. Akasema mambo mazito kweli kweli sikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudi jioni nyumbani kwangu nakuta wanawake wa CCM wote wamekimbilia nyumbani kwangu. Jamani kuna mtu kafa, hapana Mheshimiwa. Ni nini? Mwenzio amekusema mambo makubwa tumeona tukufuate. Kasema nini?

Kasema hufai Ubunge kwa sababu, jamani huku nje mnisamehe, wanangu mnisamehe na kila mtu anisamehe. Kwa sababu unampeleka mume wako polisi. Kwa hiyo, hufai Ubunge. Ikawaje, wanaume wote walinuna na sisi wanawake tuli…

Mheshimiwa Spika, nikaona hiyo ni kazi kubwa. Nikampigia mwenyekiti, nikamwambia mwenyekiti huku kuna kazi. Nikamweleza. Nikampigia mkurugenzi, nikamwambia naomba unibadilishie ratiba. Niende palepale aliposemea kesho yake. Nikaenda palepale aliposemea.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ni kweli nilikuwa nimempeleka polisi. Si ni lazima nikajitetee kwa nini nilimpeleka polisi. Ndugu zangu, wakati mnapoachana mke na mume, kuna hekaheka nyingi. Ni za kawaida. Sasa mimi ilitokea mwenzangu ameniacha kumbe alikuwa bado ananipenda penda. Akanikuta napiga pasi ili nikimbie kwenda kanisani. Akaichukua ile pasi kama ilivyo akaibandika mgongoni, ikaondoka na nyama yote. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge wote mliopo hapa, nitaenda wapi?

**MBUNGE FULANI:** Polisi.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nikakimbilia polisi nikapewa *PF3* ndiyo nikaenda kutibiwa Muhimbili. Kwa hiyo, sasa nirudi kuwaeleza wananchi kwenye ule mkutano kwamba, ni kweli nilimpeleka polisi sababu ni hiyo. ilibidi lazima, nikafungua vifungo vyote polepole nikawaonesha ule mgongo ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi, wanaume kwa wanawake wakaona ile pasi, maana ni alama kubwa. Imebidi niseme hili neno ili Serikali muone umuhimu wa huu unyanyasaji wa kikatili, unyanyasaji wa kijinsia unavyotokea huko nje kwenye kampeni. Hiki kitu ni muhimu sawasawa na rushwa, wanawake tunateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine msidhanie hawa wanawake hapa ndani hawataki kugombea majimbo wanataka, isipokuwa wanapata hofu ya kuogopa haya manyanyaso. Hofu, wanapenda na wote wanaweza.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nikwambie kitu kimoja. Hili suala la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia msilichukue kwa udogo Serikali. Sasa nawaambia, sisi Chama cha Mapinduzi tuna mgombea mwanamke wa Urais mwaka 2025 na wanawake wa Chama cha Mapinduzi nchi nzima tuna wivu mkubwa na mgombea wetu uliopitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatutokubali tukakutane na lugha hizi ilhali mgombea Urais wetu anastahili, amefanya kazi nyingi sana. Hatutotaka Mgombea Urais wetu badala ya kutetea chama chake na kazi zake alizofanya kwenye nchi yetu kwa miaka mitano aanze kuambiwa vitu vya kijinga. Kwa nini sasa Serikali msione umuhimu wakufanya hivi viwanja vya mikutano vikawa na amani kwa kuweka kwamba unyanyasaji wa kijinsia liwe ni kosa la uchaguzi? Kwa nini msiweke ili mkavifanye viwanja kuwa ni viwanja vilivyojaa amani.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inielewe, kwamba mimi ni mtu mzima nimetoa mfano ambao haukuwa wa lazima lakini Serikali mnielewe tafadhalini sana, tuna …*(Makofi)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilango, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa George Kakunda.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa msemaji, mama yangu, kwamba katika kura za maoni za mwaka 2000 alipogombea Ubungo, nafahamu jinsi alivyonyanyasika. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuzingatie kuondoa unyanyasaji kwenye uchaguzi wetu. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana, sana, sana. Lakini Waheshimiwa Wabunge, mnajua mimi ni umri wa mtu mzima mpaka nikaja nikasema kitu hicho nina wanangu nje, nina wajukuu, nina mtalaka wangu, lakini nimekisema ili Serikali muone tunateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niendelee. Mimi naomba kumnukuu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye hotuba aliyoitoa katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Mjini New York tarehe 23 Septemba, 2021. Nimejaribu kuitafsiri Kiswahili. Anasema; "Kama Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya Nchi yangu, mzigo wa matarajio ya kufikia usawa wa kijinsia ni mzito zaidi kwenye mabega yangu. Ninatambua kwamba kuwa muumini wa usawa wa kijinsia pekee haitoshi. Serikali yangu inafanya mapitio ya Sera na Sheria ili kuja na mipango inayotekelezeka na kupimika ili kuhakikisha tunafikia uwezeshwaji wa kiuchumi kwa wanawake ikiwemo pia maeneo yote yanayohusu usawa wa kijinsia."

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anataka hii 50/50, sana, ataifikiaje kama viwanja vya kampeni vitakuwa vina sura ya kuwanyanyasa wanawake kiasi hiki? Kwa sababu wanawake wote hapa wana hofu. Si kwamba hawawezi kuwa Wabunge wa Majimbo, ni hofu ya haya yanayokutana na sisi. Iwapo hii sheria itaweka hili katazo, itachukua unyanyasaji, kama ambavyo wamechua rushwa, kwamba liwe ni katazo kubwa wanawake wote watagombea Majimbo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya ukatili wa kijinsia katika uchaguzi, na jambo hili lina madhara makubwa ambayo yanafifisha demokrasia, tunapendekeza, hasa sisi akina mama, katika sehemu ya pili inayohusu makosa mengineyo katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kiongezwe kifungu kipya kama ifuatavyo; Ibara mpya itakayotambua vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika uchaguzi vitakavyofanywa wakati wote wa uchaguzi kupitia kampeni, mitandao au njia yoyote kuwa ni kosa la uchaguzi na adhabu kali itolewe, kama ambavyo imefanyika kwa vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kunisikiliza, Serikali nina wanyenyekea, hili mliangalie sana ili viwanja vyetu huko kwenye kampeni viwe na amani, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mheshimiwa Hebron Mwakagenda, ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii lakini kwa haraka kabisa nimshukuru Mheshimiwa Mama Anne Kilango, kwa sababu amechukua sehemu nzuri kabisa ya mchango wangu ambayo sitoweza kuisema vizuri kama yeye. Kwa hiyo, pengine nikifika hupo nitaachia muda ili watu wengine wachangie, namshukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo ameendelea kuweka kwa vitendo dhana yake ya *4Rs* ambayo dunia nzima inaitazama kuona nini kitafanyika kama ambavyo amekusudia. Kuna wakati nilipata fursa pamoja na Wabunge wenzangu kukutana na Wabunge wa Bunge la nchi nyingine kubwa na walionesha kwamba wanatazama kwa makini sana kwamba dhana hii na utekelezaji wake utafikia wapi. kwa hiyo, hii ni hatua kubwa ambayo nadhani pia wanaiona.

Mheshimiwa Spika, la pili niishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe pamoja na Waziri wa Nchi na Naibu, kwa kweli wameleta jambo hili kimkakati vizuri sana na kwa kiasi kikubwa tumewaelewa. Niishukuru pia Kamati yetu ya Utawala Katiba na Sheria, kwa ripoti yao nzuri ambayo inaturahisishia uchangiaji katika siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, mbele yetu tuna hii miswada mitatu; Muswada wa kwanza wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi, pili ni Muswada wa Sheria ya Uchanguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, ambapo huu unachanganya Sheria tatu kwa pamoja

na tatu ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Uchaguzi pamoja na ile Sheria ya Gharama za Uchanguzi.

Mheshimiwa spika, Miswada hii pamoja na kwamba ni Miswada tofauti lakini inahusika na eneo moja ina kitu pamoja *in common* (kitu cha pamoja) kwamba inashughulikia mambo yanayohusiana na uchaguzi. Kwa wanaopenda kusoma historia, ukisoma historia utabaini kwamba sheria za uchaguzi ni miongoni mwa sheria ambazo zimepitia kwenye mapambano makubwa sana' na linapitia kwenye mapambano na harakati kubwa sana kwa sababu ya umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, sheria za uchaguzi ndizo zinazoamua nani atawale, nani awe madarakani, aongozwe na nani na aongoze kwa muda gani. Kwa hiyo ni eneo ambalo lina ugumu sana. Na mara nyingi watawala wengi duniani wamekuwa wazito sana kupanua wigo na kuruhusu michakato ya kidemokrasia kuingia katika sheria za uchaguzi. Kwa hiyo, kama ambavyo nitaeleza hapo baadaye, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake ya awamu ya sita kwa eneo hili kwa kweli wameonyesha mfano wa pekee sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa na mifano michache juu ya harakati katika sheria za uchaguzi. Amezungumza kidogo wajina wangu Mheshimiwa Joseph Kakunda, kwamba Marekani ambayo ilipata uhuru mwaka 1776 iliwachukua karne nzima kuingiza muswada wa marekebisho ya sheria itakayopanua wigo wa uchaguzi na kuwaruhusu pamoja na watu wengine kuwaruhusu wanawake. Imeingia mwaka 1878, ikapingwa watu wakapambana wakaenda mahakamani, wakafanya maandamano lakini haikuwezekana mpaka mwaka 1920 katika marekebisho ya 19 ya Katiba ya Marekani ndipo waliporuhusu wanawake kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, kilichowasaidia hapa ni kwa sababu wanawake walishiriki katika vita kuu ya kwanza, wakaona kwamba, kwa kuwa hawa kama tumeenda nao vitani iweje wasipige kura. Uingereza yenyewe ambayo haikuwahi kutawaliwa na mtu yeyote wanawake walianza kupia kura

mwaka 1928 kwa Sheria iliyoitwa *Equal Franchise Act*. Ujerumani waliatangulia kidogo wanawake walianza kupiga kura mwaka 1918 kwa Sheria iliyokuwa inaitwa *Imperial Election Act*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hapo wameruhusu angalau wanawake lakini bado watu ambao hawalipi kodi wale maskini ambao hawana kazi yenye kipato kinachoweza kukatwa kodi, hawana biashara walikuwa hawaruhusiwi kupiga kura, kwa sababu watawala wanataka wapiga kura wawe wachache ili waweze kuwa-*control* waendelee kubaki madarakani.

Mheshimiwa Spika, ukiona kiongozi aliyopo madarakani anaita watu wadau, vyama vya siasa, viongozi wa dini sijui waganga wa kienyeji watu wote jamani leteni maoni kwamba tuendeje katika uchaguzi huu na wakakumbali kufuata maoni yao huyo kiongozi kwa kweli anapaswa kuitwa bingwa wa demokrasia kwa sababu ameonyesha kwa vitendo. Ndivyo mimi ninavyomtazama Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama ambavyo nyote mnafahamu, Muswada huu mpaka ufike hapa unaanzia kwanza kwa wadau wengi tu, bila idadi na ruhusa; wakaleta maoni yale maoni ndiyo sasa Serikali ikatengeneza Muswada na kuuleta hapa Bungeni. Pamoja na kwamba yalishachangiwa lakini walewale pamoja na wengine wakaruhusiwa tena kuja kwenye Bunge kutoa maoni na leo hii inaletwa hapa Bungeni tunaendelea kuchangia. Kwa kweli ni moja kati ya sheria ambazo zimepita kwenye chujio kali sana. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba tutaweza kupata Sheria nzuri kabisa ya uchaguzi yenye viwango.

Mheshimiwa Spika, kipimo kikubwa sana cha sheria bora ya uchaguzi duniani ni kitu kwa kizungu wanaita *Universal Suffrage*. *Universal Suffrage* ni ujumuishi, yaani ni kwa kiasi gani sheria inajumuisha watu wengei kupiga kura, ambayo hiyo inaitwa *active universal suffrage*, kutokumwekea mtu yeyote kikwazo kupiga kura na *passive universal suffrage*, ni kwa kiasi gani Sheria inaruhusu watu kugombea kupigiwa kura.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeangalia sheria yetu kwa kweli sioni mahali ambapo inambagua mtu kumzuia asipige kura au inambagua mtu kumzuia asichaguliwe. Lakini hapa lazima tukubaliane; kwamba hakuna haki ambayo haina sharti hata moja hapa duniani. Hapa tulipo wote tuna haki ya kula chakula lakini huwezi ukaingia na sahani ya ubwabwa hapa ndani ya ukumbi ukawa unakula, mimi Mpare nikaingia na makande, Mheshimiwa Ole Sendeka, akaingia na loshoro na vitu vingi; haiwezekani, ukitaka kula lazima uende *canteen,* si ndiyo? Sasa sheria hii ina masharti ya kuweza kufikia baadhi ya haki zilizopo huku lakini haya masharti yote ni yale masharti halali masharti *reasonable* labda kwa kutumia neno la kiingereza ambayo yana ruhusiwa katika sheria, hakuna haki ambayo inakwenda hivihivi bila kuwa na masharti.

Mheshimiwa Spika, miswada yote ambayo imekuja kwa ujumla wake, pamoja na mambo mengine lakini inatekeleza pia ile sura ya kwanza sehemu ya tatu ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inaanzia Ibara ya kwanza mpaka ya 28 (*article one* mpaka *article* 28) ya ile sura ambayo inazungumzia juu ya haki za msingi ambazo pia ziko kwenye ule mkataba wa haki za binadamu ambayo iliingia kwenye Katiba yetu mwaka 1984. Kwa hiyo, jambo hili linalofanyika si jambo tu la sheria zetu za ndai lakini pia kutimiza masharti ya mikataba ya kimataifa ambayo tumeingia ikiwa ni pamoja na mapendekezo *declaration of human right*. Kwa hiyo tunafanya jambo ambalo ni kubwa sana katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, twende hata kwenye mifano hapa. Amezungumza pia wajina wangu Mheshimiwa Joseph Kakunda; Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa Mheshimiwa Rais madaraka kamili ya kuteua Tume ya Uchaguzi, na inatumia neno hilohilo la kisheria, *shall,* yaani kama anavyowaona yeye kwa hiari yake ana haki ya kutengeneza Tume ya Uchaguzi. Lakini kwa mujibu wa sheria hii Serikali imeona na sisi Wabunge tumeridhia kwamba mamlaka hayo Mheshimiwa Rais, ayaachilie kwanza yaanze kutekelezwa kwa kushirikiana na watu wengine. Kwamba usahili ufanyike ndipo yeye aletewe. Hii ni

kwa hiari tu, lakini hata angeamua kuendelea bado hajavunja Katiba.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha sita cha ile Sheria ya Uchaguzi Sura ya 343 kama ilivyokuwa. Pia kwa maneno *shall,* ambayo ni maneno ya kulazimisha Rais anapewa mamlaka ya kumteua Mkurugenzi wa uchaguzi. Lakini nimeona mapendekezo ya Serikali yanasema hata hili tunaweka katika mazingira ambayo Mheshimiwa Rais, ata-*share* haya madaraka na ile Kamati ya Usahili. Huu ni uongozi shirikishi ambao kwa viwango vyote uongozi shirikishi ni uongozi bora.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi malalamiko ambayo yamekuwepo juu ya sheria yetu tangu siku zote hapa yamekuwa katika mambo ya kimuundo. Kwamba, kwa nini huyu anateuliwa na huyu, kwa nini huyu anakuwa anashika nafasi mbili na kadhalika na kadhalika. Lakini ni vizuri tukakumbuka kwamba muundo una umuhimu wake lakini chenye umuhimu mkubwa zaidi ni sheria yenyewe. Unaweza ukawa una muundo mzuri sana, mtu akapatikana kwa mchakato mzuri sana wa ushindani na kila kitu lakini bado sheria ikamuongoza kufanya kitu ambacho kikawakwaza au kikavuruga uchaguzi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, iko nchi moja hapa ambayo tunaisifia mara nyingi kwamba wana Katiba nzuri, wana Tume nzuri sana ya Uchaguzi, ambako alipatikana Mwenyekiti kwa mchakato mzuri sana kweli kweli wa ushindani akakakaa pale Mwenyekiti bora kabisa. Lakini kumbe kwenye Kanuni kuna Kanuni ambayo ina mruhusu kutangaza matokeo akiwa pekee yake bila Tume kwa hiyo mambo yakaenda wenzake wakasusa wakasema kwa hili bwana hawezi kutoboa, wakaenda katangaza matokeo, wakaenda mahakamani, Mahakama ikaishia kulalamika tu huyu jamaa amepewa nguvu nyingi mno lakini ni sheria ambayo ilikuwepo ndani ya kitabu.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Tume yetu ambao umekuwa ukilalamikiwa siku zote tukumbuke kwamba ndio huo huo ambao tangu mfumo wa vyama vingi umeanza mwaka 1992 ilikuwepo lakini kila mwaka demokrasia imeendelea kukua; katika maana

kwamba vyama vimeendelea kuwa na Wabunge wengi ndani ya Bunge na demokrasia yetu kwa kweli imekuwa ikikua.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mfupi uliobakia basi niguse lile eneo ambalo Mheshimiwa Mama Anne Kilango alishalizungumza vizuri sana. Sheria ya Vyama vya Siasa imeelekeza kwamba kila chama lazima kiwe na sera ya jinsia katika Katiba yake. Ni sahihi kabisa, Chama cha Mapinduzi tulikuwa nayo na ndiyo maana tunao Wabunge, bado tunayo na tutaendelea kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, lakini sera ikikaa pekee yake hata kama ni nzuri kiasi gani haiwezi kusaidia kitu, ni lazima iwe *backed* na sheria. Kwa hiyo pamoja na maneno mazuri sana aliyoyasema Mheshimiwa Mama Anne Kilango, mimi nakubaliana naye na kuongeza kwamba ile sura ya saba ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Madiwani na Wabunge basi ifanyiwe marekebisho pale, kiingie kifungu ambacho kitatamka dhahiri kwamba masuala ya unyanyasaji wa kijinsia ni kosa na adhabu yake pale itamkwe.

Mheshimiwa Spika, itupe raha tu, kwa sababu Mheshimiwa Mama Anne Kilango amezungumzia zaidi upande wa wanawake lakini jinsia ni wote. Itasaidia hata wanaume, itasaidia watu wote kwamba unapokuwa katika uwanja wa uchaguzi basi masuala yale ambayo yanaingia katika kuvuruga usawa wa kijinsia ambayo kwa sasa ni ajenda ya dunia inayogusa uchumi, siasa na kila kitu basi yasije yakavurugwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ailimia 100 na naamini kabisa sheria hii ni moja kati ya sheria bora ambazo tunaenda kuzitunga. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, ajiandae.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa ya kuzungumza leo na kujadili miswada hii mitatu ambayo imeletwa mbele yetu katika Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, nampongeza sana kwa sababu ameonesha nia ya dhati, ameonesha uthubutu wa hali ya juu, ameonesha namna gani anaguswa na demokrasia; ametuletea *4Rs*, ambazo tunaenda kuzitekeleza katika Bunge hili. Bunge hili ndiyo litaamua kuwa *4R's* ziende ama zisiende. Bunge hili ndiyo litaamua tumwangushe Mheshimiwa Rais ama tusimwangushe.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Muswada wa Tume ya Uchaguzi. Kwanza kabisa wadau wamekuja, wamezungumza vizuri, wamechangia mno na Kamati tumesikiliza maoni yao na tumekubaliana nao katika jina la Sheria hii ya Tume ya Uchaguzi, jina la Tume ya Uchaguzi, tunahitaji Tume hii iitwe Tume huru ya Uchaguzi kwa sababu hakuna cha kukikwepa.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Katiba imeshawekwa kwamba Tume hii itakuwa huru, kwa hiyo hakuna sababu yoyote ya kukwepa jina huru *I mean* katika Tume hii kuitwa Tume huru ya Uchaguzi. Kwa hiyo, naomba niipongeze sana Kamati pia naomba niipongeze Serikali kwa kulitambua hilo na kukubaliana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, pili katika Muswada huu umesema kabisa kwamba kutakuwa na Kamati ya Usaili, ambapo Kamati ya Usaili tulitamani nayo iwe na ushirikishwaji au uwiano wa kijinsia katika ile Kamati ya Usaili, lakini kwa sababu nafasi nyingi zinaenda kwa *advantage* au kwa wale watu ambao tayari wana nafasi hizo jambo hilo tukaona kabisa tulipeleke katika Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi inasema kwamba Mjumbe mmoja atachaguliwa kutokana na nafasi yake, lakini tunasema kabisa katika hii Kamati ya Usaili izingatie uwiano wa kijinsia. Katika zile nafasi tano ambazo si nafasi mbili zile za Mheshimiwa Rais ambazo hatuwezi kuzigusa kwa sababu Katiba inatuongoza hivyo, nafasi ya Mwenyekiti na nafasi ya Makamu Mwenyekiti itateuliwa na Mheshimiwa Rais basi nafasi zile tano zilizobakia zizingatie uwiano wa kijinsia, kwa sababu huo ndiyo wimbo wa sasa *especially* tukiwa tunajua kabisa tuna

Mheshimiwa Rais Mwanamke ambaye anahitaji kunyanyua wanawake katika maeneo tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 33 ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani inasema kupata wadhamini kwa ajili ya kukudhamini wewe kugombea nafasi. Naomba Bunge lako hili linisikilize vizuri sana. Hauwezi kuwa mgombea mzuri au huwezi kuwa kiongozi mzuri kama hujapeleka aina ya watu gani wanaonda kukudhamini. Muswada huu ulisema kabisa kwamba ni watu 200 tu bila kusema kwamba kuna issue ya *gender*. Kwa hiyo, tunachohitaji Muswada huu urekebishwe ili uweze kusema *gender* ambayo ni wanawake na wanaume ikiwezeakana na makundi maalumu ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, wewe kuwa kiongozi mzuri ni pale ambapo unaona wale wanaokudhamini ni wanaume, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ndiyo ita-*determine* uwezo wako wa uongozi na ndiyo itaweza kukusaidia wewe kujua namna gani ya kufanya kazi na kuwa mwajibikaji kwa kuamini kwamba waliokudhamini ni makundi yote, kwa sababu tunaweza tukaona kabisa hii kwa sababu tunalifumbia macho unakuta mtu anapeleka wanaume watupu wanaomdhamini hajali masuala mengine ya makundi maalumu, hatojali masuala ya kijinsia, kwa hiyo kwenye barua yako ya udhamini katika wale watu ambao unawaandika pale basi hakikisha kuna makundi. Serikali imekubaliana na hilo ina maana leo hii tutaweza kuwa na wanawake, watu wenye ulemavu pamoja na vijana. Mtu mwingine anaweza akasema kwamba hawafahamu wapi wanapatikana watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ina chama chake ambacho ni Chama cha (SHIVYAWATA) Shirikisho la Vyama Watu wenye Ulemavu, kila Mkoa kuna mwakilishi wa Mkoa, kuna mwakilishi wa Wilaya, katika Wilaya zenu kuna ofisi za watu wenye ulemavu utawapata huko kwa ajili ya kuwaandikisha watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu wa Uchaguzi, nizungumze kama walivyozungumza wenzangu. Watu

wanavyosikia ukatili wa kijinsia mawazo yao yanaweza yakaenda tu kwa ajili ya wanawake peke yake, naomba ni-*declare interest*. Mimi nina watoto watatu wa kiume, watoto watatu wa kiume sasa hivi kila ukienda kila semina tunayopata ni masuala ya wanawake, itafika kipindi wanaume watakuwa asilimia 20 tu, kuna umuhimu wa kuweka usawa wa kijinsia ili wanaume wasije kuzidiwa na wanawake.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza tena sisi watoto wetu wanatuona sisi kama viongozi, wanatuona tumesimama katika Bunge hili wanatamani kuwa kama sisi, wanatamani kuchukua nafasi zetu na kama vile Daktari mtoto wake anavyotamani kuwa daktari na ndivyo hivyo Watoto wanatamani kuwa wanasiasa. Nami nimezaa watoto wa kiume na-*declare interest* natamani usawa wa kijinsia kwa sababu naamini watoto wangu hawataachwa nyuma.

Mheshimiwa Spika, yale mawazo ya kusema usawa wa kijinsia ni kwa wanawake tu au tunapambania wanawake peke yake muyaondoe. Usawa wa kijinsia na wanaume ifike kipindi tuangalie kabisa wanaume wawepo, wanawake wawepo wote wapate wawakilishi pamoja na watu wenye ulemavu bila kusahau watu wenye ulemavu, hii itasaidia sana uwakilishi na utekelezaji wa mambo yetu ambayo tunaenda kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la unyanyasaji wa kijinsia. Unyanyasaji wa kijinsia hautokei tu kwa wanawake, unyanyasaji wa kijinsia hata kwa wanaume. Tunashuhudia ulimwengu wa sasa tunashuhudia kwenye mitandao ya kijamii wakisema kila mtu ni shoga uongo kweli? Kila mtu ushoga uwongo kweli? Ukitaka kujua wewe ni nani ongea, ukitaka kufahamu wewe unaonwajwe katika jamii ongea utatukanwa matusi yote. Mwanaume utapewa ushoga, mwanamke utapewa usagaji.

Mheshimiwa Spika, haya masuala tukemee, bila kuweka kwenye Sheria hii hatutaweza kamwe kusaidia jamii yetu na vizazi vyetu vijavyo. Tuangalie namna gani ya kuweka hili kosa kwa sababu kama tunaweka rushwa na kama rushwa ipo kwenye Sheria zingine kwa nini tusiweke ukatili wa kijinsia katika Sheria hii

ya Uchaguzi ili kama tunahukumiana tuhukumiane papo hapo, hatuhitaji tena kwenda Polisi, kesi iwe ndefu, maana yake wewe umemtukana mwenzako unatenguliwa katika teuzi zako.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana katika Bunge lako hili tutatengeneza historia ya pekee kwa kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Rais yupo Madarakani pale ambaye anapenda haki, anapenda usawa, tuhakikishe masuala haya tusiyaache. (makofi)

Mheshimiwa Spika, Sitafanya vyema kama sitozungumzia maswala ya Viti Maalum. Kuna vyama ambavyo havina utaratibu mzuri wa kuwapata Viti Maalum na sisi hapa ndani tunatengeneza sheria, tunanyanyasika, tunapata shida tunaonekana labda hivi viti ni vya kupewa tu wakati tunagombea wengine. Sasa leo hii tutengeneze sheria ya kufanya Tume ya Uchaguzi au Msajili wa Vyama vya Siasa, kati ya hawa wawili wasimamie, waelekeze katika vyama vingine watuambie wanapataje Wabunge wa Viti Maalum? Watuambie wanapatikana vipi Wabunge wa Viti Maalumu? Je, hakuna rushwa yoyote ya ngono ambayo inaendelea? Tuwe wawazi tuseme. Kwa sababu, wengine inasemekana hivyo maskini wa Mungu kwa sababu ya kutokuwa na utaratibu mzuri wa kupatikana kwa hivi viti. Kwa hiyo, mwisho wa siku kuna watu wanaweza kuweka wake zao, kuna watu wanaweza wakaweza watoto wao, sasa Tume iangalie na isimamie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili siyo kwa sababu mimi nimesema hapa hata Katiba inasema. Ibara ya 81 imesema Tume itasimamia suala la uchaguzi wa Viti Maalum, ielekeze namna ya kupokea majina lakini pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kupata Viti Maalum. Hivyo basi naomba katika hizi Sheria tusiziache. Tutatengeneza historia ya kipekee katika Bunge hili na mimi nafurahi kuwa mmoja wa kuleta mabadiliko kwa ajili ya vizazi vyangu, watoto wangu ambao wangeweza kutamani kuwa kama mimi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache nashukuru sana na mbarikiwe mno. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi kuwa sehemu ya kutoa maoni ya mabadiliko tunayoyafanya.

Mheshimiwa Spika, kwa zaidi ya miongo mitatu tumekuwa tukipambana na haki za wanawake katika uongozi na tumesema mara nyingi na wakati mwingine ndugu zetu wanaume walikuwa hawatuelewi, nimeweka hili kama utangulizi kwa sababu tunafahamu mwanamke akiwa kiongozi anaweza kusimamia kitu kikawa sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna Mheshimiwa Rais Mwanamke lakini tuna Mheshimiwa Spika wa pili ni mwanamke, tunae Katibu Mkuu wa Bunge kwa mara ya kwanza mwanamke, tunae Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar kwa mara ya kwanza ni mwanamke. Ninasema haya kwa sababu Mheshimiwa Rais ambaye ni mwanamke angalau ameonesha jitihada ya kuanzisha mchakato huu angalau tuweze kuzungumza. Hii ni dalili tosha ya kuonesha kwamba wanawake tunaweza japokuwa pembeni wanaume tunao wakitusaidia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea vyama vya siasa kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa. Kwa utangulizi nilioutoa iende ikalazimishe kwenye kila chama cha siasa katika nafasi zile kubwa tatu kwa maana Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Katibu lazima mwanamke awepo katika uongozi huo. Tunafahamu kuna vyama vimefanikiwa nafahamu *ACT* ina mwanamke katika ile tatu bora, ninafahamu CCM ina mwanamke katika ule uongozi.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa CCM ameingia kwa sababu ni Mheshimiwa Rais na Katiba yenu inasema hivyo lakini vyama vya siasa vikaweke Sheria ya kulazimisha katika nafasi tatu bora lazima mwanamke awepo kama ni watakuwa wote watatu sawa lakini asikosekane hata mmoja, ninaomba ikawe hivyo,

nimesema hapo mwanzo wanawake wakiamua kufanya jambo wanafanya vizuri kwa Taifa lao ili lisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumza hapa mambo ya unyanyasaji wa kijinsia, Katiba yetu inasema katika Ibara ya 81 ikizungumzia juu ya Viti Maalum vya Ubunge pamoja na Madiwani, nasi tunafahamu tumesaini Maputo *protocol* tukitaka wanawake waingie katika vyombo vya maamuzi lakini suala la unyanyasaji limekuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunalizungumza hili kama wanawake tunaotunga sheria sasa, ametoka kuzungumza Mheshimiwa Keisha hapa wanawake wanapogombea kwanza ni lazima mazingira yawe rafiki kwa wanawake kutamani kugombea. Haiwezekani mnakuwa na Majeshi ya Polisi kwenye mikutano ya hadhara na vitu kama hivyo, nafikiri tunapotunga sheria hizi zikaweke Kanuni ambazo zitaondoa watu wengine wataogoa kwenda kugombea kama wanawake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo lugha za unyanyasaji amesema Mama yangu hapa Mama Kilango kwamba tunapokuwa tunagombea kama wanawake unabambikiwa maneno, unabambikiwa majina yasiyofaa na mwisho wa siku wanawake wanaokuwa nyuma yetu, maana yake sisi kama viongozi lazima tu-*mentor* wasichana wadogo waingie kwenye uongozi, lakini sasa wakishaona Mama kama Mama Kilango katukanwa, mimi mwenyewe nilitukanwa.

Mheshimiwa Spika, mimi niliambiwa nina nyonyo moja, nakwambia! na waliosema hayo ni viongozi! Lakini sikujali kwa sababu mimi ninasaidiwa na familia yangu. Leo hii mimi siji huku Bungeni kunyonyesha tumekuja kufanya kazi ya wananchi, sasa maneno machafu kwenye chaguzi yawekewe msisitizo mkali wa kuwakataza wanawake kuweza kunyanyaswa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini Tume ikaweke Kanuni. Kwanza wanawake wanapochaguliwa kwenye Majimbo kwamba ni lazima Majimbo yawe na wanawake wa kutosha na tuanzie kwa asilimia 30, tukipata wanawake wanaogombea kwenye majimbo

angalau asilimia 30 tukajumuisha na viti maalum basi ile azma ya Mheshimiwa Rais ya kufika asilimia 50 kwa asilimia 50 tutaifikia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo wanawake wenzangu mnaochaguliwa hatuchagui namba tunachagua *quality* ya wanawake. Suala siyo tu kuwa na namba kubwa lakini wanawake wanaojitambua, wanawake wanaweza kufanya kazi kwa umakini na weledi hao ndiyo tunawataka kwenye Kata, Vitongoji, Vijiji, kwenye Jimbo na hata kuwa Urais kwa sababu ni mwanamke bora na wala siyo sababu yeye ni mwanamke. Tunahitaji kubadilisha sheria zetu na kuhakikisha tunawasaidia wanawake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu 74 kinazungumzia jinsi ya kutumia vyombo vya habari nyakati za chaguzi. Tunao wenzetu wenye mahitaji maalum wanaotumia nukta nundu, wanaotumia fimbo na vitu kama hivyo. Vyombo vya Habari vihakikishe vinawapa wepesi wa kuweza kutambulika wakati wanataka kugombea. Kwa hiyo, ninaomba na ninashukuru na ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa hii hatua aliyoichukua angalau tunazungumzia machozi tuliyokuwa tukiyalilia kwa muda mrefu leo tunaweza kuyazungumza. Ninaomba tunapoendelea na mijadala hii tuhakikishe haki ya mwanamke na wanaume, wengine wamesema tukiwaacha kwa mbali tutakuwa hatufanyi sahihi.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku ninaomba msisitizo katika haki ya wanawake kutokusemwa vibaya, kutokutishiwa, kutokuwekewa sheria ambazo ni kandamizi zinawafanya wao washindwe kugombea kwa wepesi. Baada ya kusema haya nami ninaunga hoja mkono kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge haya tunaendelea. Tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Said Issa atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Miswada

hii mitatu ambayo imeletwa leo hapa Bungeni. Mimi binafsi Miswada hii kwa kweli imenifurahisha sana leo. Kwanini niseme imenifurahisha, kwa sababu Miswada hii sasa kimaandishi inakuja kujibu hoja ambazo wadau wengi au wananchi wengi walikuwa wanazihitaji katika Sheria zetu za Uchanguzi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mchango mkubwa sana nimeangalia vifungu vingi sana lakini baada ya kuletwa na kusoma Sheria hii vifungu vingi ambavyo nilikuwa nimevitayarisha nimeona vimeingizwa katika Sheria hizi zote tatu. Kwanza ningependa kuwashukuru Kamati kwa kuliona hili pamoja na Wizara ili kuwajengea mustakabari Watanzania, isiwe sasa kila tunapoingia kwenye uchaguzi kunakuwa na malalamiko mengi mno, naamini sasa Sheria hizi zinakuja kupunguza yale malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanini nimeanza kimaandishi, nafikiri uliniangalia niliposema kimaandishi kwa sababu gani, amechangia Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa akasema majirani zetu walitengeneza Katiba nzuri ambayo ilisifiwa sana lakini mwisho ikaonekana kuna malalamiko makubwa kwa sababu ya kanuni.

Mheshimiwa Spika, maandishi haya yanaweza kuwa mazuri mno lakini nia na imani thabiti katika utekelezaji ndiyo jambo la msingi. Kwa hiyo, mimi niwaase wasimamiaji wa sheria hizi wawe na nia thabiti katika kuwaondolea Watanzania kero ambazo walikuwa wanaziona kwamba zinawasumbua katika nchi hii, siyo maandishi yawe mazuri lakini vitendo viwe vibaya.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tuna dini zetu hapa kuna *Quran* kwa Waislamu inaeleza vizuri sana lakini pia kuna *Bible* kwa Wakristo lakini watu wanapindisha sheria hata kwenye chaguzi zile za Makanisani na Misikitini, Baraza Kuu la Waislamu pale kunakuwa na shida kwenye uchaguzi, sasa jambo hili natoa angalizo kwamba, wale wasimamizi wa sheria wasipindishe pindishe sheria, sisi sote ni Watanzania hakuna haja ya kupindisha, mwenye haki apate…

**MBUNGE FULANI:** Haki. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, baada yakuleta utangulizi huo, ningetamani kidogo, kwanza kuna kifungu hapa Na.10(1), mwanzo kilikuwa kinampa Mheshimiwa Rais mamlaka ya kuteua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti tu, lakini kimerekebishwa vizuri na sasa kitaanzia na Kamati ya Usaili ambayo Mheshimiwa Rais atachagua kupitia majina matatu kila nafasi ambayo imepelekwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye kifungu hiki sina hoja kubwa, ila nilitamani kwenye Kifungu Na.10(1) kiongezwe Kifungu Na.10(2) kitakachosema, kwa kuzingatia usawa wa jinsia katika kutekeleza mamlaka yake kwa mujibu wa Kifungu Na.10(1), Rais atateua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwa majina matatu katika kila nafasi iliyopendekezwa na Kamati ya Usaili.

Mheshimiwa Spika, niendelee na kifungu kingine; Kifungu Na.7(1) na Kifungu Na.7(2). Sifa ambazo zimeelezwa katika kuteua wajumbe hawa hazitoshelezi kwa sababu hazikueleza kwamba asiwe ameingia kwenye mchakato wowote wa kisiasa au ni mwanachama wa chama cha siasa. Mimi nilikuwa natamani jambo hilo liongezwe ili kuleta raha katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kifungu Na. 6 (1) na Kifungu Na. 6 (2), bado kinampa Mkurugenzi wa Jiji mamlaka ya kuwa msimamizi wa uchaguzi. Jambo hili kwa kweli limekuwa linasumbua sana na limelalamikiwa sana. Naamini mambo mengi yamechukuliwa, lakini hili limeachwa na ndiyo mwarobaini wa kuondoa tatizo kwenye chaguzi zetu.

Mheshimiwa Spika, hawa Wakurugenzi, kwanza tumewaajiri, wana nafasi Serikalini ambapo chama tawala ndiyo kinawalipa mishahara, sasa leo wanaendelea kuwa Wakurugenzi wa Uchaguzi katika maeneo hayo. Hili jambo siyo sawa. Ilipaswa Tume ya Uchaguzi ichague wafanyakazi wa uchaguzi ambao watasimamia hapa, lakini sio tena wakurugenzi. Tumeona hapa katika kurugenzi zetu, ukiangalia kwenye ripoti ya *CAG*, imeeleza madudu mengi ya Wakurugenzi katika kusimamia uchaguzi.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa kaka yangu ninayemheshimu na anazungumza vizuri sana, kwamba kwa mujibu wa mapendekezo ya mabadiliko ya sheria hii, sheria inapendekeza kwamba watakaosimamia uchaguzi ni Maafisa Waandamizi wa Serikali. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa sababu nchi hii ni nchi inayotawaliwa kwa misingi ya kisheria, Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipopitia kesi ya rufaa ambayo ilikatwa Mahakama ya Rufaa, ilitoa *ruling* ya kuona hakuna tatizo la Wakurugenzi kushiriki katika kusimamia uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote naomba nimpe msemaji taarifa kwa sababu nchi hii inaongozwa kwa misingi ya kisheria na utawala bora. Tusijadili mambo ambayo mahakama zetu zimeyatolea *ruling,* tutakuwa hatuitendei haki mahakama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia bado Muswada huu pia umetaja watakaosimamia jambo hili ni Maafisa Waandamizi. Sasa hilo tulizingatie.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe kaka yangu taarifa.

**SPIKA:** Haya. Sasa ngoja niliweke sawa. Waheshimiwa Wabunge watasema mbona Spika huwa anasema taarifa moja lakini huyu amesema mbili?

Jamani tuko kwenye kutunga sheria, kwa hiyo, lazima iwe kamilifu. Kwa hiyo, lazima umsikilize mtu hoja yake anataka kutufikisha wapi? Kwa hiyo, sura ni hiyo, hakuna mabadiliko

yoyote, isipokuwa wakati wa Miswada, mjadala huwa unakuwa tofauti kidogo kwa sababu tunatunga sheria na tunataka iwe kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kingu, hayo unayoyasema kwamba Muswada ndivyo unavyosema, nadhani ni mapendekezo ya Kamati kwamba kile kifungu namna kilivyoandikwa, sasa kibadilishwe. Nafikiri kwenye upande wa Serikali wakati wanasoma ile taarifa yao, wameonesha kwamba wamekubaliana na Kamati. Kwa hiyo, wanaleta marekebisho. Nadhani ndiyo taarifa anayopewa, lakini kwa maana ya Muswada, anavyochangia yeye, ndivyo Muswada unavyosomeka.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kama yale marekebisho bado hajayaona pengine ndiyo unampa hiyo taarifa, lakini Muswada unasomeka yeye anavyosema. Isipokuwa Mheshimiwa Mohamed, nilikuwa naiweka hiyo sawa ili taarifa zetu zikae sawa. Kwa hiyo, Muswada unasema hivyo, lakini Kamati imependekeza na wametoa taarifa yao hapa kwamba Serikali ilisikiliza kwenye hoja hiyo. Kwa hiyo, liko kwa sura hiyo.

Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kutoa ufafanuzi, lakini Mheshimiwa Kingu ajue tu kwamba Mahakama hizo hizo zinatumia Katiba na sasa tunalilia kuibadilisha Katiba.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea na mchango wangu, Muswada huu unajumuisha uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, unakuja kufuta Sheria Na. 292 ya Madiwani na Sheria ya Uchaguzi Na. 343. Sasa basi, nilivyoona hapa katika jambo hili, ni kwa nini Sheria ya Uchaguzi ya Madiwani inakuja kufutwa na keshokutwa tunakuja kwenye uchaguzi huo?

Mheshimiwa Spika, maana yake Serikali za Mitaa zilitakiwa zijumuishwe hapa. Sasa sijui tunaogopa nini? Kwa sababu tungezitumia tu sheria zetu. Leo tunajadili, baadaye tutapitisha itakuwa sheria, na tutaendelea na sheria zetu. Kwa hiyo, hapa

kulikuwa hakuna cha kuogopa, ilikuwa ni kujumuisha pamoja na Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu namba tano ni suala la eneo la ulinzi katika chaguzi zetu. Naona sheria hii haikutamka. Katika chaguzi zetu, mimi ninayetokea Pemba, wakati mwingine naona kama vile kuna *double standard,* kwa sababu kule Pemba hasa, nazungumzia Pemba, kunakuwa na wasimamizi ambao ni watu wa usalama, wa kusimamia usalama wa uchaguzi; kunakuwa na Jeshi, Mgambo, Polisi, wale *KMKM,* yaani inakuwa ni vurugumechi.

Mheshimiwa Spika, mgombea ukifika pale unataka kuingia, unakuta *KMKM* amekuzuia. Tumezoea kuona kwamba Polisi ndio wanasimamia, lakini sheria haikutamka vizuri hapa. Sasa kwa kweli tunapata ukakasi kwamba ni nani anapaswa kusimamia huu usalama wa uchaguzi? Kwa sababu unaweza kukuta kwenye Kituo cha Uchaguzi kuna jeshi, kuna *KMKM*, kuna Mgambo, kuna Askari Katuni, hujui ni nani ambaye anapaswa kusimamia. Kwa hiyo, hili tunaona kuna haja ya kulirekebisha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwenye chama cha siasa, hii sheria ambayo imesema kwamba chama cha siasa kiendelee ku-*sustain* walau kiwe kimeshiriki chaguzi mbili za Taifa. Sheria hii ningependelea isonge mbele zaidi, kwa sababu chama hiki kitashiriki, lakini hata wale wadhamini wake ambao walimdhamini kuwa chama cha siasa hawakumpigia kura, maana yake hana tena *deposits.* Kwa hiyo, itamke wazi, ipate *deposit* walau ya wale wadhamini. Maana yake kama hana wadhamini, siyo chama cha siasa tena. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni suala la kwamba kama ikitokea mgombea amekuwa mmoja, apigiwe kura, ni sawa kabisa, lakini suala hili linaonekana ni sawa lakini siyo sawa, kwa sababu lina viashiria vya rushwa na mambo mengine ya utekaji. Kwa hiyo, jambo hili naona halikukaa vizuri. Inawezekana wagombea wakawa watatu, mwingine akapewa rushwa, mwingine akatekwa, akabakia mmoja, akipigiwa kura atapata kura kupitia chama chake.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili, Tanzania sote tunaijua, hakuna sehemu chama kinaweza kukosa kuweka mgombea japo vyama viwili, kwa hiyo kama kuna mgombea mmoja katika chama amebakia, basi uchaguzi huo uahirishwe mpaka wapatikane wagombea watakaoshindana na mgombea mwingine, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo kwenye mchango wako unataka kutaja kifungu, kwa sababu tunajadili Miswada mitatu kwa wakati mmoja, ili kurahisisha ufuatiliaji wa mchango wako, utaje kwamba ni kifungu namba fulani cha Muswada fulani. Kile kifungu Na.10 alichokuwa amekitaja Mheshimiwa Mohamed kuhusu uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ni kifungu kutoka kwenye Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, isomeke kwa sura hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Jumanne Miraji Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja zilizoko Mezani kwetu kuhusiana na Sheria za Uchaguzi, kwa maana ya Tume ya Uchaguzi ya Mwaka 2023, kwa maana ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani pamoja na ile Sheria ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nianze kwa kuipongeza Kamati pamoja na Serikali kwa mawasilisho yao mazuri. Mheshimiwa Dada yetu Jenista Mhagama, mdogo wangu Mheshimiwa Ummy Nderiananga, na kipekee kabisa Mwenyekiti wa Kamati Dkt. Joseph Mhagama amewasilisha vizuri. Kwa hakika sisi Wabunge tumewaelewa na mmetuchambulia mambo ambayo mengine yalikuwa yamejificha ndani ya Muswada ambayo tusingeweza kuyapata vizuri. Kwa sababu Kamati ilipata muda wa kutosha basi mmetupa nafasi nzuri ya kufahamu

Miswada hii ambayo iko mbele yetu. Hongereni na pongezi nyingi sana kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwenye hili yeye ndiye kinara. Bila kupepesa macho, kama tusingekuwa na Rais msikivu na anayependa mabadiliko, sheria isingekuja hapa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kabisa!

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Tungeishia kusikiliza kelele, mbwembwe, tungepata kila aina ya sarakasi…

**MBUNGE FULANI:** Kabisa!

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** …lakini kama Rais hajakubali sheria isingekuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi wote Watanzania lazima tuone aina ya Rais tulie naye, ana dhamira njema kwa ajili ya nchi yetu na kupitia mfumo wake wa *4Rs* anaonesha wazi kiongozi anatakiwa kuwa wa namna gani? Hata kama jambo linakusumbua na linakuuma, lazima ukubali, uweze kuvumilia usikilize hata hoja za watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili Mheshimiwa Rais amefanya jambo kubwa, anaiponya nchi, anaenda kuipeleka nchi kwenye maridhiano, maridhiano ya vitendo kwa sababu unaweza kuwa na dhamira ya mdomo lakini huna vitendo na sheria, maana yake hakuna jambo ambalo lingeendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili Mheshimiwa Rais tunampa maua yake kwa kazi nzuri anayoifanya kuipeleka Tanzania kwenye maridhiano ya kweli ambayo yanaweza kuletwa na sheria ili hata kama yeye baada ya miaka yake kumi akiondoka, maana yake anaweza kuacha sheria ya uchaguzi nchi hii ambapo nchi inaendeshwa katika sura ya maridhiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, wote tuliona, Mheshimiwa Rais alianza kwa kuruhusu Baraza la Vyama vya Siasa vikutane waweze kujadili. Aliongeza wigo mpana ambao hata yalikuwa hayapo kwenye sheria lakini alikubali, kwa sababu alitaka mawazo mbalimbali ya Watanzania yaweze kuja. Asasi za kiraia zimeshirikishwa, tumeona viongozi wa dini wameshirikishwa na makundi mbalimbali yenye mawazo yao yaliruhusiwa kuletwa. Maana yake alitaka Watanzania wote washiriki katika kujenga nchi yao.

Mheshimiwa Spika, hata walivyosema Wabunge wengine, wamesema kwamba siasa ikiendeshwa vizuri, hata maendeleo yatapatikana vizuri pia. Kwa hiyo, mimi nataka niseme, kupitia mwongozo wa Mheshimiwa Rais na kukubali haya yote, tunaiona Tanzania tunayoitamani ya watu wote kukaa pamoja inakuja, na mifano mbalimbali tumeiona kama walivyosema wengine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameweza kwenda hata kushiriki kwenye mikutano ya vyama vya upinzani na akazungumza nao na wale wa vyama vya upinzani wakafurahia kumwona kama ni sehemu yao. Hili ni jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais anatuonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye eneo hili pia kiliundwa kikosi kazi ambacho kilichambua hayo maoni kutoka kwenye Baraza la Vyama vya Siasa. Tulikusanya wasomi, viongozi wa dini, vyama vya siasa, makundi mbalimbali nayo pia yalipata nafasi ya kwenda kutoa maoni yao kwenye kikosi kazi na ndiyo yalizaa mapendekezo ambayo leo tunayaona kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake nimeambiwa hapa asilimia zaidi ya 80 ya maoni yaliyokuwa yametajwa yameingizwa kwenye sheria ambayo kiukweli ndiyo mawazo ya wadau mbalimbali wa vyama vya siasa. Kwenye eneo hili naona ni jambo zuri ambalo kwa hakika bado tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais. Tunaipongeza sana Serikali kwa kukubali kuona mambo haya yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya mambo ambayo unaweza kuwa unafanya kama kiongozi, lakini baadae unageuka. Ni kama ambavyo wewe uwe na mgeni nyumbani kwako; unatenga chakula, unaenda kuleta maji ya kunawa; wakati unaenda kuchukua maji unarudi unakuta mgeni yuko juu ya meza anakanyaga chakula. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wakati sisi tunahangaika kuleta hii Miswada Bungeni, tukaanza kuona wengine wanafanya sarakasi barabarani. Hii ni sawasawa na mgeni, umeandaa chakula, ale chakula mzungumze, lakini unamkuta amekanyaga chakula na viatu. Mgeni huyo utamwangalia kwa sura gani? Bado Serikali yetu, Rais wetu anasema, pamoja na hizo sarakasi za mgeni huyo, bado amekubali sheria ije ijadiliwe tuweze kuwatengenezea Watanzania sheria ambayo itawapeleka kwenye sheria iliyo nzuri ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka niseme, uvumilivu wa Mheshimiwa Rais ni wakiwango cha juu kabisa. Ni Rais ambaye kwa hakika dunia yote inamtazama kwa sura hiyo. Ameruhusu maandamano, wamepeleka hisia zao, wamepeleka barua huko walikopeleka ingawa walisema ilikuwa haijasainiwa, lakini katika yote, bado waliendelea kusikilizwa na leo tuko na sheria hii ambayo itaenda kutupeleka kuzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya huo utangulizi wangu, nieleze maeneo machache ambayo mimi binafsi nimeona kama yamezingatiwa sana. Kulikuwa na kelele kubwa sana kuhusu uteuzi wa Tume ya Uchaguzi. Eneo hili lilipigiwa kelele na wadau wengi. Eneo hili kama mlivyosema ni marais wachache wenye nguvu anayeweza kukubali baadhi ya mambo yake yafanywe na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekubali kwamba kuwepo na Kamati ya Usaili ambayo itamsaidia kuwachuja watu. Kamati hii inaongozwa na majaji; Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jaji wa Zanzibar. Maana yake ni kwamba Kamati hii imebeba taswira ya watu waaminifu wa *level* ya juu kabisa ambao wataenda kufanya kazi hii kwa niaba ya

Mheshimiwa Rais. Maana yake ni kwamba hata hii Kamati ya Usaili tu ambayo imetajwa, tusipoiamini, tutamwamini nani?

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba tutakapokuwa tumekubali sheria hii, tukakubali usaili utakaofanyika, maana yake tutamsaidia sana Mheshimiwa Rais kuondoa maneno ambayo yamekuwepo kwamba amekuwa akiteua peke yake. Kwa maana pamoja na kuwa tunaamini hata uteuzi wake anapofanya, hateui peke yake kwa sababu Rais ni Taasisi, anaweza kufanya na vyombo vingine vikafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado Mheshimiwa Rais amekubali, kupitia hii, itakuwepo Kamati ya Usaili ambayo itafanya kazi ya kuteua au kupendekeza majina. Mwenyekiti, majina matatu; Makamu wa Tume majina matatu; na wale wajumbe wake, watapeleka majina na Mheshimiwa Rais ataenda ku-*pick* katika yale ambayo wamependekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo kubwa ambalo ninaamini kabisa Watanzania tuunge mkono sheria hii, itakwenda kuwa ni sheria ambayo itaenda kutuletea matokeo mazuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ilikuwa ni Ibara namba 9 ya upande huu wa Tume ya Uchaguzi. Hata hivyo, ukienda kwenye Ibara namba 7 ya Tume ya Uchaguzi imeeleza sifa za hawa wa Tume ya uchaguzi na zimetajwa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, sifa mojawapo ambayo nimeipenda ni kwamba, hawa Mwenyekiti na Makamu wa Tume hii watakuwa ni sehemu ya Majaji wa Mahakama Kuu ambao wanaaminika kabisa na ambao tunawapa dhamana kubwa. Maana yake ni kwamba, tunawaamini ni watu ambao watakwenda kutenda haki katika maeneo yote. Kwa hiyo, tuendelee kuamini kwamba, tukipitisha Sheria hii tutakuwa na Tume bora ya Uchaguzi ambayo itakwenda kuwa na jibu la manung'uniko ambayo yalikuwepo siku za nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ni lile eneo ambalo limetajwa kuhusiana na wagombea. Kulikuwa na kelele kubwa ya wale wanaopita bila kupingwa. Ni jambo ambalo limesikilizwa sana, viongozi wengi wameeleza kwamba haiwezekani akaja mtu mmoja akapita bila kupingwa na akaenda kule.

Mheshimiwa Spika, lakini kupitia hii, akitokea mgombea mmoja ni lazima apigiwe kura ya ndiyo au ya hapana na baada ya pale ndiyo tutakubali kwamba huyu sasa amechaguliwa kwa kupigiwa kura. Kwa hiyo, kura ya ndiyo au hapana haijalishi anapigiwaje. Lakini kwa sababu tayari mchakato unaendelea, mgombea mmoja amepatikana, hauwezi kuzuia watu wasipate haki ya kumpata kiongozi wao katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yke ni kwamba, kupitia hii itaondoa ile *doubt* iliyokuwepo mwanzoni kwamba watu wanapitishwa tu ili waende kule wakawe viongozi bila kuwa na ruhusa kutoka kwa wananchi. Maana yake kupitia ndiyo na hapana tutakwenda kuamua. Kama hakubaliki basi si atapata kura za hapana. Msiwe na wasi wasi wowote, maana yake ni kwamba huu ni mwendo na siku zote haya mambo yanaanza taratibu huko mbele tutafika lakini kwa sasa tuanzie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie jambo dogo tu la usawa wa kijinsia. Jambo hili la usawa wa kijinsia ni kubwa na limezingatiwa na Sheria hii kwa sababu kuna baadhi ya maeneo manyanyaso ni makubwa. Tumekuwa na baadhi ya wanawake wazuri katika maeneo fulani fulani lakini wameshindwa kuchaguliwa kwa sababu tu ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na mfumo dume katika maeneo ya jamii yetu ambayo hayaamini katika mwanamke kuwa kiongozi. Kwa hiyo, kupitia Sheria hii itavilazimisha vyama vya siasa kuweka wagombea ambao ni wanawake au kama walivyosema wengine hata wanaume katika maeneo mengine ambayo hawakubaliki sana. Maana yake itasaidia kuweka usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba Sheria hii itakwenda kuwa Sheria bora, tunaomba tuipitishe na kuunga mkono Serikali ili tuipeleke na hasa tunaelekea kwenye uchaguzi. Hivyo tufanye mapema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya ninaunga mkono hoja na Miswada yote mitatu iende ikafanye kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafsi hii kukushukuru wewe kunipeleka kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria angalau nimeanza sasa kuwa mwanasheria. Kwa muda wa mwaka mmoja huu ambao nimekuwepo huko, naanza kuelewa vifungu vya Sheria vinakaaje na unaweza kuvijadili kwa namna gani. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu pamoja na Naibu wake. Kwa kweli niseme Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ilivyo ngozi yake na sura yake, hata moyo wake uko hivyo. Ni mweupe, yuko wazi kwenye Kamati mjadala haukuwa rahisi rahisi. Ulikuwa ni mgumu lakini hatukuweza kuona kama anabadilika sura au sasa anasema naondoka nakwenda, hapana. Hivyo hivyo anavumilia halafu anajua tu kwamba tutafika mahali tutaelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na sisi alituweka huru kabisa kujadili Miswada hii na ndiyo maana tukafikia hatua hii ambayo kwa Taarifa ambazo zimesomwa na Mwenyekiti wetu nadhani tumejitahidi kufanya kazi kwa uwazi lakini pia kizalendo sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuja na hizi R nne kwa sababu msingi

wa Sheria hizi ni zile R nne za Mheshimiwa Rais. *Reconciliation* (Maridhiano) tukubaliane, sasa wengine wanatafsiri vibaya, maridhiano sio kila kitu utapata wewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utakavyopata wewe na mwenzako apate. Unaona. Vilevile, *resilience* (kuvumiliana) tuvumiliane kwa sababu tuko tofauti tofauti. Itikadi tuko tofauti na mambo mengine. Sasa tuvumiliane tunapotaka kwenda kama nchi. vilevile, *reformed* (mabadiliko) tufanye mabadiliko kwa sababu yanahitajika yafanyike na ndiyo maana ya Sheria hizi kuja hapa. Lazima tufanye mabadiliko ili tufike mahali ambapo nchi yetu inataka kwenda. Pia, tunapofanya haya mabadiliko, sasa tukubali kujenga upya (*rebuilding*). Tukubali kujenga upya nchi yetu kwa sababu hii nchi ni yetu sisi wote. Tutafaidika watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya utangulizi huo, nianze kama nilivyofundishwa kujadili Miswada hii. Nitaanza na Muswada huu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Kwenye Ibara ile ya 28(8) kulikuwa na suala hilo. Hapana, nianze na Ibara ya 19, Ibara ya 20(1), hii ibara inazungumzia juu ya kadi kupotea, kadi kufutika au kadi kuharibika. Kwa kweli hapa kulikuwa na tozo na ada lakini Serikali kwa usikivu wake wamesema hiyo wameiondoa. Kwa hiyo, hakuna ada hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wadau wetu walipokuja kutoa maoni kwenye Kamati kwa kweli walizungumza sana juu ya suala la kutoa ada au pesa ili upate kitambulisho kipya. Sasa, Serikali imekubali na ndiyo maana nasema kwa kweli Serikali ni sikivu sana na Mheshimiwa Waziri alitusikiliza vizuri.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye ibara ya 23(2) kwenye kukata rufaa. Sheria hii au Muswada huu ulikuwa unasema, "Ukataji wa rufaa kwa ajili ya kukataliwa maombi ni lazima iwe mahakama ya wilaya". Hata hivyo, Serikali wamekubali kwamba sasa tunaweza kukata rufaa katika Mahakama za mwanzo ambazo ziko karibu na wananchi na ziko karibu na wapiga kura wetu. Kwa hiyo, hawatalazimika kusafiri umbali mrefu kwenda

wilayani na wakati mwingine kupoteza pesa kwa sababu lazima uwe na nauli ili ufike na wilaya zetu tunazifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara nyingine ni ya 28 (8). Sasa Kamati tulionesha wasiwasi juu ya kifungu hiki. Kifungu hiki "kinasema uhalali wa mwenendo chini ya kifungu hiki hautahojiwa kwa sababu tu Afisa mwandikishaji alisikiliza na kuamua pingamizi aliloweka yeye mwenyewe na katika hali yoyote ile utaratibu katika uchunguzi wowote chini ya Kifungu hiki utaanza katika hatua ambayo Afisa mwandikishaji atakapohitaji uthibitisho wa sifa zilizopo za mtu ambaye pingamizi limewekwa dhidi yake".

Mheshimiwa Spika, sasa tulionesha wasiwasi juu ya kipengele hiki kwa sababu ikiwa kitatumika vibaya na huyu Afisa mwandikishaji, akikitumia vibaya na kwa sababu uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho. Kwa hiyo, tulionesha wasiwasi kwamba kipengele hiki kingeweza kubadilishwa. Sasa sijasikia kama Serikali wameleta mabadiliko kwenye kifungu hiki na labda ufafanuzi zaidi tutaupata kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, niende tena kwenye kifungu kingine. Mtanivumilia kwa sababu mimi ni mwanasheri mwaka mmoja. Kifungu kingine ni kifungu cha 88(1) kinasema "Endapo mwenendo wa upigaji kura katika kituo chochote unakatizwa au kuzuiliwa kwa ghasia au vurugu wakati kuna wapiga kura waliobaki ambao hawajamaliza utaratatibu…" na maneno mengine ynanaendelea hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa pia sisi kama Kamati tulionesha wasiwasi juu ya sababu zilizoandikwa hapo. Upigaji wa kura kuzuiliwa kwa ghasia au vurugu maana yake Sheria inataja mambo mawili tu, ghasia ama vurugu. Lakini uchaguzi pia unaweza ukasimamishwa au ukakatizwa na majanga makubwa ambayo yanaweza yakatokea wakati uchaguzi unaendelea. Kwa mfano kipindupindu kimelipuka au janga lolote lile limeingia kwenye nchi kama tulivyokuwa na *COVID* wakati ule. Sasa tulidhani kwamba Sheria ingefafanua vizuri zaidi ikaingiza majanga mengine au mambo mengine ambayo yanaweza yakafanya uchaguzi ukawa umekatizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kifungu hicho niende tena kwenye kifungu kingine cha 107 kwenye Sheria hiyo hiyo. Hii Sheria inasema wasimamizi wa uchaguzi wa Tume watahakikisha nyaraka zote ambazo kifungu hiki zinatumika zinatekeketezwa baada ya kupita kipindi cha miezi sita. Sisi tuliona kipindi cha miezi sita ni kifupi sana na mashauri mengine ya uchaguzi yanakwenda miaka miwili, mitatu. Sasa kama ni kipindi cha miezi sita yanatekeketezwa, sasa ushahidi ule hautakuwepo.

Mheshimiwa Spika, sasa tulishauri, pengine Serikali wangetumia njia za kisasa zaidi. Wangetumia TEHAMA ili kupunguza mizigo ya makaratasi na vitu vingine na kuhakikisha kwamba uhifadhi wake unakuwa salama zaidi. Kwenye hii Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ninaishia hapo.

Mheshimiwa Spika, kwenye Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kulikuwa na suala la kwanza lilikuwa ni la jina. Kwa kweli tunaishukuru Serikali imekubali kwamba, Tume hii ya Uchaguzi itaitwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa huru kwa kweli kwa sababu Sheria Mama inasema hii Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara huru. hata Muswada wenyewe kwenye Ibara ya 6(1) inasema Tume hii itakuwa huru. Sasa, tulikuwa hatuoni sababu ni kwa nini sasa tusiweke neno "Huru" kwenye jina la Muswada huu wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi? Tunashukuru kwamba Serikali ilikubali.

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ambacho kwenye Sheria hii tulipata shida kidogo "Rais atatoa Mwenyekiti na Makamu…" hiki kimekwishakuwa *resolved* kwa sababu Serikali imesema Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kuna utaratibu ambao utawekwa kuhakikisha kwamba na wenyewe wanapita katika maeneo ili Rais anapopelekewa anapelekewa watu ambao watakuwa wako sahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kifungu cha 18 kwenye Sheria hii ya Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi. 18(1) inasema "kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atakayeteuliwa na Rais

baada ya kupendekezwa na Tume." Nadhani na yenyewe imezingatia kwa namna fulani. Kwa sababu, wakati wadau wamekuja walikuwa na malalamiko juu ya wajumbe wa Tume, walikuwa na malalamiko juu ya Mkurugenzi wa uchaguzi kwamba anateuliwa na Rais tu. Lakini Sheria imeweka wazi sasa na inasema, baada ya kupendekezwa na tume maana yake baada ya kupitia mchakato fulani ndipo Rais atapelekewa ili aweze kuteua Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nadhani nimekuwa nguli kiasi cha kutosha. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Seleman Jumanne Zedi, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchagia Miswada mitatu, Muswada wa Sheria ya Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa kwa mwaka 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika *perspective* mbili. Utakuwa na upande mmoja wa *perspective* ya *kihistoria (Historical perspective)* na upande wa pili nitauchambua kidogo sana kwenye *perspective* ya kisheria *(Legal perspective)*.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu la Tanzania lilipata uhuru mwaka 1961. Baada ya kupata uhuru kulikuwa na mabadiliko mbalimbali ya kikatiba, Kisheria na kiutawala kwa ajili ya kuhakikisha tunaweka uimara wa mifumo yetu ya kuendesha nchi baada ya kutoka kwenye mikono ya kikoloni.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda na mabadiliko mbalimbali ya kikatiba mpaka tukaja tukapata Katiba ya kudumu ambayo ni ya mwaka 1977 ambayo imefanyiwa tu mabadiliko mbalimbali ambayo tunadumu nayo mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata Katiba tulianza kuwa na mabadiliko mbalimbali katika uendeshaji wa nchi. Kuna mawimbi makubwa mawili ambayo tulipitia kama Taifa. Tukianza na wimbi la kwanza la mwaka 1984 ambapo ilitulazimu kuingiza mkataba wa haki za binadamu kwenye Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yalikuwa ni mabadiliko makubwa ambayo yalibadilisha sana kwa kiwango kikubwa mfumo wa uendeshaji wa nchi na ndiyo msingi wa hizi haki ambazo leo tunasema na kuziiimba kwamba, kuna haki ya kupiga kura, kuna haki ya kufanya hiki na kuna haki ya kufanya kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake baada ya ile *Bill of Right* ya Mwaka 1984 ndipo nsingi wa uendeshaji wa katiba kwa nchi yetu ukawa umewekwa na tukaanza kwenda katika mlolongo wa kufuata hizo haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, mabadiliko haya ndiyo yaliyokwenda yakasababisha tukapata Sheria ambayo leo tunakwenda kuifanyia mabadiliko, Sheria Mama ya Uchaguzi ya Mwaka 1985. Miaka takribani 40 umri wa mtu mzima na *actually* ndiyo umri wangu mimi. Leo tunakwenda kupata Sheria mpya ambayo ina mabadiliko makubwa chini ya uongozi wa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mabadiliko hayo tulikwenda tukakutana na wimbi lingine mwanzoni mwa miaka ya 90 ambapo iliundwa Tume ya Nyalali *(Nyalali Commission)* 1991 ikaja na mapendekezo na ikaja na kitu kinaitwa *The 40 Oppressive Laws* (Sheria mbaya 40). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili wimbi la pili ambalo lilikuwa ni kubwa lilikuja kufanya mabadiliko makubwa katika nchi yetu ambapo Mheshimiwa Rais katika kipindi kile Alhaji Mwinyi, alipounda hii Tume ilipokuja na mapendekezo ilisababisha tukazaa kitu kinachoitwa *Political Parties Act* ya Mwaka 1992 na ndiyo msingi wa vyama vingi vya siasa vya leo tulivyo navyo kimuundo na kiuendeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo takribani miaka 30 Mama yetu Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anakwenda kutuletea hii Sheria tunaifanyia mabadiliko makubwa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepita makwimbi makubwa mawili. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, anakwenda kuandika historia ya wimbi kubwa lingine la tatu katika nchi yetu ambapo leo tunapitisha Sheria kubwa tatu zinazokwenda kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa nchi kiutawala, kisiasa na kidemokrasia. Tumpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uamuzi mkubwa alioufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Tanzania ni moja kati ya nchi zinazoendelea ni nchi ambazo tunaitwa nchi za Dunia ya tatu. Siyo rahisi sana kwa Rais wa nchi ambaye naye atakuwa mgombea, kupeleka Bungeni Sheria tatu zifanyiwe mabadiliko makubwa na mwakani nchi yake inaingia kwenye uchaguzi. Mheshimiwa Rais ametutendea haki watanzania na Mwenyezi Mungu ambariki sana. Hii ni fahari kwa Taifa letu la Tanzania, ni fahari kwa Rais wetu lakini pia ni fahari kwa Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi Marais wao walioko madarakani wanapoelekea kwenye uchaguzi hata tu wakisemwa kidogo na vyombo vya habari inakuwa ni nongwa. Lakini mama yetu ameamua Sheria tatu kubwa zije Bungeni tuzifanyie mabadiliko tena kwa mchakato wa wazi. Wadau wanaitwa mpaka na vyombo vya habari waje kwenye ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kutoa maoni yao. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hatua kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia miswada mitatu, na mimi ningependa kidogo nichangie. Kwanza nitachangia kwenye mapendekezo yangu kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kwenye Ibara ya 76 (B). Ibara hii imetoa utaratibu kwa msimamizi kwa kuteua wale wasimamizi wasaidizi. Nimeona Ibara imeeleza lakini imesema kwamba itatoa imeweka kama *discretion* kwake yule msimamizi.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kwamba yale maelezo yaseme kwamba atateua kwa vigezo vitakavyowekwa halafu Waziri kwenye kanuni ndiko aweke sasa vigezo. Kwamba, kama msimamizi mkuu atakuwa ni mwanamume basi msimamizi msaidizi atakuwa ni mwanamke, ili tuliangalia suala la usawa wa kijinsia. Pia tuweke vigezo vya kitaaluma na vigezo kulingana na maeneo ambayo watu watakuwa wanatoka na kupatiwa. Tuweke vigezo ambavyo vinashikika na kutekelezeka. Huwezi ukahitaji uwe na wasimamizi wa uchaguzi; kwa mfano uende kwenye Kata yangu ya Mwamashimba Igunga, au uende kule Mwamakima Ipumbulya au Iborogero, uchague useme unahitaji msimamizi msaidizi awe na kigezo cha *degree* ya Kwanza utaishia kupata mtu mmoja ama wawili. Tuweke vigezo ambavyo vinatekelezeka kama ambavyo vipo katika Katiba yetu ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 50(7) ambayo ningependa kuchangia, kuna suala la wagombea kuwasilisha fomu za uteuzi. Utaratibu uliotajwa katika hii ibara unasema kwamba atakaposhindwa mgombea kuwasilisha zile fomu basi atawasilisha kiongozi mwingine wa chama kwa niaba yake. Naomba Mheshimiwa Waziri kwenye utengenezaji wa kanuni mseme ni kiongozi wa *level* gani; kama ni wa kitaifa ama ni wa kimkoa au kiwilaya. Lakini sasa, kwa kuwa kuna chaguzi za kitaifa kwa maana ya Rais, Mbunge, kwa ngazi ya wilaya na Diwani kwa ngazi ya Kata ni vyema mwakilishi akatoka kwenye ngazi husika ya uchaguzi unapofanyika. Kama ni Diwani kata Mbunge wilaya au jimbo na taifa kwa upande wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo ningependa kutoa mapendekezo jioni hii ni Ibara ya 30 ambayo inaweka utaratibu wa rufaa na zila dhamana. Kwa sasa sheria hizi tunapojadili na kupitisha tunatanua wigo wa demokrasia. Lakini Ibara hii inaminya tena wigo wa haki. Maana yake nini, tunataka twende; tunapotanua wigo wa demokrasia inabidi tutanue na wigo wa haki. Wanasheria wanasema *access to justice*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Demokrasia inaongezeka lakini unapowekwa kwamba yule mtu lazima aweke dhamana ili kukata rufaa na dhamana yenyewe hapa ikishawekwa tu kwenye

thamani ya fedha maana yake unapunguza haki ya watu tena kushiriki. Hii ni kwa sababu, fomu Tume ya Uchaguzi mtu mgombea anapewa bure, lakini iwe vipi kwenye kufuata rufaa lazima aweke dhamana *(bond)?* Kwa hiyo mimi naomba hili Mheshimiwa Waziri na Serikali tuliangalie. Kwa kuwa tumeamua kupanua wigo wa demokrasia basi tupanue na wigo wa upatikanaji wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Vyama vya Siasa. Niipongeze Serikali kwa hatua kubwa ambayo mmeifanya mpaka kufikia hatua hii ambapo Muswada umekuja. Pia niipongeze Kamati chini ya Dkt. Mhagama Monsinyori kwa kazi nzuri ambayo wameifanya wamechambua vizuri sana. Nikipitia sheria hii kwa haraka kuna maeneo kama matatu ambayo tutaenda kuyapata.

Mheshimiwa Spika, Jambo la kwanza, Sheria itaenda kujenga uwazi kwenye vyama vya siasa. Kutakuwa na uwazi katika matumizi ya fedha za umma lakini pia kutakuwa kuna uwazi katika uendeshaji na utaratibu uliowekwa katika usimamizi wa vyama. Sheria pia itajenga uwajibikaji. Viongozi wa vyama vya Siasa watawajibika kwa wanachama wao lakini watawajibika pia kwenye sheria za nchi ambazo zitakuwa zimeweka muongozo na utaratibu na kanuni zitakazotengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa la tatu, sasa Sheria hii inaenda kuhakikisha vyama vya siasa vinakuwa na mfumo unaoeleweka kitaifa na si kuwa vyama vile vya *briefcase* au vyama vya watu wachache. Unakuta mtu kasajili chama cha siasa kwa kwa malengo ya kutafuta fedha kwa wahisani au wafadhiri lakini hana ofisi nchini, hana mhuri; na kwa hiyo kinakuwa ni chama cha uchaguzi, baada ya uchaguzi kimekwisha. Kwa hiyo tunataka sasa hivi kuweka mfumo *(institutionalization)* ambapo vyama vitafuata utaratibu wa nchi na vitakwenda katika utaratibu ambao unaweza kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache nashukuru, naunga mkono hoja na naunga Taarifa ya Kamati, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na michango wako wageni ambao tunao jioni hii humu Bungeni.

Wageni 52 wa Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Bunge pamoja na Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo; hawa ni Walimu Wakuu ama Wakuu wa Shule za Wazazi za Chama Cha Mapinduzi kutoka nchi nzima, Wageni wa Waheshimiwa Wabunge hawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa ni walimu wanatoka kwenye hizo shule lakini pia wameongozana na maafisa kutoka makao makuu ya Chama cha Mapinduzi, karibuni sana Bungeni *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Selemeni Jumanne Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo Mheshimiwa Ighondo Ramadhani Abeid ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia miswada hii mitatu iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kimsingi ndiye chimbuko na msingi mkuu ambao hatimaye umetupelekea kufikia miswada hii mitatu kutokana na falsafa yake ya *4Rs,* ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameizungumzia na sina haja ya kuirudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, tukianzia na Mheshimiwa Anne Kilango ambaye amezungumzia vuzuri sana suala la unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kijinsia katika kampeni za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli sisi wote hapa ni Wabunge na tumeshiriki kwenye chaguzi na tumeona kabisa kwamba suala la ukatili na unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa wagombea wanawake

mara zote limekuwa ni kero sana kwenye chaguzi zetu. Lakini pia nimefurahishwa na Waheshimiwa Wabunge ambao wamegundua kwamba mapendekezo ya miswada hii ya sheria iliyokuja ilikuwa haijabainisha kwenye sheria kama unyanyasaji wa kijinsia au ukatili wa kijinsia kwenye uchaguzi ni kosa ambalo limo kwenye sheria na hatimaye liweze kutengenezewa adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi kama Kamati tulilibaini hilo wakati wa mijadala yetu ya miswada hii, hasa Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Tulibaini kwamba jambo hilo linakosekana kwenye Muswada, kwenye mapendekezo ya Sheria, jambo la kwamba mgombea anapofanya ukatili wa kijinsia kwa maana ya maneno machafu, matusi au jambo lolote kwa mgombea mwenzake basi liwe kosa kisheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kugundua hilo sisi kama Kamati tumekuja na jedwali la marekebisho *"schedule of amendment."* Maana yake ni kwamba tumependekeza kuingiza kifungu kipya kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais Wabunge na Madiwani, kifungu kipya ambacho hakikuwepo. Kifungu hichi sasa kinakwenda kutambua kwamba unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kijinsia ni kosa na linatakiwa lipate adhabu. Kwa hiyo niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumza kwa uchungu kabisa kuhusu jambo hili la unyanyasaji wa kijinsia kwamba halimo kwenye miswada. Ni kweli halikuwemo lakini Kamati imebaini hilo na imekuja na marekebisho yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *schedule of amendment,* "jedwali la marekebisho" la Kamati yetu limeanza kwa kuweka *marginal note* mpya ambayo itakuwepo kwenye kifungu kipya. *Marginal note* hiyo itakuwa inasema makosa ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwenye hicho kifungu kipya. Kifungu hicho kipya cha 135 ambacho ni kipya, hakikuwepo, sisi tumekipendekeza, kitakuwa kinasema mtu ambaye atatenda kitendo chochote cha unyanyasaji au ukatili wa kijinsia kwa mgombea mwenzake atatenda kosa la ukatili wa kijinsia katika uchaguzi. Na iwapo

atatiwa hatiani atatumikia kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au vyote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa mimi kwenye adhabu hapa kutokana na ukubwa wa kosa hili nashauri, Wabunge tutajadili, lakini ningeona kwamba kusiwe na *option* ya faini huyu mtu anayefanya ukatili wa kijinsia kuwe na *option* moja tu ya kufungwa na iwe ni miaka miwili kwa kima cha chini na miaka mitano ili iwe fundisho. Kwa sababu faini kuna watu ambao wana uwezo wa kuzitoa, kwa hiyo wanaweza kutoa faini na wakaendelea kunyanyasa wagombea wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumziwa sana ni Ibara ya sita ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ambayo ilikuwa inazungumzia Wakurugenzi wa Halmashauri, Majiji, Miji, Halmashauri za Wilaya kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, suala hili lilizungumziwa sana na wadau waliokuja mbele ya Kamati. Na kama ambavyo Taarifa yetu imesema, kwa mara ya kwanza Kamati yetu ilisikiliza wadau wengi sana. Ule Ukumbi wa Msekwa kila siku kwa siku zote ulikuwa unajaa sana; na tulisikiliza wadau kutoka taasisi za dini, wadau kutoka vyama vya siasa, asasi za kiraia na watu binafsi. Jumla tulisikiliza kama watu 1,700. Nadhani haijawahi kutokea hivi karibuni katika historia ya Kamati za Bunge kusikiliza maoni kutoka kwa wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili lilizungumziwa sana, na kuna baadhi ambao walisema Wakurugenzi wana shida katika kusimamia uchaguzi, lakini kuna baadhi wengine walisema Wakurugenzi hawana shida, shida inaweza ikawa jambo lingine. Ninakumbuka vizuri mojawapo ya chama cha siasa ambacho kilisimamia hoja ya kwamba pengine shida si Mkurugenzi labda kuna jambo lingine *beyond* zaidi ya Mkurugenzi ambalo hatulijui. Na walikwenda mbali mpaka wakatoa na takwimu za uchaguzi wa 2005, uchaguzi wa 2010 na uchaguzi wa 2015 na uchaguzi wa 2020, na chaguzi zote hizi zilisimamiwa na Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, walionyesha *trend* kwamba uchaguzi wa 2005 vyama vya upinzani vilipata Wabunge, na uchaguzi ulisimamiwa na Wakurugenzi na hakukuwa na malalamiko ya Wakurugenzi. Mwaka 2010 vyama vya siasa viliongeza idadi ya Wabunge na uchaguzi huo pia ulisimamiwa na Wakurugenzi na hakukuwa na malalamiko ya Wakurugenzi. Mwaka 2015 vyama vya upinzani viliongeza zaidi idadi ya Wabunge wa majimbo na chaguzi hizo zilisimamiwa na Wakurugenzi na hakukuwa na malalamiko ya Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo 2005 hakukuwa na malalamiko ya Wakurugenzi 2010, hakukuwa na malalamiko ya Wakurugenzi 2015 hakukuwa na malalamiko ya Wakurugenzi 2020 idadi ya Wabunge wa vyama vya upinzani *graph* ilivyoshuka ndipo kukawa na malalamiko ya Wakurugenzi. Kwa hiyo moja wapo ya chama cha siasa kilisema pengine kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kuona kwamba pengine Mkurugenzi kama Mkurugenzi inaweza isiwe shida labda shida nyingine ni *beyond* ya ile nafasi ya ukurugenzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari yote sisi kama Kamati tumeleta tena *schedule of amendment,* yaani marekebishoya sheria ambayo hii inakuja kwenye Muswada. Na tumezingatia haya maoni ya wadau lakini tumezingatia pia maelezo ya Serikali, kwa hiyo tumeamua ku-*strike a balance,* kwamba tumeona hakuna ulazima sana wa kumtamka Mkurugenzi moja kwa moja kwenye sheria. Sisi tukapendekeza kwamba ile ibara ya sita tumeleta mabadiliko ya kufuta Ibara ndogo ya kwanza ya pili na ya tatu na kuiandika upya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tumesema kwamba kwa madhumuni ya uchaguzi utakaofanyika chini ya Sheria hii Tume ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi itateua kwa kuzingatia nafasi aliyonayo mtu katika Ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa watumishi wa umma waandamizi wenye sifa na kwa idadi kuwa wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata. Kwa hiyo mapendekezo yetu sisi kama Kamati kwenye jedwali la

marekebisho, *(schedule of amendment)* tumependekeza kuondoa hilo neno kwamba Mkurugenzi *automatically* ndiye atakuwa msimamizi wa uchaguzi na badala yake tumesema Tume itateua afisa mwandamizi miongoni mwa watumishi wa umma kutokana na sifa zitakazo kuwepo ambaye ana sifa ya kuwa msimamizi wa uchaguzi ndiye atakuwa msimamizi wa uchaguzi badala ya Mkurugenzi. Kwa hiyo hilo ndilo pendekezo ambalo tumelileta pia kwenye *schedule of amendment.*

Mheshimiwa Spika, mambo mengine mengi ambayo Kamati ilikuwa imashauri kimsingi Serikali ilikubali. Na niungane na Waheshimiwa wengine akiwemo Mheshimiwa Ndaki na wengine, kwamba kwa kweli Serikali chini ya Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera na Uratibu amekuwa msikivu sana wakati tulipokuwa tukifanya majadiliano na Kamati na walikuwa wana *respond* kwa haraka na kwa umakini. Kwa kweli walikuwa *very objective,* na kama kamati tulifurahishwa sana na *attitude* yao ya kuyaangalia mambo kwa busara, kwa hekima na upana bila kujali tu kwamba sheria imesimama vipi. Kwa hiyo kimsingi mambo mengi sana Serikali tulipopeleka hoja zetu mbele yao waliyachukulia *positively* na mengi wamekubali. Na kama hotuba yao ilivyosema, mambo mengi wataleta. Wameshaandaa *schedule of amendment* kwa ajili ya kukubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo ya Kamati ya Usaili sina haja ya kuyarudia, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, Wajumbe wa Tume namna ambavyo watachaguliwa kwamba sasa hivi kutakuwa na *transparence* hasa wale wajumbe watano na wale wawili wengine ambao kutakuwa na namna fulani ya *procedure* ambayo itafanyika kabla ya kupelekwa kwa Rais ambako Rais hatimaye atafanya uteuzi wa mwisho. Jambo hili halikuwepo nyakati za nyuma, na ni hatua kubwa ambayo itakuwa imepigwa kuhakikisha kwamba tuna tume huru ya uchaguzi ambayo inatenda haki. Lakini jambo lingine ambalo pia Serikali imekubali ni kuondoa ada ili kumwezesha mwananchi asizuiliwe ama asipate kikwazo chochote katika kutumia haki yake ya msingi sana ya kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miswada ilikuja na mapendekezo ya ada na tozo mbalimbali, hata kwa mambo mengine ya kawaida pale mtu ambapo amepoteza kadi, kadi imefutika, na kwamba mtu anataka kubadilisha taarifa zake. Mambo yote yalikuwa na ada lazima ulipe hela ndipo haya mambo yafanyike lakini nadhani kwa busara haya mambo sasa ada hazitakuwepo ili wananchi waweze kutumia haki yao ya kimsingi ya kuweza kupiga na kuchagua viongozi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa sababu hoja zingine zote nilizokuwa nimepanga kuzizungumza pia zimezungumzwa vizuri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba kuunga mkono na kuwashawishi Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja hii miswada mitatu kwa manufaa ya wananchi wetu ili tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha falsafa yake ya *4Rs* inatimia na inapokelewa vizuri na wananchi

Mheshimiwa Spika, ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimewataja hapa Wabunge wawili ambao wangefuata lakini nimeletewa ujumbe hapa kwamba hawa wawili watachangia kesho, sasa tutaendelea na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, ajiande.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuchangia kwenye Miswada iliyopo mezani, Muswada wa Sheria ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi na Muswada wa *Political Parties Affairs* (Muswada wa Vyama vya Siasa) lakini kabla sijaenda kwenye *content* ya mchango wangu, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kuwaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikupongeze wewe kwa jinsi unavyoendelea kulisimamia Bunge. Niipongeze pia Kamati kwa niaba ya Bunge lote chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Mhagama kwa jinsi walivyotuwakilisha Wabunge wote kwenye kusimamia Miswada hii. Mimi siyo Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa hiyo sikupata nafasi ya kusikiliza wakati wanakutana na wadau lakini nimepata bahati ya kusikiliza ripoti yao walioileta Bungeni leo. Kwa hiyo, mchango wangu utajikita kwenye yale mambo ya jumla ambayo kama msomi wa nchi hii nataka niyachangie na ni mambo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ninataka kulichangia ilikuwa ni hoja ambayo imebebwa na Mama Anne Kilango Malecela, nampa pole kwanza sana kwa yaliyomtokea. Mchango huo pia ukabebwa pia na Mheshimiwa Keisha, mchango huo pia utasemwa na Mama Mwakagenda, mchango huo pia ukasemwa na Mheshimiwa Mtaturu, kuhusu hoja ya kuweka kosa la jinai la udhalilishaji liwe kosa la uchaguzi, lakini wakati nasikiliza mchango wa Mheshimiwa Zedi hapa akiwa kama Mjumbe wa Kamati akawa kama vile amejibu hoja ambayo mimi nilitaka kuisema lakini pia majibu yake hayajotosha. Kwa sababu amesema kama Kamati wametengeneza *schedule of amendment* ya kuliweka kosa ambalo halikuwepo kama ilivyopendekezwa na Wajumbe wengine kwenye Kifungu Kipya cha 135.

Mheshimiwa Spika, bado kulifanya kuwa kosa la jinai la kawaida ambalo mchakato wake utasubiri kama mchakato wa jinai nyingine uende yaani ukashtaki uliyedhalilishwa, Polisi wapeleleze, upelekwe Mahakamani, utiwe hatiani halafu ufungwe kati ya miaka miwili na mitano. Huyo uliye m-*defame*, uliyemdhalilisha, uliyemtukana kipindi cha kampeni ameshapata *damage*, *damage* ambayo hairekebishiki tena, *irreparable,* hairekebishiki tena. Hoja ya walitoa mchango ambayo na mimi ninayo ni makosa haya ya udhalilishaji ambayo siyo lazima yawatokee wanawake, makosa haya yanaweza yakamtokea mtu yeyote yule, iwe ni kosa la uchaguzi ambalo linatolewa adhabu kipindi hicho hicho cha uchaguzi na mtu anaweza

kuenguliwa kuendelea na uchaguzi ikiwa atalifanya kosa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka wakati tukiwa *high school* huko yaani kwenye *higher learning institutions* tulipokuwa tunasoma tulikuwa tunafanya uchaguzi ambao ilikuwa ina-*tensions* kubwa sana. Kwa kwetu kule Zanzibar tulishafika wakati wa uchaguzi wa Rais wa Chuo tuko kwenye *tension* ya uchaguzi na kampeni vikasambaa vikaratasi anaambiwa mgombea mmoja kwamba ni *gay*. Sijui niseme neno gani la Kiswahili liingie kwenye *Hansard*? Baradhuli eeh?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. RAMADHANI SULEIMAN RAMADHAN:** Basi ni baradhuli. Kumuita mtu baradhuli kwetu kule ni ngumi na ugomvi, *reputation* yake unaipoteza yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mpaka unataka kurejesha *reputation* yake muda umeshapita. Hiyo ndio hoja waliyoitoa ambayo na mimi naisimamia. Kwa hiyo, *schedule of amendment* ambayo Kamati wanasema haitoshi bado kulifanya hilo kosa la kawaida la jinai inahitaji *first track* ili kuzia watu wasilifanye. Mnaona ukubwa wa *damage* aliyehadithia hapa leo, Mama Kilango. Sisi sote tumeumiza na jambo lililomtokea, maana yake kama siyo ujasiri wake ingekuwa ndiyo amepita kwa uongo aliozuliwa, hiyo ilikuwa sehemu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu yangu ya pili ya mchango ni kwamba kulikuwa na kilio cha muda mrefu sana…

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan kunywa maji kidogo hapo nimekuagizia maji hayo. *(Makofi)*

*(Hapa mhudumu wa Bunge alimpelekea maji ya kunywa Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan)*

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu pili, nataka kuzungumza na Watanzania kupitia Spika na kiti chako. Kumekuwa na upotoshaji wa muda mrefu sana au malalamiko ya baadhi ya wadau wa demokrasia kutaka mabadiliko kwenye Sheria za Uchaguzi. Kwa muda mrefu sana, watu wamelia, watu wengi hoja wakisamama kila kwenye *platform* wanasema sheria hizi hazifai zinahitaji zifanyiwe mabadiliko. Sheria hizi mbovu zinahitaji zifanyiwe mabadiliko, tuna sheria za zamani zinahitaji zifanyiwe mabadiliko. Kaingia Rais mwenye dhamira ya dhati ya kutaka kufanya mabadiliko, wamebadilisha kibao hao hao, saa hivi wamekuja na kauli mbiu kwamba hawaoni dhamira ya dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nawashangaa hamuoni dhamira ya dhati kwenye Miswada hii, mnataka mkaione dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais wapi tena? Wale ndiyo wamekuwa wakilalamika mambo ambayo Miswada hii ndiyo imekuja kuleta mwarobaini wa suluhisho ya yale malalamiko yao. Kwa muda mrefu sana wamelalamika. Sasa Miswada imekuja na majibu, wanarudi kusema hawaoni dhamira ya dhati, wanataka dhamira ya dhati gani tena zaidi ya haya yaliyoweka humu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja, wamelalamika kwa muda mrefu sana kuhusiana na mgombea kupita bila kupingwa, mgombea pekee. Wamelalamika uchaguzi wa mwaka 2020 kumezaliwa Wabunge karibia 26 ambao walipita bila kupingwa na yalikuwa malalamiko makubwa tena makubwa, sasa kumekuja mwarobaini kwenye Miswada hii kunaondoa kwamba mgombea hautapita bila kupingwa jambo hilo halipo tena, unataka dhamira ya dhati gani? Unaipima, unapata *guts* ya kupima dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais kwenye jambo hili kweli? Jambo hili umelililia linaondoshwa unataka nini tena? Hiyo dhamira ya dhati unayoitaka ya Mheshimiwa Rais ni ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sheria hii inaenda kuondoa hiyo hoja ya kwamba kuna watu watapita bila ya kupingwa na haya yalikuwa ni maamuzi ya Mahakama kwenye shauri la Kikatiba lililofunguliwa, shauri Namba 19 la mwaka 2021, Mahakama Kuu

walisema vipengele vya Sheria ya Uchaguzi *(National Election Act)* ambayo ilikuwa inaruhusu jambo hilo litokee ni *unconstitutional* toka 2021. Sasa Mama anaenda ku-*accommodate* maamuzi ya Mahakama kwenye Muswada huu halafu na maoni ya wadau kwenye Muswada huu, wewe bado unapita kusema kwamba huoni dhamira ya dhati! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ilikuwa ni mamlaka aliyonayo Rais aliyopewa na Katiba ni makubwa sana yamesemwa na kila mtu hapa leo, kuhusiana Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba yeye ndiye ana mamlaka ya kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. Wajumbe wengine wa Tume watachaguliwa kulingana na sheria itakayotungwa na Bunge lakini mamlaka hayo yalikuwa ni ya kwake pekee yake na wameyalalamikia kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais sasa ameleta Miswada Bungeni yenye dhamira ya dhati, wewe unaenda ku-*question* dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais, kwenye Mamlaka anapunguza baadhi ya nguvu zake kimamlaka aliyopewa na Katiba kwa ajili ya kupunguza hayo malalamiko yako. Yeye alikuwa ana mamlaka ya kuchagua hao Wajumbe bila kumshirikisha mtu yeyote yule. Sasa kaenda kwenye miswada hii kusema kwamba kutakuwa na Kamati za usaili za kumsaidia ili yeye awe mtu wa mwisho baada ya watu hao kufanyiwa usaili, unataka kupima dhamira ya dhati, unataka dhamira ya dhati gani tena?

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya 74 ya Katiba, Ibara ndogo ya Tano, Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya Kikatiba ya kumuondoa Mjumbe yeyote, ilikuwa anamuondoa Mjumbe yeyote kwa muda ambao yeye ataona na mazingira yaliyowekwa pale, katika Miswada hii utaratibu umegeuza kidogo kwamba sitamuondoa isipokuwa nitaunda Kamati ya Uchunguzi halafu Kamati ya Uchunguzi itanishauri mimi. Unataka dhamira ya dhati gani?

Mheshimiwa Spika, unapita ukiwadanganya Watanzania kwamba miswada hii iondoshwe Bungeni si mizuri, haifai kana kwamba humu hakuna chochote kilichofanywa. Tunataka nini tena? Hiyo dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais unataka upewe nini tena? Tunaelekea kwenye uchaguzi mwaka ujao, hapa imesemwa *nature* ya viongozi wakuu wa nchi hasa hizi zinazoendelea, hili jambo siyo rahisi lisingetokea, lakini dhamira ya dhati hiyo ambayo wewe unai-*question* ndiyo imempelekea Mheshimiwa Rais kukubali miswadi hii ije. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani na Serikali za Mitaa, sheria hizi zinaunganishwa pamoja na Sheria hii ya Uchaguzi wa Rais na Uchaguzi wa Wabunge na Madiwami kwa pamoja, hilo lilikuwa ni moja kati mambo waliyoyalamikia. Kwenye ile Tume au kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia na vyama vingi vya siasa vilikuja na mapendekezo 83, mapendekezo 61 yamefanyiwa kazi, unataka dhamira ya dhati ipi tena? Unataka kupima dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais awe na dhamira gani tena ya dhati zaidi ya hiyo, 61 yamefanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo 12 yako kwenye *process* yanaendelea sasa hivi kufanyiwa kazi, kati ya hayo yaliyobaki ukitoa 61 katika 83. Tunapima dhamira ya dhati tena ipi? Kwa hiyo watanzania wenzangu chonde chonde msikubali kudanganywa, msikubali kupotoshwa, msikubali kugombanishwa na Rais wenu. Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan anayo dhamira ya dhati ya kutaka kuleta maridhiano, kuleta mabadiliko, kudumisha demokrasia kwa sababu mambo haya yalishalalamikiwa na wao wakati wa kukusanya maoni waliitwa kwenye hizo kamati, wakaenda wakatoa maoni yao na ndiyo mapendekezo haya yakapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo ndiyo ambayo nilitaka kusema na kuonesha na kuwaambia Watanzania kwamba kwenye Miswada hii, kuna dhamira ya dhati ya kutaka kuleta mabadiliko ya kweli kwenye demokrasia ya nchi hii. Kwa hiyo, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais na nawaomba Wabunge wenzangu tuipitishe Miswada hii na tuunge mkono hoja sote kwa pamoja ili

uchaguzi wetu unaofuata wa 2025 ukawe miongoni mwa chaguzi itakayoweka historia kubwa ya Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, katika Nchi yetu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu kuasisiwa kwa Taifa letu Mwenyezi Mungu ametusaidia kupata Miamba Sita kwa Awamu Sita za Uongozi, na katika Miamba Sita hii Mwenyezi Mungu ametusaidia kuonesha jinsia zote mbili miongoni mwa Miamba Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo yalikuwa yakitusumbua katika Taifa letu ni katika kugusa sheria hizi tatu ambazo zimeletwa leo mbele yetu. Maneno yalitokea mpaka 2014 tulikuwa tuna nia ya dhati ya kuona kwamba sasa tuandike Katiba mpya, hata hivyo ilishindikana. Leo tumempata Rais wa Awamu ya Sita, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa jinsia ya kike amethubutu kwamba sasa tunataka tufanye marekebisho kwenye zile sehemu nyeti kabisa ambazo ukizigusa unakuwa umegusa utamu wa Madaraka ya Rais na ya sisi tulioko hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ameonesha kwa nia ya dhati kutoka kwenye moyo wake na kuyajengea falsafa na kuamua kuchukua hatua thabiti za kuhakikisha kwamba sasa tunakwenda kufanya mabadiliko. Katika Biblia kitabu cha Mwanzo 11:6 inasema hivi; "Mungu akasema tazama watu hawa ni Taifa moja na lugha yao ni moja na haya ndiyo wanayoamua kuyafanya, hawatashindwa na hakuna kitakachoweza kuwazuilia".

Mheshimiwa Spika, ni kwamba wameamua kuwa wamoja, kuongea lugha moja na wana mambo wamekusudia kuyafanya kama Taifa lao moja hakuna kitakachowazuilia. Ili sisi kuwa

wamoja, kuweza kujiletea maendeleo, kujenga Taifa letu lazima tuongee lugha moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaongeaje lugha mmoja tusipokuwa na maridhiano? Mheshimiwa Rais akaamua kwamba sasa tufanye maridhiano na ili ufanye maridhiano, kwa nafasi yake ilivyo kubwa, mambo ya maridhiano au mahusiano hata Mwenyezi Mungu aliyafanya. Wanadamu walipopotea Mungu aliamua kuja kufanya *reconciliation* lakini ili kufanya *reconciliation* ile ilimtaka ashuke aje kwenye *level* ya binadamu. Mama Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye jinsia ya kike, akashuka kuja kwenye *level* ya watu wa kawaida, akiwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu. Akatengeneza urafiki na wale wenye maneno maneno akaenda nao hadi kwenye sherehe zao akala nao. Akawaita watu bila kuangalia itikadi za imani zao, dini zao, uwezo wao, vyama vyao vya siasa, watu wa chini akakaa nao kwa pamoja, akatengeneza Kamati ya Maridhiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakakaa kwa pamoja ni kipi ambacho kinasemwa semwa kwenye Taifa letu kinatufanya tusiende pamoja? Wakakaa wakiongozwa na kiongozi mkubwa wa dini wakajadili. Wakapata mambo 83 yanayofanya tusiwe wamoja kwenye nchi yetu, yamkini tushindwe kufikia maksudi yetu. Katika 83 Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mambo 64 wameyatekeleza ikiwepo na pamoja kwamba sasa kama mikutano ya hadhara ilikuwa haipo fanyeni mikutano ya hadhara, na wengine waliokimbia wakajiona wakimbizi kwenye nchi hii rudini, *enjoy* maisha kwenye nchi yenu. Sasa walioko nje sasa hivi siyo wakimbizi wako tu wana-*enjoy* wanatumia haki yao ya msingi *universal right* ya kuishi popote wanapotaka lakini si kwa wasiwasi wa kukaa kwenye nchi hii. Hiyo ni nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walipotaka kuandamana wasaidizi wake wakasema siku hiyo tutakuwa tunafanya usafi wa mitaa, akasema tulieni waacheni waandamane, wapeni na *ambulance,* wapeni na ulinzi waseme wanachokitaka. Nia ni *reconciliation* tufikie maridhiano tuwe wamoja, sisi ni Taifa moja tuongee lugha

moja, lolote tunalokusudia katika kujenga uchumi wa nchi yetu tutaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kufanya haya bila kuwa mstahimilivu, kuamua kuacha yale matashi yako yote ya Uamiri Jeshi Mkuu ukashuka ukakaa na watu huwezi kuyafanya, akafanya yeye kwa matendo kuja kukaa na watu wa chini kabisa, lakini hatuwezi kufanya hii bila *reform* lazima tukubali kufanya mageuzi ya dhati. Watu wameogopa kuigusa Tume ya Uchaguzi, kuitengenezea sheria mimi naigusa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunakwenda kushughulika na Tume. Kama tatizo ni Tume tuishughulikie Tume, kama tatizo ni mimi Rais kuwa na Madaraka mengi basi sawa naachia Madaraka kwenye Kamati ya Usaili nipendekezeeni hao watu mnaowataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni kifaru alinyofoa pembe yake akampa mtu mwingine, ingekuwa ni tembo amenyofoa meno yake akampa mtu mwengine. Nia yake ya dhati ni kuona kwamba tunakuwa wamoja tulijenge Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akasema, kufanya mageuzi haikuwa rahisi, hata sisi tulio wa kwake, maana katika watoto wa mama kuna mtoto mmoja yaani huyo huwaga yuko kwenye pochi, lakini kuna mwingine anaweza kuwa yuko pembeni kidogo; hata watoto wake wengine hawakuelewa. Akasema, mtatakiwa kuelewa, lazima twende kwa *style* hii ili tufanye *reformation* ili tufanye *rebuilding,* tuwe wamoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameanza kufanya *rebuilding* kwa kusema sasa tunaenda kufanya mageuzi ya kuandika. Tunaleta sheria Bungeni, tunafanya mabadiliko ili watu wajisikie wako huru, halafu baada ya hapo twende mbele tufanye kazi ya kujenga Taifa letu. Sasa tupambane na umasikini, tupambane na maradhi, tupambane na upungufu wa ajira kwenye Taifa letu, tuijenge nchi yetu, tuache maneno maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Watanzania tufike mahali na sisi tuungane na Mheshimiwa Rais kwenye nia zake za *4R,* tufanye

*rebuilding* ya Taifa letu. Hili ndilo Taifa Mungu alilotupa, hatuna Taifa lingine, na wengine wana-*quote* na kujifunza kutoka kwa watu wengine, lakini nataka nikwambie huko tunakojifunza ndiyo kubaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, amesema hapa Mheshimiwa Tadayo wengine mataifa yao yalipata uhuru tangu miaka ya 1776 mpaka 1919 bado walizuia wanawake miaka 144 mbele, bado haki ya demokrasia kwa wanawake ilikuwa haiwezi kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka miaka ya 1960 sisi tumepata uhuru bado kuna mataifa haya tunayodhani kwamba ni bora sana, watu weusi walikuwa hawaruhusiwi kupiga kura. Ili upige kura lazima kwanza ufanye; kuna kile kipengele kimoja wanasema ukatengeneze mazingira mazuri na jirani yako mweupe ili kupiga kura ulipe kodi ya kura, ili kupiga kura kama wewe ni mlafi mlafi tu, huruhusiwi kupiga kura. Sijui huo ulafi walikuwa wanaupimaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hao ndiyo tunataka tujifunze kutoka kwao! Watanzania tutakurupuka kutoka kwao. Haya huwa wanasema, ilikuwa ni miaka 144 baada ya kupata uhuru, sisi Taifa letu lina miaka 62. Ina maana tungekuwa kwenye nchi hizo mpaka leo sisi wanawake humu tusingekuwepo, kwa sababu haturuhusiwi kuchagua wala kuchaguana, wala Mheshimiwa Rais asingekuwepo. Sasa wakati mwingine, nasi tumepewa akili. Usipende kulazimisha ubongo au unajizima *data* unabaki *airplane mode. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanatakiwa kuja kujifunza kutoka kwetu sisi. Rais wetu miaka 62 amewezaje kufanya demokrasia? Waliwezaje wale miamba sita akiwepo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuwashirikisha wanawake kwenye harakati za mapambano ya uhuru na kuwafanya wachaguliwe *day one from the day of independence? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wao wameshindwa! Tuache kujizima *data,* wanatamani kuja kujifunza. Ukiona mtu anakushawishi bwana, unajua kule sijui Marekani, sijui wapi, sijui wapi; mwambie

sisi ni Watanzania, ni Taifa moja na Mungu alitupa ubongo, tuna uwezo wa kupanga mambo yetu wenyewe kabla hatujaiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania tumuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili sasa tuache hizi kelele na mbambamba za haturuhusiwi kusema; haturuhusiwi sijui nini; tuelekeze akili zetu kufanya *innovation* na *creativity* ya kulijenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwasihi wanawake, tujifunze kutoka kwa mwamba huyu wa Awamu ya Sita, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye jinsia ya kike. Tusilielie. Mungu akawaambia watu fulani Taifa moja, nawapeleka ninyi vitani siyo kwamba siwapendi, nawapeleka vitani ili mkajifunze vita. Kwa hiyo, wakati mwingine wanawake ukitukanwa mwambie *yes,* hapa ndiyo kwenyewe; unafundishwa vita ya kupambana. Usipoenda vitani utakuwa huwezi kupigana; na majibu huwa yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naweza nikatolea mfano, nilitukanwa Iringa pale, nikaambiwa Jesca Msambatavangu huwa mnamchagua Mbunge hana mume. Nikajibu tu jukwaani, wewe unayelalamika kwamba sina mume, ndio mwanaume, katoe posa Kamati Kuu ya CCM, njoo unioe, vinginevyo utakuwa una matatizo ya kiume. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Weweee!

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, tusilie, mama ameshaonesha njia, mwamba wa Awamu ya Sita, unalilia nini? Simama tumepata fursa sawa. Wanawake tusimame twende tukagombee, tuitetee nchi yetu, na tunamwona mama ndiye Rais aliyesema, natoa mamlaka yangu ya Tume ya kuteua sijui Wajumbe wa Tume, nayatoa napeleka kwenye Kamati, si amepeleka! Si mambo mazuri! Watu wanaandamana, situmii nguvu, natumia akili. Ndiyo maana Biblia inasema, "*Ishi na mwanamke kwa akili.*" Kwa sababu mwanamke ni *very intelligent,* anatumia akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaandamana, peleka *ambulance,* peleka Polisi awasindikize, watafanya nini? Hata sisi mama siku ile amebeba khanga ameingia kwenye ule ukumbi anacheza, nikasema jamani, yule ni mama ana khanga ya chama kile, hee! Yaani mimi alinifundisha kitu kipya sana. Nikapiga magoti nikamwambia Mungu, nakushukuru. Akaingia, akatoka salama. Wewe unaogopa nini? Huyo aliyekusema, utanyofoka ngozi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi nchi tunasema hizi, nchi hizi ambazo tunawasifia, mtu huruhusiwi kupiga kura, hiyo miaka hiyo sasa. Mpaka miaka ya sitini sitini, huruhusiwi kupiga kura kama hujui kusoma na kuandika wala huruhusiwi kupelekwa na mwenzio kukupigia kura. Kama huwezi kutoa kiapo kwa mdomo, huruhusiwi kupiga kura. Sasa kama mtu ni kiziwi, labda ana ulemavu inakuwaje? Sisi tunataka tuwaambie jamani eh, msitupeleke mputa. Sisi Taifa hili ni changa, lina miaka 62, ninyi mna miaka 200, mtusubirishe kidogo, tunajipanga. *Afterall, we are well off* kuliko ninyi mlivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme, haya mambo yalitukuta kule nyuma. Kule nyuma watu walileta vurugu kwenye Katiba Mpya, wakafikiri kuna mtu wanamkomesha, lakini ile Katiba Mpya mimi nilivyoiona, ilipendekeza hata Tume hiyo huru waliyosema. *Afterall* hii Tume ni huru kwa sababu hiyo ibara ya 74 (7) inasema Tume hiyo itakuwa huru, kwenye Katiba iko.

Mheshimiwa Spika, Mgombea binafsi aliruhusiwa, haya mambo yote ambayo tunayafanyia *amendments* yaliruhusiwa, lakini watu wakajizima *data,* wakabaki *airplane mode,* wakajifanya wanatoka, leo tena wanatusumbua turudi kwenye mambo yale yale. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hamna kubaki kindege, mtu ajifungue *data,* tuunge mkono hii hoja, tupitishe nchi yetu. Tuna mambo ya maana ya kufanya kuliko haya maandamano ambayo tunafanya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tutamsemea, tutamtetea popote na Mungu atusaidie. Wanawake sikilizeni niwaambie, watu wa Taifa fulani wakamwambia Mfalme Daudi; "Wewe ni mfalme wetu." Alikwenda kwenye vita akanusurika kufa, aliporudi, walivyopata ile habari wakasema, "Wewe ni mfalme wetu, hatutaruhusu tena uongozane na sisi kwenye vita ili hiyo taa isije ikazima, halafu wote tukazima Taifa zima." Wanawake tunatakiwa tutoke na kauli moja. Sisi lazima tumtetee Mama Samia ili ile taa ya wanawake isije ikazima kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba wanaume, mnapomuongelea Mama Samia muongelee kama binti yako wa kike, mwongelee kama mama yako mzazi, mwongelee kama *your baby* ambaye unataka kumuoa, sio yule ambaye mmetengana vyumba. Taa hiyo ikizima, mmezima ndoto za binti zenu, taa hiyo ikizima mmezima ndoto za mama zenu, taa hiyo ikizima, tumezima ndoto za wanawake wa Tanzania, na Afrika inataka kujifunza kutoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatumpi sifa za bure, kasema Mheshimiwa Mwakagenda, kura siyo namba, kura ni uwezo na umahiri. Wale miamba sita walifanya mambo mema, lakini hili waliogopa kuligusa, mwanamke ameligusa na tunakwenda kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya, nawaomba Watanzania, tuache ushabiki, sisi ni Watanzania, wala tusijidhalilishe, Mungu anatupenda, nchi hii imekuwa ya ahadi, siku zote imepokea watu wanaopata shida kwenye nchi zao, tumekuwa wa kwanza kupigania uhuru upande wa *Southern SADC;* sisi ndio tumeongoza mapambano, tuliwasaidia hata *South Africa, no matter economically* wako mbali, lakini tulishirikiana; na ndiyo chama kimebakia ambacho hatusemi kama ni vipi, lakini ndicho kilichozaa na vyama vingine vyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi ni nchi makini, tuko *strategically, spiritually, physically and mentally.* Kwa hiyo tusijidhalilishe Watanzania tupambane twende na hoja zetu.

Tunapitisha Muswada huu kwa nia njema Miswada mitatu ili muwe huru kugombea, kuchagua wagombea mnaowapenda. Mliambiwa kwamba ooh, mtu anapita bila kupingwa hampati fursa ya kuchagua; sasa mnakwenda kupata fursa, akipita peke yake mpeni kura za ndiyo au hapana halafu ataonekana kama mnamhitaji, lakini tumewapa fursa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nimalizie.

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga ahsante sana.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie moja tu. Naomba tuaminiane, tupendane, tuheshimiane, hakuna mtu mwingine atakuja kuijenga nchi yetu. Leo humwamini Jaji wa Mahakama ya Rufani, leo humwamini Mkurugenzi, hivi ninyi wanaume, sasa hii nchi ataongoza nani? Tukakodi Wakurugenzi? Tukodi Majaji wa kuja kutuongoza na ninyi mpo na mmesoma?

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, huwezi kusema Wakurugenzi wote wabaya, majaji hawafai, wako *presidential officials* kivipi? Ninyi ndio ninyi, nchi hii mmepewa kurithi, tutatumia majaji wetu, wasomi wetu kwa ajili ya mambo yetu kama ambavyo tukipata shida wanatusaidia. Tutatumia Wakurugenzi kama ambavyo wanasimama Maafisa Waandamizi; kama vituo vya afya wanasimamia, ujenzi wa shule wanasimamia, leo unashindwa kumwamini kulinda kura, kivipi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa siku yetu ya kwanza ya Mkutano huu wa Kumi na Nne na sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.51 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 31 Januari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*